

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 10 Mei, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MHE. ROSE S. TWEVE K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

SPIKA: Ahsante sana, Katibu!

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali Waheshimiwa Wabunge tunaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi sasa aulize swali lake.

Na. 161

Utekelezaji wa Ahadi za Rais - Arusha Dc

MHE. NOAH L. SAPUTU aliliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Jengo la Wagonjwa wa Nje, Jengo *X-Ray*, Jengo la Watoto na Jengo la Utawala katika Hospitali ya Wilaya Olturumet Halmashauri ya Arusha?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Rais-TAMISEMI mwezi Aprili, 2021 ilipokea maombi maalum ya shilingi milioni 800 kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa Hospitali ya Olturumet ambayo miundombinu yake imechakaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga shilingi bilioni 16.55 kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali Kongwe 19 nchini. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa awamu kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ajili ya ujenzi na ukarabati wa Hospitali Kongwe nchini ambapo Hospitali ya Olturumet itapewa kipaumbele.

SPIKA: Mheshimiwa Naoh Saputu, swali la nyongeza.

MHE. NOAH L. SAPUTU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kuuliza maswali mawili. Kwa kuwa ujenzi wa hospitali hii na upanuzi wake ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muda mrefu sasa na haikuweza kutekelezwa.

Je, nini kauli ya Serikali kwa wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi ambao wanategemea hospitali hiyo kwa asilimia kubwa na hajajengwa mpaka sasa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kutembelea hospitali hiyo ili ajlonee halli halisi ya wagonjwa walivyo wengi na upanuzi wa hospitali hiyo haikuweza kufanyika kwa muda mrefu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeza sana Mheshimiwa Noah Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi kwa namna ambavyo anawasemea kwa dhati wananchi wa jimbo lake. Nimhakikishie kwamba Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaendelea kushirikiana naye kuhakikisha wananchi wanapata matunda ya Serikali yao sikivu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ahadi ya Mheshimiwa Rais, ni kwamba ahadi za viongozi wetu wakuu wa nchi ni maelekezo, na ndiyo nimemuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye mwaka ujao wa fedha 2022/2023 tutatafuta

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

fedha ili tuweze kuanza utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais katika ukarabati hii ya Arumeru.

Mheshimiwa Spika, pili, nipo tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge, tutakubaliana hili baada ya Bunge twende tukaitembelee hospitali hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Aleksia Kamguna swali la nyongeza.

MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kituo cha afya cha Mtimbila kina *x-ray* lakini hakina jengo la *x-ray* wala hakina mhudumu wa *x-ray*. Je, ni lini Serikali itaenda kujenga hilo jengo na hatimaye kupeleka mhudumu ili watu wapate huduma hizo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aleksia Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba vituo vyetu vya afya ambavyo havina miundombinu ya majengo yanayostahili kuwepo, ikiwemo majengo ya *x-ray* ni kipaumbele cha Serikali kujenga majengo yale. Kwa hiyo, tutahakikisha kwa sababu tayari kuna *x-ray* machine katika kituo hiki lakini hatuna jengo, tutaweka kipaumbele ili tuanze ujenzi wa jengo hilo kuititia mapato ya ndani lakini pia tutatafuta fedha Serikali Kuu.

SPIKA: Mheshimiwa Grace Tendega swali la nyongeza.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Zahanati ya Kata ya Lumuli ambayo iko katika Jimbo la Kalenga, ziko mbili. Katika Zahanati hizi, wananchi walishapaua na wameshajenga majengo yako vizuri lakini hakuna samani, vitendanishi na vifaa tiba, ni lini Serikali itapelekea hivyo vitu ili wananchi waweze kupata huduma ya afya?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze sana wananchi wa Iringa kwa kujenga zahanati hizi na kuzikamilisha. sasa niseme, kwamba vifaa tiba vinavyohitajika katika ngazi ya zahanati, gharama yake siyo kubwa sana ni imani yangu kwamba mkurugenzi wa halmashauri husika, wana uwezo wa kutenga kati ya ile asilimia 40 na 60 kununua vifaa tiba hivi. Kwa hiyo, naelekeza halmashauri, wakurugenzi watenge fedha, wanunue vifaa tiba zahanati hizi zisajiliwe ziweze kutoa huduma ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Swali langu, ni lini Serikali itatathimini upya uhitaji wa eneo la zaidi ya eka 35, 30 ili kujenga hospitali za wilaya. Ni sehemu zippi utapata eneo kubwa kiasi hicho, kwanini tusitafute namna ya kujenga hizi hospitali hata kuweka ghorofa moja moja badala ya kutafuta eneo kubwa kiasi hicho?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika ujenzi wa hospitali za halmashauri yako ya aina mbili. Kuna maelekezo ambayo yanaendana na halmashauri za vijiji, ambako ardhi ni kubwa wanahitaji kutenga angalau ekari 30 na kuendelea kwa sababu hospitali zile tunazojenga

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tunatazama miaka 50 au mia moja ijayo, haituangalii miaka mitano au kumi ijayo. Kwa hiyo, tunahitaji kuwekeza katika maeneo makubwa ili hata baada ya miaka 100 miundombihu tu itabadilika lakini eneo litaweza kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, kwa maeneo ya mijini tunaweka eneo siyo kubwa sana, inategemeana na eneo, lakini tunapendekeza kujenga majengo ya kwenda juu kwa maana ya maghorofa. Kwa hiyo, maeneo yote mawili yametazamwa, maeneo ya mijini, tunakwenda kwa maghorofa, kama eneo halitoshi lakini maeneo ya vijiji tunataka angalau eka 30 kwa sababu tunaona miaka mingi ijayo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, swali namba 163 kwa sababu linamhusu Naibu Waziri huyu amalize maswali yake halafu akienda hatarejea tena hapa mbele. Kwa hiyo tutaruka swali la Mheshimiwa Bonnah, tutalirejea baadaye kidogo. Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma Mbunge wa Bububu sasa aulize swali lake.

Na. 163

Mafunzo kwa Makundi ya Vijana na Wanawake Wanaopata Mikopo

MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa mafunzo kwa makundi ya vijana na wanawake wanaopata mikopo ili waweze kujiwesha kiuchumi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mwantakaje Haji Juma Mbunge wa Jimbo la Bububu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 23 ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu pamoja na marekebisho yake, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeelekezwa kutenga fedha kutoka katika fedha za marejesho ya mikopo hiyo kwa ajili ya kuwajengea uwezo pamoja na ufuatiliaji wa shughuli za vikundi kwa vikundi vilivyokubaliwa kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya vikundi 6,317 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika halmashauri zote nchini vimepatiwa mafunzo kuhusu masuala ya uongozi, usimamizi wa fedha, uendeshaji wa miradi na utoaji wa taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Mwantakaje Juma, swali la nyongeza.

MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali la nyongeza.

Katika vikundi hivyo 6317 kwa upande wa Zanzibar ni vingapi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma, Mbunge wa Jimbo la Bububu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana kwa kazi nzuri kubwa anayofanya, lakini naomba niichukue hili ili tukafanye mchanganuo kuona kwa upande wa Zanzibar vilikuwa vikundi vingapi katika hivi vilivyoinishwa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Wengi wanaochukua mikopo hiyo ni pamoja na kinamama ambao wanakuwa na vikundi vyao vya vikoba, lakini hela zao huwa zinazunguka kwenye makasiki na wakati mwingine kasiki linaibiwa.

Ni lini sasa Serikali itazungumza na mabenki ili waweze kuongezewa angalau asilimia moja ya kuweka kwenye account zao kuendesha viofisi vidogo dogo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba akina mama na vikundi vingine na hususani akina mama wanakopa lakini pia wana shughuli za vikoba, na kuna *risk* hizo za mara nyininge kupoteza fedha kwa njia mbalimbali. Nimepokea wazo lake, tumepokea kama Serikali tutalifanyia tathmini kuona namna ya kuongea na benki ili tuone njia sahihi ambayo inaweza kufanyika kunusuru changamoto.

SPIKA: Mheshimiwa Agnes Hokololo, swali la nyongeza.

MHE. AGNES E. HOKOLOLO: Mheshimiwa Spika, ahsane kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha vile vikundi vyta wanawake na vijana ambao wanapata mikopo ili mikopo hiyo isipotee wafanyiwe tathmini ya kazi wanazokwenda kuzifanya?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agnes Hokororo Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya vikundi hivi yya wanawake, vijana na wenyewe ulemavu havijapewa mikopo, moja ya kigezo muhimu ni kufanya tathmini ya uwezo lakini na utayari wao wa kuanza kufanya shughuli hizo za ujasiliamali ili kuhakikisha zile fedha wanazokopeshwa zinaleta tija, lakini pia hazipotei. Tumeendelea kufanya hivyo na ndiyo maana tumeona matokeo mazuri ya urejeshaji ukiangalia kwa miaka inavyokwenda mpaka sasa kuna *improvement* kubwa na tutaendelea kufanya hivyo.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa vikundi vingi ambavyo vinapata mkopo wengi wanatoka maeneo ya mijini. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba elimu inatolewa ili wanawake na vijana wa vijiji pembezoni waweze kupata mkopo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika halmashauri zetu zote zikiwemo za vijiji kuna fungu ambalo linatengwa kuitia maafisa maendeleo ya jamii kwa ajili ya kuhamasisha, kuelimisha, wanawake vijana na watu wenyewe ulemavu kunufaika na fursa za mikopo hiyo. Kwa hiyo suala hilo tunalifanya na jambo kubwa ambalo tunaendelea kulifanya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ni kuongeza nguvu ili wananchi wapate nguvu ya kutosha waweze kunufaika na mikopo hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea sasa aulize swali lake.

Na. 162

Serikali Kujenga Nyumba za Walimu Nchini

MHE. BONNAH L. KAMOLI aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo kwa kuhakikisha inajenga nyumba za Walimu kama inavyofanya kwa Majeshi ya Ulinzi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya TAMISEMI – Mheshimiwa David Silinde majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya mahitaji ya Nyumba za Walimu Nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo, Serikali itaendelea kupeleka fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ikiwemo ujenzi wa nyumba za walimu kulingana na upatikanaji wa fedha kuititia vyanzo mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga shilingi bilioni 37.85 kwa ajili ya ujenzi wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nyumba za walimu katika shule za Sekondari na shilingi bilioni 43.63 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu katika Shule za Msingi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya nyumba za walimu katika maeneo ambayo kunauhitaji mkubwa likiwemo na jimbo la Segerea kadri fedha zitakavyopatikana.

SPIKA: Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, swali la nyongeza.

MHE. BONNAH L. KAMOLI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nilikuwa nataka commitment ya Serikali ni lini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nilikuwa nauliza kwa kuwa sasa hivi mfumo ndiyo unaochagua wapi nyumba ziende. Kwanini sasa Wizara isipeleke hizi nyumba kwa majimbo badala ya mfumo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Jimbo la Segerea kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali imeshaweka *commitment* ya kwa kutenga fedha katika bajeti yake, na ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha ambao tumepitisha bajeti ya TAMISEMI, tumetenga jumla ya bilioni 81.48 ambazo zitatumikwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu katika shule za misingi na sekondari.

Kwa hiyo, ni *commitment* kubwa ya Serikali. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba tutafanya hivyo katika maeneo yote nchi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, ni kwamba amekuja tu mfumo kwamba tupeleke katika majimbo. Niseme tutaendelea kuzingatia maeneo yote yenye uhitaji mkubwa ikiwemo katika jimbo lake kama ambavyo ameainisha. Kwa sababu lengo la Serikali ya Awamu ya Sita ya Mama Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kwamba tunamaliza hii kero kwa kadri fedha itakavyokuwa inapatikana. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Longido ina changamoto kubwa sana ya nyumba za walimu ambayo inasababisha ukosefu mkubwa wa walimu katika wilaya hii. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto hii?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zaytun Swai Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi kwamba fedha tumetenga kwa mwaka huu unaokuja lakini vile vile tutazingatia maeneo ya pembezoni ikiwemo Longido kama ambavyo ameainisha. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mohamed Monni swali la nyongeza.

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Chemba ina jumla ya shule za msingi 103 za Serikali na tumeongeza shule nane kwa matokeo ya fedha za UVIKO, lakini asilimia 70 ya shule zote hizi zipo vijijini ambavyo ni ngumu sana kupata nyumba

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

za kupanga, naomba kujua mna mkakati gani wa maksudi wa kujenga nyumba za Walimu kwenye shule hizo? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Monni Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Serikali ni kujenga nyumba maeneo ya pembezoni na mionganini mwa mikakati ambayo nimeainisha ni pamoja na kutenga fedha, vilevile tuna miradi mbalimbali ambayo tumeiainisha ikiwemo *BUST*, *EP4R*, *EQUIP 2* yote hii lengo lake ni kuhakikisha kwamba tunapunguza hiyo adha kwa hiyo tutazingatia maeneo hayo ikiwemo Jimbo la Chemba. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Dorothy Kilave swalii la nyongeza.

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Spika, Ahsante. Sambamba na nyumba za Walimu Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga ofisi za Walimu au kukarabati ofisi zilizopo kwa ajili ya Walimu na kuweka samani zake ndani ya ofisi hizi, hasa katika Jimbo letu la Temeke? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dorothy Kilave Mbunge wa Temeke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama tulivyojibu kwenye upande wa nyumba za Walimu sasa hivi moja ya mkakati wetu mkubwa ni kuhakikisha kila tunapokenga madarasa tunaweka na ofisi za Walimu, kwa hiyo huo ndio mkakati wa Serikali ili kuhakikisha kwamba walimu wanakuwa na maeneo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mazuri ya kukaa ambayo yatawasaidia katika utendaji wao wa kazi wa kila siku. Hivyo, hilo lipo na limezingatiwa na Serikali ya Awamu ya Sita. Ahsante sana. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa George Kakunda swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Hili linahusu Majimbo yote ya Vijiji hasa hasa kule ambako kumejengwa shule shikizi, nyumba nyingi za Walimu zilizopo zimejengwa kwenye maeneo ambayo angalau Mwalimu anaweza akapata nyumba za kupanga, sasa hizi shule ambazo ziko kwenye maeneo ambayo Mwalimu hapati hata nyumba za kupanga.

Je, kwa nini hizo shilingi bilioni 43 zisielekezwe kwenye maeneo kama hayo badala ya kuangalia maeneo mengine? (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa George Kakunda Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nilipokuwa najibu swali nimeainisha kwamba maeneo ambayo tutayazingatia zaidi ni maeneo yenye uhaba, maeneo ya pembezoni kwa hiyo ni moja ya jambo ambalo sisi tumelizingatia. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge sasa aulize swali lake.

Na. 164

Kutengewa Bajeti Barabara inayounganisha Tanzania na Uganda

MHE. FLORENT L. KYOMBO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaitengeta bajeti barabara inayounganisha Uganda na Tanzania ya Kibaoni - Kakunyu kwenda Bugango mpakani ambayo iko chini ya *TARURA* wakati taratibu za kupandishwa hadhi zikiendelea ili iweze kupidika wakati wote?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi Rais, TAMISEMI naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hiyo ya Kakunyu - Bugango ni muhimu kwa kuwa inaungaisha Nchi jirani ya Uganda pia hutumika katika kukuza shughuli za kiuchumi kwa wananchi wa Missenyi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu huo, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Vijiji na Mijini (*TARURA*), kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilitenga jumla ya Shilingi Million 41.08 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo katika maeneo korofu yenye urefu wa kilomita 3.0 na kazi hiyo imefanyika na kukamilika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali imeendelea kuona umuhimu wa kuhakikisha kuwa wananchi wa Missenyi wanaweza kufika katika mpaka wa Bugango kwa kutenga jumla ya Shilingi Milioni 34.92 katika mwaka wa fedha 2021/

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

2022 kwa ajili ya matengenezo ya barabara nyingine iliyopo jirani iitwayo Missenyi Ranchi - Bugango jumla ya kilomita 17.3 ambapo Mkandarasi yupo eneo la kazi anaendelea ukamilishaji wa matengenezo hayo. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Florent Kyombo, swali la nyongeza.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Naomba niongezee maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 12 kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri ni ya muhimu sana kwa wananchi wa eneo hilo ikitokea Lubira, Kyabunaga, Bugango mpaka mpakani.

Je, sasa ni lini Serikali itaona umuhimu wa barabara hiyo kwakuwa inakidhi vigezo vyote vya kuhudumia na *TANROAD* dipandishwe hadhi kwenda kule iwe imepata bajeti ya uhakika?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, barabara ya kutokea Kiwanda cha Kagera *Sugarkwenda Kijiji* cha Bubali imekuwa ina changamoto kwa muda mrefu na inahitaji matengenezo makubwa.

Je, ni lini barabara hiyo itatengewa bajeti ili iweze kutengenezwa na wananchi waweze kutumia barabara hii? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mbunge ameomba barabara hiyo kupandishwa hadhi na jukumu hilo kubwa linafanywa na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wenzetu wa *TANROAD*, kwa kuwa Serikali ni moja basi sisi tutalipokea hilo ombi ka niaba ya *TANROAD*na watakwenda kulifanyia kazi kwa kufuata zile taratibu ambazo zinatakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Kagera Sugar kwenda Bubali ambapo ameainisha hapo ni lini itapangiwa fedha, mimi nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba nitawaagiza Maneja wa *TARURA* wa Wilaya na Mkoa wa Kagera waende wakafanye tathmini ili sisi tutafute fedha kwa ajili ya barabara hiyo. Ahsante sana. (*Makofî*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa Mbunge wa Busanda sasa aulize swalii lake.

Na. 165

Hitaji la soko la Maziwa Nchini

MHE. TUMAINI B. MAGESSA aliuliza:-

Je Serikali ina mkakati gani wa kushughulikia soko la ndani la maziwa kwa kuhimiza na kuhamasisha unywaji wa maziwa shulenii kabla ya kutafuta masoko ya nje?

SPIKA: Mheshimiwa naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Ulega majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini, Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na mkakati wa kukuza soko la maziwa nchini kwa kuimarisha na kuendeleza programu mbalimbali zinazochochaea unywaji wa maziwa ikiwemo programu ya unywaji wa maziwa shulenii. Mpango

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa unywaji maziwa shulenii umeweza kuwafikia watoto 90,000 wa shule za msingi 39 katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Iringa, Mbeya, na Tanga.

Vilevile Serikali inaendelea kuhamasisha unywaji maziwa nchini, kwa kutoa elimu kupitia vyombo vya habari, maonesho mbalimbali ya Wiki ya Maziwa Kitaifa inayoahimishwa mwezi Mei kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali itakutana na wadau mbalimbali wakiwemo wa tasnia ya maziwa ili kuandaa mikakati thabitii kwa lengo la kuongeza idadi ya shule zinazotoa huduma ya unywaji wa maziwa. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Ulega haujamaliza bado, bado haujamaliza kujibu maswali. Mheshimiwa Bryceson Tumaini Magessa swali la nyongeza.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ni dhahiri kwamba ndani ya nchi hii nzima wameshahamasisha shule 39 tu, sasa unaweza ukajua nchi hii ina shule ngapi na sasa zimehamasisha shule 39 tu kunywa maziwa na watu waliohamasisha ni 90,000. Sasa swali langu la nyongeza ni hili.

Mheshimiwa Spika, kwakuwa Mikoa yote iliyotajwa bahati mbaya sana ni kama Mikoa mitatu, minne na Mikoa tunayo mingi tu na hasa Mkoo ninaotoka mimi Mkoo wa Geita haukutajwa.

Ni nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha maziwa mengi yanayopotea huko vijiji kwa sababu yamekosa hifadhi yanaweza kupata hifadhi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili nini mkakati wa Serikali kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kuchakata maziwa ili tuwe na uelewa kwamba wafugaji ambao wanafuga sasa wana uwezo wa kufuga kwa tija zaidi? (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bryceson Tumaini Magessa Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mikakati yetu kama Wizara ni pamoja na kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa maana ya TAMISEMI ili kuweza kutanua wigo zaidi wa kuongeza idadi ya shule. Ni kweli kwamba shule hizi tulizozisema ni chache na kwa hiyo kwa kushirikiana na wenzetu tunayo imani ya kwamba tutaongeza idadi ya shule.

Mheshimiwa Spika, namna gani ya mkakati wa kuweza kuyakusanya maziwa ya vijijiini, ukitazama katika bajeti yetu ya mwaka 2021/2022 tunayoimaliza, Serikali iliondoa kodi ya vikusanyio kwa maana ya *cans* zile za *stainless steel* ambazo zilikuwa zikiuzwa takribani Shilingi 260,000, hivi sasa zinauzwa Shilingi 219,000. Hii imerahisisha kuongeza idadi ya *cans* za kukusanyia maziwa.

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine ni juu ya nini tulichonacho sasa kwa ajili ya kuongeza viwanda vidogo vya kutengeneza maziwa na kukusanyia maziwa kule vijijiini. Katika mwaka huu wa fedha wa 2022/2023 katika vitu vikubwa tutakavyokwenda kuvifanya ni pamoja na kuhakikisha kwamba tunatattua zile changamoto zinazowakabili wafugaji wetu na kupelekea kushindwa kusindika maziwa yao, ikiwa ni pamoja na kuondoa tozo zile ambazo ni kikwazo.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo naomba nimuhidi Mheshimiwa Magessa yeye na Wabunge wengine wakereketwa wa viwanda vidogo wakae tayari katika kutushauri na kuweza kufikia lengo hili.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri unasimama hapo hapo mpaka umalize, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Lindi Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 166

**Kujenga Chuo Kikuu Cha Uvuvi na Usafirishaji
Bahrini – Lindi**

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo Kikuu cha Uvuvi na Usafirishaji bahrini katika eneo la Kikwetu - Lindi ambapo tayari Ekari 150 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi haina mpango wa kujenga Chuo Kikuu cha Uvuvi katika eneo la Kikwetu Lindi Mjini. Hata hivyo, Serikali kupitia Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kwa maana ya *NIT* imepewa eneo lenye ukubwa wa ekari 125 liliopo Kikwetu Lindi. Eneo hilo ambalo tayari *NIT*imekamilisha taratibu za kumiliki, litatumika kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Lindi ya Chuo cha Taifa cha Usafirishaji ambacho kitatoa kozi katika ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada katika fani mbalimbali za usafirishaji na uchukuzi ikiwemo Utengenezaji wa meli, uendeshaji wa vyombo vya majini na huduma za bandari.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2022/2023 kazi zitakazofanyika katika eneo hilo ni kuandaa mpango kabambe wa matumizi bora ya ardhi katika eneo hilo. Sambamba na maelezo hayo, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inatarajia kujenga Kitivo cha Kilimo katika Halmashauri ya Lindi Mjini ambapo tayari wameomba kupatiwa hekta 500.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mipango ya maandalizi ya ujenzi wa chuo hicho inaendelea kwa ushirikiano kati ya Mkoa wa Lindi, Halmashauri ya Lindi Mjini na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

SPIKA: Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah swalilala nyongeza.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya Serikali ambayo yameonesha matumaini sasa ya kuanza mchakato wa ujenzi wa Chuo cha Usafiri na Usafirishaji pale Kikwetu.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi tumetoa Hekari 125 bure kwa Ndugu zetu hawa wa *NIT*, lakini hekari 150 kwa Ndugu zetu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Kilimo pale Lindi Mjini, sasa ni miaka mitatu, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

SPIKA: Mheshimiwa Maswali hayo unayotaka kuuliza kwa sababu umeshajieleza mwanzoni nenda moja kwa moja kwenye maswali.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, Je, ni lini sasa Serikali itawawezesha ndugu zetu wa *NIT* kuwapatia fedha kwa ajili ya kuharakisha ujenzi wa chuo hiki cha Usafiri na Usafirishaji? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalilala pili tunategemea kwamba chuo cha Kilimo Kampasi ya Lindi tungependa sasa kuongeza Kitivo cha Uvuvi na masuala ya kilimo cha Mwani kutoa fursa ya ajira kwa vijana na wananchi wa maeneo hayo ya Lindi na Mtwara. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa maswali mawili ya nyongeza ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Hamida Abdallah Mbunge wa Lindi Mjini. Mbunge huyu ni katika Wabunge wafuatiliaji sana wa masuala ya Wavuvi

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ni hili la lini watapewa fedha *N/T*. Nafikiri ni wakati mzuri ameuliza swali hili kwa sababu ni kipindi ambapo Serikali tupo katika kuwasilisha bajeti hapa Bungeni na kwa hivyo chuo cha *N/T* ni chuo cha Serikali na kipo katika hodhi ya Wizara zetu na hili litajibowi wakati Wizara husika itakapokuwa ina wasilisha bajeti yake hapa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni juu ya jambo la Kitivo ha Kilimo kuhusianisha na *course* za mifugo na uvuvi. Wazo na fikra aliyooitoa Mheshimiwa Hamida ni nzuri na mimi naomba niichukue kwa niaba ya Serikali ya Serikali na kwa hivyo basi tutaipeleka kwa wenzetu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama ilivyo desturi wawzeze kuunganisha fani hizi nazo ziweze kutolewa pale pindi chuo kitakapokuwa tayari. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Niabu Waziri Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaingia Wizara ya Maji niwakumbushe tena maswali mafupi sekunde 30 na majibu vivyo hivyo upande wa Serikali majibu mafupi, niwakumbushe tena. Wizara ya maji Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe sasa aulize swali lake.

Na. 167

Tatizo la Majisafi na Salama katika Mji wa Tukuyu

MHE. ANTON A. MWANTONA aliuliza:-

Je, ni lini mradi wa maji wa Tukuyu utakamilika?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa Mahundi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Wizara ya Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anton Albert Mwantona Mbunge wa Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa maji wa Tukuyu Mjini ambapo kazi zilizopangwa ni pamoja na uhifadhi wa chanzo, ulazaji wa bomba kuu Kilometra 9.5, ulazaji wa mabomba ya usambazaji Kilometra 20 na ujenzi wa tenki la ukumbwa wa lita 1,500,000.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa kazi zilizofanyika ni pamoja na uboreshaji wa chanzo cha maji na ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa Kilometra tatu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huo ulianza mwezi Septemba, 2021 na unatarajiwaa kukamilika ifikapo mwezi Machi, 2023. Mradi huo utasaidia kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Tukuyu kutoka asilimia 67 na kufika asilimia 90.

SPIKA: Mheshimiwa Anton Albert Mwantona swali la nyongeza.

MHE. ANTON A. MWANTONA: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, mradi unasuasua hauendi vizuri sana kwa sababu ni mwezi wa Nane sasa hivi hakuna kinachoendelea kule kwenye mradi, ukiuliza kwanini unasuasua wanatuambia kwamba ni kwa sababu unatekelezwa kwa *force account* na watumishi wapo *busy* na mambo mengine.

SPIKA: Mheshimiwa Mwantona swali.

MHE. ANTON A. MWANTONA: Je, Serikali ipo tayari kutafuta Mkandarasi badala ya kutumia *force account* ili

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mradi uweze kwenda haraka na wananchi wapate huduma ya maji? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza na Mheshimiwa Mwantona kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nipende kukupongeza kwa ufuatilaji mzuri wa hili suala la maji la Tukuyu Mjini na hata jitihada ambazo zimefikiwa kwa kilometra tatu ni kwa sababu ya ushirikiano, hivyo ninapende kukuondoa hofu.

Mheshimiwa Spika, *force account* ni moja ya namna ambavyo inasaidia katika Wizara na miradi inakuwa vizuri, lakini suala la kuweka Mkandarasi kwa baadhi ya maeneo naomba tuseme tumeipokea na tutaweza kushauriana namna bora ya kulifanyia kazi. (*Makofij*)

SPIKA: Mheshimiwa Genzabuke swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika Mji wa Kasulu maji yanayotoka kwenye mamombaa ni machafu na yana tope, tulileta ombi hili ndani ya Bunge lako na Waziri akaahidi kumaliza tatizo hilo. Je, ni lini sasa tatizo hilo la maji katika Mji wa Kasulu litapatiwa majibu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum Kasulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maji machafu na tope; hii tunaendelea kufanya kazi kuona tunajenga machujio, lakini vilevile kutumia dawa kutibu maji haya ili yaendelee kuwafikia wananchi yakiwa safi na salama.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Mrisho Gambo, swali la nyongeza.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa changamoto iliyopo Rungwe inafanana na Mradi wa Maji katika Jiji la Arusha.

Je, Wizara ina mpango gani kuhangaika na changamoto ya malalamiko ya wananchi ya *bill* kubwa za maji?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mrisho Gambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *bill* kubwa za maji tunaendelea kulifanya kazi kwa kutoa ushirikiano wa wasoma mita na mtumia maji, lakini vilevile tuna mfumo ambao tayari baadhi ya mikoa umeanza kutumika kuona kwamba unatumia *message* una hakiki kwamba ndicho ulichokitumia kisha unaletewa *bill*sasa ya malipo. Hivyo *bill*kubwa ukomo wake umeshafikia kwa sababu ya *unified billing system*.

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

MHE. IDDI KASSIM IDDI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka kumuuliza Naibu Waziri; Kata ya Mwanase, Mradi wa Maji wa Izuga umechukua muda mrefu sana. Sasa ni lini Serikali itapeleka fedha ya kuwalipa wakandarasi ili waweze kumaliza mradi huo wa maji wa Izuga?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

MHE. NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Iddi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupeleka fedha; tayari wakandarasi wanaendelea kulipwa, hivyo ninaamini hata

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mkandarasi huyu naye yupo kwenye foleni ya kulipwa. Tayari Katibu Mkuu pamoja na timu nzima inayohusika inaendelea kufanyia kazi suala hili la malipo.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 168

Ujenzi wa Mradi wa Maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji wa Kintinku- Lusilile katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni?

SPIKA: Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Kintinku-Lusilile ni mradi uliopangwa kuhudumia Vijiji 11 vya Chikuyu, Mwiboo, Mbwasa, Makutupora, Mtiwe, Chilejeho, Maweni, Mvumi, Ngaiti, Kintinku na Lusilile. Mradi huo unatekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza ilikamilika mwezi Oktoba, 2021 na Vijiji vitatu vya Chikuyu, Mwiboo na Mbwasa vinapata huduma ya maji. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2022 na kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika vijiji vyote 11.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, swali la nyongeza.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali, lakini nimshukuru

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waziri kwa majibu mazuri na kwa juhudini ambazo wanaendelea kuzifanya kuhakikisha kwamba huu mradi unakamilika.

Mheshimiwa Spika, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa tayari vijiji vitatu vimeanza kupata maji, ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba zile Jumuiya za Watumia Maji zinakuwa jumuiya endelevu zenye uongozi imara hususani kuweka mafundi katika ngazi ya kata ili waweze kusaidia?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; kuna maeneo ambayo Wizara imechimba visima mara tatu wamekosa maji, kwa mfano; Kijiji cha Mpapa, Igwamadete na hata Mazuchii. Nini mpango wa Serikali kuja na njia mbadala kunusuru vijiji hivi? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

MHE. NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swalii la nyongeza la Dkt. Pius Chaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nipende kupokea pongezi zake, lakini ni kwa sababu ya mashirikiano aliyonayo Mheshimiwa Mbunge na tuendelee kushirikiana lengo ni kuona tunapeleka maji kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na jumuiya kuwa na mafundi ngazi ya kata tayari hili ni agizo limeshatolewa na Mheshimiwa Waziri na maeneo yote yameshafanya. Hivyo nipende kutoa agizo kwa watendaji waliopo katika jimbo lako kama hawajafanya hivyo wanapaswa kufanya hivyo haraka iwezekanavyo kuwa na fundi ngazi ya kata.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na njia mbadala; sisi kama Wizara maeneo yote ambayo yana changamoto ya maji ardhini, tunaendelea kuona chanzo kilicho karibu kiweze kuleta maji safi na salama. Mheshimiwa Mbunge hili tuendelee kushirikiana kama ambavyo tumekuwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tukishirikiana, lengo hivi vijiji ambavyo maeneo haya maji ardhini ni shida, basi nao tuweze kuwapelekea kuitia njia nydingine.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Venant Daud Protas.

Na. 169

Kuboresha Mfumo wa Tiketi wa Reli ya Kati

MHE. VENANT D. PROTAS K.n.y. MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha mifumo ya upatikanaji wa tiketi kwa wasafiri wa reli ya kati?

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kabla sijamuita Mheshimiwa Naibu Waziri kuja kujibu Mheshimiwa Chaya wakati ukitaja swali lako 168 nadhani umesema 165.

Kwa hiyo, Makatibu mtarekebisha Taarifa Rasmi za Bunge, ni swali namba 168 na si 165.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (*TRC*) imekamilisha na imeanza matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwa maeneo yote yenye huduma ya *internet* ikiwemo Tabora kwa ajili ya kuboresha huduma na kurahisisha upatikanaji wa tiketi mtandao kwa wananchi. Mfumo wa ukatishaji tiketi kwa maana ya *e-ticketing* ulizinduliwa mwezi Aprili, 2020, kwa lengo la kupunguza matumizi, kuongeza mapato na ufanisi wa Shirika pamoja na kuondoa mianya ya upotevu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Serikali inaendelea na jitihada za kuongeza vitendea kazi kwa maana ya injini na mabehewa kwa lengo la kuboresha huduma kwa kuhudumia wananchi wengi zaidi. Tayari pia imesaini mkataba wa ununuzi wa mabehewa 22 ya abiria na vipuri kwa ajili ya ukarabati wa mabehewa 37 ya abiria.

Aidha, kuongezeka kwa vitendea kazi hivi kutaongeza idadi ya safari za treni za abiria na hivyo kupunguza changamoto ya upatikanaji wa tiketi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Venant Protas Daudi, swalii la nyongeza.

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swalii la kwanza; kumekuwa na mrundikano sana wa abiria katika stesheni ya Tabora Mjini na Stesheni zinazofuata za Goweiko, Tula na Malongwe wakienda pale wanakosa tiketi au tatizo la mfumo. Je, Serikali haioni haja ya kuongeza mabehewa ili wananchi wanapokwenda kupata huduma hiyo waweze kupata huduma na seat ili waweze kusafiri?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; kumekuwa na changamoto ya mfumo wakienda pale mfumo ukiwa chini hawawezi kupata tiketi na wakipanda kwenye treni wanapigwa faini asilimia 100. Je, Serikali haioni haja ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuboresha hii mifumo ili abiria akienda pale asipate usumbufu wa kupata tiketi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Igagula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia masuala haya ya mifumo pamoja na Wabunge wote wa Mkoa wa Tabora. Hata hivyo ameomba suala zima la kuongezewa mabehewa ili kuweza kuwa na *route* nyingi katika kusafirisha wananchi ama abiria kutoka Tabora mpaka Dar es Salaam, nataka nimhakikishile Mheshimiwa Mbunge kwamba Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan tayari alishatoa idhini na tulishasaini mkataba wa ununuzi wa mabehewa mengine mapya 22 yenye thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 14, lakini pamoja na hilo tutakarabati behewa 37 ili kuongeza safari za kutoka Tabora kuja Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, anasema changamoto za mfumo; ni kweli wakati mwingine kunakuwa kuna changamoto za mfumo kwa sababu ya *internet*. Nilishatoa maelekezo kwa uongozi wa *TRCkwamba* sasa wafikiri nje ya mfumo huu ili watumie mfumo unaoitwa *USSD* kwa maana ni *Unstructured Supplementary Service Data* ili kuweza kupatikana mfumo wakati wote, lakini hata hivyo mfumo tulionao unaruhusu kufanyakazi kwa njia ya *offline mode*.

Mheshimiwa Spika, nitoe maelekezo na maagizo kwa Ma-*TT*pamoja na wote wanaohusika na masuala ya *booking clerk* kwamba wahakikishe tiketi zinapatikana hata kama mfumo haupatikani kwa sababu unaruhusu mfumo wa *offline mode*.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 170

Ujenzi Wa Daraja La Kalebe – Bukoba Vijijini

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Daraja la Kalebe – Bukoba Vijijini ili kuwezesha magari yenye uzito zaidi ya tani kumi kupita kwenye daraja hilo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza maandalizi ya kujenga Daraja la Kalebe ambapo kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa daraja hili inaendelea chini ya Mkataba wa Usanifu wa Barabara ya Kyaka II – Kanazi – Kyetema. Kazi ya usanifu imepangwa kukamilika mwezi Oktoba mwaka huu wa 2022.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, swali la nyongeza.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; daraja hili ni la muda mrefu sana mimi napenda Serikali itueleze uhimilivu wa daraja hili ni wa kiwango kipi? (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Serikali kutojenga daraja hili ni kuendelea kuwapa adha wasafirishaji wanaosafirisha mizigo zaidi ya tani 10 ambao wanalazimisha kufanya mzunguko kuititia barabara ya Kyaka kwenda mpaka Bukoba Manispaa.

Je, hawaoni kwamba wanaendelea kuwapa adha wasafirishaji hawa?

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge mnapiga kelele sana, tuzungumze kwa sauti za chini, pamoja na mambo mengine humu Bungeni hatuko peke yetu, wapo watu waliokuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi, kwa hiyo, tuzungumze kwa sauti za chini.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, daraja alilolitaja la Kalebe tunavyoongea sasa hivi mkandarasi yupo anafanya kazi na tunategemea akamilishe mwezi Oktoba japo kwa jinsi anavyokwenda anaweza akamaliza hata kabla. Lengo kuu la kufanya usanifu huu upya ni ili daraja hili liweze kubeba mizigo zaidi ya tani 10 kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera na yapo madaraja mengine pia tunafanya usanifu ili kuyapa uwezo zaidi wa kubeba mizigo tofauti na ilivyo sasa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 171

Matukio ya Moto kwenye masoko Nchini

MHE. CECILIA D. PARESSO aliuliza:-

Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya matukio ya moto katika Masoko kwenye maeneo mbalimbali nchini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI, alijibu:-

Mheshimiwa Spika; kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresto, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na matukio ya moto katika baadhi ya masoko nchini. Uchunguzi uliofanywa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kushirikiana na vyombo vingine umebaini sababu mbalimbali za matukio hayo. Sababu hizo ni pamoja na uunganishwaji holela wa mifumo ya umeme, kutokuzingatia tahadhari za moto kwa mama lishe na baba lishe na shughuli za uchomeleaji holela wa vyuma katika masoko.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na vyanzo vya matukio hayo umefanyika ukaguzi wa kinga na tahadhari ya majanga ya moto sambamba na utoaji wa elimu na mafunzo ya matumizi ya vifaa vya awali vya kuzima moto katika masoko nchini. Aidha, Serikali kuititia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inashirikiana na Halmashauri zote kuboresha miundombinu ya kuzima moto katika masoko na kuhakikisha ramani za masoko mapya zinakaguliwa na zinakidhi vigezo vya kinga na tahadhari dhidi ya majanga ya moto.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kusisitiza uwepo wa vifaa vya awali vya uzimaji moto, uwepo wa ulinzi wa masoko kwa saa 24 na kuzingatia utekelezaji wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mapendekezo ya taarifa maalum za kaguzi zinazotolewa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Nashukuru.

SPIKA: Mhehimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa matukio haya ya kuungua masoko yamekuwa yaktokea kwa masoko haya ambayo hayajajengwa kisasa kwa sababu ya ukosefu wa miundombini hiyo ya uzimaji wa moto na kwa kuwa Serikali wamekuwa wakichukua kodi au tozo katika haya masoko kwa sababu kuna wafanyabiashara humo.

Je, sasa Serikali haloni ni muhimu kufikiria namna ya kuwalipa fidia wale wananchi ambao waliumizwa na matukio haya? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa hayo masoko ya zamani hayana miundombini, je, Serikali haionti umuhimu wa kuwa-*train* vijana mionganii mwao wanaofanya biashara na kuwawezesha wawe na vifaa vyote ili inapotokea majanga haya basi iwe ni raihisi wao wenyewe waweeze...

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Paresso, kama ifuatavyo:-

Mhehimiwa Spika, kuhusu suala la kulipa fidia hili ni suala la kisheria kwa mujibu wa sheria tulizonazo, sasa hatuwezi kusema lolote kwa sababu Bunge lako halijatoa utaratibu kama huo. Hata hivyo, nadhani lililo la umuhimu ni elimu ya kinga dhidi ya majanga haya ili yasitokee kwenye maeneo yetu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la mafunzo hilo ni jambo jema na tumeanza kutoa kupitia kwa *Scout*, lakini vilevile na mifumo yetu ya Serikali za Mitaa ili kuwawezesha watu hawa kujikinga na majanga ya moto au kuzima yanapotokea katika hatua za awali. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Manispaa ya Moshi kumekuwa na matukio mengi sana ya kuungua masoko, lakini jambo la kusikitisha ni kwamba manispaa haina ya magari ya kutosha ya kuzimia moto tunategemea magari kutoka *TPC*. Hivyo basi husababisha mali za wananchi kupotea. Je, ni lini Serikali itanunua magari ya kuzimia moto katika Manispaa ya Moshi? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, nashukuru, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuena Bushiri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Bushiri amekuwa akifuatilia kwa karibu masuala ya Kilimanjaro kuhusiana na Zimamoto, Polisi na mambo yote yaliyo chini Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mhehimiwa Spika, tunafahamu kama tulivyosema katika hotuba yetu iliyosomwa na Waziri wiki iliyopita maeneo mengi yana changamoto ya magari, lakini katika bajeti ijayo tumetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari, tutayapeleka kwenye maeneo *strategic* maeneo ya kimkakati ambayo yamekuwa yanakumbwa na tatizo la namna hii. Hata hivyo, uwepo wa magari tu si suluhisho la kudumu, bali utayari wa wananchi kukabiliana na mambo haya, lakini vile vile kinga dhidi ya majanga ya moto.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Josephat Gwajima, swali la nyongeza.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Matukio ya ujambazi, watu kupigwa, panya *roads* kwenye maeneo ya Kawe, Kunduchi na maeneo mengine yamezidi sana. Sasa ni nini tamko la Serikali?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali ya nyongeza la Mheshimiwa Josephat Gwajima, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kwa namna anavyofuatilia suala hili, kuna wakati ameongea kwenye *YouTube* tumeona, lakini baadhi ya taarifa hazikuwa kweli sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujambazi nakupigwa ni ni jukumu la msingi la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na hususani Jeshi la Polisi. Nadhani mmemsikia Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, *IGP* na Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam. Tumeahidi kushughulika na vijana hawa, tumesema wakitu-beep sisi tutawapiglia. Kwa hiyo, kwa tahadhali hiyo, tunaomba watafute kazi nydingine ya kufanya badala ya uhalifu wanaofanya dhidi ya binadamu kwani hatutauvumilia. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwa Wabunge na majibu kutoka upande wa Serikali. Wako Wabunge nawaona wamesimama, watafute viti vilivyo karibu nao wakae.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wabunge wanaotembea wakae viti vilivyo karibu nao.
Ahsante sana.

Tunaanza na wageni walioko jukwaa langu pale, nao katika kundi la wageni waliokaa hapo tunaanza na wageni wangu.

Waheshimiwa Wabunge, leo sijui mnataka kutajwa majina! Nikiwa nimesimama huruhusiwi kuongea Mheshimiwa Chaya na Mheshimiwa Genzabuke. Bunge linapaswa kuwa na utulivu, usikilize unaambibiwa nini? (*Makofi*)

Kwanza tunaanza na wageni wangu walioko kwenye jukwaa langu pale juu. Tunaanza na Mheshimiwa Habib Iddrisu ambaye ni Naibu Mnadhimu wa Kwanza wa Serikali Bungeni na Kiongozi wa Msafara. Hawa ni wageni wangu kutoka Ghana. Karibu sana. (*Makofi*)

Yupo pia Mheshimiwa Ahmed Ibrahim ambaye ni Naibu Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya walio wachache. Karibu sana. (*Makofi*)

Pia yupo Mheshimiwa Joycelyn Tetteh ambaye ni Mbunge. Karibu sana. Yupo pia ndugu Rosemary Arthur ambaye ni Afisa wa Bunge. Karibu sana. (*Makofi*)

Yupo pia Joseph Armo Ndah ambaye ni Afisa wa Bunge. Karibu sana. Yupo pia Ndugu Adam Jabiri ambaye ni Afisa wa Bunge. Karibu sana, sana, sana wageni wetu kutoka Ghana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, moja ya mambo ambayo tulijifunza kutoka kwenye Bunge la Ghana ni Wabunge walio wachache Bungeni kuitwa wachache badala ya kuitwa Kambi ya Upinzani. Ndiyo maana mmesikia pale kwamba viongozi wao anakuwa ni Mkuu wa Kambi ya Walio Wachache. Sasa hapa inabidi leo wajifunze tu Kiswahili pale juu, halafu sijui kama mwenyeji wao amekaa nao. Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Ndani, aah yuko humu ndani! (*Kicheko/Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Any way; since you don't understand Kiswahili I believe your host will translate at you later what we are discussing about you. But we learnt from Ghana about the majority and minority comes in the House. We used to call the minority 'oppositions,' so now we have changed our rules and copied the Ghana's style. (Makof)

So, we will talk more when we meet later but you are warmly welcome. And the fact that the members of Parliament are actually banging their tables, they are appreciating your coming. (Makof)

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda ambaye ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na hawa ni Watendaji Wakuu wa Wizara hiyo ambao wako kwenye jukwaa la Spika. Kwanza ni Profesa Eliamani Sedoyeka ambaye ni Katibu Mkuu, karibu sana; yupo pia Profesa James Mdoe ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, karibu sana; yupo pia Dkt. Carolyne Nombo ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, karibu sana; wapo pia Wenyeekiti wa Bodi na Kamati mbalimbali na tunaanza na Profesa Joseph Semboja ambaye ni Mwenyeekiti wa Kamati ya Mapitio ya Sera ya Elimu, karibu sana. (Makof)

Yupo pia Profesa Makenya Maboko ambaye ni Mwenyeekiti wa Kamati ya Mapitio ya Mitaala – Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, karibu sana; yupo pia Profesa Maulid Mwatawala ambaye ni Makamu Mwenyeekiti wa Bodi, Taasisi ya Elimu Tanzania – Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, karibu sana. (Makof)

Yupo pia Dkt. Jennifa Sessabo ambaye ni Makamu Mwenyeekiti Kamati ya Mapitio ya Mitaala – Chuo Kikuu cha Kilimo, Sokoine, karibu sana; yupo pia Profesa Khamisi Dihenga ambaye ni Mwenyeekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na pia ni Katibu Mkuu Mstaafu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, karibu sana; yupo pia Dkt. Lyabene Mtahabwa ambaye ni Kamishna wa Elimu, karibu sana. (Makof)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, leo humu ndani kuna wageni wengi sana wa Profesa Mkenda, nikawa najishawishi hapa kama wote niwataje ama wengine niwataje kwa makundi. Yupo mke wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Dkt. Beatrice Kalinda. Karibu sana. (*Makofi*)

Haya ahsante sana. Nadhani watu wamefurahi sana humu ndani leo. Wapo pia Wakuu wa Taasisi wa Mamlaka za Elimu wakiongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ardh Profesa Evaristo Liwa na Mtendaji Mkuu, *UNESCO*, Profesa Hamisi Malebo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo pia wadau wa maendeleo katika elimu kutoka nje ya nchi wakiongozwa na Dkt. Daniel Baleta, karibuni sana. Wapo pia wadau wa Maendeleo katika elimu ya ndani ya nchi wakiongozwa na Ndugu Faraja Nyarandu, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia Wakurugenzi Watendaji wa Wizara wakiongozwa na Ndugu Moshi Kabengwe ambaye ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wadau wa elimu wakiongozwa na Profesa Peniina Mlama, karibuni sana; wapo wabunifu wakiongozwa na Ndugu Masudi Kipanya na Ndugu Salum Hamadi kutoka Zanzibar, karibuni sana. (*Makofi*)

Masudi Kipanya na mbunifu mwenzako hapo juu, kwa namna ya kipekee hayo makofi yanaashiria yale magari Wabunge wanayasubiri Majimboni kwao. (*Makofi*)

Tunao pia wadau wa elimu kutoka Benki ya NMB wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu Ndugu Ruth Zaipuna, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 43 wa Mheshimiwa Profesa Mkenda ambaa ni Viongozi wa CCM na Waheshimiwa Madiwani kutoka Wilaya ya Rombo, Mkoani Kilimanjaro wakiongozwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na Mwenyekiti wa CCM Wilaya, Ndugu Anthony Tesha; karibuni sana. (*Makofi*)

Sasa bahati mbaya yule mtoto pale sijapewa utambulisho wake, lakini naamini yeye siyo Diwani. Anaweza kuwa labda Kiongozi wa vijana ama chipukizi; anaweza kuwa Mwenyekiti wa chipukizi huyu.

Wageni wanne wa Mheshimiwa Mkenda tena ambaao ni Ndugu Silvest Massawe, Mwenyekiti wa Chama, Kata ya Tarakea Motamburu na Ndugu Alvin Mhindii ambaye ni msanii aliyetunga wimbo wa Mama Samia. Sijui ndio yupi huyu! Hebu ngoja kwanza. Huyu Alvin Mhindii aliyetunga wimbo wa Mama Samia ndio yupi?

Ahaa kumbe ndio yule ambaye jina lake nilikuwa sijalijua hapa! Haya mtoto mzuri, tunakushukuru sana kwa wimbo mzuri wa kumponeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsante sana. (*Makofi*)

Wako pia Ndugu James Silayo na Ndugu Herry Boniface au MADONA, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia makundi mbalimbali ya wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni wageni watatu wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambaao ni wadau wa elimu, yaani HAKI ELIMU kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Mhandisi Samwel Hhayuma ambaao ni watoto wake kutoka Hanang Mkoani Manyara, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Florent Kyombo ambaao ni Viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kutoka Mkoani Kagera. Sijajua wamekaa upande gani, lakini yupo Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Kagera, Ndugu Eumachius Kalinjuna na Ndugu Jonathan Lutanjuka ambaye ni Makamu Mwenyekiti *Red Cross* Kagera, karibuni sana. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava ambao ni wadogo zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 20 wa Mheshimiwa Mariam Kisangi ambao ni wajasiriamali kutoka Sinza Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Meshack Mafyeko. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Nicholaus Ngassa ambao ni Viongozi wa Dini kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dorothy Kilave ambao ni wapiga kura wake kutoka Temeke Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Isaya Njendaluzi. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Mkenda tena, eh, humu ndani leo! Haya, wageni watatu wa Mheshimiwa Mkenda ambao pia wanatoka Rombo. Wageni watatu wa Mheshimiwa Mkenda. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mwantumu Zodo ambaye ni rafiki yake kutoka Mkoani Tanga. Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Rose Tweve ambao ni rafiki zake na Wahadhiri kutoka Chuo cha Uhasibu (*IAA*) cha Jijini Arusha. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Bahati Kenneth Ndingo kutoka Mbeya. Haya, karibuni sana. Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Emmanuel Oleshangai ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Ngorongoro Mkoani Arusha, karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni pia waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na leo tunaye mgeni mmoja ambaye ni Ndugu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mariilyan Domasa Lugutu kutoka Jijini Dar es Salam, karibu sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mengine mawili. Kwanza mnatangaziwa na Katibu wa Bunge kwamba Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Ofisi ya Bunge, wataalam wa afya kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na *Ocean Road* wapo kwenye Kituo chetu cha Afya cha Bunge kwa ajili ya Kliniki Maalum ya Uchunguzi wa Magonjwa ya Wanawake, Magonjwa ya Wanaume na Njia ya Mkojo, Afya ya Moyo, Kansa, Mifupa na Magonjwa ya Ajali, Masikio, Pua na Koo pamoja na Huduma za Ushauri wa Afya. Huduma hii itatolewa kuanzia leo tarehe 10 mpaka siku ya tarehe 21 Mei, 2022. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge wote na Watumishi wa Bunge, mnaombwa kutumia huduma hiyo ambayo ipo karibu kabisa hapo ili tuweze kuzijua afya zetu.

Kwa hiyo, hapa yametajwa magonjwa mengi kabisa kwa hiyo, nenda pale ukatazamwe.

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine linatoka pia kwa Katibu wa Bunge. Wapo Wabunge ambao bado hawajachukua mchele wao na *juice* zao, wakachukue kuanzia saa saba eneo la *Basement*. Sasa hapa naulizwa kama kuna *juice*? Sifahamu, kwa sababu mimi mwenyewe sijaenda bado. Kwa hiyo, nitakapoenda nitajua.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

MHE. DKT. THEA N. NTARA: Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Aliyesema Mwongozo wa Spika ni nani?

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Thea Ntara.

SPIKA: Mheshimiwa Thea Ntara.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimesimama kwa Kanuni ya 75. Kuna jambo lilitokea jana tarehe 9 Mei, Mheshimiwa Condester alitoa taarifa kwa Katibu wa Bunge kwamba anataka kuchangia na mchango wake utafanya ulinganisho wa pombe za kisasa na pombe zinazozalishwa nje ya nchi na pombe za kwetu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuingiza taratibu zote za usalama zilizingatiwa na pombe zilikabidhiwa kwa Wasaidizi wa Katibu wa Bunge ambapo walizihifadhi; na jana tarehe 9 Mei, 2022 chupa za pombe husika zililetwa wakati wa mchango wa Mheshimiwa Condester ambapo alikabidhiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wake, zilirejeshwa kwa wasaidizi wa Katibu wa Bunge na zimehifadhiwa.

Ibara ya 100 Uhuru wa Majadiliano: Mheshimiwa Condester alikuwa ndani ya wigo wa Ibara ya 11; hakutukana, hakuvunja sheria, hakudhalilisha mtu, maelezo yake kuhusu pombe yaliungwa mkono na Mheshimiwa Profesa Kitila, lakini Mheshimiwa Simbachawene akatoa maelezo mazuri tu. Hakukosea na hakukuwa na uhalali wa Mheshimiwa Tabasam au mtu mwingine ye yeyote kumdhihaki na kumshambulia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kauli ya Mheshimiwa Tabasam kwanza inaingilia uhuru wa majadiliano na utaratibu wa shughuli za Bunge kwa kumshambulia Mbunge binafsi na kudhalilisha Mamlaka ya Kiti hususan kiongozi aliye kuwa anaongoza kikao husika kwamba aliruhusu masuala yasiyo na maana kujadiliwa Bungeni. Amekiuka Kanuni za Bunge kwa kuwa Kanuni zinazelekeza, kama Mbunge hajaridhika na jambo, anasimama mahala pake na kuomba 'Kuhusu Utaratibu,' 'Mwongozo wa Spika', au 'Taarifa'; na akaliongea humu humu ndani ya Bunge. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Tabasam hakutumia maneno ya Kibunge isipokuwa kama ametoa kauli za kulishambulia na kulidhalilisha Bunge kuhusiana na shughuli zillizokuwa zinaendelea. Kwa mfano, Mbunge wa ajabu; kuwa wa ajabu kwa sababu ni msichana au kwa sababu ni mwanamke? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kauli hizo kisaikolojia Mbunge huyu atakuwa ameathirika sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nirejee tena, Wabunge waliosimama na Wabunge wanaozungumza. Amesimama Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara kwanza kasema anatumia Kanuni ya 75 ambayo inahusu utaratibu, lakini ye ye amesema anaomba Mwongozo na alipomaliza maelezo yake tena, akasema anaomba Mwongozo. Ila Kanuni hii aliyosimama nayo inahusu utaratibu kwa maana ya kwamba kuna kanuni ambayo itakuwa imevunjwa.

Sasa kwa maelezo aliyyoatoa hapa, yanaashiria kwamba kanuni zillivunjwa lakini siyo hapa ndani kwa maelezo aliyyotoa. Ni kwamba Mbunge alitoka hapa ndani, baada ya mchango wa Mheshimiwa Condester Sichalwe, akaenda kuzungumza maneno yaliyoashiria kwamba jambo ambalo limefanyika hapa ndani ni kinyume na utaratibu.

Sasa ametoa maelezo kwa kirefu na kwa sababu sote tumemsikia, sitayarejea hayo maneno. Ila kwa sababu ni jambo ambalo ye ye amesimama ‘Kuhusu Utaratibu’ na pia ameeleza kuhusu uhuru wa majadiliano humu ndani na namna Mbunge huyu aliposimama na alipochangia katika Hotuba iliyokuwepo Mezani ama hoja iliyokuwepo Mezani; maneno mahsus i ambayo ameyatumia Mheshimiwa Tabasam nje ya hapa kuashiria kwamba Mbunge huyu aliyechangia jana pengine amekosea hapa na pale, kwa kadri ya maelezo aliyyoatoa Mheshimiwa Thea Ntara, hayo maneno siyo mazuri. Hayo maneno siyo mazuri, yanamfanya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mbunge awe hana uhakika anaweza kuzungumzia nini kuhusu watu wake? (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge Katiba inavyolinda uhuru wa mawazo humu ndani ni kwamba inaangalia ukubwa wa nchi yetu na tofauti za jimbo moja na lingine na shughuli za wananchi wanazozifanya katika maeneo husika. Mimi niliwahi kusema, na nini rejee tena, ni kazi yangu kuwalinda Wabunge humu na ndani na nje pia, kwa hivyo asitokee Mbunge wa kumdhalilisha Mbunge mwininge humu ndani wala nje. Humu ndani hakuna Mbunge wa ajabu Wabunge wote wana kiapo kimoja na wote wana heshima sawasawa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge sisi wenyewe tunaitana Waheshimiwa na hata mimi kiongozi wenu mliyenipa fursa ya kuwa mbele yenu nawaita ninyi Waheshimiwa, mmeheshimiwa na wananchi wa nchi hii, hakuna Mbunge wa ajabu humu Bungeni, Wabunge wote mna hadhi sawa mtaheshimiwa sawasawa na michango yenu pia itaheshimiwa na kupewa uzito ule ule unaostahili. Humu ndani,, na kwa sababu wamezungumza hoja moja kwamba wamedhalilishwa kwa sababu pengine ni binti au mwanamke michango ya namna hiyo imeshawahi kutokea huko nyuma. Mheshimiwa Msukuma ameshachangia mara kadhaa kuhusu bangi humu ndani hakuna Mbunge aliyahi kumwita yeye ni Mbunge wa ajabu, Mheshimiwa Kishimba ameshawahi kuchangia kuhusu gongo humu ndani na hakuna Mbunge amewahi kumwita Mbunge wa ajabu.

Kwa hivyo mchango wa Mheshimiwa Condester Sichalwe ulivyochangiwa humu Bungeni na hoja iliyokuwepo mezani ilikuwa ni hoja ya uwekezaji viwanda na biashara. (*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge unapotaja biashara humu ndani Waheshimiwa Wabunge tunalipwa mishahara ambazo baadhi ya kodi zake zinatokana na mauzo hayo. Kwa hiyo viwanda vyetu vya pombe tunaviheshimu na uwa tunaenda kule kukagua sisi kama Bunge, kwa hiyo hakuna biashara ambayo itasemwa humu ndani kwa namna ambayo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mbunge ataonekana ni wa ajabu, hakuna Mbunge wa ajabu wala hakuna mawazo ya ajabu. (*Makofi*)

Sasa nimalize kwa kusema hivi, kwanza Waheshimiwa Wabunge siku zote kanuni hizi zinataka tutunziane heshima humu ndani na nje pia.

Kwa hiyo, Wabunge wote tuheshimiane. Kama ukubaliani na Mbunge fulani wazo lake sema ukiwa humu ndani ndio maana kanuni zinakuruhusu kutoa taarifa au kusimama kuhusu utaratibu kama unahisi kuna kanuni inavunjwa au kuna sheria inavunjwa. Usitoke humu ndani kwenda kuutweza mchango wa Mbunge mwengine, hairuhusiwi.

Sasa kikanuni nilikuwa na namna mbili; moja ni kumpeleka Mbunge husika, kwa sababu jambo alilolisema limetokea humu ndani, kwenye kamati yetu ya maadili, lakini pia ninayo nafasi ya kutoa onyo; sasa nitoe onyo Waheshimiwa Wabunge, tuheshimiane. (*Makofi*)

Kwa hiyo Mheshimiwa Condester Sichalwe kwa sababu jambo hili lilitokea limeleta mtikisiko wa mawazo mimi kwa niaba ya huyo Mbunge ambaye alifikiri wewe ni wa ajabu nikuombe radhi kwamba wewe sio Mbunge wa ajabu, ni Mbunge wa kawaida kabisa na heshima zote kama ambavyo wananchi wako wamekuheshimu wamekuleta humu ndani hizo biashara ulizozisema ndizo zinazofanywa na wanawake huko ulikotoka, kwa hiyo ni halali yako kuwatetea humu ndani. (*Makofi*)

Kwa hiyo uwe na amani kabisa michango yako mingine huko baadaye usijisie vibaya kitu kinakulinda huko salama kabisa na wewe ni Mheshimiwa Mbunge kama Wabunge wengine. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Katibu!

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:

KAULI ZA MAWAZIRI

SPIKA: Kauli za mawaziri Waheshimiwa Wabunge nimwite Waziri wa Nishati Mheshimiwa January Yusuf Makamba.

KAULI YA WAZIRI WA NISHATI KUHUSU ONGEZJKO LA BEI ZA MAFUTA NCHINI

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe tano mwezi Mei mwaka huu katika kikao cha 16 cha Mkutano wa Saba wa Bunge letu hili la 12 Waheshimiwa Wabunge walijadili kuhusu ongezeko la bei za mafuta nchini na kutoa ushauri maoni na mapendekezo mbalimbali. Baada ya mjadala huo Mheshimiwa Spika ilitoa maelekezo kwa mujibu wa kanuni ya 56 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kwamba Waziri atoe kauli rasmi Bungeni kuhusu hatua za kupunguza athari za kupanda kwa bei ya mafuta nchini.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuendelea napenda kuwalishwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alituita wasaidizi wake tukiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, akatuweka kitako usiku mkubwa akazungumza na sisi, akasema mengi akaongea kwa uchungu mkubwa, akaonyesha masononeko. Kwa kweli Mheshimiwa Rais katika mazungumzo yetu tuliyofanya alielezea kuguswa kwake na kusononeka kwake, na juu ya kupanda kwa gharama za mafuta nchini na gharama za bidhaa mbalimbali. Na akasema kwamba, hata kama bei ya mafuta duniani iko juu hata kama takwimu na namba zinaleta mantiki lakini tutangulize utu na huruma kwanza katika kulishughulikia jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, bila shaka kwa wale waliomtazama jana akizungumza na Taifa kwenye *television* watakuwa wameona utu imani na kujali kwake katika uso na sauti yake. Isingekuwa uungwana wake wa kuheshimu mamlaka na mipaka ya Bunge kauli hii ninayoitoa leo angeitoa jana muda uleule. Lakini akaniambia kwamba

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maadam Bunge lilikuelekeza wewe uwasilishe taarifa basi busara ya kiuongozi inataka Bunge lisikie taarifa hii kutoka kwako. Kwa hiyo Mheshimiwa Spika, nimetumwa hapa kuja kwenu leo kuwaletea habari njema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa habari hizo na sijafikisha ujumbe huo na kueleza hatua ambazo Serikali zinachukuwa katika kushughulikia jambo hili naamini kwamba ili kuongeza uelewa na kujenga muhtadha wa jambo lenyewe basi ni vema nikaeleza kuhusu mwenendo wa bei za mafuta katika soko la dunia pamoja na kutoa mnyambulisho wa garama zinazojumuisha katika kupiga hesabu ya bei ya mafuta kwenye *pump*.

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika, nchi yetu haina visima vya mafuta wala mitambo ya kuchakata mafuta ghafi. Kama zillizo nchi nydingi duniani sisini wapokeajili wa bei. Kwa maana hiyo ni wahanga wa bei za mafuta duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kwa mafuta ya *diesel* mchango wa bei katika soko la dunia kwenye bei ya mwisho ya mlaji ni asilimia 64. Kwa kiwango kikubwa uzalishaji na matumizi ya mafuta utegemea matukio ya kiuchumi na kisiasa hasa kwenye mataifa yanayozalisha mafuta na kwenye mataifa yenye uchumi mkubwa duniani.

Mheshimiwa Spika, mfano wa matukio ya aina hiyo ni kama vile vizuizi vya mauzo ya mafuta viliviyowekwa na nchi za kiarabu mwaka 1973 (*Arab oil embargo*), mapinduzi ya Iran ya mwaka 1979 vita kati ya Iraq na Iran mwaka 1980 vita kati ya Iraq na Kuwait mwaka 1990 pamoja na mdololo wa kiuchumi duniani mwaka 2008/2009 lakini pia na vuguvugu la mabadiliko ya kisiasa katika nchi za kiarabu (*Arab Spring*) mwaka 2010/2013.

Mheshimiwa Spika, matukio haya kama unavyofahamu yaliathiri uzalishaji wa mafuta duniani na kusababisha mahitaji ya mafuta kuwa makubwa kuliko wazalishaji na hivyo kusababisha bei za mafuta kuongezeka. Kwa mfano wakati huo hasa wa vuguvugu la *Arab Spring*

bei ya mafuta duniani ilifikia dola126 kwa pipa kwa mwaka 2012, hivyo kupelekeea bei ya petron kwa mfano hapa nchi kwa mwezi Aprili mwaka 2012 kufikia Shilingi 2,231 kwa lita, ambayo ni sawa na Shilingi elfu 3,121 kwa thamani ya Shilingi za sasa kwa mujibu wa wataalam wa Beniki Kuu. Hii bei iliyofikiwa mwaka 2012 ni sawa na bei ya petroli ya sasa.

Mheshimiwa Spika, vilevile bei ya mafuta duniani ni nyenzo na silaha ya kiuchumi ya nchi zinazozalisha mafuta ambazo zimeunda umoja wao unaitwa *Organization of Petroleum Exporting Countries OPEC*. Nchi hizi kuna nyakati kwa makusudi kabisa upunguza uzalishaji wa mafuta chini ya uwezo walionao wa kuzalisha ili bei za mafuta wanayoyauza zisishuke na kuathiri mapato yao.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2020 kama wote tunavyofahamu palitokea milipuko wa ugonjwa wa corona ambapo nchi nyingi zilisitisha shughuli za kiuchumi na kijamii na zikaenda kwenye kitu kinaitwa *lock down*; hii ilipelekeea kupunguza matumizi ya mafuta. Kutokana na kupungua kwa mahitaji ya mafuta uzalishaji wa mafuta nao ukasimama, shida ya kusimama kwa uzalishaji haikuonekana sana kwa sababu pia shughuli za kiuchumi nazo zilisimama.

Mheshimiwa Spika, katikati ya mwaka jana 2021 dunia ilipopata chanjo na kuanza kufunguka kasi ya uzalishaji wa mafuta haikuendana na kasi ya kufunga kwa uchumi wa dunia, kwa hiyo kukawa na uhaba mkubwa wa mafuta na tukaanza kuona ongezeko la mafuta hata hapa nyumbani. Wakati huohuo wa corona nchi za Urusi na Saudi Arabia ambao ni wazalishaji namba mbili na namba tatu wa mafuta duniani baada ya ugomvi wao kuhusu kiwango cha uzalishaji zilifikia makubaliano ya kupunguza uzalishaji wa mafuta kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na makubaliono hayo ambayo pia yaliziusisha nchi za *OPEC*, na baadaye ya kutokana na dunia kufunga baada ya janga la corona kuanza kufifia bei za mafuta hata hapa nyumbani zilipanda kwa kasi kubwa. Kwa mfano kwa lita ya *petrol/ilipanda* kutoka

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

shilingi 1520 mwezi Juni 2022 hadi kufikia shilingi 2511 kwa mwezi Septemba 2021, ambalo ni ongezeko la zaidi ya Shilingi elfu moja katika kipindi kifupi.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza makali ya ongezeko la bei za mafuta nchi mnamo mwezi Oktoba mwaka 2021 Serikali ilichukwa hatua mbalimbali za kupunguza tozo zifuatizo. Kwanza tuliondoa tozo ya matumizi ya miundombinu ya bandari *wharfage* iliyokuwa inalipwa kwa mamlaka ya Bandari. Pili Serikali iliondoa tozo ya kuchakata nyaraka za forodha (*Customs Processing Fee*) inayolipwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Tatu Serikali ilipunguza tozo ya kupima na kuthibitisha viwango vya mafuta vinavyopokelewa nchini iliyokuwa inalipwa kwa Wakala wa Vipimo Tanzania *WMA*. Nne Serikali ilipunguza tozo ya kupima na kuthibitisha ubora wa mafuta iliyokuwa inalipwa kwa *TBS*. Tano Serikali ilipunguza tozo ya Wakala wa Meli inayolipwa kwa Shirika la Wakala wa Meli yani *TASAC*; na Sita Serikali ilipunguza tozo kwa ajili ya kudhibiti biashara ya mafuta *regulatory levy* iliyokuwa inalipwa kwa *EWURA*.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya tozo hizo Serikali pia iliondoa tozo ya huduma *service levy* kwa wafanyabiashara wa jumla walikuwa wanalipa kwa halmashauri au Manispaa za Dar es salaam, Tanga na Mtwara hizi Manispaa zenye Bandari za kupokelea mafuta na maghala ya kuhifadhi mafuta. Vilevile Serikali ilipunguza gharama za kuweka vina saba kwenye mafuta.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hatua hizi zilizochukuliwa mwezi Oktoba 2021 tozo zilipunguzwa kwa jumla ya Shilingi 29 na senti 38 kwa lita ya petrol Shilingi 30 na senti 5 kwa lita ya diesel na Shilingi 26 na senti 99 kwa lita ya mafuta ya taa. Hatua hii ya kupunguza tozo hii maana yake ni kwamba Serikali haitakusanya takribani Shilingi bilioni 102 kwa mwaka na hivyo kutoa unafuu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, wakati tukiwa katika mategemeo ya manufaa ya hatua hizi zilizochukuliwa na Serikali mwezi Oktoba 2021 miezi miwili baadaye, yaani Disemba palianza

kutokea tetesi na hofu ya vita kati ya Urusi na Ukrain. Hofu hii ya vita ilifanya wafanyabiashara wa mafuta duniani kuamini kwamba kungetokea uhaba wa mafuta kwa kuwa Urusi ni nchi ya pili kwa uzalishaji wa mafuta duniani. Matokeo yake mahitaji ya mafuta katika soko la dunia yaliongezeka kuzidi uzalishaji vita ilipoanza tarehe 24 Februari 2022 bei za mafuta ghafi ziliongezeka kiasi cha kufikia kiwango cha Dola cha kimarekani 100 kwa pipa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na vita hii nchi za Ulaya ziliweka vikwazo vyta kiuchumi na vizuizi vyta manunuzi ya nishati kutoka Urusi. Kwa vikwazo hivyo nchi za Ulaya zilianza kununua mafuta kutoka nchi za Uarabuni, mafuta ambayo sisi katika zetu za Afrika ikiwemo Tanzania ndiyo ambayo tumekuwa tukiyategemea. Hali hiyo ikapelekeea changamoto ya mafuta yaliyoko sokoni kutotosheleza mahitaji. Hali hii pia ilisababisha bei za mafuta kuendelea kuongezeka kwa kazi kiasi cha tarehe 7 mwezi Machi mwaka huu bei ya mafuta ghafi kutoka Uarabuni ilifikia Dola za kimarekani 139 kwa pipa. Bei hii haikuwahi kufikiwa katika kipindi cha miaka 14 iliyopita

Mheshimiwa Spika, ifahamike kwamba kwa mfumo wa uagizaji uzalishaji na uchakataji wa mafuta ghafi bei ya mafuta yanayoingizwa hapa nchini uhakisi bei ya mafuta ghafi katika soko la dunia kwa miezi miwili iliyopita. Kwa hiyo bei kubwa ya mafuta tunayoionna katika mwezi huu wa Mei hapa nchi kwa sehemu kubwa ni kutokana na bei kubwa ya mafuta duniani mnamo mwa mwezi wa Machi mwaka huu, bei ambayo kama nilivyosema awali haikupata kuonekana katika kipindi cha miaka 14 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, ukiacha ongezeko la bei ya mafuta katika soko la dunia, gharama za kukodi meli za kusafirishia mafuta nazo zimeongezeka. Hii ni kutokana na kwamba bei ya mafuta yanayotumika kwenye meli zimeongezeka na gharama za bima zimeongezeka kutokana na hatari ya athari ya vita (*war risk premium*). Pia kumekuwepo na uhaba wa meli kutokana na vikwazo vilivyowekwa na nchi za Ulaya kwa Urusi lakini pia meli zilizokuwa zinategemewa kutuletea mafuta katika nchi zetu

za Afrika sasa zinafanya masafa mafuta zaidi kupeleka mafuta kwenye nchi za Ulaya.

Mheshimiwa Spika, vilevile hiyo sasa imepelekea kupunguza upatikanaji wake meli katika soko la kwetu, vilevile meli nyingi za Urusi zimeondoka kwenye biashara ya kusafirisha mafuta hatu yale mafuta yasiyokuwa ya Urusi kutokana na vikwazo. Matukio ya namna hii kwa kuzingatia ongezeko la bei za mafuta katika soko la dunia na ongezeko la gharama za uagizaji wa mafuta, bei ya mafuta hapa nchini ziliongezeka kwa kiwango kikubwa namno mwezi Mei, mwaka huu yaani mwezi huu kufikia shilingi 3,148 kwa lita ya petroli, shilingi 3,258 kwa lita ya dizeli na shilingi 3,112 kwa lita ya mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, bei hizi za mwezi huu inajumuisha gharama zifuatazo: Kwanza, kuna gharama za mafuta ambayo ni mafuta ya bei ya mafuta katika soko la dunia na gharama ya uagizaji wa mafuta ambayo inayojumuisha gharama za usafirishaji, bima na faida ya mletaji wa mafuta (*supplier*). Katika bei za Mei 2022 yaani za sasa, gharama hizi ziliikuwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Petroli; bei ya soko la dunia ilikuwa ni shilingi 1,821 kwa lita na gharama ya uagizaji ilikuwa shilingi 89 kwa lita, hivyo, gharama ya mafuta hayo hadi yanafika katika bandari ya Dar es Salaam kwa bei ya mwezi huu ilikuwa ni shilingi 1,910 kwa lita.

(ii) Dizeli; bei ya soko la dunia ilikuwa ni Shilingi 2,088 kwa lita na gharama ya uagizaji ilikuwa shilingi 54 kwa lita, na hivyo gharama ya mafuta ya dizeli hadi yanafika katika bandari ya Dar es Salaam ilikuwa ni shilingi 2,142 kwa lita.

(iii) Mafuta ya taa; bei ya soko la dunia ilikuwa ni shilingi 1,917 kwa lita na gharama ya uagizaji ziliikuwa shilingi 135 kwa lita, na hivyo gharama ya mafuta hayo hadi yanafika katika bandari ya Dar es Salaam ilikuwa ni shilingi 2,052 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, bei inayotumika kushinda zabuni za kuleta hapa mafuta nchini (*premium*), ambayo imezungumzwa sana, kwa kawaida inachangia asilimia Mbili mpaka asilimia Saba ya bei ya mafuta kwenye vituo vya mafuta nchini huku sehemu kubwa ya gharama ya bei ya mafuta ikiwa ni bei halisi ya mafuta yenyewe kwenye soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, pili, kuna tozo za Taasisi za Serikali ambazo zinazungumzwa sana ambazo ni takribani shilingi 38 tu kwa lita na hizo zinajumuisha zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, gharama ya matumizi ya bandari zinayolipwa kwa mamlaka ya Bandari Tanzania ya shilingi 15 kwa lita; Tozo ya huduma (*service levy*) inayolipwa kwenye Halmashauri shilingi 8 kwa lita; Tozo ya Udhibiti inayolipwa *EWURA* ni katiki ya shilingi 3.20 na shilingi 5.50 kwa lita; Tozo katika biashara ya jumla na rejareja kwa ukaguzi wa miundombinu inayolipwa kwa Wakala wa Vipimo (*WMA*), Baraza la Mazingira (*NEMC*), Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (*OSHA*) na Kikosi cha Zimamoto (*FRF*) ambapo jumla yake ni shilingi 6.47 kwa lita kwa taasisi zote hizi; pia ipo tozo ya huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), Wakala wa Vipimo (*WMA*), Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (*TASAC*) wakati ya kupokea mafuta ikiwa ni shilingi 2.81 kwa lita ya petroli, shilingi 1.02 kwa lita ya dizeli na shilingi 4.67 ya lita ya mafuta ya taa, hizi zote jumla yake ni shilingi 38. Taasisi ni nyngi lakini kiwango ni hicho.

Mheshimiwa Spika, tatu, tunazo kodi za Serikali katika mafuta ambazo kwenye petroli ni shilingi 920.65 kwa lita ya petroli, shilingi 800.13 kwa lita ya dizeli na shilingi 745.77 kwa lita ya mafuta ya taa na hizi inajumuisha yafuatayo:

Kwanza, shilingi 186 kwa *TANROADS* Mfuko wa Barabara; shilingi 177 kwa *TARURA*; na shilingi 50 kwa maji vijijini. Pia tunayo ada ya mafuta ya shilingi 100 kwa lita ya petroli na dizeli na shilingi 250 kwa mafuta ya taa kwa ajili ya miradi ya kusambaza umeme vijijini – *REA*.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, pia tuna ushuru wa forodha wa shilingi 379 kwa lita ya petroli, Shilingi 255 kwa lita ya dizeli na shilingi 465 kwa lita ya mafuta ya taa. Pia tunayo Tozo ya maendeleo ya reli ya ambayo ni asilimia 1.5 ya gharama ya mafuta yaliyofikishwa Tanzania. Gharama hii hubadilika kila mwezi kulingana na gharama ya mafuta yanapofikishwa Tanzania. Kwa mwezi huu wa Mei 2022, tozo hii ya maendeleo ya reli ilikuwa ni shilingi 28.65 kwa lita ya petroli, shilingi 32.13 kwa lita ya dizeli na shilingi 30.77 kwa mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, Nne, ni gharama za uendeshaji wa biashara ya jumla na faida ya wafanyabiashara naomba nirudie gharama ya nne inayoingia kwenye mafuta ni za uendeshaji wa gharama za uwendeshaji wa biashara ya jumla na faida ya wafanyabiashara hao ambayo kwa ujumla ni Shilingi 161.18 kwa lita ya petroli, shilingi 160.67 na shilingi 159.36 kwa lita ya mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni gharama za uendeshaji wa biashara ya rejareja, yaani vituo yaani vituo vya mafuta na faida ya wafanyabiashara hao ambayo kwa ujumla ni shilingi 118 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, kwa bei za Mei, 2022 tukichukulia dizeli kama mfano, mchango wa gharama kwenye bei ya mwisho kwa mlaji ni kama ifuatavyo:

Bei katika soko la dunia ilichangia asilimia 63 bei ya sasa ya dizeli, gharama ya uagizaji (*premium*) ni asilimia Mbili, tozo za taasisi ni asilimia Moja, miradi ya barabara na maji ni asilimia 13 kama nilivyoitaja; ushuru wa forodha ni asilimia nane; miradi ya *REA* ni asilimia tatu; kodi ya maendeleo ya reli ni asilimia moja; gharama za uendeshaji kwa wafanyabiashara wa jumla ni asilimia tano na gharama za uendeshaji kwa wafanyabiashara rejareja ni asilimia nne.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuwa bei ya mafuta ghafi imeendelea kuwa juu, bei ya dizeli inaongezeka kwa kasi zaidi kutokana na uhaba wa mafuta hayo kwa kuwa baadhi ya viwanda vya kusafisha mafuta ghafi (*refineries*)

ya dizeli vilivyopo Afrika, ikiwemo Ghana na Afrika Kusini, kufungwa au kutegemewa kufungwa kutokana na viwango vya sulphur katika mafuta ya dizeli kupunguzwa kutoka PPM 50 kwenda 10 wakati viwanda hivyo havina uwezo wa kuzalisha dizeli ya viwango vipyta. Kwa maana hiyo, nchi kubwa yenye uchumi mkubwa kama Afrika ya Kusini inayotumia mafuta mengi sasa tunagombea soko la dizeli na nchi nyingi zaidi kuliko huko nyuma, kwa maana hiyo bei za dizeli zinategemea kuongezeka katika miezi inayokuja.

Mheshimiwa Spika, katika mjadala wa bei za mafuta kumekuwepo na kulinganisha bei za nchi yetu na bei za nchi mbalimbali hasa majirani zetu. Kulinganisha bei lazima kuendane na kulinganisha kila kitu kinachoingia katika bei, kwa kiingereza wanasema "*all things being equal*", ikiwemo viwango vya kodi na tozo mbalimbali, gharama za kuendesha blashtara za mafuta, kama bei zillizowekwa mitandaoni zimejumuisha ruzuku au la, kama tarehe ya kutangazwa bei hizo ilikuwa moja, kama ulinganisho huo umetoka kwenye vyanzo rasmi na vya kuaminika, pamoja mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, sisi kama nchi tumeweka kodi ya shilingi zaidi 900 kwenye kila lita ya petroli ili tujenge barabara vijijiini, tupeleke umeme vijijiini, tupeleke maji vijijiini, tujenge reli, tukarabati barabara zetu za Kitaifa, na tusomeshe watoto wetu bila kulipia karo.

Mheshimiwa Spika, kupanga ni kuchagua pamoja na kwamba bado, kila kitu kikipimwa sawa, *all things being equal*, bado bei zetu ni nzuri kuliko nchi nyingi lakini tukilinganisha bei tuzingatia kwamba tuliamua kufanya kodi katika mafuta kama chanzo kikubwa cha mapato ya kusukuma maendeleo ya nchi yetu hasa ya vijijiini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, mwezi Oktoba 2021, Serikali ilipunguza tozo za Taasisi za Serikali na sasa hivi tozo hizo zimebaki kuwa ni shilingi 38 tu kwa lita. Punguzo zaidi la tozo hizi haliwezi kuleta ahueni inayostahili

ya bei ya mafuta kama inavyotegemewa kutokana na kuendelea kupanda kwa kasi kwa bei ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, sisi kama Serikali tutaendelea kulitazama jambo hili, kuendelea kufanya utafiti kuhusu ulazima wa tozo hizi kuona kama taasisi hizi zinaweza kupata fedha katika vyanzo vingine kuliko katika mafuta na hilo tatalizungumza katika bajeti zetu zinazokuja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivyo kwa kuzingatia hilo kwamba bei ya mafuta inaenda kwa kasi, tozo za taasisi ni ndogo, pesa nyingi tumezipanga kwenye vitu tunavyovitaka vya maendeleo kutokana na hivyo, Serikali ilianza taratibu za kuchukua mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia na kutoka Shirika la Fedha Duniani (*IMF*) kwa ajili ya kuweka ahueni kwenye bei za mafuta na bidhaa nyinginezo zinazogusa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuchukua mkopo huo upo mbioni kukamilika na ahueni kwenye kupanda kwa bei ya mafuta na bei ya bidhaa mbalimbali itapatikana kutokana na mkopo huu katika mwaka ujao wa fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na mahitaji ya wananchi, kutokana na maoni, ushauri na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge, kutokana na maelekezo ya Chama chetu cha Mapinduzi, kutokana na ujasiri wa Rais wetu Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kwamba, mwaka ujao wa fedha ni mbali kusubiri ahueni hiyo na akaelekeza kwamba ahueni itafutwe haraka zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Mheshimiwa Rais ameelekeza katika kipindi hiki kabla hatujafikia mwaka mpya wa fedha, Serikali ijibane, ijinyime na zitolewe Shilingi Bilioni 100 kwa ajili ya kupunguza bei za mafuta hapa nchini. Kwa hiyo, Serikali imeamua kutoa Shilingi Bilioni 100 sasa kwa ajili ya kutoa ahueni kwa ajili ya mafuta. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ruzuku hii inatolewa kwa kupunguza matumizi ya Serikali katika kipindi kilichobaki cha mwaka huu wa fedha. Kutolewa kwa ruzuku hii hakutagusa miradi ya maendeleo ambayo inaendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hii nafuu ya Shilingi Bilioni 100 ni nafuu ya kipindi cha mpito kuelekea kwenye mwaka mpya wa fedha, ambapo nafuu nyingine inayotokana na mikopo niliyoieleza awali, itakuja katika mwaka ujao wa fedha na itaelezwa kwa kina zaidi na Waziri wa Fedha kwenye Bajeti ya Serikali mwezi ujao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ruzuku hii ya Shilingi Bilioni 100 itatolewa kwa ajili ya kupunguza bei za mafuta kuanzia tarehe Mosi Juni 2022 kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais jana. Hii ni kutokana na kuwa, wafanyabiashara kwa jmfumo wa biashara ya mafuta, wafanyabiashara wa jumla wamekwishalipia gharama ya mafuta ambayo imejumuishwa kwenye bei na wafanyabiashara wa mafuta katika vituo wamekwisha kununua mafuta kwa bei inayotumika sasa.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zisizo za kifedha zinazochukuliwa na Serikali ni pamoja na hizi zifuatazo:-

Kwanza; tumezingatia maoni na ushauri na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge ya kuruhusu watu wenye uwezo wa kuleta mafuta kwa bei nafuu kufanya hivyo.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri kengele ya pili imeshagonga. Kwa hivyo ili uweze kumalizia haya maelezo yako nakuongeza dakika saba umalizie. (*Makof*)

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha taratibu kwa ajili ya jambo hilo na mipango hii ikileta matokeo yanayotarajiwa bei za mafuta zinaweza kuanza kupungua zadi kuanzia mwezi Agosti, 2022.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, pili; Serikali tayari imekamilisha utaratibu wa kuanzisha Mfuko wa kuhimili bei za mafuta yaani *Fuel Price Stabilization Fund*.

Mheshimiwa Spika, tatu; tumekamilisha utaratibu wa kuanzisha hifadhi ya mafuta ya kimkakati (*National Strategic Petroleum Reserve*) na marekebisho ya Kanuni kwa ajili hiyo yamekwisha fanyika, jambo hili litatuwezesha kupata unafuu wa bei za mafuta siku zijazo katika vipindi kama hivi.

Mheshimiwa Spika, nne; tumekamilisha utaratibu wakuwa na kituo cha mafuta (*Petroleum Hub*) na ndani ya mwezi huu Serikali itakamilisha makubaliano ya kujenga maghala makubwa ya kuhifadhi mafuta kwa ajili ya kuuzwa nje ya nchi kulingana na uhitaji.

Mheshimiwa Spika, tano; tayari tumeshaanzisha upokeaji wa mafuta katika ghala moja (*Single Receiving Terminal*) kuititia maghala ya *TIPER* ili kupunguza na kuondoa gharama za meli kusubiri na kuchukua muda hivyo kuongeza bei za mafuta.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inaendana na kuyafanya maghala haya kuwa *Customs Bonded Warehouses* ili kushamirisha biashara ya mafuta yanayokuja nchini na yanayoenda kwenye nchi nyininge.

Mheshimiwa Spika, sita; tunaiongezea uwezo *TPDC* ili iweze kufanyabiashara ya mafuta ambapo mara ya mwisho ilifanya shughuli hiyo miaka 20 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, saba; mwsiho tunaimarisha utendaji na weledi wa taasisi za Serikali zinazoshughulika na biashara ya mafuta ikiwemo *EWURA* na Wakala wa Uagizaji wa Pamoja wa Mafuta.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zitafafanuliwa kwa kirefu na Waheshimiwa Wabunge watapata fursa ya kutoa maoni na ushauri wao wakati wa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nishati wiki tatu zijazo.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako litakuwa limebaini changamoto ya foleni na vurugu katika vituo vya mafuta katika nchi nyingine kutokana na uhaba wa mafuta. Pamoja na changamoto ya bei, jambo ambalo siyo letu peke yetu, usimamizi wa sekta ya mafuta hapa nchini, hasa katika kipindi hiki kigumu, umekuwa wa utulivu na wa umakini. Hii siyo kwasababu ya ajali, bali ni kwa jitihada za makusudi za Serikali kwa ushirikiano wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, bei za mafuta kupanda ni janga lakini hatari kubwa zaidi hata kwa usalama wa nchi ni pale mafuta yanapokosekana. Sisi kama nchi hatujafikia huko kwa sababu ya jitihada za Serikali. Leo tunapozungumza tunayo pamoja na sheria yetu kututaka tuwe na mafuta ya siku 15 za ziada ndiyo kanuni, lakini leo tunapozungumza tunayo dizeli ya kutosheleza, tunayo petroli ya kutosheleza siku 34, tunayo dizeli ya kutosheleza siku 27, mafuta ya taa siku 81 na mafuta ya ndege siku 26.

Mheshimiwa Spika, zipo nchi ambazo zina dizeli ya siku Nne, siku Sita, siku Saba sisi tunayo ya siku 26, hii si ajali ni usimamizi makini wa sekta (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inawapongeza wadau wa mafuta nchini, hasa kuititia vyama vyao vya TAOMAC na TAPSOA, kwa uelewa na ushirikiano wao na uvumilivu katika kipindi hiki. Pia, naipongeza na kuishukuru sana Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kwa ushauri mzuri ambao imekuwa inautoa kwa Wizara katika usimamizi wa sekta.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe binafsi, kwanza mashauriano na uongozi wako kwenye jambo hili la usimamizi wa sekta, pia kwa wewe kutoa fursa kwa Bunge kuchukua nafasi yake katika kuvisimamia na kuishauri Serikali kwenye jambo hili la muhimu.

Mheshimiwa Spika, kipekee nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake na ujasiri wake wa kuchukua hatua ambazo tumezieleza hapo awali. Ni dhahiri kabisa kwamba yeche binafsi, Serikali yake na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

chama anachokiongoza wanawajali wananchi na wanatoa majawabu kwa mahitaji yao. Binafsi namshukuru kwa kunipa miongozo na kunitia moyo na kunihimiza uvumiliu. Namuahidi Mheshimiwa Rais na kuwaahidi Watanzania kwamba tutaendelea kuisimamia sekta hii kwa weledi na uadilifu mkubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kunipa maelekezo mbalimbali na kwa wakati wote kuulizia mwenendo wa bei za mafuta na hatua tunazochukua. Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa usimamizi na maelekezo yake. Namshukuru Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushiriki wake kwenye suala hili. Namshukuru sana ndugu yangu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa ushirikiano wake wa karibu wakati wote kwenye kushughulikia jambo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru sana na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kusimama kidete kuwatetea wananchi wanaowawakilisha na kwa dhamira yao ya dhati kuona kwamba sekta hii inasimamiwa vizuri, inaendeshwa vizuri na nafuu ya bei inapatikana kwa wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni zetu, Kauli ya Waziri haijadiliwi, lakini imejieleza hapo kwa kirefu sana na kama Bunge lilivyokuwa limeshalijadili jambo hili na kuielekeza Serikali cha kufanya, basi Serikali imefanya kwa sehemu yake.

Katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba Bunge tulitaraji taarifa ambayo ingekuja ingekuja inahusu pengine ni yale mambo tu ya muda mfupi, lakini nichukue fursa hii kuipongeza sana sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutueleza Wabunge siku ya leo ndani ya muda huu mfupi na hatua mbalimbali za hapo

baadaye zitakazochukuliwa. Kwa hiyo nampongeza sana sana Mheshimiwa Rais kwa kulisimamia jambo hili, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri mwenye sekta na Mawaziri wote ambao wamehusika kuhakikisha tunafika hapa tulipo. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, nadhani nyinyi wote ni mashahidi, jambo hili Mheshimiwa Rais tunavyomtaja hapa ni kwa sababu sote tunao ushahidi kwamba jana alikuwa na kikao mpaka usiku kuhakikisha leo Bunge linapewa taarifa kama ambavyo tulikuwa tumeiambia Serikali kwamba tunahitaji taarifa hiyo.

Kwa hiyo, ni jambo la kushukuru sana kwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa na ye ye mwenyewe Rais akiwa anaongoza vikao vya kuhakikisha tunafika hapa.

Sasa kwa mujibu wa haya maelezo yaliyotoka Waheshimiwa Wabunge na sisi ni kazi yetu kwa sababu ndio tuliyosikia hapa kwa niaba ya wananchi kufafanua sasa haya tuliyoyasikia hapa kwa wananchi, kwamba ule unafuu ambao Wabunge tuluijadili hapa kwa kirefu utaanza mwezi Juni, siku ya bei mpya zitakavyotangazwa. Fedha hii kiasi cha bilioni 100 ambacho Serikali itaingiza kama ruzuku, basi tutaanza kuona nafuu wakati huo, ili maelezo yakae vizuri kwa wananchi. Kwa hiyo, pamoja na pongezi hizo ni kazi yetu sasa Wabunge kwa sababu Serikali imeshachukua hatua na sisi tuendelee kuchukua hatua. (*Makof*)

Jambo lingine kuhusu hili kwa sababu Bajeti ya Nishati bado haijapita hapa na hotuba yao bado. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuendelee kujielemisha ili itakapokuja hotuba hiyo wakati wake hapa basi tuendelee kuboresha ushauri ule ambao tuliutoa kwa haraka tuanze kutafuta sasa na taarifa za ziada ili wakati wa kushauri hasa katika hizi hatua mbalimbali za muda mrefu tuwe na mambo ya kuipa Serikali ili iende kuyafanya kazi, kwa sababu ninyi ni mashahidi yale tunayoyasema Serikali inayafanya kazi. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo nimalize kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ushirikiano mkubwa anaotupa Bunge, kwa sababu... (*Makof*)

Ahsanteni sana, Waheshimiwa Wabunge nasema hivyo kwa sababu ninyi ni mashahidi nchi zingine huwa ni mpaka zivutane namna hii ndiyo hatua zinachukuliwa. Kwa hiyo, tunapopata ushirikiano katika mambo yale tunayoyaamua hapa ndani lazima tutambue kwamba Serikali iko tayari kushirikiana nasi katika yale mambo tunayoyasema na kuyaamua kwa niaba ya wananchi.

Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, lakini tunawashukuru Mawaziri wote, kila mtu aliyehusika kwa sehemu yake na kipekee kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni wameendelea kuingia hapa naona leo Mheshimiwa Mkenda amejaza Bunge kabisa, kwa hiyo nimpongeze na yeye kwa kujaza Bunge. Kuna wageni wengine wameingia hapa hawa nalazimika kuwatangaza kwa sababu kuna watu huko nje wanajiita Maprofesa, lakini sasa ndiyo hivyo tena. Hawa ni Maprofesa wa kisomo jamani. Profesa Costa Mahalu, hawa ni Maprofesa wa kisomo na maandiko, Profesa Chambi Chachage, karibu sana. (*Makof*)

Tunao Esther Mgogo, Daktari Ikande Kwayu huyu naye ni daktari wa kisomo, maana sasa hivi inabidi tuwe tunatofautisha kidogo. Alexander Kimario, haya Sinyo Swai, Priver Shayo, Tripris Kamando, Nice Taskanje, Temi Isdori ambaye anatoka Bodi ya Michezo Rombo. Haya nadhani ni hao. (*Makof*)

Halafu yupo mgeni wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, naye Profesa Kilita Mkumbo jamani ni Profesa wa kisomo. Inabidi tuwe tunaweka hizi taarifa za ziada, na yeye ana mgeni wake hapa Daktari Richard Shukia kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, huyu naye ni daktari wa kisomo. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu, lakini sasa ataendelea na ratiba Mheshimiwa Naibu Spika.

Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Elimu.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na muda naomba Hotuba yangu yote iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) kama iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilisha ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii...

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge kuna Wizara muhimu, Mheshimiwa Waziri endelea.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilisha ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, iliyochambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Fungu 46 na Fungu 18 la Tume ya Taifa (*UNESCO*), naomba kutoa hoja sasa kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Fungu 46 na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Fungu 18 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kuendelea kutimiza majukumu yangu na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kila kitu hasa kwa amani na mshikamano wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunitfea kuwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na kwa kuendelea kumwamini Mheshimiwa Omari Juma Kipanga kuwa Naibu Waziri. Napenda pia kumshukuru Rais kwa Uongozi na miongozo anayotupatia ambayo imetusaidia sana katika kusimamia Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia Mheshimiwa Daktari Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo wamekuwa wakimsaidia Rais katika kutusimamia na kutuongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Daktari Tulia Ackson Mwansasu, kwa Uongozi wake mahiri wa Bunge lako Tukufu. Nakushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wao.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu. Nakupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa pole kwako wewe na kwa Bunge lote Tukufu kwa kuwapoteza Waheshimiwa Wabunge wafuataao, Hayati Elias John Kwandikwa aliyekuwa Mbunge wa Ushetu na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Hayati William Tate Ole Nasha aliyekuwa Mbunge wa Ngorongoro na Naibu Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji; na Hayati Irene Alex Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa. Natoa pole kwa ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na wapendwa wetu na kwa namna ya pekee natoa pole kwa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe Mbunge kwa kufiwa na mtoto wake. Naungana na familia, ndugu, jamaa na marafiki kumwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru kwa namna ya pekee Mwenyezekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo; Makamu Mwenyezekiti, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba; Mbunge na wajumbe wote wa Kamati kwa kuchambua na kuishauri Wizara kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2022/2023. Kamati hii ni makini sana na imekuwa ikitoa maoni na ushauri wenye lengo la kuhakikisha tunaendelea kuboresha elimu na kuendeleza sayansi na teknolojia kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwapongeza Wabunge waliochaguliwa hivi karibuni kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni Mheshimiwa Emmanuel Leklshon Shangai, Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Jimbo la Ushetu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana mtangulizi wangu, Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako na Katibu Mkuu aliystaafu kwa heshima zote,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Daktari Leornard Akwilapo, kwa kazi nzuri walizofanya katika Wizara. Wameiacha Wizara pazuri na wameturahisishia kazi zetu sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana mke wangu Beatrice, watoto na familia kwa upana wake wote, ikiwa ni pamoja na mama mzazi Sekunda, kwa upendo na ukaribu ambao wamekuwa wakinipa na kunijaza nguvu na ari ya kuchapa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa ya utelekezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Fungu 46 na Fungu 18 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi 1,519,316,801,000.00 kwa ajili ya Fungu 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo shilingi 480,474,878,000.00 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 1,038,841,923,000.00 zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo bajeti ya maendeleo inajumuisha ongezeko la fedha za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVICO 19.

Aidha, kupitia Tume ya UNESCO yaani Fungu 18 Bunge liliidhinisha kiasi cha shilingi 2,679,073,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo yanajumuisha shilingi 1,146,780,000 za Mishahara na shilingi 1,532,293,000.00 za Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara kupitia Fungu 46 ilitarajia kukusanya maduhuli yenye thamani ya shilingi 540,943,008,495.63 ambapo kiasi cha shilingi 8,680,999,000.00

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zilipangwa kukusanya Idara na Vitengo na shilingi 532,262,013,495.63 zilipangwa kukusanya na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2022 Wizara imekusanya shilingi 415,796,161,776.80 sawa na asilimia 77 ya makadirio ambapo shilingi 7,622,836,164.00 zimekusanya na Idara na Vitengo na shilingi 408,172,325,612.80 zimekusanya na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2022, Wizara imepokea Jumla ya shilingi 396,962,728,624.62 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kupitia Fungu 46, ambazo ni sawa na asilimia 83 ya bajeti. Aidha, kupitia Tume ya UNESCO - Fungu 18 Wizara imepokea jumla ya shilingi 1,723,003,183.30 sawa na asilimia 76 ya bajeti yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia Aprili, 2022, Wizara imepokea jumla ya shilingi 994,711,772,676.29 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 96 ya bajeti iliyoitengwa. Kati ya fedha hizo shilingi 684,470,232,276.01 ni fedha za ndani na shilingi 310,241,540,400.29 ni fedha za nje. Aidha, kiasi cha fedha za nje kinajumuisha shilingi 64,297,963,057.82 kwa...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, hebu subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge humu ndani mazungumzo yamekuwa mengi mno na Hotuba hizi za Bajeti ya Wizara zote zinatakiwa Wabunge mzi-own ili muweze kuwaeleza wananchi wenu. Haiwezekani kila mtu anazungumza kwa sauti kubwa, niwaombe tuzingatia maelekezo ya Kiti.

Mheshimiwa Waziri endelea.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa kuzingatia vipaumbele vyake. Taarifa hiyo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

inapatikana katika ukurasa 19 mpaka 69 katika kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo. Ili kufikia azma hiyo, Serikali imeandaa miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma ya Chakula na Lishe kwa Wanafunzi wa Elimumsingi kwa lengo la kuimarisha mahudhurio ya wanafunzi na kuboresha ujifunzaji.

Aidha, inaendelea kukamilisha miongozo mingine ikiwemo Mwongozo wa Viwango na Uendeshaji wa Elimu ya Awali (*National Operational Guidelines and Minimum Standards for Pre-Primary Education*) pamoja na Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo huo, Mwongozo wa Uanzishaji, Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo Shikizi vyta Shule na Mwongozo wa Utoaji wa Elimu ya Kujitegemea katika Shule za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha utoaji wa elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi, Serikali imeboresha utekelezaji wa miongozo ifuatayo, Mwongozo wa Utekelezaji wa Programu ya Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala, Mwongozo wa Kutoa Huduma kwa Wanafunzi katika Programu ya Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala na Mwongozo wa Wawezeshaji katika Programu ya Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala. Utekelezaji wa miongozo hiyo umewezesha kuwarejesha shulenii wasichana 3,333 ikilinganishwa na lengo la kurudisha wasichana 3,000 walioacha shule kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha Elimu Msingi na inatolewa kwa usawa inatolewa kwa malezi bora na usalama kwa mtoto shulenii, Serikali imetekeliza yafutayo:-

(i) Inaendelea na ukamilishaji wa mwongozo wa Programu ya Shule salama, vilevile inaendelea kutekeleza mkakati wa kuongeza udahili wa wasichana katika shule za sekondari;

(ii) Imechapa na kusambaza miongozi ya kutoa ushauri nasaha na unasihi nakala 44,400 ambayo itasaidia walimu kutoa huduma ya ushauri na unasihi kwa wanafunzi; na imetua mafunzo kuhusu huduma ya malezi, unasihi na ulinzi wa mtoto shulenii kwa walimu 243 wa shule za msingi na sekondari kutoka maeneo ambayo yalikuwa hayajafikiwa na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji katika elimu kwa lengo la kuongeza fursa za utoaji wa elimu bora nchini. Mafanikio ya uwekezaji katika elimu ni kama ifuatavyo:-

(i) Usajili wa shule 741 ikilinganishwa na lengo la shule 550 zilizolengwa kama ifuatavyo; Shule za Awali pekee zisizo za Serikali 33, Shule za Awali na Msingi 511, Sekondari 196 na Chuo cha Ualimu kimoja kisicho cha Serikali; na

(ii) Kuwezesha ujenzi wa shule mpya 175 ambapo ujenzi wa shule 33 umekamilika na ujenzi wa shule 143 za sekondari upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Aidha, imewezesha ujenzi wa madarasa 3,283, mabweni 112, Ofisi 10, matundu ya vyoo 8,096, usimikaji wa vifaa vya kunawia mikono na ununuvi wa matenki ya kuhifadhi maji safi katika shule za msingi 235.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa Elimu Msingi nchini, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imewezesha ununuvi wa magari 187 kwa ajili ya Maafisa Elimu Msingi katika Halmashauri 184 na magari matatu kwa ajili ya Baraza la Mitihani. Aidha, inaendelea na taratibu za ununuvi wa magari 185 kwa ajili ya Maafisa Elimu Sekondari nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu katika ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari kwa lengo la kuimarisha uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja. Serikali imeendelea pia kuimarisha huduma za maktaba nchini kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

lengo la kuhamasisha ari ya Watanzania, kupenda kujisomea na kuelimika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufikia azma hiyo, imefanya ukaguzi na kutoa ushauri wa usimamizi na uendeshaji wa Maktaba 13 zikiwemo Maktaba za Mikoa ya Singida, Mwanza, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Dodoma, Ruvuma, Mbeya, Kagera, Morogoro na Iringa pamoja na Maktaba ya Wilaya ya Mbulu na Maktaba ya Kijiji cha Mbweera iliyopo Wilaya ya Hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa elimu ya msingi na sekondari nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:-

(i) imeandaa mfumo wa kieletroniki wenyе moduli, miongozo na vitabu mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia kwa njia ya mtandao utakaotumika kutoa elimu endelevu kwa walimu kazini na imeboresha maktaba mtandao ya Taasisi ya Elimu Tanzania kwa kuongeza uwezo wa kubeba maudhui katika miundo mbalimbali na kuongeza baadhi ya vitabu ambavyo havikuwepo. Maktaba hiyo inapatikana bure kwa anuani <https://ol.tie.go.tz> ambayo imerahisisha upatikanaji wa vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kusimamia upimaji na tathmini ya wanafunzi wa Elimu Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu hapa nchini. Aidha, Serikali imeendelea kukusanya maoni kuhusu mitaala inayotumika katika ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari, ualimu kutoka kwa wadau wa elimu ambapo hadi sasa jumla ya wadau 103,210 wametoa maoni. Wadau walioshiriki katika kutoa maoni ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii; Taasisi za Kidini, Taasisi Binafsi, Wataalam mbalimbali wa Elimu na wananchi kwa ujumla.

Aidha, maoni hayo yamekusanya Tanzania Bara na Visiwani na yatazingatiwa wakati wa uandaaji wa mitaala mipyä itakayowajengea wanafunzi ujuzi na maarifa yanayoendana na mahitaji ya jamii katika nchi, kikanda na kimataifa. Vilevile, mitaala hiyo itawezesha kuandaa wanafunzi kuendelea na ngazi ya elimu inayofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuongeza fursa za Elimu ya Ualimu kwa udahili wa jumla 19,314 kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada ambapo Vyuo vya Ualimu vya Serikali vilidahili wanafunzi 19,178 na visivyo vya Serikali vimedahili wanafunzi 136. Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Ualimu, kwa kujenga upya Vyuo vitatu ambavyo ni Sumbawanga, Dakawa, na Mhonda. Vilevile, imeendelea na ujenzi wa Chuo kipya cha Ualimu Ngorongoro kitakachokuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha utendaji wa kazi kwa wakufunzi kwa kutoa mafunzo kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa somo la hisabati, sayansi na TEHAMA kwa wakufunzi 355. Aidha, imetoa mafunzo kuhusu uzalishaji na Uendeshaji wa Vituo vya Walimu wawezeshaji 30,490 wakiwemo walimu wa elimu ya awali na msingi 26,657, walimu wa elimu maalum 1,882 na wawezeshaji wa MEMKWA 1,951.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha uendelezaji wa Elimu Msingi na Sekondari nchini unafanyika kwa kuzingatia usawa, Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa elimu jumuishi kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2021/2022 - 2025/2026 pamoja na kuzalisha nakala kwa maandishi ya kawaida, maandishi ya nukta nundu na maandishi yaliyokuzwa kwa ajili ya wanafunzi wasioona na wenye uoni hafifu; na imenunua viti mwendo 365 na vishikwambi 285 kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wa viungo na viziwi walioko katika shule za msingi na sekondari. Aidha, imenunua na kusambaza vifaa vya kielimu na saidizi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

413 vikiwemo bajaji, kompyuta mpakato, vishikwambi, *embosser machine* na vifaa vya usikivu kwa ajili ya wanafunzi wasioona, vizivi na wenyewe ulemavu wa vilungo katika ngazi ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha Elimu ya Michezo na Mafunzo ya Skauti katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu kwa kutoa mafunzo kuhusu namna bora ya uendeshaji wa Skauti na namna ya kukabiliana na majanga kwa Walimu Walezi wa Skauti 100 katika mikoa ya Mwanza, Dodoma, Manyara, Kigoma, Geita, Mara, Simiyu, Shinyanga, Tabora, Katavi na Singida. Aidha, imeendesha mashindano ya michezo na sanaa katika Vyuo vya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Ufundini na Mafunzo ya Ufundini Stadi nchini Kwa lengo la kuongeza idadi ya wahitimu katika ngazi hizo. Katika kufikia azma hiyo, yafuatayo yametekelizwa:-

(i) Imedahili wanafunzi 266,236 katika ngazi Astashahada ya Awali, Stashahada na Stashahada katika fani za Sayansi na Teknolojia Shirikishi, afya na sayansi shirikishi, biashara, utalii na mipango;

(ii) Imedahili wanafunzi 90,712 katika lengo la wanafunzi 142,150 katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ambapo wanafunzi 428 ni wenyewe mahitaji maalum. Aidha, imedahili wanafunzi 15,037 katika Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi;

(iii) Imeanza ujenzi wa Chuo cha Ufundini Dodoma – DTC chenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,500 katika awamu ya kwanza;

(iv) Imeendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundini Stadi na Huduma cha Mkoa wa Kagera; na

(v) Imeendelea na ujenzi wa mabweni mawili, katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Karume - Zanzibar yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,536 ambapo ujenzi umefikia asilimia 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kufanya mapitio ya mitaala na miongozo ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa lengo la kuhakikisha mafunzo yanayotolewa katika ngazi hiyo yanaendana na mipango ya nchi na mahitaji ya soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufikia azma hiyo, Serikali kuitia Baraza la Elimu ya Ufundini na Mafunzo ya Ufundini Stadi imehakiki mitaala 51 kati ya 150 ilioandalishi na Vyuo vya Elimu ya Ufundini na kutoa mafunzo ya namna ya upimaji na ufundishaji wa mitaala inayozingatia umahiri kwa wanafunzi 653. Aidha, imeandaa na kuhuisha mitaala 27 ya fani mbalimbali katika sekta tano ambazo ni umeme, magari, mitambo, kilimo na ukarimu. Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Elimu ya Ufundini na Mafunzo ya Ufundini Stadi nchini inatolewa kwa vitendo kwa lengo la kukuza na kuendeleza ujuzi na umahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha utendaji kwa kujengea uwezo rasilimaliwa katika taasisi za Elimu ya Ufundini na Mafunzo ya Ufundini Stadi nchini, kuwawezesha watumishi 31 kuhudhuria mafunzo katika ngazi za Shashahada, Shahada ya Kwanza na Umahiri. Vilevile imetoe mafunzo kwa watumishi 1,177 wa Elimu ya ufundi katika mafunzo ya ufundi stadi kulingana na maeneo ya ubobezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha Elimu ya Juu inayotolewa nchini inazingatia sheria na kanuni, miongozi na taratibu na inaendana na mipango ya nchi, soko la ajira la Kikanda na Kimataifa. Serikali imetekeleza yafuatayo: imewezesha tathmini ya Mitaala 72 iliyowasilishwa na Vyuo vikuu nchini na kutoa ithibati kwa mitaala 31. Imetambua na kukagua taasisi saba za nje zilizowasilisha maombi ya kuanza kupeleka wananchi vyuo vya nje ya nchi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, imefanya ufuutiliaji katika taasisi 14 zinazopeleka wanafunzi kusoma nje ya nchi; na imefanya ukaguzi katika Vyuo Vikuu 30 kwa lengo la kuhakiki ubora wa utoaji elimu ya juu. Vilevile, imetathmini na kutambua tuzo 2,111 kati ya 2,531 zilizowasilishwa ambazo zilitolewa na Vyuo vya Elimu ya Juu nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa Umma unapata taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi za Elimu ya Juu, Serikali imefanya maonesho ya 16 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ambapo jumla ya taasisi 74 za ndani ya nchi zilishiriki na wadau 55,000 walihudhuria. Maonesho hayo yalitoa fursa kwa wananchi kufahamu kazi mbalimbali zinazofanywa na Taasisi za Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na Mataifa mengine katika uendelezaji wa Elimu ya Juu nchini kwa lengo la kuhakikisha wataalamu wetu wanapata uzoefu na ujuzi wenye kuendana na mahitaji ya Kikanda na Kimataifa. Katika kufika azma hiyo, Serikali imehuisha Hati za Makubaliano baina ya Tanzania na nchi rafiki ambazo ni Msumbiji, Algeria, Morocco, Zimbabwe, Poland, Umoja wa Falme za Kiarabu pamoja na Jumuiya ya Madola.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha utoaji wa elimu na mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini, Serikali imeendelea kutekeleza yafuatayo: imewezesha upanuzi wa maabara ya viumbehai katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu, Mkwawa ambapo ujenzi umefikia asilimia 80; imeanza ujenzi wa Maabara Kuu ya Kemia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambayo itatumika kwa ajili ya utafiti na kutoa huduma za kupima sampuli za viwandani; imekamilisha ujenzi wa kituo cha Umahiri cha Afrika Mashariki cha Magonjwa na Moyo na Mishipa ya Damu cha Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili Kampasi ya Mloganzila.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia taasisi za Elimu ya Juu, imeendelea kutoa huduma za ushauri wa

kitaalam katika kazi za ujenzi na ukarabati wa majengo mbalimbali kama ifuatavyo: imetoa ushauri wa kitaalam kuhusu ujenzi wa nyumba za Bunge eneo la Kilimani - Dodoma; majengo ya Mchapishaji Mkuu wa Serikali, Kituo cha Taifa cha Kukabiliana na Maafa – Dodoma; majengo ya Ofisi ya Waziri Mkuu; Ofisi ya Maji na Wizara ya Nishati; na pia imetoa ushauri wa kitaalam kuhusu ukarabati wa majengo ya Balozi za Tanzania katika nchi za *DRC*, Rwanda, Oman, Saudi Arabia, Msumbiji, Malawi, Burundi na Marekani na Chuo cha Ualimu Ndala na Mpwapwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika kupambana na athari za ugonjwa wa UVICO - 19 kuititia sekta ya elimu iliidhinisha afua tatu muhimu za kukabiliana na athari hizo kuititia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVICO - 19. Katika utekelezaji wa Mpango huo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitekeleza maeneo matatu ambayo ni kuboresha utoaji wa elimu maalum, kuongeza fursa na ubora wa Elimu ya Ualimu na Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha uwezo wa watumishi kusimamia, kuratibu na kuendeleza Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini kwa kutekeleza yafuatayo: imetoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoka katika Halmashauri 184 za Tanzania Bara kwa lengo la kuboresha uratibu wa masuala ya teknolojia na ubunifu hususan katika kuibua, kutambua na kuendeleza wavumbuzi na wabunifu wachanga nchini; imewajengea uwezo watumishi 182 kati ya 300 walilengwa katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam kama sehemu ya maandalizi ya kupata ithibati ya viwango vya ubora vya kimataifa (*International Organization for Standardization - ISO Certification*); na imewezesha jumla ya watumishi 170 wa taasisi zinazohusika na uendelezaji wa sayansi, teknolojia na ubunifu nchini kuhudhuria masomo ya muda mfupi na muda mrefu katika kozi mbalimbali ambapo kati yao watumishi 31 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi 139 mafunzo ya muda mrefu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa kazi za ubunifu na matokeo ya tafiti yanatambuliwa Kitaifa na Kimataifa na kuendelezwa ili kuongeza kasi ya matumizi yake katika kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufika azma hiyo, Serikali imewezesha bunifu 26 kuingia sokoni kati ya bunifu 200 zilizoendelezwa na Serikali ambazo zilipatikana katika MAKISATU ya mwaka 2019 hadi 2021. Aidha, imetambua teknolojia mpya 90 zilizozalishwa nchini na hivyo kufanya jumla ya teknolojia zilizotambuliwa kufikia 479 katika kanzidata ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa sayansi, teknolojia na ubunifu nchini, kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Imeratibu ushiriki wa nchi katika Mkutano Mkuu wa 65 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki uliofanyika Vienna, Austria mwaka 2021 ambapo Mtafiti Mtanzania Ndugu Salum Faki Hamad, kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (*ZARI*) alipata tuzo ya uzalishaji wa mbegu bora ya mpunga inayostahimili chumvi na magonjwa; na

(ii) Imeshirikiana na mradi wa *South African Innovation Support* ili kuendeleza kazi za ubunifu nchini ambapo ushirikiano huo umeziwezesha kampuni changa mbili za *Fundi App* na *Exam Net* kushiriki katika mashindano ya *Slush* 2021 yaliyofanyika Helsinki Finland. Kupitia mashindano hayo, mshiriki mmoja, Ndugu Godfrey Gervas Kilimwomeshi kutoka Tanzania aliibuka mshindi wa jumla na kupata zawadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO – FUNGU 18. Taarifa hiyo inaptikana katika ukurasa 70 – 72 katika kitabu cha hotuba. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO imetekeleza yafuatayo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(i) Imeshiriki katika Mkutano Mkuu wa 41 wa UNESCO uliofanyika nchini Ufaransa mwezi Novemba, 2021. Katika Mkutano huo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichaguliwa kuwa Mjumbe wa Bodi Tendaji ya UNESCO; na

(ii) Imefanikisha Lugha ya Kiswahili kuwa Lugha ya kwanza Afrika kutambuliwa na Baraza la Umoja wa Mataifa na kupewa siku maalum ya tarehe 7 Julai kuadhimishwa kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe mwelekeo wa Mpango wa Bajeti wa Wizara - Fungu 46 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Taarifa hiyo inapatikana katika ukurasa 72 – 108 katika kitabu cha hotuba. Kazi kubwa inayofanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2022/2023 itakuwa ni kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 kwa minajili ya kufanya maamuzi kuhusu masuala kadhaa ambayo Sera imeainisha lakini hayajatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Sera inaanisha kwamba elimu ya lazima (*compulsory education*), itakuwa ni ya miaka kumi, lakini bado tunatoa elimu ya lazima ya miaka saba. Wizara inatarajia kuwa kabla ya mwisho wa mwaka huu uchambuzi utakuwa umefanyika na kukamilika kuhusu Sera hiyo ili maamuzi yaweze kufanyika kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uchambuzi huo, juhudzi za kukusanya maoni ya wadau zinaendelea ili maamuzi yatakapofanyika yazingatie maoni hayo na uchambuzi wa kitaaamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Sera yatatoa dira ya mabadiliko yanayohitajika katika Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978. Hivyo, Wizara inatarajia kuwa ifikapo Desemba, 2022 itakuwa imekamilisha rasimu ya mabadiliko ya mitaala itakayozingatia maoni ya wadau na mwelekeo wa Sera ya Elimu utakaokuwa umependekezwa. Matokeo ya zoezi hilo yatawezesha uboreshaji wa elimu inayojielekeza katika elimu

ya ufundi na ujuzi utakaomsaidia mhitimu kuweza kujajiri na kuajirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo na mabadiliko ya mitaala ambayo Serikali inakusudia kukamilisha yataleta mageuzi makubwa ya elimu kupata kutokea hapa nchini. Wizara inatoa wito kwa wadau kuendelea kutoa maoni yao kwa sababu azma ya Serikali ni kufanya mageuzi makubwa yanayozingatia matakwa ya wananchi, kuongeza ubora wa elimu, kuwezesha wahitim ukujamini, kuajirika na kujajiri na kuwawezesha wahitim kumudu utandawazi na kukidhi mahitaji ya uchumi wa nchi yetu. Kwa ujumla mambo yafuatayo yataangaliwa na kuzingatiwa:-

- (i) Mapitio ya Sera;
- (ii) Mapitio ya Sheria;
- (iii) Mabadiliko ya Mitaala;
- (iv) Mahitaji, yaani Idadi ya Walimu, Wakufunzi na Wahadhiri;
- (v) Ubora Stahiki wa Walimu, Wakufunzi na Wahadhiri;
- (vi) Mahitaji ya Miundombinu; na
- (vii) Mahitaji ya Vitendeakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya saba ni budi yazingatiwe ili kuhakikisha kwamba mageuzi ya elimu tunayoyatarajia yatakuwa kweli yanakidhi mahitaji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mapitio ya sera na mabadiliko makubwa ya mitaala, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2022/2023, utajielekeza kutekeleza maeneo ya kimkakati yafuatayo:-

- (i) kupanua na kuimarisha elimu ya ufundi nchini;

(ii) kuhimiza uandishi, uchapishaji na uchapaji wa vitabu hapa nchini. Moja ya hatua zitakazochukuliwa ni Serikali kulipia gharama za uchapishaji na uchapaji wa riwaya bora kila mwaka itakayoandikwa na Mtanzania ili kusaidia na kuimarisha juhudzi za uandishi hapa nchini;

(iii) kutekeleza juhudhi za kukuza sayansi hapa nchini kwa kufanya mambo yafuatayo:-

Kwanza, kutoa ufadhili wa asilimia 100 wa kulipia gharama za masomo za Chuo Kikuu kwa wanafunzi watakaoongoza katika mitihani ya masomo ya sayansi ya Kidato cha Sita.

Pili, kutekeleza llani ya CCM, kutoa *scholarship* kwa Watanzania watakaofanya vizuri sana katika masomo yao ya vyuo vikuu kwenye taasisi za sayansi, teknolojia na tiba ili kwenda kusoma kwenye vyuo vilivyo bora zaidi duniani kama vile *MIT*.

Tatu, kuhimiza utafiti wa kisayansi na tiba katika vyuo vyetu vikuu kwa kutoa tuzo ya shilingi milioni 50 kwa mhadhiri ye yote atakaeweza kuchapisha matokeo ya utafiti wake kwenye majorida yenye hadhi ya juu kabisa ya sayansi na ya elimu ya tiba; kuhamasisha sekta binafsi na wadau mbalimbali kufadhili Watanzania kwenda kusoma katika vyuo bora kabisa duniani.

Hadi sasa mikakati imeanza kuandaliwa kwa kushirikiana na Bwana Rupin Rajan ambaye yupo kwenye *Speaker's Gallery* pale na wadau wengine ili kufanikisha azma hii. Kama nitakavyo eleza, tayari Benki ya NMB imekubali kutenga Shilingi bilioni 200 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi.

Nne, kuongeza wigo wa shule za ufundi za elimumsingi na sekondari kwa lengo la kuwajengea vijana wetu stadi na maarifa yanayohitajika katika soko la ajira; na

Tano, kuimarisha ujifunzaji kwa vitendo katika taasisi za Elimu ya Juu kwa kuanza kujenga kampasi za vyuo zenyet kujielekeza katika mafunzo kwa vitendo katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maeneo hayo ya kimkakati yatakwenda sambamba na utekelezaji wa vipaumbele vifuatavyo:-

Sambamba na mapitio ya sera na sheria Serikali itaandaa miongozo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mwongozo wa Usimamizi na Utawala Bora Katika Elimu Katika Mamlaka za Serikali za Mtaa, Mwongozo wa Kuwatambua na Kuwaendeleza Wanafunzi wenyewe Vipawa na Vipaji Katika Shule za Msingi na Sekondari, Mwongozo wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu ya Nje ya Mfumo Rasmi Kwa lengo la kuboresha mafunzo na usimamizi wa elimu katika ngazi husika na Mwongozo wa Kuanzisha, Kukarabati na Kuendesha Maktaba kwa lengo la kuweka utaratibu unaofaa wa kuanzisha, kukarabati na kuendesha maktaba zote hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wenyewe sifa za kujunga katika ngazi mbalimbali za elimu nchini wakiwemo wanafunzi wenyewe mahitaji maalum wanapata fursa sawa na kuhitimu. Adhma hiyo itafikiwa kwa kutekeleza afua mbalimbali ikiwa ni pamoja na;

i. Itafanya ufuatiliaji kwa lengo la kubaini watoto wote wenyewe umri wa kwenda shule na kuwapa fursa ya elimu.

ii. Itaendelea kuimarisha mazingira ya ushiriki wa wadau katika utoaji wa elimu nchini na;

iii. Itaendelea kuimarisha ushiriki wa mtoto wa kike katika elimu kwa kutatua changamoto zinazomkabili ikiwa ni pamoja na ulinzi aendapo shulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi na sekondari na kuhamasisha tabia ya wanafunzi kupenda kujisomea vitabu. Katika kufikia azma hiyo Serikali itawezesha Taasisi ya Elimu Tanzania kuchapa na kusambaza nakala milioni mbili za vitabu vya masomo ya *mathematics, physics, chemistry* na *biology*. Vilevile, itachapa na kusambaza vitabu vya kimacho na nukta nundu kwa ajili ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wenyewe uoni hafifu. Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi na

uendelezaji wa elimu ya ufundi nchini kwa kutoa mafunzo ya elimu ya ufundi katika vyuo vya ualimu kutoka vyuo viwili vilivyopo sasa hadi kufikia vyuo saba. Vyuo hivyo vitawezeshwa vifaa, mashine, karakana na walimu wa masomo ya ufundi pamoja na kutoa mafunzo kwa wanafunzi 1,000 wa masomo ya ufundi katika vyuo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha na kusogeza huduma za udhibiti bora wa elimu katika ngazi za elimu msingi, sekondari na vyuo vya ualimu Serikali itajenga ofisi tano za udhibiti ubora wa shule katika Halmashauri za Pangani, Ubungo, Bunda, Njombe na Tarime na kununua magari 20.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza fursa za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi nchini Serikali inatarajia kusajili vyuo 20 vya elimu ya ufundi na vyuo 80 vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi na hivyo kuwa na jumla ya vyuo 538 vya elimu ya ufundi na vyuo 830 vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Aidha, itaendelea kusimamia ujenzi wa Chuo cha Ufundi cha Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha wahitimu wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi wanapata ujuzi na stadi za kuwawezesha kujajiri na kuajiriwa, Serikali itajenga karakana sita za uchomeaji na uungaji wa vyuma katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi na huduma vya Mkoa wa Manyara, Pwani pamoja na karakana za umeme, bomba, magari na uashi katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma cha Kihonda.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika vyuo vikuu Serikali itajenga maabara 21, mabweni 19, madarasa 77, kumbi za mihadhara 13, maktaba tisa, ofisi 71, mifumo ya maji minne, vituo atamizi vitatu na studio moja. Vile vile itakarabati mabweni 11, madarasa 50, maabara mbili, nyumba za watumishi 15, ofisi 25 katika vyuo mbalimbali vya elimu ya juu. Aidha, itajenga ndaki ya uchumi na mafunzo ya biashara awamu ya pili katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na ndaki ya uchumi na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mafunzo ya biashara katika Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere cha Kilimo na Teknolojia Butiama.

Serikali itaendelea kuwaibua, kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu nchini kwa lengo la kuendeleza matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika ajenda ya maendeleo. Serikali kupitia Tume ya Nguvu za *Atomic* itaendelea kuimarisha usimamizi, udhibiti na matumizi salama ya mionzi ya nyuklia nchini kwa kupima na kudhibiti viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,064 wanaofanya kazi katika mazingira ya vyanzo vya mionzi. Aidha itafanya ukaguzi katika vituo 120 vinyavyotoa mionzi isiyoinishia *non-ionizing radiation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuimarisha uwezo wa ndani wa Taasisi za Elimu, Sayansi na Teknolojia na ubunifu kufanya tafiti zeye tija na kutumia matokeo ya tafiti hizo katika ajenda ya maendeleo ya nchi. Katika kufikia adhma hiyo Serikali itawezesha kufanyika kwa tafiti 252 katika maeneo ya kipaumbele ikiwemo mazingira, TEHAMA, nishati, kilimo na chakula, utawala na maendeleo, mifugo, biashara na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia naomba nitoe shukurani napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Omar Juma Kipanga (Mb), Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa jinsi tunavyofanya kazi vizuri pamoja na mchango wake katika kuandaa Wasilisho hili. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Profesa Eliamani Sedoyeka, Naibu Katibu Wakuu Profesa James Mdoe na Profesa Caroline Nombo ambaao wameongoza kwa umakini na juhudhi kubwa timu ya Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi na watumishi wote katika kuandaa hotuba hii. Ninawashukuru kwa dhati kwa juhudhi hizi na kwa kazi kubwa walizofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru viongozi wa vyama vya wafanyakazi, watumishi wa Wizara na Taasisi zake, Walimu, wanafunzi na wadau wote wa elimu kwa ushirikiano wao. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wamiliki na mameneja wa shule, Vyuo na Taasisi binafsi ambaao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutoa huduma ya elimu nchini. Nawashukuru sana nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Rombo kwa kuniamini na kunichagua kuwa mwakilishi wao nawaahidi utumishi uliotukuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru washirika wa maendeleo na wadau wa elimu wote ambao wamechangia kufanikisha utekelezaji wa mipango na miradi ya elimu, sayansi na teknolojia. Naomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Algeria, Umoja wa Falme za Kiarabu, Australia, Brazil, Canada, China, Cuba, Finland, Hungary, India, Indonesia, Italia, Israel, Japan, Korea Kusini, Marekani, Malaysia, Misri, Morocco, Zimbabwe, Netherlands, New Zealand, Norway, Palestine, Romania, Saudi Arabia, Sweden, Thailand, Ufaransa, Urusi, Uswiss, Uingereza, Uholanzi, Ujerumani na Venezuela. Aidha, natambua pia mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kushukuru Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa yaliyochangia kufanikisha miradi na *programza elimu, sayansi na teknolojia ambayo ni pamoja na Benki ya Dunia, Foreign Commonwealth and Development Office, Swedish International Development Agency (SIDA), Umoja wa Nchi za Ulaya, Benki ya Maendeleo Afrika, Jumuiya ya Madola, Global Partnership in Education, United Nations International Children's Emergency Fund (UNICEF), United Nations Development Program (UNDP), United Nations Education, Scientific and Cultural Organization (UNESCO), United States Agency for International Development (USAID), Inter-University Council for East Africa, Human Development Innovation Fund (HDIF), Accademist Austigia Dutch, British Council, Campaign for Female Education, Commonwealth Secretariate, Aga Khan Education Services, Japan International Cooperation Agency, Karibu Tanzania Organization, Korea International Cooperation Agency, Water Aid, Plan International, Tanzania Education Network (Mtandao wa Elimu wa Tanzania), Mo Foundation, Christians Social Sciences Commission na Baraza Kuu la Waislam Tanzania – BAKWATA.* (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa malengo kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,493,004,355,000 kwa mchanganuo ufuatao: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Shilingi 533,456,916,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara ambapo shilingi 500,196,732,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 33,260,184,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Pia shilingi 959,547,439,000 zinaombwa ka ajili ya miradi ya maendeleo ambapo shilingi 778,083,678,000 ni fedha za ndani na shilingi 181,468,761,000 ni fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Fungu 18 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,709,163,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo mishahara ni shilingi 1,176,870,000 na matumizi mengineyo ni shilingi 1,332,293,000 hii ni kwa ajili ya Fungu 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Bajeti Fungu 46 na Fungu 18 yenye jumla ya shilingi 1,495,713,518,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika Tovuti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofij*)

HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA PROF. ADOLF FAUSTINE MKENDA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/23 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

A. UTANGULIZI

- 1. Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lakoTukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii iliyochambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 la Tume ya Taifa ya UNESCO, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 kwa mwaka wa fedha 2021/22. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/23.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema, kuniwezesha kuendelea kutimiza majukumu yangu na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2022/23. Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kila kitu, hasa kwa amani na mshikamano wa Taifa letu.

3. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunitfea kuwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na kwa kuendelea kumuamini Mheshimiwa Omary Juma Kipanga (Mb) kuwa Naibu Waziri. Napenda pia kumshukuru Rais kwa uongozi na miongozo anayotupatia ambayo imetusaidia sana katika kusimamia Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nawashukuru pia Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango Makamu wa Rais, na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo wamekuwa wakimsaidia Rais katika kutusimamia na kutuongoza.

4. Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb) kwa uongozi wako mahiri wa Bunge letu tukufu. Nawashukuru pia Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb) na wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wao. Nakupongeza pia Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu. Nampongeza pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu.

5. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika na kwa Bunge lako Tukufu kwa kuwapoteza waheshimiwa wabunge wafuataao; Hayati Elias John Kwandikwa aliyekuwa Mbunge wa Ushetu na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa aliyefariki tarehe 2 Agosti, 2021, Hayati William Tate Ole Nasha aliyekuwa Mbunge wa Ngorongoro na Naibu Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu - Uwekezaji, aliyefariki tarehe 27 Septemba, 2021, na Hayati Irene Alex Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Rukwa aliyefariki tarehe 24 Aprili, 2022. Natoa pole kwa ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na wapendwa wetu, na kwa namna ya pekee natoa pole kwa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe (Mb) kwa kufiwa na mtoto wake; naungana na familia, ndugu, jamaa na marafiki kumuombia Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

6. Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru kwa namna ya pekee Mwenyezekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb), Makamu Mwenyezekiti, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba (Mb), na wajumbe wote wa Kamati kwakuchambua na kuishauri Wizara kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2022/23. Kamati hii ni makini sana, na imekuwa ikitoa maoni na ushauri wenye lengo la kuhakikisha tunaendelea kuboresha elimu na kuendeleza sayansi na teknolojia kwa manufaa ya Taifa letu.

7. Mheshimiwa Spika, Napenda pia kuwapongeza wabunge waliochaguliwa hivi karibuni kuwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni Mheshimiwa Emmanuel Leklshon Shangai Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani Mbunge wa Jimbo la Ushetu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

8. Mheshimiwa Spika, Napenda kumshukuru sana mtangulizi wangu, Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako (Mb), na Katibu Mkuu aliystaa fu kwa heshima zote, Dkt. Leornard

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Akwilapo, kwa kazi nzuri walizofanya katika Wizara. Wameiacha Wizara pazuri na wameturahisishia kazi sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana Ajira na wenye Ulemavu.

9. Mheshimiwa Spika, namshukuru sana mke wangu Beatrice, watoto na familia kwa upana wake wote, ikiwa ni pamoja na mama mzazi Sekunda, kwa upendo na ukaribu ambao wamekuwa wakinipa na kunijaza nguvu na ari ya kuchapa kazi.

10. Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 kwa Mwaka wa Fedha 2021/22, na Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2021/22

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI

11. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 1,519,316,801,000.00** kwa ajili ya FUNGU 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo **Shilingi 480,474,878,000.00** ziliikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,038,841,923,000.00** ziliikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo bajetiya maendeel o inajumusi ha ongezeko la fedha za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19. Aidha, kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO - FUNGU 18 liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 2,679,073,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha **1S,1h4i6in,7g8i 0,000.00** za **mishahara** na **Shilingi 1,532,293,000.00** za matumizi mengineyo.

Ukusanyaji wa Maduhuli

12. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/22, Wizara kupitia FUNGU 46 ilitarajia kukusanya maduhuli yenye

thamani ya **Shilingi 540,943,008,495.63** ambapo kiasi cha **Shilingi 8,680,995,000.00** kilipangwa kukusanya na idara na vitengo na **Shilingi 532,262,013,495.63** zilipangwa kukusanya na taasisi zillizo chini ya Wizara. Vyanzo vya maduhuli haya ni ada, ushauri elekezi, ukaguzi wa shule na utoaji wa huduma mbalimbali.

13. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2022 Wizara imekusanya **Shilingi 415,796,161,776.80** sawa na **asilimia 77** ya makadirio ambapo **Shilingi 7,622,836,164.00** zimekusanya na idara na vitengo na **Shilingi 408,173,325,612.80** zimekusanya na taasisi zillizo chini ya Wizara.

Matumizi ya Kawaida

14. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2022, Wizara imepokea Jumla ya **Shilingi 396,962,728,624.62** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kupitia Fungu 46, ambazo ni sawa na **asilimia 83** ya fedha za Matumizi ya Kawaida zillzoidhinishwa. Aidha, kupitia Tume ya UNESCO –Fungu 18 Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 1,723,003,183.30** sawa na asilimia **76** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Miradi ya Maendeleo

15. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo hadi kufikia Aprili, 2022, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 994,711,772,676.29** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambazo ni sawa naasilimia **96** ya bajeti iliyotengwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 684,470,232,276.01** ni fedha za ndani na **Shilingi 310,241,540,400.29** ni fedha za nje. Aidha, kiasi cha fedha za nje kinajumuisha **Shilingi 64,297,963,057.82** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVKO 19

C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA

16. Mheshimiwa Spika, sehemu hii inaelezea utekelezaji wa majukumu na mafanikio ya Wizara kwa kuzingatia vipaumbele vyake. Taarifa inatoa ufanuzi wa maeneo ya msingi ya utekelezaji wa Wizara kwa kutoa takwimu na matokeo ya utekelezaji huo. Maeneo yanayotolewa taarifa yamegawanyika kimajukumu kama ifuatavyo:

Usimamizi wa Elimumsingi na Sekondari

17. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Elimumsingi inatolewa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Ili kufikia azma hiyo, Serikali imeandaa miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma ya Chakula na Lishe kwa Wanafunzi wa Elimumsingi kwa lengo la kuimarisha mahudhurio ya wanafunzi na kuboresha ujifunzaji. Mwongozo tayari upo katika utekelezaji. Aidha, Serikali imeandaa miongozo mingine mitatu ambayo ipo katika hatua ya uchapaji na usambazaji. Miongozo hiyo ni:

- (i) Mwongozo wa Viwango na Uendeshaji wa Elimu ya Awali -*National Operational Guidelines and Minimum Standards for Pre-Primary Education* pamoja na Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo huo;
- (ii) Mwongozo wa Uanzishaji, Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo Shikizi vya Shule; na
- (iii) Mwongozo wa Utoaji wa Elimu ya Kujitegemea katika Shule za Msingi na Sekondari.

18. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utoaji wa elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi, Serikali imeboresha na kutekeleza miongozo mitatu ambayo ni: Mwongozo wa Utekelezaji wa Programu ya Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala; Mwongozo wa Kutoa Huduma kwa Wanafunzi katika Programu ya Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala; na Mwongozo wa Wawezeshaji katika Programu ya Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala. Utekelezaji wa miongozo hiyo umewezesha kuwarejesha shulenii wasichana 3,333 kwa mwaka 2022 ukilinganisha na lengo la kurejesha wasichana 3,000 walioacha shule kwa sababu mbalimbali.

19. Mheshimiwa Spika, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ni sehemu ya Elimumsingi. Katika eneo hili, Serikali imeendelea na uimarishaji wake kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) imeongeza wigo wa utoaji wa programu za elimu masafa mikoani na kuendesha jumla ya programu 13 katika kampasi za Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ya; Dar es Salaam, Morogoro na Mwanza. Programu hizo zimewezesha utoaji wa mafunzo ya ualimu na usimamizi wa elimu ya watu wazima kwa vijana na watu wazima 7,185, kati yao wanawake walikuwa 4,075 na wanaume ni 3,110;
- (ii) imesogeza huduma ya Elimu kwa Njia Mbadala kwa wanafunzi walioacha shule kwa sababu mbalimbali kwa kuwezesha ujenzi wa vituo tisa na kukarabati majengo matano ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima; na
- (iii) imeendelea kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya sekondari kuititia Elimu kwa Njia Mbadala kwa kufanya mapitio ya mihtasari na moduli za Elimu Nje ya Mfumo Rasmi kwa hatua ya kwanza ya Kidato cha 1 na 2 na hatua ya pili ya Kidato cha 3 na 4 kwa masomo saba ambayo ni: *English, Kiswahili, Geography, History, Civics, Biology* na *Mathematics*.

20. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza ujuzi na maarifa kwa watumishi wanaotekeleza na kusimamia uendelezaji wa Elimumsingi na Sekondari nchini, Serikali imeendelea kutoa mafunzo kama ifuatavyo:

- (i) imetoa mafunzo kuhusu huduma ya malezi, unasihi na ulinzi wa mtoto shulenii kwa walimu 243 (wanawake 151 na wanaume 92) wa shule za msingi na sekondari kati ya walimu 200 waliolengwa kutoka katika maeneo ambayo yalikuwa hayajafikiwa na mafunzo hayo. Mafunzo hayo yameimarisha stadi za utoaji wa huduma hizo na kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto;
- (ii) imetoa mafunzo ya utekelezaji wa mtaala wenye kuzingatia umahiri kwa walimu 4,241 (msingi 2,300 na sekondari 1,941) ambayo yameimarisha uwezo wa walimu kufundisha kwa kuzingatia umahiri;

(iii) imetoa mafunzo ya mbinu bora za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la hisabati kwa walimu 846 wa shule za msingi na sekondari (wanawake 213 na wanaume 633) kutoka katika halmashauri 20 zenyе ufaulu hafifu nchini; na

(iv) imewezesha mafunzo kwa walimu wawezeshaji 736 wa masomo ya sayansi na hisabati kwa lengo la kuwajengea uwezo katika uwezeshaji wa walimu wa sekondari 20,000 wa masomo husika katika ngazi ya Halmashauri.

21. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na uwekezaji katika sekta ya elimu. Uwekezaji huo unalenga katika kuongeza fursa za utoaji wa elimu bora. Mafanikio ya uimarishaji wa mazingira hayo ni kama ifuatavyo:

(i) usajili wa jumla ya shule 741 zilizokidhi vigezo kati ya shule 450 zilizolengwa. Mchanganuo wa shule hizo ni kama ifuatavyo; shule za awali pekee (zisizo za Serikali 33), shule za awali na msingi 511 (za Serikali 363 na zisizo za Serikali 148), sekondari 196 (za Serikali 151 na zisizo za Serikali 45) na Chuo cha Ualimu kimoja kisicho cha Serikali;

(ii) utoaji wa vibali vya kuanzisha shule 88 zilizokidhi vigezo kati ya 182 zilizoomba. Kati ya hizo, shule za awali pekee ni saba, za awali na msingi 65 na sekondari 16;

(iii) kutoa uthibitisho wa wamiliki wa Shule 237 na mameneja 237 kati ya wamiliki 331 na mameneja 331 walioomba ambapo wamiliki wa shule za awali pekee 16, za awali na msingi 181 na sekondari 40;

(iv) kutoa vibali vya kuanzisha huduma ya bweni katika shule 68 (shule za awali na msingi 46 na sekondari 22) zilizokidhi vigezo, kati ya shule 75 zilizoomba ili kupunguza adha kwa wanafunzi kutembea umbali mrefu;

(v) kutoa vibali vya kuongeza mikondo kwa shule 21 (awali na msingi 14 na sekondari 7) pamoja na kutoa vibali vya

kuongeza tahasusi katika shule za sekondari 19 zilizokidhi vigezo;

(vi) kuwezesha ujenzi wa shule mpya 175 (msingi 9 na sekondari 166) ambapo ujenzi wa shule 33 (msingi 9 na sekondari 24) umekamilika na ujenzi wa shule 142 za sekondari upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Aidha, imewezesha ujenzi wa madarasa 3,283, mabweni 112, ofisi 10, matundu ya vyoo 8,096, usimikaji wa vifaa vya kunawia mikono na ununuzi wa matenki ya kuhifadhi maji safi katika shule za msingi 235; na

(vii) kuendelea na ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Mfano lyumbu - Jijini Dodoma itakayokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000.

22. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa Elimumsingi nchini, Serikali kuititia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imewezesha ununuzi wa magari 187 kwa ajili ya maafisa elimu msingi katika halmashauri 184 na magari matatu kwa ajili ya Baraza la Mitihani. Aidha, inaendelea na taratibu za ununuzi wa magari 185 kwa ajili ya maafisa elimu sekondari nchini. Lengo la utekekelezaji wa afua hiyo ni kuendelea kuimarisha mazingira ya ufanyaji kazi kwa maafisa elimu na kusogea huduma karibu na wananchi kwa usimamizi bora wa elimu.

23. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu katika ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari kwa lengo la kuimarisha uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja na hivyo kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na kujenga utamaduni wa wanafunzi kupenda kujisomea vitabu. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeliza yafuatayo:

(i) imeimarisha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi kwa Darasa la VI – VII kwa kuwezesha uchapaji na usambazaji wa nakala 9,903,453 za vitabu vya kiada vya masomo 14 na Kiongozi cha Mwalimu nakala 599,928 ambapo kwa sasa uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi umefikia 1:1;

- (ii) imechapa na kusambaza vitabu vya kiada nakala 3,139,500 vya masomo ya Elimu ya Awali na Msingi Darasa la I – V vitakavyosaidia kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;
- (iii) imechapa na kusambaza vitabu vya kiada vya maandishi yaliyokuzwa nakala 20,422 kwa masomo 44 ya Darasa la I – VII kwa ajili ya wanafunzi wenyewe uoni hafifu.
- (iv) imeendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu kwa wanafunzi wa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi kwa kuwezesha kuchapa na kusambaza katika halmashauri zote za Tanzania Bara nakala 1,510,832 za vitabu vya kiada vya Kundirika la Kwanza na la Pili, Kiongozi cha Mwalimu nakala 137,500 na mihtasari nakala 16,041;
- (v) imekamilisha uchapaji wa nakala 6,074,000 za vitabu vya kiada aina 29 vya Sekondari Kidato cha 1 - 4 kwa masomo ya *Biology, Physics, Chemistry, Mathematics, Agriculture, Home Economics, Kiswahili, Civics, Information and Computer Studies, Geography, History* na *English*. Kazi ya kusambaza nakala hizo katika halmashauri zote Tanzania Bara inaendelea; na
- (vi) imeendelea na uandishi wa vitabu 34 vya masomo ya ufundu kwa ajili ya wanafunzi wa Kidato 1 – 4 ambavyo viro katika hatua za ukamilishaji.

24. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa elimu ya Msingi na Sekondari nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayayo:

- (i) imeandaa maudhui ya kielektroniki ya wanafunzi wa Elimu ya Awali jumla ya Masomo 58 ambapo Lugha ya Kiswahili ni 29 na Kiingereza 29 kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK;
- (ii) imeandaa mfumo wa kielektroniki (Learning Management System - LMS) wenyewe moduli, miongozo na vitabu mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia kwa njia ya mtandao

utakaotumika kutoa Mafunzo Endelevu kwa Walimu Kazini (MEWAKA);

(iii) imeboresha Maktaba Mtandao ya Taasisi ya Elimu Tanzania kwa kuiongezea uwezo wa kubeba maudhui katika miundo mbalimbali na kuongeza baadhi ya vitabu ambavyo havikuwepo. Maktaba hiyo inapatikana bure kwa anwani <https://ol.tie.go.tz> ambayo imerahisisha upatikanaji wa vitabu;

(iv) imekamilisha uandishi wa vitabu aina 34 vya masomo mbalimbali kwa ajili ya wanafunzi wa Kidato cha 1 – 6 na kuviweka katika maktaba mtandao inayopatikana bure. Vilevile, imefanya tathmini na kutoa ithibati ya vitabu vya ziada 53 na maudhui ya kielektroniki 17. Aidha, miswada 90 ipo katika hatua mbalimbali za tathmini; na

(v) imenunua vifaa vya *studio* ya televisheni na redio kwa ajili ya kuandaa programu mbalimbali za kielimu ambazo zitasaidia kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

25. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za maktaba nchini kwa lengo la kuamsha ari ya Watanzania kupenda kujisomea na kuelimika. Katika kuflikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imefanya ukaguzi na kutoa ushauri wa usimamizi na uendeshaji wa Maktaba 13 zikiwemo Maktaba ya Mkoa wa Singida, Mwanza, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Dodoma, Ruvuma, Mbeya, Kagera, Morogoro na Iringa pamoja na Maktaba ya Wilaya ya Mbulu na Maktaba ya Kijiji cha Mbweera iliyopo Wilaya ya Hai;

(ii) imetoa ushauri wa kitaalamu katika vituo 286 kati ya vituo 350 vya huduma ya maktaba viliviyolengwa ambapo ushauri ulihusu uanzishaji, upangaji na uendeshaji wa Maktaba za Shule 171, Vyuo 11, Taasisi 82 na Halmashauri 22;

(iii) imewajengea uwezo wakutubi 120 kutoka vituo 42 vinavyotoa huduma za maktaba kuhusu namna bora ya kuhudumia jamii; na

(iv) imewezesha ukarabati wa maktaba ya Mkoa wa Tabora, Iringa, Kilimanjaro, Kigoma, Rukwa, Morogoro na Kagera.

26. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhamkisha Elimumsingi inatolewa kwa usawa na kuzingatia malezi bora na usalama wa mtoto shulenii pamoja na upangaji na usawazishaji wa walimu wa sekondari katika maeneo yote nchini, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) inaendelea na ukamilishaji wa Mwongozo wa Programu ya Shule Salama; Mkakati wa Kitifa wa Upangaji na Usawazishaji wa Walimu wa Sekondari; Mkakati wa Kuimarisha Matumizi ya TEHAMA; na Mkakati wa Kuongeza Udhili wa Wasichana katika Shule za Sekondari; na

(ii) imechapa na kusambaza Miongozo ya Kutoa Ushauri Nasaha na Unasihi nakala 44,400 kwa ajili ya wanafunzi wa Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari kwenda Halmashauri zote Tanzania Bara. Miongozo hiyo itasaidia walimu kutoa huduma ya ushauri na unasihi kwa wanafunzi.

27. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kusimamia upimaji na tathmini ya wanafunzi wa Elimumsingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu nchini kwa kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) imeendesha upimaji wa Darasa la Nne (SFNA) 2021 kwa watahiniwa 1,561,599 kat i ya watahiniwa 1,678,209 waliosajiliwa;

(ii) imeendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) 2021 kwa watahiniwa 1,108,023 kat i ya watahiniwa 1,132,084 waliosajiliwa;

(iii) imeendesha Upimaji wa Kidato cha Pili (FTNA) 2021 kwa watahiniwa 602,955 kat i ya watahiniwa 652,611 waliosajiliwa;

- (iv) imeendesha Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2021 kwa watahiniwa 521,351 katи ya watahiniwa 538,024 waliosajiliwa. Aidha, imeendesha Mtihani wa Maarifa (OT) 2021 kwa watahiniwa 8,324 katи ya watahiniwa 9,874 waliosajiliwa;
- (v) imesajili watahiniwa 88,805 wa Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE) na watahiniwa 7,115 wa Mitihani ya Ualimu (Astashahada na Stashahada). Mitihani hiyo imeanza kufanyika tarehe 9 Mei, 2022;
- (vi) imeendesha Upimaji wa Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa sampuli ya wanafunzi 32,043 wa Darasa la Pili ambapo asilimia 67.00 walifikia kiwango tarajiwa cha ufaulu;
- (vii) imechapa na kusambaza nakala 561,581 za *Pupil Item Response Analysis* (PIRA) 2020 na *Candidates Item Response Analysis* (CIRA) 2020 za vitabu vya taarifa za uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji na mitihani ya Kitaifa kwa lengo la kuvisambaza na kusaidia walimu na wanafunzi kuelewa mada zilizoonesha ugumu katika ujifunzaji na ufundishaji; na
- (viii) imekamilisha mfumo wa usahihishaji kwa njia ya kielektroniki (E - Marking) katika ngazi ya Elimu ya Ualimu kwa lengo la kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji wa mitihani.

28. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kukusanya maoni kuhusu mitaala inayotumika katika ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu kutoka kwa wadau wa elimu ambapo hadi sasa jumla ya wadau 103,210 wametoa maoni. Wadau walioshiriki katika kutoa maoni ni pamoja na; Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Taasisi za kidini, Taasisi binafsi, Wataalamu mbalimbali wa elimu, na Wananchi kwa ujumla. Aidha, maoni hayo yamekusanya Tanzania Bara na Zanzibar na yatazingatiwa wakati wa uandaaji wa mitaala mipya itakayowajengea wanafunzi ujuzi na maarifa yanayoendana na mahitaji ya jamii katika nchi, Kikanda na Kimataifa. Vilevile,

mitaala hiyo itawezesha kuwaandaa wanafunzi kuendelea na ngazi ya elimu inayofuata.

Usimamizi wa Elimu ya Ualimu

29. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuongeza fursa za Elimu ya Ualimu kwa kudahili jumla ya wanafunzi wa Astashahada ya Elimu ya Msingi kuwa 10,975 (wanawake 5,824 na wanaume 5,151), Stashahada ya Ualimu Sekondari miaka miwili 2,663 (wanawake 1,037 na wanaume 1,626) na Stashahada maalum ya ualimu sekondari sayansi miaka mitatu 5,540 (wanawake 1,973 na wanaume 3,567) na hivyo kufanya Vyuo vya Ualimu vya Serikali kuwa na jumla ya wanafunzi 19,178. Aidha, katika Vyuo vya Ualimu visivyo vya Serikali, jumla ya wanafunzi 136 (wanawake 87 na wanaume 49) wamedahiliwa na hivyo kufanya jumla ya wanafunzi wanaosoma elimu ya ualimu kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada kuwa 19,314 (wanawake 9,113 na wanaume 10,201).

30. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Ualimu, Serikali imetekeleza afua zifuatazo:

(i) inajenga upya Vyuo vya Ualimu vitatu ambavyo ni Sumbawanga, Dakawa, na Mhonda kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ambapo ujenzi upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Aidha, Serikali inajenga Chuo Kipywa cha Ualimu Ngorongoro kitakachokuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi 400;

(ii) imejenga jumla ya madarasa 44, maktaba tatu, maabara mbili, kumbi za mihadhara nne, nyumba za watumishi 18, mabweni matano, na jengo la utawala moja katika Vyuo vya Ualimu 23;

(iii) imekarabati jumla ya madarasa 16, maktaba moja, ukumbi wa mihadhara mmoja, nyumba za watumishi nane, mabweni saba, bwalo moja, majengo ya utawala mawili na vyoo; na

(iv) imewezesha ununuzi wa kompyuta 425 ili kuboresha ufundishaji wa somo la TEHAMA. Aidha, Serikali imeimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya sayansi kwa vitendo kwa kununua vifaa na kemikaliza Maabara za Sayansi katika Vyuo 35 vya Ualimu vya Serikali.

31. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu ya Ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa somo la hisabati, sayansi na TEHAMA kwa wakufunzi 355 (wanawake 83 na wanaume 272);

(ii) imetoa mafunzo kazini kwa wakufunzi 1,168 wa Vyuo vya Ualimu kuhusu utekelezaji wa mitaala yenyewe kuzingatia umahiri kwa lengo la kuimarisha uandaaji wa walimu tarajali wenye uwezo wa kufundisha kwa umahiri;

(iii) imetoa mafunzo ya Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo vya Walimu (TRCs) kwa viongozi wasimamizi wa elimu 985 wakiwemo Maafisa Elimu Mkoa 26, Maafisa Elimu Taaluma Mkoa 26, Maafisa Elimu Msingi wa Wilaya 144, Maafisa Elimu Taaluma Wilaya 144, Wathibiti Ubora Kanda 11, Wathibiti Ubora wa Wilaya 144, Maafisa Elimu Kata 346, na Makatibu Wasaidizi Tume ya Utumishi wa Walimu
– TSC 144;

(iv) imetoa mafunzo kwa walimu kazini kuhusu uanzishaji na uendeshaji wa Vituo vya Walimu kwa walimu wawezeshaji 30,490 wakiwemo walimu wa elimu ya awali na msingi 26,657, walimu wa elimu maalum 1,882 na wawezeshaji wa MEMKWA 1,951. Mafunzo hayo yametolewa katika Vituo vya Walimu (TRCs) na baadhi ya shule za msingi kupitia Mpango wa Mafunzo Endelevu kwa Walimu Kazini (MEWAKA) kwa lengo la kujenga umahiri katika ufundishaji;

(v) imetoa mafunzo kuhusu ufundishaji na ujifunzaji kwa Wakufunzi wa Elimu ya Awali na masomo ya lugha 479 (Wanawake 253 na Wanaume 226); na

(vi) imetoa mafunzo kuhusu ujumuishwaji wa elimu ya usawa wa kijinsia kwa wakufunzi wa vyuo vya ualimu 834 (wanawake 336 na wanaume 498) wa masomo ya sayansi, hisabati, TEHAMA, elimu ya awali na masomo ya lugha.

32. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kusimamia uendelezaji wa Elimu ya Ualimu kwa lengo la kuimarisha ubora elimu hiyo. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo ya uongozi, usimamizi na uendeshaji wa elimu kwa wajumbe wa bodi 325 wa vyuo vya ualimu kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kiutendaji;

(ii) imeandaa mwongozo wa kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kutoa Mafunzo Kazini kwa Walimu; na

(iii) imeandaa Mwongozo wa Uendeshaji wa Vituo vya Walimu na Vyuo vya Ualimu utakaobainisha majukumu ya watendaji kulingana na ngazi zao.

33. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha Vyuo vya Ualimu vinatoa mafunzo yanayoendana na mahitaji ya sasa, Serikali imeendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea na ukarabati wa maabara za sayansi na TEHAMA katika Vyuo vya Ualimu vya Butimba, Dakawa, Morogoro, Patandi, Tukuyu, Mpwapwa na Kasulu; na

(ii) imeendelea kuvunganisha Vyuo vya Ualimu 15 vya Serikali katika Mkongo wa Taifa kwa lengo la kuimarisha mawasiliano, ufundishaji na ujifunzaji kwa njia ya kielektroniki.

Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu

34. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu inayotolewa nchini inazingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu, Serikali imetekeleza yafuatayo:

- (i) imetoea mafunzo ya kuimarisha Uthibiti Ubora wa Shule wa Ndani kwa Walimu Wakuu 7,612 kati ya Walimu Wakuu 7,679 waliolengwa na Maafisa Elimu Kata 3,860 kati ya Maafisa Elimu Kata 3,901 pamoja na wajumbe wa Kamati za Shule wapatao 487 waliokuwa katika mpango wa mafunzo;
- (ii) imetathmini jumla ya asasi 6,524 kati ya lengo la asasi 7,263 ambazo ni: shule za Awali na Msingi 5,332; Shule za Sekondari 1,162; na Vyuo vya Ualimu 30 kwa lengo la kuinua ubora wa elimu;
- (iii) imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa ushauri uliotolewa katika asasi 1,516 ukilinganisha na lengo la asasi 1,453. Kati ya asasi hizo, Shule za Awali na Msingi 1,156, Sekondari 358, na Vyuo vya Ualimu viwili (2) vilifuatiliwa ili kutathmini utekelezaji wa mapendeleko na ushauri uliotolewa katika tathmini za awali;
- (iv) imefanya tathmini maalum ya maombi ya usajili katika asasi 698 zikiwemo shule za awali na msingi 492, sekondari 204 na vyuo vya ualimu viwili kwa lengo la kubaini endapo zinakidhi vigezo vya usajili.

35. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha uongozi na usimamizi wa elimumsingi, sekondari na ualimu, Serikali imedahili walimu 1,819 kati ya walimu 2,515 waliolengwa katika ngazi ya Astashahada, Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu kuhusu Uthibiti Ubora wa Shule kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM).

Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu Maalum

36. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha uendelezaji wa elimumsingi na sekondari nchini unafanyika kwa kuzingatia usawa kwa watoto wote, Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa elimu jumuishi kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2021/22 - 2025/26 pamoja na kuzalisha nakala kwa maandishi ya kawaida, maandishi ya breli na maandishi yaliyokuzwa

kwa ajili ya wanafunzi wasioona na wenyewe uoni hafifu kwa lengo la kuelekeza namna ya kutoa elimu bora kwa wanafunzi wenyewe mahitaji maalum kuanzia ngazi ya Elimu ya Awali hadi Elimu ya Juu;

(ii) imetoa mafunzo kazini kwa walimu 1,985 wanaofundisha wanafunzi wenyewe mahitaji maalum kwa lengo la kuboresha mbinu za kufundishia na kujifunzia. Vilevile, imetoa mafunzo kwa Wathibiti Ubora wa Shule 206 kwa lengo la kuboresha uthibiti ubora wa darasa jumuishi na ufanyakij tathmini ya miundombinu kwa kuzingatia mahitaji ya watoto wenyewe mahitaji maalum;

(iii) imewezesha wanafunzi 91 wenyewe mahitaji maalum wanaotoka katika kaya zenyekipato duni kwa Kuwalipia ada wanafunzi watano; Kuwanunulia vifaa saidizi wanafunzi 50; Kuwalipia BIMA ya afya kwa wanafunzi 28; na Kuwasaldia fedha za kujikimu wanafunzi nane kwa lengo la kuhakikisha kuwa wanafunzi hao wanapata fursa ya elimu na wanamaliza masomo yao bila changamoto;

(iv) imenunua viti mwendo (wheelchairs) 365 na vishikwambi (tablets) 285 kwa ajili ya wanafunzi wenyewe ulemavu wa viungo na viziwi walioko katika shule za msingi na sekondari kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji;

(v) imewezesha ununuzi wa vifaa vya wanafunzi wenyewe mahitaji maalum kwa shule za msingi 654 na sekondari 67;

(vi) imenunua na kusambaza vifaa vya kielimu na saidizi 413 vikiwemo bajaji, kompyuta mpakato, vishikwambi, *embosser machine* na vifaa vya usikivu. Vifaa hivyo ni kwa ajili ya wanafunzi wasioona, viziwi na wenyewe ulemavu wa viungo katika ngazi ya Elimu ya Juu; na

(vii) imeandaa muhtasari na mwongozo wa kufundishia wanafunzi wenyewe uziwikutoona na kupatiwa ithibati na mamlaka husika. Nyaraka hizo zitatumika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi hao.

37. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha elimu ya michezo na mafunzo ya skauti katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu nchini, kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) imetoa mafunzo kwa walimu walezi wa skauti 100 (wanawake 28 na wanaume 72) kutoka shule za msingi katika mikoa ya Mwanza, Dodoma, Manyara, Kigoma, Geita, Mara, Simiyu, Shinyanga, Tabora, Katavi na Singida. Mafunzo hayo yalihusu namna bora ya uendeshaji wa skauti katika shule za msingi na namna ya kukabiliana na majanga ikiwemo janga la moto; na
- (ii) imeendesha mashindano ya michezo na sanaa (UMISAVUTA) katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali 35 kwa lengo la kuimarisha stadi za michezo vyuoni na kuimarisha afya za wanafunzi katika vyuo hivyo.

Uimarishaji wa Elimu ya Ufundsi na Mafunzo ya Ufundsi Stadi

38. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Ufundsi na Mafunzo ya Ufundsi Stadi nchini Kwa lengo la kuongeza idadi ya wahitimu katika ngazi hiyo. Katika kufikia azma hiyo, yafuatayo yametekelezwa:

- (i) imedahili wanafunzi 266,236 (wanawake 132,766 na wanaume 133,470) kati ya lengo la wanafunzi 159,500 waliorajiwu kudahiliwa katika vyuo vya ufundi nchini kwa mchanganuo ufuataao: Astashahada ya Awali 133,118 (wanawake 66,383 na wanaume 66,735); Astashahada na Stashahada katika fani za Sayansi na Teknolojia Shirikishi wanafunzi 63,832 (wanawake 34,016 na wanaume 29,816); fani ya afya na sayansi shirikishi wanafunzi 50,368 (wanawake 26,119 na wanaume 24,249) na fani ya biashara, utalii na mipango wanafunzi 18,918 (wanawake 6,248 na wanaume 12,670);
- (ii) imedahili wanafunzi 90,712 (wanawake 31,033 na wanaume 59,679) kati ya lengo la wanafunzi 142,150 katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ambapo wanafunzi 428

(wanawake 162 na wanaume 266) ni wenye mahitaji maalum;

(iii) imeidhinisha kuanzishwa kwa idara 20 katika vyuo 15 vya ufundu kwa lengo la kuendesha programu za NTA katika bodi za masomo yafuatayo: afya na sayansi shirikishi nane, biashara, utalii na mipango sita na sayansi na teknolojia shirikishi sita;

(iv) imedahili wanafunzi 15,037 katika Vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi;

(v) imewezesha vyuo 12 vya maendeleo ya wananchi kujenga ushirikiano wa kitaaluma na vyuo sita vya nchini Canada kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kukuza ujuzi na maarifa;

(vi) imeanza ujenzi wa Chuo cha Ufundu Dodoma – DTC chenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,500 kinachojengwa katika eneo la Nala. Kukamilika kwa chuo hicho kutaongeza fursa za elimu ya ufundu na mafunzo ya ufundu stadi nchini;

(vii)imeendelea na ujenzi na ukarabati wa vyuo 14 vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs);

(viii)imeendelea na ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundu Stadi na Huduma cha Mkoa wa Kagera ambapo ujenzi huo upo katika hatua za ukamilishaji;

(ix)imeendelea na ujenzi wa mabweni mawili, maktaba mbili, nyumba za watumishi kumi, bwalo moja, maabara moja, jengo la utawala moja, kumbi za mihadhara tatu, zahanati moja, hosteli mbili, karakana tatu, kantini moja, chumba cha usanifu kimoja pamoja na kukarabati mtambo mmoja wa kufua umeme kwa kutumia nguvu za maji katika taasisi za elimu ya ufundu na mafunzo ya ufundu stadi;

(x)inaendelea na ujenzi wa mabweni mawili katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Karume - Zanzibar yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,536

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(wanawake 768 na wanaume 768) ambapo ujenzi umefikia asilimia 30; na

(xi) imewezesha ununuvi wa samani na vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Chuo cha Ufundisti ya Kongwa, Kasulu, Nyasa na Ruangwa.

39. Mheshimiwa Spika, katika kuwajengea umahiri wahitimu wa Elimu ya Ufundisti na Mafunzo ya Ufundisti, Serikali inaendelea na ujenzi wa vituo vya umahiri katika Chuo cha Ufundisti Arusha, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji katika Nyanja za Nishati, Usindikaji wa Ngozi, Uchukuzi na TEHAMA.

40. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha ubora wa Elimu ya Ufundisti na Mafunzo ya Ufundisti nchini, Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya utoaji wa elimu na mafunzo kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imetoa namba ya uhakiki wa tuzo (Award Verification Number - AVN) kuititia Baraza la Elimu ya Ufundisti na Mafunzo ya Ufundisti kwa wahitimu wa vyuo vya ufundisti 23,332 kati ya lengo la tuzo 20,000 ili kuepuka udanganyifu wa wahitimu wanaoendelea na Elimu ya Juu na kuvirahisishia vyuo kufanya uhakiki wa Stashahada;

(ii) imefanya ulinganifu wa tuzo 143 ili kuthibiti viwango vya elimu ya ufundisti nchini;

(iii) imeandaa rasimu ya Mfumo wa Tuzo wa Taifa (*National Qualifications Framework – NQF*) na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Ufundisti na Mafunzo ya Ufundisti (The Technical and Vocational Education and Training Development Plan 2021/22 – 2025/26);

(iv) imetunga na kuendesha Mitihani ya Taifa ya Mafunzo ya Ufundisti (CBA na NABE) ambapo jumla ya watahiniwa 34,531 walifanya mitihani hiyo;

(v) imevijengea uwezo vyuo 33 vya ufundi kwa ajili ya kupata usajili kamili ambapo kati ya hivyo, vyuo 17 vilihakikiwa kwa lengo la kuvisajili katika bodi za masomo kama ifuatavyo: afya na sayansi shirkishi vyuo 11, biashara, utalii na mipango vyuo vitano na bodi ya sayansi na teknolojia shirkishi chuo kimoja; na

(vi) imefanya ufuatiliaji wa uendeshaji wa vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi kwa lengo la kuhakiki ubora wa mafunzo yanayotolewa ili kubaini endapo vinakidhi viwango vinavyohitajika.

41. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufanya mapitio ya mitaala na miongozo ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa lengo la kuhakikisha mafunzo yanayotolewa katika ngazi hiyo yanaendana na mipango ya nchi na mahitaji ya soko la ajira. Katika kufikia azma hiyo, Serikali kuititia Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, imetekeleza yafuatayo:

(i) imehakiki mitaala 51 kati ya 150 ilioandaliwa na vyuo vya elimu ya ufundi kwa lengo la kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanakidhi mahitaji ya soko la ajira;

(ii) imeandaa na kuhuisha mitaala 27 ya fani mbalimbali katika sekta tano ambazo ni: umeme (5), magari (8), mitambo (5), kilimo (5) na ukarimu (4). Aidha, mitaala 19 katika fani ya Biashara, Usafirishaji, Ujenzi na Mitambo ya Magari Moshi imeanza kuandaliwa;

(iii) imehuisha mihtasari nane kwa ajili ya masomo bebezi na mtambuka ambayo ni Stadi za Maisha, Ujasiriamali, TEHAMA, Sayansi ya Ufundi, Michoro ya Kiufundi, Lugha ya Kiingereza, Lugha ya Kifaransa na Biashara ya Utalii;

(iv) imeandaa mwongozo wa mitaala ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na mwongozo wa kuwezesha wanafunzi kusajiliwa kusoma na kubadilishana watumishi katika vyuo vya ATC, NIT na DIT; na

(v) imefanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mitaala na mihtasari iliyotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili katika Vyuo 21 vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs).

42. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi nichini inatolewa kwa vitendo kwa lengo la kukuza na kuendeleza ujuzi na umahiri. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imerasimisha ushirikiano na mashirika na taasisi 17 kutoka katika sekta rasmi ili kuwezesha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi na walimu. Mashirika hayo ni; Shirika la Umeme Tanzania, Wakala wa Ufundu na Umeme (TEMESA), TPM (1998) Ltd Morogoro, TOYOTA, Bakhresa Co. Ltd, Kilombero Sugar Co, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Tume ya Sayansi na Teknolojia, Benki ya Azania, SIDO, SFD, NSSF, NEEC, JUVE na COMPASSION;

(ii) imeweza wafanyakazi 15 na wanafunzi 2,222 kwenda viwandani kwa ajili ya kupata mafunzo na kuongeza ujuzi na stadi zinazohitajika;

(iii) imeweza na kugharamia mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 7,605 wa fani mbalimbali; na

(iv) imetoa mafunzo ya namna ya upimaji na ufundishaji wa mitaala inayozingatia umahiri kwa Wakufunzi 653 katи ya 1,000 waliolengwa ambapo Wakufunzi hao walitoka katika Vyuo 37 vya Elimu ya Ufundu.

43. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuboresha utendaji kwa kujengea uwezo rasilimaliwatu katika taasisi za Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi nichini, kwa lengo la kuwezesha usimamizi wa utoaji wa elimu, kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeweza watumishi 31 kuhudhuria masomo katika ngazi za Stashahada, Shahada ya Kwanza na Umahiri. Vilevile imetoa mafunzo kwa watumishi 1,177 (wanawake 591,

wanaume 586) kulingana na maeneo ya ubobezi kwa lengo la kuimarisha utendaji;

(ii) imetoa mafunzo ya uongozi na maadili kwa viongozi 17 wa sekta ya umma na binafsi na wanafunzi wahitimu wapya 2,118 kupitia Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere;

(iii) imetoa mafunzo kuhusu uandishi wa maandiko ya tafiti kwa Wahadhiri 30 wenye Shahada ya Uzamivu;

(iv) imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi 2,400 kutoka Vyuo vya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi (VETA) na Vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi;

(v) imetoa mafunzo kuhusu programu ya Elimu Haina Mwisho katika vyuo 13 vya Maendeleo ya Wananchi kwa lengo la kuanzisha programu hiyo katika vyuo husika; na

(vi) imewezesha mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 25 kutoka katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na watumishi 93 kutoka Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi (VETA).

44. *Mheshimiwa Spika*, katika kuzijengea taasisi za Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi nchini uwezo wa kuandaa na kufanya tafiti zenyetija, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imewezesha kufanyika kwa tafiti 20 ukilinganisha na tafiti 14 zilizolengwa kufanyika kwa lengo la kutoa maarifa na kutatua changamoto mbalimbali za kijamii;

(ii) imewezesha kukamilishwa kwa taarifa za tafiti za Soko la Ajira katika sekta za umeme, vipodozi, madini na uchapishaji kwa ajili ya mapitio ya mitaala itakayoboresha elimu na mafunzo ya ufundi stadi; na

(iii) imeandaa mapendekezo ya tafiti na ukusanyaji wa taarifa za soko la ajira katika sekta za Biashara, Usafirishaji, Ujenzi na Mitambo na Magari Moshi.

Usimamizi na uendelezaji wa Elimu ya Juu

45. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Elimu ya Juu inayotolewa nchini inaendana na mipango ya nchi, soko la ajira la Kikanda na Kimataifa, Serikali imetekeliza yafuatayo:

- (i) imefanya tathmini ya Mitaala 72 iliyowasilishwa na Vyuo vikuu nchini na kutoa ithibati kwa mitaala 31. Aidha, mitaala 41 iko katika hatua mbalimbali za kupatiwa ithibati;
- (ii) imeandaa programu saba za masomo kati ya 15 ambazo ni: Stashahada katika Menejimenti ya Serikali za Mitaa; Shahada ya Kwanza ya Utawala wa Umma katika Maendeleo na Uongozi wa Vijana; Shahada ya Kwanza katika Ufutiliaji na Tathmini; Shahada ya Umahiri katika Maadili na Uongozi; Shahada ya Umahiri katika Ukaguzi; Shahada ya Umahiri katika Fedha za Maendeleo; na Shahada ya Uzamivu katika Utawala wa Umma kwa ajili ya kuimarisha umahiri, ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi;
- (iii) imehuisha programu mbili za mafunzo ili ziendane na uhitaji wa soko la ajira na kuandaa programu mpya mbili kwa lengo la kuongeza wigo wa mafunzo na fursa ya elimu kwa watanzania;
- (iv) imeanzisha programu mbili za shahada ya umahiri (Umahiri wa Sayansi katika Kemia ya Viwanda na Umahiri wa Sanaa katika Tathmini ya Maendeleo) kuititia Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam. Programu hizo zitaongeza wataalam watakaochochea maendeleo ya sayansi na teknolojia; na
- (v) imeanzisha programu mpya moja ya *Masters of Science in Urban Governance and Environmental Studies* – URGES kati ya tano zilizotarajiwa kuanzishwa katika Chuo Kikuu Ardhi. Uanzishwaji umezingatia uhitaji wa soko la ajira na ukuaji wa uchumi wa Tanzania, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Dunia kwa ujumla.

46. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia uzingatiaji wa sheria, kanuni, miongozo na taratibu katika usimamizi na uendelezaji wa Elimu ya Juu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) imekagua na kutambua taasisi saba za nje zilizowasilisha maombi ya kuanza kupeleka wanafunzi vyuo vya nje ya nchi (Overseas Students Recruitment Agencies - OSRA) kwa lengo la kuzisajili. Vilevile, imefanya ufuatiliaji katika Taasisi 14 zinazopeleka wanafunzi kusoma nje ya nchi kwa lengo la kuhakiki utekelezaji wa miongozo iliowekwa;
- (ii) imefanya ukaguzi katika Vyuo Vikuu 30 kwa lengo la kuhakiki ubora wa vyuo hivyo katika utoaji wa Elimu ya Juu; na
- (iii) imetathmini na kutambua tuzo 2,111 kati ya 2,531 zilizowasilishwa ambazo zilitolewa na Vyuo vya Elimu ya Juu nje ya Nchi. Aidha, maombi 420 yalirudishwa kwa waombaji ili kufanya kazi mapungufu yaliyobainika.

47. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Vyuo Vikuu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) imeratibu maombi ya wanafunzi 112,228 kati ya maombi 120,000 yaliyolengwa kwa wanafunzi kujunga na Shahada ya Kwanza katika Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu 74 nchini. Kati ya maombi hayo, jumla ya waombaji 100,620 wamedahiliwa katika Vyuo Vikuu mbalimbali. Vilevile, imeratibu udahili wa waombaji 24,839 wa ngazi ya Astashahada na Stashahada katika Vyuo Vikuu ambapo jumla ya waombaji 23,110 walidahiliwa katika kozi mbalimbali;
- (ii) imeratibu ufadhili wa masomo unaotolewa na nchi rafiki kwa wanafunzi wa kitanzania 111 (Shahada ya kwanza 9, Uzamili 74, na Uzamivu 28) kama ifuatavyo: Uingereza (12), Hungaria (23), China (72), na Mauritius (4);
- (iii) imewevesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wahadhiri na watumishi 4,664 (muda mfupi 3,782 na muda mrefu 882) kutoka katika taasisi za Elimu ya Juu;
- (iv) imeanza ukarabati wa kituo shikizi cha kufundishia na kujifunzia katika kituo cha Bagamoyo (Satellite Teaching

Facilities) kupitia Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili – MUHAS kwa lengo la kuongeza fursa za elimu ya afya na sayansi shirkishi;

(v) imeendelea na upanuzi wa Hosteli ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa ghorofa mbili (2) zaidi zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,280 ambapo hatua ya usanifu imekamilika. Kwa sasa hostel hiyo ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,840 na kukamilika kwa upanuzi huo kutawezesha kuchukua jumla ya wanafunzi 5,120;

(vi) imejenga vituo vitano vya Mikoa vya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania katika Mkoa wa Geita, Kigoma, Simiyu, Lindi na Manyara. Aidha, inaendelea na ukarabati wa Kampasi ya Zanzibar ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90;

(vii) imeendelea na ujenzi wa jengo la utawala ambalo litaongeza ofisi 50 kwa ajili ya wafanyakazi na ofisi za utafiti katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam.

Aidha, imeanza ujenzi wa maabara nne na vyumba vya madarasa kwa shule ya sekondari ya mazoezi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 920 ambapo ujenzi umefikia asilimia 12;

(viii) imeanza ujenzi wa Jengo la Shule Kuu ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika Kampasi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambapo ujenzi umefikia asilimia 15. Aidha, imeendelea na ukamilishaji wa awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kituo cha Wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa lengo la kutoa huduma mbalimbali kwa wanafunzi ambapo ujenzi umefikia asilimia 97;

(ix) imejenga nyumba 30 za wafanyakazi katika Chuo Kikuu cha Dodoma kati ya nyumba 33 zilizopangwa kujengwa ambapo kati ya hizo nyumba 13 zimekamilika na nyumba 17 zipo katika hatua za ukamilishaji. Aidha, imekarabati mabweni sita, madarasa manne (4), ukumbi wa Chimwaga na majengo 34 ya taaluma na utawala;

(x) imeendelea na upanuzi wa maabara ya Baiolojia katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa ambapo utekelezaji wake umeflikia asilimia 75; na

(xi) imeweka samani katika hosteli nne (4) zenyewe uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,024 zilizopo Kampasi Kuu ya Chuo Kikuu Mzumbe kwa lengo la kuongeza nafasi za malazi.

48. *Mheshimiwa Spika*, Serikali katika kuongeza fursa na kuimarisha mafunzo katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, imejenga jengo la maabara mtambuka lenye maabara nane na madarasa nane lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 3,200 kwa wakati mmoja ambapo ujenzi huo umeflikia asilimia 98. Vilevile, imeendelea na ujenzi na ukarabati wa madarasa, mabweni ya wanafunzi na viwanja vya michezo katika Kampasi ya Mizengo Pinda - Katavi. Aidha, imenunua vifaa vya kisasa vya maabara, mahema pamoja na kufungua shule ya udereva wa mitambo ya kilimo kwa lengo la kuimarisha mafunzo kwa vitendo.

49. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha kuwa umma unapata taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi za Elimu ya Juu nchini, Serikali imeendelea kutekeleza yafuatayo:

(i) imefanya maonesho ya 16 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ambapo jumla ya taasisi 74 za ndani ya nchi zilishiriki na wadau 55,000 walihudhuria. Maonesho hayo yalitoa fursa kwa wananchi kufahamu kazi mbalimbali zinazofanywa na Taasisi za Vyuo Vikuu;

(ii) imeendelea kutoa elimu ya ushirika kupitia redio mbalimbali ambapo vipindi 23 vilirushwa kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na vipindi 11 kupitia redio za kijamii zilizopo mkoani Kilimanjaro. Elimu iliyotolewa ililhusu ushirika na viwanda, mikakati ya kufufua ushirika, kubaini sababu za kudorora kwa vyama vya ushirika na uendeshaji wa vyama vya ushirika wa kahawa na maziwa; na

(iii) imeratibu kongamano la kitaalam la kukuza taaluma ya usimamizi wa ardhi na kukabiliana na mabadiliko ya

tabianchi 'Pursuing Knowledge Frontiers on Land Management and Climate Change Adaptation' kuitia mradhi wa Sida unaofadhiliwa na Serikali ya Sweden. Matokeo ya tafiti kuhusu ufumbuzi wa masuala mbalimbali ya kijamii ikiwa ni pamoja na mazingira, ardhi, makazi ya watu, maafa, maendeleo ya miji na vijiji, ujenzi na miundombinu yaliwasilishwa na kujadiliwa na wadau.

50. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na mataifa mengine katika uendelezaji wa Elimu ya Juu nchini, kwa lengo la kuhakikisha wataalamu wetu wanapata uzoefu na ujuzi wenye kuendana na mahitaji ya Kikanda na Kimataifa. Azma hii imefanyika kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) imehuisha Hati za Makubaliano baina ya Tanzania na nchi rafiki ambazo ni: Msambiji, Algeria, Morocco, Zimbabwe, Poland, Umoja wa Falme za Kiarabu pamoja na Jumuiya ya Madola kwa lengo la kuongeza fursa za Elimu ya Juu;
- (ii) imewezesha kusainiwa kwa hati mbili za makubaliano baina ya Tanzania na Misri, na Tanzania na Kenya zinazolenga kuimarisha na kuendeleza elimu, sayansi na teknolojia;
- (iii) imeratibu mikutano ya wadau ya kubadilishana uzoefu na kuandaa miongozo linganifu minne katika programu za Shahada ya Kwanza ya Udaktari na Shahada ya Kwanza ya Uuguzi. Aidha, inaendelea na ukamilishaji wa miongozo linganifu miwili katika programu za Shahada za Huduma, Ukarimu na Utalii na TEHAMA; na
- (iv) imeshiriki vikao vyta ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa vyta IUCEA, SADC, EAC na UNESCO kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kukuza ubora na maendeleo ya Elimu ya Juu.

51. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuongeza fursa za Elimu ya Juu kwa kuboresha huduma za upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini. Lengo la uboreshaji wa huduma ya mikopo ni kuwezesha wanafunzi wenye

sifa na uhitaji kuendelea na Elimu ya Juu bila vikwazo. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

- (i) imetoe mikopo yenyeye thamani ya **Shilingi bilioni 569** kati ya **Shilingi bilioni 570** zilizopangwa kutolewa kwa wanafunzi 148,581. Fedha hizo zimetolewa kwa wanafunzi 177,777 kati yao wanafunzi 69,333 ni wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 108,444 wanaoendelea na masomo. Kipaumbele cha utoaji wa mikopo kimezingatia waombaji wenye uhitaji mkubwa hasa wale wenye ulemavu, yatima na wanaotoka katika kaya maskini zikiwemo zilizopo chini ya mpango wa TASAF;
- (ii) imekusanya **Shilingi 156,806,093,384.02** sawa na asilimia 78 ya lengo la **Shilingi 201,319,005,000.00** zilizokadiriwa kukusanywa kutokana na mikopo iliyoiva. Makusanyo hayo yamechangiwa na mikakati iliyowekwa ya kuelimisha jamii, kuwabaini wanufaika wapya 17,977, utoaji wa ankara za mikopo mipyä zipatazo 8,848; ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria kwa waajiri wapatao 1,521; na uelimishaji jamii katika urejeshaji wa mikopo;
- (iii) imefanya maboresho katika mifumo ifuatayo: Mfumo wa Usimamizi wa Mikopo - *Integrated Loan Management Systems* (iLMS), Mfumo wa Ulipaji wa Mikopo - *Digital Disbursement System* (DIDIS), Mfumo wa Urejeshaji Mikopo - *Individuals and Employers Repayment Portals*, na Mfumo wa Usimamizi Fedha - *VoteBook Financial Management System* (VFMS). Maboresho ya mifumo hiyo yamepunguza muda wa kuomba mikopo na kurahisisha uhakiki, uchambuzi wa maombi ya mikopo na utoaji wa taarifa;
- (iv) imekamilisha uunganishaji wa Mfumo wa Mikopo (iLMS) na Mfumo wa Mishahara wa Serikali (HCMIS). Uunganishaji huu umewezesha ulinganifu wa deni la mnufaika katika kanzidata ya Bodi ya Mikopo na kanzidata ya mishahara;
- (v) imekamilisha tathmini ya awali ya namna bora ya usimamizi wa ugharimiaji wa wanafunzi wenye ufaulu wa juu na wale wanaopata ufadhilli wa nje ya nchi;

(vi) imekamilisha mapitio ya tathmini ya awali kuhusu vigezo na mahitaji ya kuongeza wigo wa mikopo kwa ngazi ya Stashahada hususan za taaluma za ujuzi wa kuajirika na kujajiri zinazoweza kuchocheara tija katika uzalishaji na mserereko wa kuelekea katika uchumi wa kat;

(vii) imeboresha mwongozo wa kutoa mikopo kupitia maoni yaliyokusanywa kutoka kwa wadau. Aidha, maandalizi ya mapitio na utafiti wa kina kwa lengo la kuboresha na kuhuisha viashiria na vigezo vya utambuzi wa uhitaji na urejeshaji wa mikopo yamekamilika;

(viii) imefanya mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Bodi kwa miaka minne iliyopita na kufanya upembuzi wa hali ilivyo sasa kwa lengo la kukamilisha Mpango Mkakati wa Tano wa Bodi ya Mikopo kwa mwaka 2022/23 – 2026/27; na

(ix) imeanzisha ofisi mpya Dar es Salaam kwa lengo kuhudumia kanda ya Mashariki. Hivyo kuongeza jumla ya ofisi za kiutendaji kuwa saba ambazo ni; ofisi ya Zanzibar, ofisi ya Dodoma na ofisi za Kanda ya Mbeya, Arusha, Mtwara, Mwanza na Dar es Salaam.

52. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha utoaji wa elimu na mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini, Serikali imeendelea kutekeleza yafuatayo:

(i) imewezesha upanuzi wa maabara ya viumbehai katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa ambapo ujenzi umefikia asilimia 80. Kukamilika kwa mradi huo kutaimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa vitendo;

(ii) imeanza ujenzi wa maabara kuu ya kemia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambayo itatumika kwa ajili ya utafiti na kutoa huduma za kupima sampuli za viwandani na hivyo kuongeza wigo wa wanafunzi kujifunza kwa vitendo;

(iii) imeanza hatua za awali za ujenzi wa miundombinu ya Kituo cha Utafiti wa Viumbe Maji Baridi yaani *Multi-Disciplinary Freshwater Research Centre - Chato*, Mkoani Geita kupitia Chuo

Kikuu cha Dar es Salaam; imeboresha na kuendeleza Shamba la Mafunzo kwa kupanda miche 500 ya michikichi, malisho ya ng'ombe, kuweka uzio, kufunga mfumo wa umwagilaji wa matone, ukarabati wa mabwawa matano ya samaki na mabwawa 12 madogo kwa ajili ya vifaranga vya Samaki katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo;

(iv) imejenga maabara katika ndaki ya sayansi asilia na hisabati ya Chuo Kikuu Dodoma; na

(v) imekamilisha ujenzi wa kituo cha Umahiri cha Afrika Mashariki cha Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu cha Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili Kampasi ya Mloganzila kilichozinduliwa rasmi Desemba, 2021 na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kituo hicho kitaongeza mafunzo na huduma za kibingwa katika matibabu ya moyo na mishipa ya damu.

53. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kuitia taasisi za Elimu ya Juu imeendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalam katika kazi za ujenzi na ukarabati wa majengo mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) imetoa ushauri wa kitaalam kuhusu ujenzi wa nyumba za Bunge eneo la Kilimani - Dodoma; majengo ya Mchapishaji Mkuu wa Serikali, Kituo cha Taifa cha Kukabiliana na Maafa – Dodoma; majengo ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Maji na Wizara ya Nishati;

(ii) imetoa ushauri wa kitaalam kuhusu ukarabati wa majengo ya Balozi za Tanzania katika nchi za DRC, Rwanda, Oman, Saudi Arabia, Msumbiji, Malawi, Burundi na Marekani, pamoja na Chuo cha Ualimu Ndala – Tabora na Chuo cha Ualimu Mpwapwa – Dodoma; na

(iii) imetoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uimara wa udongo, kokoto na lami zinazotumika katika ujenzi wa miundombini mbalimbali na kupima ubora wa maji, usanifu wa miradi ya maji na ujenzi.

54. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha miradi ya ujenzi na ukarabati inafanyika kwa ufanisi kwa kutumia wataalam wa ndani, Serikali kuititia taasisi za Elimu ya Juu imeendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalam kuhusu usanifu na usimamizi kama ifuatavyo:

- (i) usanifu na usimamizi wa kampasi ya Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Julius K. Nyerere – Butiama;
- (ii) usanifu na usimamizi wa vituo vya michezo katika miji ya Dodoma, Geita na Dar es Salaam, Kituo cha mafunzo ya michezo '*Centre of Excellence and Academy*' katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya pamoja na kituo cha taarifa za afya '*Health Promotion Centre*' – Singida;
- (iii) usanifu na usimamizi wa mradi wa ujenzi katika vyuo vinne vya VETA ambavyo ni Kasulu, Ruangwa, Kongwa na Nyasa, Vyuo 20 vya Maendeleo ya Wananchi (FDC), Vyuo vya Ualimu 14 na stendi kuu ya mabasi ya Kahumo -Wilayani Chato - Geita;
- (iv) usanifu na usimamizi wa miradi ya ujenzi katika vyuo vitano (5) vya VETA pamoja na jengo la madarasa la Chuo cha Ufundji Arusha; na
- (v) usanifu na usimamizi wa ujenzi wa nyumba za watu binafsi pamoja na upimaji wa udongo kwa makampuni ya ujenzi.

55. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika taasisi za Elimu ya Juu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) imenunua *Backup Software* katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam na kitunzia taarifa (data storage) katika mkongo wa Taifa na kuongeza uwezo wa mtandao kutoka 50 Mbps hadi 60 Mbps. Aidha, imetoa mafunzo kwa wanafunzi 1,391 wa mwaka wa kwanza kuhusu ulinzi wa kimtandao;

(ii) imeboresha kiungo cha chelezo cha mtandao “internet backup link” hadi kufikia 100 Mbps katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili;

(iii) imeweka mfumo wa *wireless* katika Maktaba ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa mtandao kwa watumiaji. Aidha,imeendelea na uboreshaji wa miundombinu ya elimu kwa njia ya kielektroniki kwa kuongeza viunganisho vya “fibre optic” kutoka maeneo ya Kampasi ya Muhimbili; na

(iv) imeendelea kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Vyuo Vikuu (University Management Information System - UMIS) unaotumika katika ukusanyaji na utoaji wa takwimu na taarifa mbalimbali katika taasisi za Elimu ya Juu.

56. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuzingatia masuala mtambuka ikiwa ni pamoa na HIV/UKIMWI, Rushwa na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza katika utoaji wa elimu kwa ngazi zote za elimu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kwa Walimu 3,800 wa shule za Msingi na Sekondari kuhusu stadi za maisha zinazozingatia afya ya uzazi, jinsia, na VVU na UKIMWI kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kufundisha wanafunzi stadi za maisha;

(ii) imetoa mafunzo kwa Wanachuo 1,819 wanaosoma usimamizi na uongozi wa elimu kuhusu stadi za maisha zinazozingatia afya ya uzazi, jinsia, VVU na UKIMWI, masuala ya rushwa na namna ya kupambana na rushwa kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kufundisha wanafunzi stadi za maisha;

(iii) imetoa mafunzo kwa washiriki 4,174 (wafanyakazi 405 na wanafunzi 3,769) katika taasisi za Elimu ya Juu kuhusu Rushwa, Unyanyasaji wa Kijinsia, VVU na UKIMWI pamoa na huduma ya ushauri nasaha;

(iv) imeandaa moduli nne za kufundishia elimu ya stadi za maisha zinazozingatia afya ya uzazi, elimu ya jinsia, VVU na

UKIMWI ambapo moduli hizo zitatumika kuendesha mafunzo kwa walimu kazini; na

(v) imetoa elimu ya VVU na UKIMWI, rushwa na majanga mbalimbali kwa Watumishi 123. Pia, wateja waliohudhuria mafunzo walipata huduma ya ushauri nasaha na uelewa wa masuala ya rushwa na namna ya kupambana na rushwa.

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya Uviko 19

57. Mheshimiwa Spika, Serikali katika kupambana na athari za ugonjwa wa UVIKO 19 kuititia sekta ya elimu iliidhinisha afua tatu muhimu za kukabiliana na athari hizo kuititia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVICO – 19. Katika utekelezaji wa mpango huo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitekeleza maeneo matatu ambayo ni; Kuboresha utoaji wa elimu maalum, Kuongeza fursa na ubora wa Elimu ya Ualimu, na Elimu ya Ufundis na Mafunzo ya Ufundis Stadi. Kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo:

Afua za Elimu Maalum

(i) imeandika na kuchapa nakala 57,756 za vitabu vya Kiada, Kidato cha 1 - 4 vya maandishi yaliyokuzwa kwa masomo ya *Biology, Physics, Chemistry, Mathematics, Agriculture, Home Economics, Kiswahili, Civics, Information and Computer Studies, Geography, History* na *English*. Aidha, imeandika, kuchapa na kusambaza vitabu vya nuktanunu nakala 9,178 kwa masomo hayo ya sekondari kwa ajili ya wanafunzi 353 wasioona. Vitabu hivyo vimeimarisha ujifunzaji na ufundishaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(ii) imewezesha ununuvi vifaa vya wanafunzi wa Elimu ya Juu wenye mahitaji maalumu katika Vyuo Vikuu 11 vya Umma kwa lengo la kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji;

Afua za Elimu ya Ualimu

(iii) imewezesha ujenzi wa madarasa 41, kumbi za mihadhara tatu na mabweni 15 katika Vyuo vya Ualimu 23 vilivyonufaika na mpango huo. Ujenzi wa miundombinu hiyo utasaidia katika

kupunguza msongamano wa wanafunzi na hivyo kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

Afua za Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi

(iv) inaendelea kuwezesha ujenzi wa vyuo vipyta vya ufundu stadi vya Mikoa vinne na ununuzi wa samani katika Vyuo vya Wilaya 25 vya VETA. Aidha, inaendelea na ununuzi na usambazaji wa vifaa na mashine za kufundishia katika vyuo 34 vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs). Utekelezaji wa afua hizo unalenga katika kuongeza fursa na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Ununuzi na usambazaji wa vifaa na mashine za kufundishia katika Vyuo 34 vya Maendeleo ya Wananchi utekelezaji umefikia asilimia 30;

(v) inaendelea na ujenzi wa jengo la maabara, madarasa na ofisi katika Chuo cha Ufundu Arusha (ATC) kwa lengo la kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji kwa vitendo pamoja na kuimarisha mazingira ya watumishi kufanya kazi; na

(vi) inaendelea na ujenzi wa mabweni mawili katika chuo cha Ualimu wa Ufundu Morogoro kwa lengo la kuongeza fursa katika uandaaji wa walimu wa ufundu na mafunzo ya ufundu stadi.

Usimamizi na uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

58. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha uwezo wa watumishi kusimamia, kuratibu na kuendeleza Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoka katika Halmashauri 184 za Tanzania Bara kwa lengo la kuboresha uratibu wa masuala ya teknolojia na ubunifu hususan katika kuibua, kutambua na kuwaendeleza wavumbuzi na wabunifu wachanga nchini;

(ii) imewajengea uwezo watumishi 182 kati ya 300 walioengwa katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ili kuongeza viwango vya ubora katika ufundishaji na utawala kama sehemu ya maandalizi ya kupata ithibati ya viwango vya

ubora vya kimataifa (*International Organization for Standardization - ISO Certification*);

(iii) imewezesha jumla ya watumishi 170 wa taasisi zinazohusika na uendelezaji wa sayansi, teknolojia na ubunifu nchini kuhudhuria masomo ya muda mfupi na muda mrefu katika kozi mbalimbali ambapo kati yao watumishi 31 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi 139 mafunzo ya muda mrefu (Shahada ya Uzamivu 83, Shahada ya Uzamili 40, Shahada ya Kwanza 12 na Astashahada wanne); na

(iv) imetoa mafunzo kwa wabunifu 82 waliopatikana kuitia Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) katika utafutaji wa masoko, taratibu za usajili wa hatimiliki, ujasiriamali pamoja na kuandaa michanganuo ya biashara ili ubunifu uwe fursa ya ajira na kipato kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

59. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa kazi za bunifu na matokeo ya tafiti yanatambuliwa Kitaifa na Kimataifa na kuendelezwa kwa lengo la kuongeza kasi ya matumizi yake katika kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imewezesha bunifu 26 kuingia sokoni kati ya bunifu 200 zinazoendelezwa na Serikali ambazo zilipatikana katika Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu mwaka 2019 hadi 2021. Bunifu hizo zitaleta tija ya uzalishaji na huduma katika sekta ya Kilimo, Maji, Nishati, Madini, Afya, TEHAMA na Elimu;

(ii) imewaunganisha wabunifu sita na Makampuni ya Kibashara kupitia Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia ili waweze kupata mbinu na uzoefu wa namna ya kuanzisha na kuendesha biashara na makampuni; na

(iii) imetambua teknolojia mpya 90 zilizozalishwa nchini na hivyo kufanya jumla ya teknolojia zilizotambuliwa hadi sasa

kufikia 479 kwa lengo la kuwa na kanzidata ya kitaifa itakayorahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu kuhusu teknolojia na bunifu nchini.

60. Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika taasisi zinazosimamia maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu nchini. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

- (i) imeanzisha vitalu nyumba (*screen houses*) vinne katika Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia vyenye ukubwa wa mita za mraba 4,900 kwa ajili ya tafiti za kilimo, kutoa mafunzo kwa vitendo, kufanya majaribio ya teknolojia zilizobuniwa na watafiti pamoja na kuzalisha mazao mbalimbali;
- (ii) imeendelea na ujenzi wa madarasa matano yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 50 kila moja na mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 160 katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam Kampasi ya Myunga ambapo ujenzi umefikia hatua ya umaliziaji. Aidha, imeweka samani katika jengo la kufundishia la Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam Kampasi Kuu; na
- (iii) imeendelea na ujenzi wa miundombinu katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kama ifuatavyo: maktaba yenye uwezo wa kuchukua watumiaji 2,500 kwa wakati mmoja; mabweni ya wanafunzi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800; na maabaraza za kufundishia zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 600. Ujenzi wa majengo hayo upo katika hatua mbalimbali.

61. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa sayansi, teknolojia na ubunifu nchini, kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) imesimamia utekelezaji wa mradi wa vituo vinne vya umahiri "*African Centres of Excellence (ACE - II)*" katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya

Sayansi na Teknolojia. Lengo la kuanzishwa kwa vituo hivyo ni kujenga uwezo katika utoaji wa Elimu ya Juu na utafiti katika maeneo ya Afya na Biolojia ya Molekuli; Kilimo; Maji na Nishati Jadidifu;

(ii) imewezesha kuanzishwa kwa kumbi za ubunifu 10 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vya: Chisalu - Dodoma, Kisangwa - Mara, Sengerema - Mwanza, Kasulu - Kigoma, Katumba - Mbeya, Kilwa Masoko - Lindi, Mto wa Mbu - Arusha, Newala - Mtwara, Kiwanda – Tanga, na Njombe. Lengo la kuanzishwa kwa kumbi hizo ni kuimarisha mfumo wa uendelezaji wa wabunifu;

(iii) imeratibu ushiriki wa nchi katika Mkutano Mkuu wa 65 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA) uliofanyika Vienna, Austria mwaka 2021 ambapo Mtafiti Mtanzania (Ndugu Salum Faki Hamad) kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI) alipata tuzo ya uzalishaji wa mbegu bora ya mpunga inayostahimili chumvi na magonjwa;

(iv) imeimarisha uhusiano kati ya wadau wa kimataifa, kikanda na kitaifa katika masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ambapo wadau wa kimataifa wameongezeka kutoka washirika 39 hadi 44, kanda ya Afrika Mashariki wameongezeka kutoka 42 hadi 46 na ndani ya nchi kutoka 23 hadi 29. Ushirikiano huo umekuza ujuzi na maarifa katika tafiti mbalimbali zinazolenga kutatua changamoto za jamii na kiuchumi;

(v) imeshirikiana na mradi wa South African Innovation Support (SAIS) ili kuendeleza kazi za ubunifu nchini ambapo ushirikiano huo umeziwezesha kampuni changa mbili za Fundi App na *Exam Net* kushiriki katika mashindano yanayo julikana kama Slush 2021 yaliyofanyika Helsinki - Finland. Kupitia mashindano hayo, mshiriki mmoja (Ndugu Godfrey Gervas Kilimwomeshi) kutoka Tanzania aliibuka mshindi wa jumla na kupata zawadi ya vocha yenyeh thamani ya EURO 3,000; na

(vi) imefanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi 10 ya utafiti inayotekelizwa kwa ushirikiano kati ya Shirika la Kimataifa la

Nguvu za Atomiki - IAEA kuitia Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania katika Sekta ya Maji, Afya, Kilimo na Mifugo na kubaini kuwa utekelezaji wa miradi hiyo unafanyika kulingana na makubaliano.

62. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu uendelezaji wa sayansi, teknolojia na ubunifu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imezalisha na kusambaza taarifa za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu zinazohusiana na uhawilishaji na uendelezaji wa Teknolojia kuitia mabango, vijarida viwili, vipeperushi vinne, *factsheet* moja na *bulletin* moja. Taarifa hizo zipo katika Lugha ya Kiingereza na Kiswahili; na

(ii) imezalisha na kusambaza *infographics* na taarifa za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya habari kwa mchanganuo ufuataao: *Infographics* 489; taarifa nne za utafiti, moja ya ubunifu na makala fupi 47.

63. Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imeendelea kuimarisha na kuhimiza matumizi ya TEHAMA katika taasisi zinazosimamia uendelezaji wa sayansi, teknolojia na ubunifu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeboresha na kuimarisha miundombinu na mfumo wa TEHAMA wa Menejimenti ya Utafiti na Ubunifu kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kuchakata maombi ya vibali vya utafiti, ufadhilli wa miradi na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za watafiti na wabunifu; na

(ii) imeandaa vipaumbele vya utafiti nchini kwa lengo la kutoa mwelekeo wa shughuli za utafiti kulingana na Mpango wa Tatoo wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Taifa.

64. Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Tume ya Nguvu za Atomiki imeendelea kuongeza miundombinu na kuhakiki vifaa vya mionzi kwa lengo la kudhibiti athari zitokanazo na mionzi ya nyuklia isiyo salama katika jamii na mazingira kwa ujumla kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa maabara changamano itakayoboresha utoaji wa huduma na kuongeza ufanisi katika kudhibiti matumizi salama ya mionzi na kuendeleza teknolojia ya nyuklia ambapo ujenzi umefikia asilimia 95;

(ii) imeendelea na ujenzi wa maabara na ofisi katika Kanda ya Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza. Kukamilika kwa ujenzi huo kutasogezza huduma za matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia kwa wananchi na wafanyabiashara ambapo ujenzi upo katika hatua mbalimbali;

(iii) imefanya matengenezo na kuhakiki vifaa na mitambo 40 inayotumia teknolojia ya nyuklia ili kuimarisha ubora wa vifaa, usalama wa wafanyakazi na jamii inayowazunguka; na

(iv) imefanya matengenezo na kuhakiki vifaa 40 vya nyuklia kwa matumizi ya ujenzi na viwandani (nuclear gauges and industrial), na mashine za kupima magonjwa (medical x-rays equipment).

65. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kuititia Tume ya Nguvu za Atomiki imeendelea kuimarisha usimamizi, udhibiti na matumizi ya mionzi ya nyuklia nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imesajili vituo vipyta 44 vinavyotumia vyanzo vya mionzi nchini kwa lengo la kuimarisha matumizi salama ya mionzi;

(ii) imepokea na kutathmini maombi 514 ya umiliki, utumiaji na usafirishaji wa vyanzo vya mionzi kati ya lengo la kupokea vibali 600;

(iii) imesajili wataalam 109 wa kutoa huduma za mionzi kwa wagonjwa ili kudhibiti matumizi salama ya mionzi; na

(iv) imetoea leseni 375 za kumiliki na kutumia vyanzo vya mionzi ikilinganishwa na leseni 333 zilizotolewa katika mwaka wa fedha 2020/21. Leseni hizo zimetolewa kwa mchanganuo ufuatao:

- a. kumiliki na kutumia vyanzo vya mionzi (329);
- b. uingizaji wa vyanzo vya mionzi nchini (36);
- c. kusafirisha vyanzo vya mionzi nje ya nchi (1);
- d. usafirishaji wa vyanzo vya mionzi ndani ya nchi (7);
- e. uchunguzi wa madini ya urani (1); na
- f. upembuzi na ujenzi wa mgodi wa madini ya Urani (1).

66. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki imeendelea kuimarisha usalama wa jamii ikiwemo kulinda afya za wafanyakazi wanaotumia teknolojia ya nyuklia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imekusanya mabaki ya vyanzo vya mionzi kutoka katika vituo vinne ambavyo ni: TANROADS – Kagera (1); Geita Gold Mine (1); na *Estim Construction Company* Dar es Salaam (2) na kuyahifadhi mabaki hayo katika kituo maalum cha kuhifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi. Jumla ya mabaki ya vyanzo vya mionzi 149 yameendelea kuhifadhiwa katika Jengo la Kuhifadhi Mabaki ya Vyanzo vya Mionzi (CRWMF);

(ii) imekagua vituo 14 vinavyomiliki na kutumia vyanzo vya mionzi kwa ajili ya kudhibiti hali ya usalama kwa wagonjwa, wafanyakazi na jamii;

(iii) imepima viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,065 wanaofanya kazi katika vyanzo vya mionzi kati ya wafanyakazi 1,920 walio lengwa ambapo ilibainika kuwa viwango vya mionzi vilivyopo vinakubalika kisheria. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 107 ya wafanyakazi waliosajiliwa katika sekta ya mionzi nchini;

(iv) imepima sampuli 31,371 za vyakula, mbolea, na bidhaa za tumbaku ambapo kati ya hizo vyakula kutoka nje ya nchi 9,732, vyakula vinavyosafirisha nje ya nchi 17,864, mbolea 924, na tumbaku na bidhaa nyingine 2,851; na

(v) imepokea na kuchanganua sampuli 510 za mazingira ili kutambua viasili vya mionzi na kuwalinda wananchi na mazingira kwa ujumla.

Kuimarisha na Kuendeleza Tafiti na Matumizi ya Matokeo yake katika Ajenda ya Maendeleo

67. Mheshimiwa Spika, utafiti ni nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo, kutatua changamoto mbalimbali za kijamii na kiuchumi pamoja na kuibua maarifa mapya. Serikali kupitia taasisi za elimu, mafunzo, sayansi na teknolojia imeendelea kuimarisha na kuendeleza tafiti na matumizi ya matokeo yake katika kuleta maendeleo na kuboresha ustawi wa jamii. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imewezesha kufanyika kwa tafiti mbalimbali kama ifuatavyo:

- (i) imefanya jumla ya tafiti 143 ukilinganisha na lengo la tafiti 129 zilizolengwa kufanyika katika taasisi za Elimu ya Juu kwa kushirikiana na wadau ndani na nje ya nchi. Tafiti hizo zipo katika maeneo ya elimu, mazingira, kilimo, afya, madawa, jinsia, afya za wanyama, samaki, utengenezajiwa bidhaa zitokanazo na mmea ya asili, kilimo endelevu cha mazao mbalimbali, mabadiliko ya tabianchi, misitu na rasilimalimaji. Aidha, imeandaa mapendekezo 39 ya maeneo ya kufanyia tafiti (research area) katika maeneo ya vipaumbele vya Taifa;
- (ii) imeendelea kugharimia tafiti na mafunzo katika Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia kupitia miradi 24 ya utafiti kwa lengo la kuzalisha wataalam na teknolojia za kisasa katika maeneo ya Kilimo, TEHAMA, Chakula na Lishe; na
- (iii) imeendelea kugharimia miradi 32 ya utafiti, ubunifu na miundombinu ya utafiti (tafiti 13, bunifu 16 na miundombinu 3) inayoratibiwa kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH). Matokeo ya miradi hiyo yatasaidia kutatua changamoto mbalimbali katika jamii.

68. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa tafiti na maandiko ya kitaaluma yanatunzwa kwa rejea na matumizi kwa utatuzi wa changamoto mbalimbali za kijamii, Serikali imeendelea kutekeleza yafuatayo:

- (i) imeandaa jumla ya machapisho 2,498 ukilinganisha na lengo la machapisho 1,402 katika taasisi za Elimu ya Juu

ambayo yapo katika majarida ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;

(ii) imetambua matokeo ya tafiti na vifaa vya kufanya tafiti katika Taasisi za umma 154 ambazo ni: Utafiti na Maendeleo, Wakala za Serikali na Taasisi za Elimu ya Juu. Vilevile, imeandaa taarifa inayoinisha matokeo ya tafiti hususan zenyenye manufaa ya moja kwa moja kwa jamii pamoja na uwezo wa vifaa na wataalam katika taasisi hizo; na

(iii)imeandaa mapendekezo ya tafiti na ukusanyaji wa taarifa za soko la ajira katika sekta za biashara, usafirishaji, ujenzi na mitambo na magari moshi.

69. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia taasisi za Elimu ya Juu imeendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalam na ugani katika nyanja za kilimo, ufugaji, ushirika, utawala, uongozi na ardhi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa kazi za maendeleo ya jamii kama ifuatavyo:

(i) imetoa huduma za ushauri na ugani kwa mashirika, wakulima, wafugaji pamoja na kutoa mafunzo ya utengenezaji wa mitego ya kunasa panya kwa wakulima wa mpunga na ufugaji bora wa samaki;

(ii) imetoa huduma za kijamii na ushauri kuhusu usimamizi na uendeshaji wa vyama vya ushirika kwa washiriki 6,878 (wanawake 6,239 na wanaume 4,239) kutoka vyama vya ushirika na vikundi vya wadau mbalimbali;

(iii) imetoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo ya utawala, uongozi, fedha na biashara, sheria na ujasiri amali;

(iv) imetoa huduma za urasimishaji ardhi kwa wakazi wa kata tisa za Wilaya ya Mbarali - Mbeya ambapo jumla ya viwanja 29,400 vimepimwa na hati 3,020 zimetolewa kwa wananchi na

(v)imeendesha mafunzo ya usimamizi wa ardhi kwa viongozi wa mitaa na wataalam 207 kutoka katika Halmashauri ya Kilwa, Mtama na lleje za Mkoa wa Lindi na Songwe.

D. TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)

70. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO imetekeleza yafuatayo:

- (i) imeshiriki katika Mkutano Mkuu wa 41 wa UNESCO uliofanyika nchini Ufaransa mwezi Novemba, 2021. Katika mkutano huo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichaguliwa kuwa Mjumbe wa Bodi Tendaji ya UNESCO;
- (ii) imefanikisha Lugha ya Kiswahili kuwa Lugha ya kwanza Afrika kutambuliwa na Baraza la Umoja wa Mataifa na kupewa siku maalum ya tarehe 7 Julai kuadhimishwa kila mwaka;
- (iii) imetoa mafunzo kuhusu elimu ya sayansi na hisabati inayozingatia jinsia kwa watumishi 41 wa sekta ya elimu kutoka Pemba na Unguja;
- (iv) imeratibu upatikanaji na ushiriki wa vijana 80 katika shindano la kimataifa masuala ya Urithi wa Dunia liliolohusisha nchi ambazo ni Wanachama wa UNESCO katika Kanda ya Afrika ikiwa ni muendelezo wa kusheherekeea Siku ya Urithi wa Dunia – Afrika;
- (v) imewezesha utekelezaji wa mradi wa *Strengthening the Contemporary Dance Scene in East Africa* kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali liitwalo MUDA Africa kupitia Mkataba wa UNESCO wa mwaka 2005 unaohusu *Protection and Promotion of the Diversity of Cultural Expressions*;
- (vi) imefanikiwa kusimamia na kuratibu utekelezeji wa miradi sita iliyoafadhiliwa na Shirika la Elimu Duniani la UNESCO kama ifuatavyo:
 - a. Mradi wa Kukabiliana na Matendo Potofu ya Unyago "Confronting Gender Disparity on Girls' Initiation Malpractice" ambapo Wadau 40 kutoka Wilaya ya Masasi katika Mkoa wa Mtwara walishiriki;

- b. Mradi wa Mafunzo kuhusu Utoaji Elimu ya Sayansi na Hisabati kwa kuzingatia jinsia "*Training on Gender Responsive STEM Education*" yalifanyika mkoani Morogoro ambapo washiriki 43 kutoka Zanzibar na washiriki 40 kutoka Tanzania Bara walipata fursa ya kushiriki;
- c. Mradi wa Kuimarisha Radio za Kijamii "*Empowering Community Radios: Enhancing Content Diversity and Community's Participation*" ambapo washiriki 35 kutoka mikoa tisa (9) ya Tanzania Bara ambayo ni Geita, Simiyu, Mwanza, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Iringa na Mtwara, na washiriki 22 kutoka Unguja na Pemba walipewa mafunzo kuhusu kuimarisha maudhui na ushirikishaji wa jamii kupata habari;
- d. Mradi wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia "*Fighting Against Physical and Sexual Violence in the Local Communities*" uliohusisha washiriki 70 kutoka Mkoa wa Tabora walipata fursa ya kujadili, kujifunza njia mbalimbali ambazo wanaweza kutumia katika kutoa elimu kwa jamii kuhusu namna ya kushiriki katika kупинга vitendo vya ukatili wa kijinsia;
- e. Mradi wa Uhifadhi wa Magofu ya Kale ya Kihistoria ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara; na
- f. Mradi wa Uhifadhi na Utunzaji wa Michoro ya Miambani ya Kondoa.

E. MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

71. *Mheshimiwa Spika*, Kazi kubwa itakayofanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 itakuwa ni kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 kwa minajili ya kufanya maamuzi kuhusu mambo kadhaa ambayo Sera imeainisha lakini hayajatekelezwa. Kwa mfano, Sera inaainisha kwamba elimu ya lazima, yaani *compulsory education*, itakuwa ni ya miaka kumi, lakini bado tunatoa elimu ya lazima ya miaka saba. Tunatarajia kuwa kabla ya mwisho wa mwaka huu uchambuzi utakuwa umefanyika na kukamilika kuhusu Sera hii ili maamuzi yawewe

kufanyika kuhusu utekelezaji. Pamoja na uchambuzi huo, juhudii zitaendelea za kukusanya maoni ya wadau wote ili maamuzi yatakapofanyaika yazingatia maoni ya wadau wote na uchambuzi wa kitaaamu. Mapitio ya Sera yatatoa dira ya mabadiliko yatakayohitajika katika Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978. Tunataraja pia kuwa ifikapo Desemba 2022 Wizara itakuwa imekamilisha rasimu ya mabadiliko ya mitaala itakayozingatia maoni ya wadau na mwelekeo wa Sera ya Elimu utakaokuwa umependekezwa. Zoezi hilo litazingatia sana uboreshaji wa elimu na uthangeza sana elimu ya ufundi na ujuzi itakayomsaidia mhitimu kuweza kujiajiri na kuajirika.

72. Mheshimiwa Spika, mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo na mabadiliko ya mitaala ambayo Serikali inakusudia kukamilisha yataleta mageuzi makubwa ya elimu kupata kutokea hapa nchini. Tunatoa wito kwa wadau kuendelea kutoa maoni yao kwa sababu azma ya Serikali ni kufanya mageuzi makubwa yanayozingatia matakwa ya wananchi, kuongeza ubora wa elimu, kuwezesha wahitimu kujiamini, kuajirika na kujiajiri na pia kuwawezesha wahitimu kumudu utandawazi na kukidhi mahitaji ya uchumi wa nchi yetu. Kwa ujumla mambo yafuatayo yataangaliwa na kuzingatiwa:

- A. Mapitio ya Sera;
- B. Mapitio ya Sheria;
- C. Mabadiliko ya Mitaala;
- D. Idadi (mahitaji) ya Walimu, Wakufunzi na Wahadhiri;
- E. Ubora Stahiki wa Walimu, Wakufunzi na Wahadhiri;
- F. Mahitaji ya Miundombinu; na
- G. Mahitaji ya Vitendeakazi.

Maswala haya saba ni budi yazingatiwe ili kuhakikisha kwamba mageuzi ya elimu tunayoyatarajia yatakuwa kweli yanakidhi mahitaji yetu.

73. Mheshimiwa Spika, pamoja na mapitio ya sera na mabadiliko makubwa ya mitaala Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/23, utajielekeza katika kutekeleza maeneo ya kimkakati yafuatayo:

- (i) kupanua na kuimarisha elimu ya ufundi nchini;
- (ii) kuhimiza uandishi, uchapishaji na uchapaji wa vitabu hapa nchini. Moja ya hatua zitakazo chukuliwa ni Serikali kulipia gharama za uchapishaji na uchapaji wa riwaya bora kila mwaka itakayoandikwa na Mtanzania ili kusaidia na kuimarisha juhudzi za uandishi hapa nchini;
- (iii) kutekeleza juhudzi za kukuza sayansi hapa nchini kwa kufanya mambo yafuatayo. Kwanza, kutoa ufadhilli wa asilimia mia wa kulipia gharama za masomo za chuo kikuu kwa wanafunzi watakaoongoza katika mitihani ya masomo ya sayansi ya kidato cha sita. Pili, katika kutekeleza llani ya CCM, kutoa *scholarship* kwa Watanzania watakaofanya vizuri sana kwenye masomo yao ya vyuo vikuu kwenye nyanja za sayansi, teknolojia na tiba ili kusoma kwenye vyuo vilivyo bora zaidi duniani kama vile MIT. Tatuhii, kuhimiza utafiti wa kisayansi na tiba kwenye vyuo vyetu vikuu kwa kutoa tuzo ya shilingi milioni hamsini kwa mhadhiri ye yeyote atakaeweza kuchapisha matookeo ya utafiti wake kwenye majarida yenyehadhi ya juu kabisa ya sayansi na ya elimu ya tiba. Nne, kuhamisha sekta binafsi na wadau mbalimbali kufadhilli Watanzania kwenda kusoma kwenye vyuo bora kabisa duniani. Tayari mikakati imeanza kuandaliwa kwa kushirikiana na Bwana Rupin Rajan na wadau wengine ili kufanikisha azma hii. Kama nitakavyoeleza, tayari benki ya NMB imekubali kutenga Shillingi billioni mia mbili (200) kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi.
- (iv) kuongeza wigo wa shule za ufundi za elimu msingi na sekondari kwa lengo la kuwajengea vijana wetu stadi na maarifa yanayohitajika katika soko la ajira; na
- (v) kuimarisha ujifunzaji kwa vitendo katika taasisi za Elimu ya Juu kwa kuanza kujenga kampasi za vyuo zenye kujielezeza katika mafunzo kwa vitendo katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

74. *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa maeneo hayo ya kimkakati utaenda sambamba na utekelezaji wa vipaumbele vifuatavyo:

a. Kuhuishsha Sera, Sheria na Miongozo ya Utoaji wa Elimu Nchini

75. *Mheshimiwa Spika*, mapitio ya Sera ya Elimuna Mafunzo ya mwaka 2014 yataruhusu mapitio ya Sheria ya Elimu Sura 353 na mitaala ya Elimu katika ngazi zote za elimu na mafunzo kwa lengo la kuhakikisha kuwa inakidhi mahitaji ya sasa na wakati ujao Kitaifa na Kimataifa. Sambamba na mapitio ya sera na sheria, Serikali itaandaa miongozo mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

- (i) mwongozo wa usimamizi na utawala bora katika elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (ii) mwongozo wa kuwatambua na kuwaendeleza wanafunzi wenyе vipawa na vipaji katika shule za msingi na sekondari;
- (iii) mwongozo wa usimamizi na ufuutiliaji wa elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi kwa lengo la kuboresha mafunzo na usimamizi wa elimu katika ngazi husika; na
- (iv) mwongozo wa kuanzisha, kukarabati na kuendesha maktaba kwa lengo la kuweka utaratibu unaofaa wa kuanzisha, kukarabati na kuendesha maktaba nchini.

b. Kuendelea Kuhakikisha Watoto wote wenyе Umri wa Kwenda Shule Wanapata Fursa

76. *Mheshimiwa Spika*, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wenyе sifa za kujiunga katika ngazi mbalimbali za elimu nchini wakiwemo wanafunzi wenyе mahitaji maalum wanapata fursa sawa na kuhitim. Azma hiyo, itafikiwa kwa kutekeleza afua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

- (i) itafanya ufuutiliaji kwa lengo la kubaini watoto wote wenyе umri wa kwenda shule wanapata fursa sawa ya elimu;
- (ii) itaendelea kutatua changamoto za utoaji wa elimu nchini pamoja na kuhakikisha wanafunzi wote wanapata fursa sawa ya elimu;
- (iii) itaendelea kuimarisha mazingira ya ushiriki wa wadau katika utoaji wa elimu nchini; na

(iv) itaendelea kuimarisha ushiriki wa mtoto wa kike katika elimu kwa kutatta changamoto zinazomkabili ikiwa ni pamoja na ulinzi wa mtoto aendapo na atokapo shulenii.

c. Kuendelea Kuongeza Fursa na Ubora wa Elimu ya Awali, Elimumsingi na Sekondari, na Elimu ya Ualimu

77. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu katika ngazi ya elimu ya awali, elimumsingi, sekondari na elimu ya ualimu na kutoa mafunzo kwa kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) itaendelea kutekeleza sera ya elimu bila ada katika ngazi ya elimu ya awali na elimumsingi kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wote wanapata fursa ya elimu;

(ii) itasajili taasisi za elimu 500 (shule za awali na msingi 350, shule za sekondari 148 na vyuo vya ualimu 02) ili kuongeza fursa ya upatikanaji wa Elimu;

(iii) itakamilisha mfumo wa usajili wa shule kwa njia ya kielektroniki (online school registration system) kwa lengo la kurahisisha utaratibu wa usajili wa shule;

(iv) itatoa mafunzo ya Mwongozo wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shulenii (School WASH Guidelines) kwa Waratibu wa Mikoa 17 na Halmashauri 86 pamoja na Wathibiti Ubora wa Shule 61 kutoka mikoa ya Mwanza, Mara, Simiyu, Kagera, Kigoma, Shinyanga na Tabora ili kuimarisha usimamizi ufuatilaji katika ujenzi wa vyoo na miundombini ya maji shulenii;

(v) itatoa mafunzo kwa walimu 3,600 wa shule za sekondari kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Shule Salama pamoja na mafunzo ya uelewa kuhusu usawa na ukatili wa kijinsia;

(vi) itawezesha ujenzi wa madarasa yenyewe uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 katika Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM); na

(vii) itaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa Ofisi ya Mamlaka ya Elimu Tanzania Jijini Dodoma ili kusogea huduma karibu na wananchi.

78. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania itatekeleza yafuatayo:

(i) itawezesha ujenzi wa madarasa 90 katika shule 20 za msingi na 10 za sekondari ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(ii) itawezesha ujenzi wa matundu ya vyoo 1,200 katika shule 30 za msingi na 20 sekondari zenyenye upungufu ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(iii) itawezesha ujenzi wa maabara za sayansi 15 kwa shule za sekondari 15 zenyenye upungufu ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia na hivyo kuongeza ufaulu katika masomo ya sayansi;

(iv) itawezesha ukarabati wa shule kongwe za sekondari tano ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(v) itawezesha ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa shule 30 za msingi na sekondari;

(vi) itawezesha ujenzi wa nyumba 80 za walimu katika shule 15 za sekondari na tano za msingi zilizopo katika maeneo yenye mazingira magumu kwa lengo la kuimarisha makazi ya walimu na kuongeza ufanisi; na

(vii) itaendelea kutekeleza miradi ya kukuza ujuzi nchini kupitia Mfuko wa Kukuza Ujuzi - *Skills Development Fund* katika vyuo mbalimbali kwa kutoa mafunzo ili kuongeza wigo wa ajira nchini.

79. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha utoaji wa elimu nje ya mfumo rasmi kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Serikali itatekeleza yafuatayo:

- (i) itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kisomo na Elimu kwa Umma (NALMERS) unaolenga kupunguza kiwango cha watu wasiojua kusoma na kuandika kwa kuwajengea uwezo maafisa na wataalamu wa kisomo;
- (ii) itawezesha wasichana takribani 3,000 walioacha shule kwa sababu mbalimbali ikiwemo ujauzito kupata elimu ya sekondari kwa njia mbadala;
- (iii) itaendelea kuongeza fursa za mafunzo na ujuzi kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu kupitia Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana walio Nje ya Mfumo Rasmi wa Elimu (IPOSA); na
- (iv) itaongeza udahili wa wanafunzi wa Astashahada, Stashahada na Shahada kutoka 4,430 hadi 5,200.

80. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha na kuendeleza elimu ya ualimu nchini, Serikali itawezesha Vyuo vya Ualimu kujinga na umoja wa Maktaba za tafiti na Vyuo Vikuu Tanzania - *Consortium of Tanzania University and Research Libraries* (COTUL) kwa ajili ya kupata maarifa yaliyo katika mfumo wa kielektroniki (E-resources). Aidha, itaendelea na uunganishaji wa Vyuo vya Ualimu katika Mkongo wa Taifa - *National Fiber Optical*.

81. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha ubora wa elimu ya awali, elimumsingi, sekondari na kuendeleza elimu ya ualimu, Serikali itatekeleza yafuatayo:

- (i) itaendelea kukuza ujuzi wa uandishi (writing skills) kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini kwa kuratibu mashindano ya uandishi wa insha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika; na
- (ii) itawezesha uchapaji na usambazaji wa nakala 2,000 za Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu 2021/22 - 2025/26 pamoja na kutoa mafunzo kwa Maafisa Elimu 26 wa Mikoa na 184 wa Halmashauri kuhusu uandaaji wa mipango ya elimu kwa kuzingatia mpango huo na kufanya ufuatiliaji na tathmini.

82. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha upimaji na tathmini ya elimumsingi, sekondari na vyuo vya ualimu, Serikali itatekeleza yafuatayyo:

- (i) itaendesha upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa watahiniwa 1,716,776 wanaotarajiwa kufanya upimaji huo mwezi Novemba, 2022;
- (ii) itaendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 1,376,169 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Oktoba, 2022;
- (iii) itaendesha Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili kwa watahiniwa 694,336 wanaotarajiwa kufanya upimaji huo mwezi Novemba, 2022;
- (iv) itaendesha Mtihani wa Kidato cha Nne kwa watahiniwa 596,272 na Mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa 8,505 wanaotarajiwa kufanya mitihani hiyo mwezi Novemba, 2022;
- (v) itaendesha Mtihani wa Kidato cha Sita kwa watahiniwa 93,594 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Mei, 2023;
- (vi) itaendesha Mtihani wa Astashahada na Stashahada ya Ualimu kwa watahiniwa 7,135 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Mei, 2023;
- (vii) itaendesha upimaji wa umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa sampuli ya wanafunzi 32,363 wa darasa la pili mwezi Januari, 2023;
- (viii) itawezesha uchapaji wa vitabu vya uchambuzi wa matokeo ya upimaji wa darasa la pili 2021 (PIRA - STNA), vitabu vya uchambuzi wa matokeo ya upimaji wa darasa la nne, 2021 (PIRA - SFNA) na vitabu vya uchambuzi wa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi 2021 (PIRA - PSLE); na
- (ix) itaendelea kuimarisha mfumo wa usahihishaji wa mitihani kwa njia ya kielektroniki (e-marking) kwa lengo la kuendelea kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa mitihani.

83. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara itaendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ngazi ya Elimumsingi nchini kwa kutoa mafunzo kazini kuhusu matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu 1,500 kutoka katika shule za sekondari 750. Vilevile, itatoa mafunzo kazini kwa walimu 10,000 wa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo hayo.

84. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi na sekondari, na kuhamasisha tabia ya wanafunzi kupenda kujisomea vitabu. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

- (i) itatoa tuzo kwa waandishi bora wa vitabu vya riwaya zitakazotumika katika kufundishia na kujifunzia;
- (ii) itawezesha Taasisi ya Elimu Tanzania kuchapa na kusambaza nakala 2,000,000 za vitabu vya masomo manne ya *Mathematics, Physics, Chemistry na Biology*;
- (iii) itaendelea na uandishi wa vitabu vya kiada ngazi ya sekondari na elimu ya ualimu (Astashahada na Stashahada) kwa lengo la kupunguza changamoto ya upatikanaji wa vitabu vya kufundishia na kujifunzia; na
- (iv) itachapa na kusambaza vitabu vya kimacho na nuktanundu kwa ajili ya shule za msingi na sekondari kwa lengo la kusaidia ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenyewe uoni haffifu na wasioona.

85. Mheshimiwa Spika, katika kutoa nafasi kwa umma wa watanzania kutumia maktaba za umma kwa ajili ya kupata taarifa sahihi na maarifaili kujikwamua katika ujinga, umaskini na maradhi; Serikali kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania itaaniszisha kanzi data ya kitaifa itakayosaidia kupata taarifa mbalimbali za machapisho na taarifa nyingine za Kiserikali kama vile hotuba za viongozi na hansadi za Bunge. Aidha, itaongeza idadi ya udahili kwa wanafunzi kutoka 618 hadi kufikia 800 katika Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka (SLADS).

86. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa hamasa ya usomaji wa vitabu na elimu kwa umma kwa: kuendesha programu za usomaji kwa jamii -outreach programme; kufanya makongamano ya usomaji wa vitabu na maonesho ya vitabu; na kuendesha programu maalum za usomaji kwa watoto kwa lengo la kuongeza ari ya usomaji.

87. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba itaendelea kuongeza wigo wa utoaji wa elimu kwa jamii kwa kuimarisha upatikanaji wa machapisho ya kielektroniki (e-books), vitabu veya nuktanunu na vifaa muhimu veya kujifunzia. Vilevile, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya maktaba kwa; kujenga na kukarabati maktaba ya Mkoa wa Tanga, Mara, Mwanza, Singida, maktaba ya Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka Bagamoyo pamoja na kuongeza nakala za vitabu hadi kufikia 2,300,000 kwa lengo la kuboresha huduma za maktaba nchini. Vilevile, Serikali itaendelea kutangaza huduma za maktaba kupitia njia za mawasiliano kama vile runinga, redio, tovuti, mitandao ya kijamii, magazeti na vipeperushi ili kuwajengea uelewa wadau mbalimbali kuhusu majukumu na kazi za Bodi.

88. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa elimu ya ualimu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaendeleza mafunzo ya elimu ya ufundi katika vyuo veya ualimu kutoka vyuo viwili vilivyopo sasa hadi kufikia vyuo saba kwa kuviwezesha kuwa na; vifaa, mashine, karakana na walimu wa masomo ya ufundi. Vilevile, itawezesha mafunzo kwa wakufunzi 100 wa masomo ya ufundi katika vyuo hivyo;

(ii) itaendelea kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo veya Ualimu 35 veya Serikali kwa kununua vitabu veya kiada na rejea veya kielektroniki (E-Text books and references) pamoja na samani;

(iii) itakarabati maabara za sayansi na TEHAMA pamoja na maktaba katika Vyuo veya Ualimu saba kwa lengo la

kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo katika Vyuo vya Ualimu; na

(iv) itawezesha utoaji wa mafunzo kuhusu utunzaji na menejimenti ya maabara za sayansi kwa wataalamu 50 wa maabara.

89. Mheshimiwa Spika, Serikali itatoa mafunzo ya ufundishaji wa masomo ya michezo na biashara kwa wakufunzi 100. Masomo hayo ni; *Physical Education, Fine arts, Music, Theatre Arts, Home Economics and Nutrition, Commerce na Book-keeping*. Lengo la mafunzo hayo ni kuendelea kuimarisha uwezo wa wakufunzi kufundisha masomo ya michezo na biashara. Vilevile, Serikali itaendelea kuratibu mashindano ya michezo na sanaa (UMISAVUTA) kwa lengo la kuimarisha afya na kuibua vipaji katika Vyuo vya Ualimu.

90. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la hisabati katika elimu ya msingi, sekondari na Vyuo vya Ualimu, Serikali itaendelea kukiimarisha Kituo cha Hisabati – *Mathematics Centre* kilichopo Chuo cha Ualimu Morogoro kwa ajili ya kuanzisha programu za mafunzo endelevu kwa walimu.

91. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha elimu inatolewa kwa kuzingatia usawa wa jinsia wenye kuzingatia malezi bora na usalama wa mtoto shulen na vyuoni, Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Jinsia - *Gender Strategy* pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mkakati huo. Aidha, Serikali itatoa mafunzo kwa walimu 200 kuhusu unasihi na ulinzi wa mtoto ili kuboresha huduma hiyo katika shule za msingi na sekondari.

92. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha inasimamia utekelezaji wa miongozo na mikakati mbalimbali ya kusaidia wanafunzi walioacha shule kwa sababu mbalimbali kwa kusimamia utekelezaji wa: Mwongozo wa Utekelezaji wa Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala -*Alternative Education Pathway Implementation guideline*; Mwongozo wa Wanafunzi wa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi; na Mwongozo wa Wawezeshaji.

93. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza afua mbalimbali zenyelengo la la kupunguza mdondoko wa wanafunzi kuititia utekelezaji wa programu ya shule salama. Aidha, Serikali itatoa mafunzo kuhusu utekelezaji wa mpango huo kwa walimu 3,600 wa sekondari pamoja na kutoa mafunzo ya uelewa kuhusu usawa na ukatili wa kijinsia.

94. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa elimu maalum, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itafanya ufuutiliaji na tathmini katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu vinavyopokea wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa lengo la kubaini changamoto zilizopo na kutoa ushauri wa kitaalamu;

(ii) itatoa mafunzo kwa wathibiti ubora wa shule 150 kuhusu ufuutiliaji na tathmini ya utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum; na

(iii) itaendelea kuandika, kuchapa na kusambaza vitabu vya sekondari katika mfumo wa brela na maandishi yaliyokuzwa kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na wasioona ili kuwawezesha kusoma kwa urahisi.

d. Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Utoaji wa Elimu Kuanzia Elimumsingi, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, na Elimu ya Juu

95. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha uthibiti ubora wa elimu katika ngazi ya elimumsingi, sekondari na Vyuo vya Ualimu, Serikali itaendelea kusogea huduma ya uthibiti ubora wa shule na Vyuo vya Ualimu katika ngazi ya Halmashauri kwa kujenga ofisi tano za Uthibiti Ubora wa Shule katika Halmashauri ya Pangani, Ubungo, Bunda, Njombe na Tarime. Vilevile, itawezesha ununuzi wa magari 20 ili kuwawezesha kazi za uthibiti ubora wa shule.

96. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha miongozo, sheria, kanuni na taratibu za elimu zinazingatiwa katika utoaji wa elimu, Serikali itatekeleza kazi zifuatazo:

(iv) itafanya tathmini ya jumla - *whole school visits* katika asasi 19,800 zikiwemo shule za msingi 17,164, sekondari 2,578 na vyuo vya ualimu 58; na

(v) itafanya ufuatiliaji – *followup visit* katika asasi 6,994 zikiwemo shule za msingi 5,676, sekondari 1,289 na vyuo vya ualimu 29. Aidha, itafanya ufuatiliaji maalum katika asasi 745.

97. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa elimu kwa kuwajengea uwezo Wakuu wa Shule za sekondari 5,264 kwa lengo la kuimarisha uthibiti ubora wa ndani ya shule ili kuinua ubora wa elimu inayotolewa katika shule husika. Aidha, Serikali imelenga kuandaa mfumo wa kielektroniki wa uthibiti ubora wa shule ili kurahisisha ukusanyaji wa taarifa na kurahisisha kufanya maamuzi.

98. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi na utoaji wa elimu bora katika ngazi za elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu, Serikali kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM), itadahili walimu 2,343 watakaosoma Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu (DEMA) na Stashahada ya Uthibiti Ubora wa Elimu (DSQA).

99. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa elimumsingi nchini kwa kuziwezesha taasisi za uendelezaji wa elimu katika ngazi hiyo. Taasisi hizo ni pamoja na: Taasisi ya Elimu Tanzania (TET); Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) pamoja na Idara za Wizara. Uimarishaji huo utafanyika kupitia; ununuzi wa magari 17 kwa ajili ya usimamizi wa afua za elimumsingi.

100. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya shule na matumizi ya fedha, Serikali itatoa mafunzo ya muda mfupi kwa walimu 28,074 (21,274 usimamizi wa fedha na 6,800 uongozi na usimamizi wa elimu).

101. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha utendaji kazi wa wasimamizi wa elimu nchini kwa kutoa mafunzo kwa Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya, na Wathibiti Ubora wa Shule wa Kanda na Wilaya wapatao 3,829 (tathmini ya kiutendaji

1,836, umahiri wa ufundishaji na ujifunzaji 1,626, na mpango wa ufuatiliaji na tathmini 367). Aidha, Serikali itatoa mafunzo ya uthibiti ubora wa elimu kwa Wathibiti Ubora wa Vyuo vya Elimu ya ufundi wapatao 319.

102. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa taaluma ya uongozi na usimamizi wa elimu, Serikali kuptitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) itatekeleza yafuatayo:

- (i) itakamilisha ujenzi na uwekaji wa samani katika jengo la ghorofa lenye kumbi nne za mihadhara zenyne uwezo wa kuchukua wanafunzi 564 pamoja na ofisi 10 katika Kampasi ya Mbeya;
- (ii) itakarabati ofisi nne , kumbi za mihadhara tatu na nyumba tatu za watumishi katika Kampasi ya Bagamoyo; na
- (iii) itaanza ujenzi wa Kampasi ya ADEM - Mwanza.

103. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia na kuendeleza Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini, Serikali itaendelea kuimarisha utoaji wa mafunzo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 kwa lengo la kuhakikisha mafunzo yanayotolewa yanakidhi viwango vinavyohitajika. Vilevile, itaandaa mfumo wa utunzaji na uchakataji wa taarifa za mafunzo ya ufundi stadi (VETdataMIS) nchini.

104. Mheshimiwa Spika, katika kusogeza huduma ya mafunzo ya ufundi stadi kwa wananchi, Serikali itajenga Ofisi ya VETA Makao Makuu Jijini Dodoma. Aidha, Serikali itakamilisha ujenzi wa ofisi tano za Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) za kanda katika mkoa wa Arusha, Mbeya, Mwanza, Tabora na Mtwara pamoja na kuanza ujenzi wa ofisi – Dodoma.

105. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha uthibiti ubora wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) itawezesha uandaaji wa miongozo ya mitaala na uhakiki wa ubora wa Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi;
- (ii) itawezesha NACTVET kufanya mapitio ya miongozo ya uandaaji wa mitaala na kutoa ithibati ya mitaala katika vituo vya umahiri (Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam - DIT, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji – NIT, Chuo cha Ufundu Arusha - ATC) vinavyotekeliza afua za kimkakati ambazo ni maendeleo ya TEHAMA na sekta ya ngozi, usafiri wa anga na nishati jadidifu;
- (iii) itakamilisha Kiunzi cha Ulinganifu wa Sifa na Tuzo za Kitaaluma na Kitaalamu Tanzania ambacho kitaoanisha sifa na ngazi zote za elimu na mafunzo;
- (iv) itasimika mtandao wa mawasiliano wa ndani (LAN) na nje (WAN) katika vyuo 30 vya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi;
- (v) itafanya ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa elimu ya ufundu na mafunzo ya ufundu stadi katika vyuo 400 kati ya vyuo 1,298 kwa lengo la kuhakiki ubora wa elimu inayotolewa katika vyuo vya ufundu; na
- (vi) itanunua magari 20 kwa ajili ya matumizi ya Ofisi za Makao Makuu, Kanda na Vyuo.

106. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha uthibiti ubora wa elimu katika ngazi ya Elimu ya Juu, Serikali itatekeleza yafuatayo:

- (i) itafanya mapitio ya Sheria ya Vyuo Vikuu Sura 346 kwa lengo la kuihuisha ili iendane na mahitaji ya sasa;
- (ii) itavijengea uwezo Vyuo Vikuu katika masuala ya ithibati na uthibiti ubora wa ndani ili kuimarisha ubora wa Elimu ya Juu;
- (iii) itashiriki katika makongamano na mikutano inayohusu uimarishaji wa uthibiti ubora kikanda na kimataifa kwa lengo la kuongeza ujuzi na weledi katika uthibiti ubora wa Elimu ya Juu nchini;

(iv) itaboresha mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji na utoaji taarifa za Elimu ya Juu kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati na matumizi yake katika kupanga mipango na kufanya maamuzi; na

(v) itaendelea kusimamia utendaji wa Vituo vya Umahiri vya Afrika katika Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini -*African Centre of Excellence- ACE* //ambavyo vipo katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela.

107. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Elimu ya Juu inayotolewa nchini inazingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu, Serikali itaendelea kutekeleza yafuatayo:

(i) itafanya ufuutiliaji na tathmini katika Vyuo Vikuu 30 kwa lengo la kuhakiki ubora;

(ii) itafanya tathmini ya tuzo 3,000 zilizotolewa katika Vyuo Vikuu vya nje ya nchi na kuzitambua zitakazokidhi vigezo;

(iii) itafanya tathmini ya programu 300 za masomo mbalimbali katika Vyuo Vikuu nchini na kuzipa ithibati programu zitakazokidhi vigezo; na

(iv) itakagua Asasi/Kampuni tano zinazojishughulisha na uratibu wa wanafunzi wanaokwenda kusoma nje ya nchi kwa lengo la kuzitambua na kuzisajili zile zitakazokidhi vigezo.

e. Kuendelea Kuongeza Fursa na Ubora wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi

108. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza fursa za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini, Serikali itaendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji na utoaji wa elimu na mafunzo hayo. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itasajili vyuo 20 vya elimu ya ufundi na vyuo 80 vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi na hivyo kuwa na jumla ya vyuo 538

vya elimu ya ufundi na vyuo 830 vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi mtawalia;

(ii) itahakiki udahili wa wanafunzi takribani 250,000 (vyuo vya Serikali 200,000 na vyuo visivyo vya Serikali 50,000) kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;

(iii) itaongeza ushiriki wa wanafunzi wa kike katika mafunzo ya elimu ya ufundi stadi kutoka asilimia 41 hadi kufikia asilimia 45;

(iv) itaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu ya ufundi stadi na elimu ya wananchi kwa washiriki 15,000 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 kwa lengo la kuwapatia ujuzi na maarifa yatakayowawezesha kujajiri au kuajiriwa;

(v) itaendelea kusimamia ujenzi wa Chuo cha Ufundi cha Dodoma (DTC) kinachojengwa katika eneo la Nala kwa lengo la kuongeza fursa ya utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi;

(vi) itakamilisha ujenzi na uwekaji samani katika Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi vya Wilaya 25 na vyuo vinne vya Mikoa. Aidha, itaweka zana za msingi za mafunzo katika vyuo vikongwe 15 vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi;

(vii) itafanya maonesho ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kuendeleza bunifu baina ya wadau mbalimbali wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi;

(viii) itajenga mabweni nane katika Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi vya Wilaya tano ambazo ni Namtumbo 2, Kasulu Vijijini 1, Ileje 2, Simanjiro 1 na Itilima 2;

(ix) itajenga mabwalo manne ya chakula katika Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi vya Wilaya ya Namtumbo, Itilima, Ileje na Urambo;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- (x) itakamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara na darasa katika Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufund Stadi cha Utalii na Ukarimu cha Njiro;
- (xi) itajenga vyuo viwili vya huduma katika Mkoa wa Songwe na Dar es Salaam (Kampasi ya Kigamboni);
- (xii) itaendelea kukamilisha ujenzi wa vyuo vya Ufund Stadi vya Wilaya ya Wanging'ombe na Wilaya ya Newala;
- (xiii) itakarabati vyuo viwili vya Ufund Stadi na Huduma vya Mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma;
- (xiv) itaanza ujenzi wa ofisi ya VETA Makao Makuu jijini Dodoma; na
- (xv) itatunuku wanagenzi 2,800 kutoka sekta isiyo rasmi na kutoa mafunzo kwa wajasiliamali 3,000 kwa utaratibu wa *Integrated Training for Entrepreneurship Promotion (INTEP)*.

109. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya watumishi katika utoaji wa Elimu ya ufund na mafunzo ya ufund stadi nchini, Serikali itajenga nyumba nane za watumishi katika Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufund Stadi vya Wilaya ya Namtumbo 1, Itilima 2, Kasulu Vijijiini 3, na lleje 2. Vilevile, Serikali itakarabati nyumba 25 za watumishi katika Chuo cha Moshi – Kilimanjaro (10), Singida (2), Kigoma (3), Tabata – Dar es Salaam (10).

110. Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha wahitimu wa elimu ya ufund na mafunzo ya ufund stadi wanapata stadi za kuawesha kujiajiri na kuajiriwa, Serikali itaendelea kuimarisha ujuzi na umahiri kwa wahitimu kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) itajenga karakana sita za uchomeleaji na uungaji wa vyuma katika Vyuo vya Mafunzo ya Ufund Stadi na Huduma vya Mkoa wa Manyara na Pwani, pamoja na karakana za umeme, bomba, magari na uashi katika Chuo cha Mafunzo ya Ufund Stadi na Huduma cha Kihonda;

(ii) itaviwezesha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 kwa kuvinunulia vifaa vya kiufundi vya kufundishia na kujifunzia. Aidha, itaviwezesha Vyuo 47 vya Elimu na Mafunzo ya Ufund Stadi kwa kuvinunulia vitabu na kompyuta 1,175 kwa lengo la kuhakikisha ujuzi wa wahitimu unaendana na mipango ya nchi na soko la ajira;

(iii) itaendelea kutoa mafunzo kwa wakufunzi 100 katika Taasisi za Elimu ya Ufund na Mafunzo ya Ufund Stadi kwa lengo la kuimarisha ufanisi wa ufundishaji wa mitaala inayoendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya soko la ajira; na

(iv) itawajengea uwezo walimu 1,000 kutoka katika Vyuo vya Elimu ya Ufund na Mafunzo ya Ufund Stadi 50 kuhusu utoaji wa Elimu ya Ufund na Tathmini ya Mitaala ya Umahiri (CBET). Mafunzo hayo yatasaidia kuwa na walimu mahiri wa kuzalisha nguvu kazi illyo tayari kutumika katika uzalishaji viwandani.

111. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha elimu ya ufund na mafunzo ya ufund stadi yanayotolewa yanakidhi mahitaji ya soko la ajira, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itafanya ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa Elimu ya Ufund na Mafunzo ya Ufund Stadi kwa lengo la kuhakikisha ubora unazingatiwa katika utoaji wa elimu ya ufund na mafunzo ya ufund stadi; na

(ii) itahakiki mitaala 180 ya Vyuo vya Elimu ya Ufund na Mafunzo ya Ufund Stadi kwa lengo la kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanakidhi soko la ajira.

f. Kuendelea Kuongeza Fursa na Ubora wa Elimu ya Juu

112. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Juu nchini, Serikali itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itaratibu udahili wa wanafunzi 133,000 wa mwaka wa kwanza wanaotarajiwu kuomba udahili katika Vyuo vya Elimu ya Juu kwa lengo la kuijunga na programu mbalimbali za masomo kwa ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada

ya Kwanza na Shahada ya Umahiri. Vilevile, itaaniszisha mpango wa fursa za ziada kwa wanawake kwa kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike katika programu za sayansi (Science, Technology, Engineering and Mathematics (STEM);

(ii) itaratibu maonesho ya 17 ya Elimu ya Juu nchini kwa lengo la kutoa elimu kwa umma kuhusu vyuo na programu mbalimbali zitolewazo;

(iii) itaratibu maombi, uchambuzi na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi 205,893 katika Taasisi za Elimu ya Juu. Aidha, itafanya ukaguzi kwa waajiri 8,000 kwa lengo la kuwabaini wanufaika wapya takribani 30,000 ili kuwezesha ukusanyaji wa **Shilingi 241,419,005,000.00** kutokana na mikopo ilioiva kutoka **Shilingi 201,319,005,000.00** za mwaka wa fedha 2021/22;

(iv) itahuisha mwongozo wa utoaji mikopo kwa lengo la kuboresha utoaji wa mikopo kwa wanufaika; na

(v) itaendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika taasisi 19 za Elimu ya Juu katika ufundishaji, ujifunzaji na usimamizi kwa lengo la kuimarisha mazingira ya utoaji wa elimu katika ngazi hiyo.

113. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya kugharimia Elimu ya Juu nchini kwa lengo la kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Juu ili kuendana na mahitaji yanayotokana na ongezeko kubwa la uhitaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu. Katika kufanikisha hilo, Benki ya NMB imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 200** kwa kuanzia katika mwaka wa fedha 2022/23 kwa ajili ya kuanza kutoa mikopo ya elimu.

114. Mheshimiwa Spika, Fedha hizo zitasimamiwa na NMB Benki kwa utaratibu maalum wa kibenki na kwa mujibu wa makubaliano rasmi katika ya Wizara na NMB ambapo mikopo hiyo itaongozwa na masharti yafuatayo:

(i) itatoleta kwa riba nafuu;

(ii) itatolewa kuanzia ngazi ya stashahada (Diploma) na masomo ya Umahiri (Postgraduate) ambapo Bodi ya mikopo haijaanza kutoa mikopo katika ngazi hizo; na

(iii) itatolewa kwa wazazi au walezi ambao ni waajiriwa wa Serikali na sekta binafsi/ au kwa wafanyakazi wanaotaka kuijendeleza.

115. Mheshimiwa Spika hii itasaidia kupunguza idadi ya waajiriwa wanaowaombea watoto wao mikopo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na hiyo kutoa fursa zaidi kwa waombaji wenyе uhitaji zaidi. Kutokana na fursa hiyo, Kipekee naomba niishukuru Benki ya NMB kwa kuunga mkono jitihada za Serikali za ugharamiaji wa Elimu ya Juu. Vilevile, nitambue uwepo wa Mtendaji Mkuu NMB Benki **Bi. Ruth Zaipuna** ambaye tumemkaribisha katika Bunge lako tukufu. Aidha, nitoe wito kwa taasisi nyingine kuunga mkono jitihada za Serikali za kugharimia elimu nchini.

116. Mheshimiwa Spika, katika kuwajengea uwezo wa utendaji kazi watumishi katika taasisi za Elimu ya Juu nchini, Serikali itaendelea kutoa ufadhili kwa Wanataluma na Wataalam 1,401 kuhudhuria masomo ya muda mfupi 500 na muda mrefu 836. Aidha, Serikali itatoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 65 wenyе ufaulu uliojipambanua katika masomo ya sayansi hususan wanafunzi wa kike waliohitimu mitihani ya Kitaifa ya Kidato cha 6 na Shahada ya Kwanza.

117. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha uhusiano na mataifa mengine katika uendelezaji wa Elimu ya Juu nchini kwa kutoa ufadhili kwa wanafunzi wa kigeni 10 wa Shahada ya Umahiri katika Lugha ya Kiswahili. Vilevile, itaratibu nafasi 200 za ufadhili wa masomo kutoka nchi rafiki na mashirika mbalimbali nje ya Bara la Afrika.

118. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za mikopo kwa wanufaika kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaunganisha mifumo ya TEHAMA ya Bodi na wadau wa kimkakati kwa lengo la kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa za utoaji na urejeshaji wa mikopo; na

(ii) itaendelea kusajili wanafunzi walionufaika na mikopo katika mfumo wa malipo wa kielektroniki (DIDiS) kwa lengo la kuwezesha wanufaika kupata mikopo kwa wakati na kurahisisha ufuutiliaji wa mikopo iliyotolewa.

119. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo Vikuu, Serikali itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itajenga maabara 21, mabweni 19, madarasa 77, kumbi za mihadhara 13, maktaba tisa, ofisi 71, mifumo ya maji minne, vituo atamizi vitatu na studio moja;

(ii) itaendelea na ukarabati wa mabweni 11, madarasa 50, maabara mbili, nyumba za watumishi 15 na ofisi 25;

(iii) itanunua magari mawili na kuongeza vitendea kazi katika ofisi ya Makao Makuu Dodoma na Kituo Mahsus Cha Wateja - *Dedicated Customer Relations Centre* cha Dar es Salaam kwa lengo la kuimarishe huduma za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu; na

(iv) itajenga Ndaki ya Uchumi na Mafunzo ya Biashara awamu ya pili katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Ndaki ya uchumi na mafunzo ya biashara katika Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Kilimo na Teknolojia - Butiama.

120. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Elimu ya Juu inayotolewa nchini inaendana na mahitaji ya soko la ajira, Serikali itaandaa mitaala ya programu nane mipya katika ngazi ya Shahada ya Kwanza na Umahiri pamoja na kuanzisha Shahada mpya za awali tano na Shahada za Uzamili tatu. Aidha, Serikali itaanzisha programu nne na kuhuishwa mitaala ya programu 24 kwa lengo la kuwezesha wahitimu kujajiri na kukidhi mahitaji ya soko la ajira.

121. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini, Serikali itaongeza vitengo mbalimbali katika taasisi za Elimu ya Juu ikiwemo shule ya meno na kuanza mpango wa ujenzi wa Kliniki ya Uporoto (Uporoto Polyclinic) kwa lengo la kuimarisha huduma za tafiti na tiba. Vilevile, itaendeleza vituo atamizi, mashamba darasa, semina na kozi fupi ili kuongeza uzalishaji wenyе tija.

g. Kutegemeza Matumizi ya Sayansi na Teknolojia Katika Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Maendeleo ya Taifa

122. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwaibua, kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu nchini kwa lengo la kuendeleza matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika ajenda ya maendeleo. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itawaibua, kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu na wagunduzi wachanga kupitia Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) kwa lengo la kuwezesha ubunifu wao katika kuchangia kikamilifu katika ujenzi wa uchumi wa viwanda. Wabunifu hao watatoka katika Shule za Msingi na Sekondari, Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi, Vyuo vya Ufundi, Vyuo Vikuu, Vituo vya kuendeleza teknolojia, Taasisi za Utafiti na Maendeleo pamoja na Mfumo usio rasmi;

(ii) itaratibu maadhimisho ya Wiki ya Ubunifu Kitaifa kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya bunifu na teknolojia katika shughuli za maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii;

(iii) itaandaa mukutano wa wadau wa sayansi teknolojia na ubunifu na Watanzania wanaoishi nje ya nchi utakaojulikana kama *The First Multistakeholder and Diaspora Forum on Science Technology and Innovation* kwa lengo la kujadili ushiriki wao katika kuendeleza Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini;

(iv) itaandaa maadhimisho ya siku ya kimataifa ya wanawake na wasichana katika sayansi kwa ajili ya kuhamasisha ushiriki

wao katika kukuza mchango wa sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati kwenye maendeleo ya kiuchumi na kijamii; na

(v) itawaendeleza wabunifu 70 walioibuliwa kupitia MAKISATU katika mwaka wa fedha 2021/22.

123. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wabunifu na wagunduzi wapya wanatambuliwa pamoja na kazi zao kufikia hatua za ubiasharishaji, Serikali itaimarisha uratibu wa shughuli za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika ngazi mbalimbali kwa kushirikiana na Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa lengo la kuwafikia wabunifu na wagunduzi wachanga hususan katika maeneo ya vijijini.

124. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA nchini kwa kuunganisha taasisi za utafiti na Mkongo wa Taifa. Vilevile, itajenga kituo cha kikanda cha umahiri wa TEHAMA chenyehadhi ya kimataifa, itaandaa mfumo wa uhawilishaji wa teknolojia kupitia uwekezaji nje ya nchi na itahakiki teknolojia zinazoibukia - *Inventory of emerging technologies*.

125. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utoaji wa mafunzo ya sayansi, teknolojia na ubunifu, Serikali itaanza ujenzi wa majengo ya Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia, Ndaki ya Usanifu majengo na Teknolojia ya Ujenzi na Kujenga jengo la kitaaluma la Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya - Kampasi ya Rukwa.

126. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC) itaendelea kuimarisha usimamizi, udhibiti na matumizi salama ya mionzi ya nyuklia nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itapokea na kutathmini maombi 600 ya vibali vya umiliki, utumiaji na usafirishaji wa vyanzo vya mionzi ili kuhakikisha usalama wa wananchi;

(ii) itaendelea kuendesha kituo cha kupima uchafuzi wa hewa katika anga unaotokana na majaribio ya silaha za nyuklia chini

ya mkataba wa kimataifa wa *Comprehensive Nuclear Test - Ban Treaty (CTBT) for Non-Proliferation Test (NPT) of Nuclear weapons;*

(iii) itapima na kudhibiti viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,064 wanaofanya kazi kwenye mazingira ya vyanzo vya mionzi;

(iv) itaimarisha na kupima mionzi katika mazingira kwenye vituo 40 ambavyo vimeduwa vikiendeshwa kwa ushirikiano na Taasisi nyingine; na

(v) itafanya ukaguzi katika vituo 120 vinavyotoa mionzi isioyayonisha (Non-Ionizing Radiation) kwa mfano minara ya simu, redio, runinga na vifaa vingine vya mionzi ili kubaini usalama wa wakazi wa maeneo husika.

127. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha huduma ya teknolojia ya nyuklia zinazotolewa na TAEC, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itasajili vituo vipyta 60 vinavyotumia vyanzo vya mionzi ambapo ongezeko hilo litawezesha kufikia vituo 1,129 vilivyosajiliwa nchini;

(ii) itaanzisha kituo cha mafunzo ya usalama wa mionzi na nyukilia ili kuongeza wataalamu na wigo wa udhibiti wa matukio hatarishi ya kinyuklia;

(iii) itaendelea na ujenzi wa maabara na ofisi katika Kanda ya Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza;

(iv) itaendelea kupima sampuli 28,000 za vyakula, mbolea na tumbaku na bidhaa nyingine zote katika mnyororo wa chakula zinazotoka na kuingia nchini kwa lengo la kubaini endapo hazina madhara ya mionzi;

(v) itafungua ofisi tatu katika Kanda na mipaka mbalimbali nchini ili kuongeza uwezo wa udhibiti mionzi na kuwashudumia wananchi;

(vi) itaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuhifadhi mazao ya kilimo ikiwemo vyakula viharibikavyo kirahisi (perishable), vifaa tiba na vya viwandani kwa kutumia teknolojia ya mionzi - *Multipurpose Irradiator Facility*;

(vii) itakagua vituo 600 vyenye vyanzo vya mionzi ili kubaini hali ya usalama wa mionzi kwa wagonjwa, wafanyakazi na umma kwa ujumla. Vilevile, itakagua migodi saba ya madini kwa lengo la kubaini hali ya usalama wa mionzi kwa wafanyakazi katika migodi hiyo; na

(viii) itaendelea na ujenzi wa maabara za kanda katika Mkoa wa Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma na kuanza ujenzi wa maabara katika Mkoa wa Mbeya na Zanzibar kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki. Aidha, itaendelea na ujenzi wa maabara changamano (Complex Multipurpose Laboratory) awamu ya pili kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma.

128. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika taasisi za sayansi, teknolojia na ubunifu, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaanza ujenzi wa jengo la ghorofa sita lenye vyumba vya madarasa, ofisi na maabara katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam;

(ii) itajenga mabweni mawili katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 na kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa bweni moja katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 180;

(iii) itaanza ujenzi wa jengo la utawala katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST);

(iv) itajenga viwanda vinne vya kufundishia na kujifunzia kwa vitendo - teaching factory katika taasisi ya DIT, MUST, SUA na ATC;

(v) itajenga hosteli mbili katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam zenyе uwezo wa kuchukua wanafunzi 160 na kukamilisha ujenzi wa hosteli mbili katika Kampasi Kuu ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya zenyе uwezo wa kuchukua wanafunzi 800 kwa wakati mmoja; na

(vi) itanunua vifaa vya kisasa vya maabara na karakana kwa lengo la kuboresha utoaji wa mafunzo katika fani mbalimbali za sayansi na teknolojia ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia duniani.

129. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza ufanisi kwa wataalamu na wanataaluma wa taasisi za sayansi, teknolojia na ubunifu nchini, Serikali itafadhili watumishi 300 kuhudhuria masomo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi. Aidha, itaendesha kozi fupi za ubobezi katika TEHAMA, Sayansi ya Maabara na Teknolojia ya Ngozi kwa washiriki 250.

130. Mheshimiwa Spika, katika kuimarishe mafunzo kwa vitendo katika taasisi zinazosimamia na kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu nchini, serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaendeleza dhana ya mafunzo viwandani - *industrial attachment* itakayowawezesha wahitimu katika kila ngazi kupata ujuzi unaokidhi soko la ajira; na

(ii) itawezesha ujenzi wa viwanda vya kufundishia na kujifunzia (teaching factories) katika Chuo cha ufundi Arusha (ATC), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

h. Kuimarishe na Kuendeleza Tafiti na Matumizi ya Matokeo yake katika Ajenda ya Maendeleo

131. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarishe uwezo wa ndani wa kufanya tafiti na kutumia matokeo ya tafiti katika kuchangia ajenda ya maendeleo ya nchi kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) itafanya tafiti 252 katika maeneo ya mazingira, TEHAMA, nishati, kilimo na chakula, uongozi na biashara, maendeleo ya utalii, sheria, uthibiti wa ubora, utawala na maendeleo, watu wenye ulemavu na mahitaji maalum, maliasili, umaskini, utamaduni, haki za binadamu, maendeleo ya watu na mawasiliano, mifugo, biashara, uvuvi, elimu, sayansi, lugha na fasihi;
- (ii) itaongeza utoaji wa elimu na ushauri kwa washiriki 2,500 wakiwemo wakulima, maafisa ugani na watafiti kwa kutumia mbini mbalimbali kama vile vituo atamizi, mashamba darasa, semina, kozi fupi, runinga na redio ili kuongeza uzalishaji wenye tija. Aidha, itatoa huduma za ushauri wa kitaalam kuhusu matumizi bora ya ardhi, upimaji na tathmini, usanifu majengo na usimamizi wa ujenzi;
- (iii) italmarisha makundi ya kitafiti - *Research Clusters* na kutoa mafunzo kwa viongozi wa makundi hayo ili kujenga uwezo wa ndani wa kuandaa na kufanya tafiti zenye tija katika kutatua changamoto mbalimbali; na
- (iv) itatoa tuzo kwa tafiti bora zitakazochapishwa katika majarida yenye hadhi ya juu Kimataifa "High Impact Factor Journals" kwa lengo la kuongeza hamasa ya watafiti.

132. Mheshimiwa Spika, katika kuzijengea uwezo wa kuandaa na kufanya tafiti zenye tija kwa taasisi zinazoendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu nchini, Serikali itafanya tafiti 34 na kutoa huduma 34 za ushauri elekezi.

F. TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)

133. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO itaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Tume kama ifuatavyo:

- (i) itaendelea kusimamia utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali iliypitishwa katika mpango wa Tume wa Mwaka 2022 – 2029 katika nyanja za elimu, sayansi, utamaduni, habari na mawasiliano;

- (ii) itaratibu vikao vya Kamati ya Kitaifa ya kudhibiti matumizi ya dawa na mbinu za kuongeza nguvu michezoni kwa kushirikiana na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo;
- (iii) itakarabati jengo la ofisi la Tume, itaboresha mifumo ya TEHAMA na kununua gari moja na samani za ofisi; na
- (iv) itafungua ofisi ya Tume mjini Unguja, Zanzibar kwa lengo la kusogeza huduma za Tume katika visiwa vya Unguja na Pemba.

134. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha utekelezaji wa majukumu ya Tume unazingatia kanuni, sheria, taratibu na miongozo, Serikali kupitia Tume itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itafuatilia na kutathmini utekelezaji wa mikataba 10 ya Tume iliyordhiwa pamoja na miradi inayotekelze hapa nchini;
- (ii) itatathmini utekelezaji wa maamuzi ya Kamati ya Urithi wa Dunia katika maeneo yaliyo katika orodha ya urithi wa dunia ambayo ni Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, Eneo la Hifadhi la Ngorongoro, Mamlaka ya Mji Mkongwe wa Zanzibar, Michoro ya Miambani ya Kondoa, Magofu ya Kilwa Kisiwani na Magofu ya Songo Mnara;
- (iii) itatathmini ushiriki wa wananchi katika uhifadhi na utalii wa maeneo ya urithi wa dunia na kijiolojia pamoja na kuhamasisha wananchi kuhama kwa hiari kutoka eneo la urithi wa dunia la Hifadhi ya Ngorongoro; na
- (iv) itapitia sheria na muundo wa Tume kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Tume.

135. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia Tume itaendelea kuratibu maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani ambayo itakuwa ikifanyika tarehe 7 Julai kila mwaka. Aidha, itaongeza idadi ya Taasisi za Elimu zinazojunga na Mitandao ya Elimu ya UNESCO (ASPnet, UNESCO Chairs, UNEVOC Networks na UNESCO

Global Networks of Learning Cities) kwa lengo la kuongeza maarifa.

G. SHUKRANI

136. Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Omari Juma Kipanga (Mb), Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa jinsi tunavyofanya kazi vizuri pamoja na mchango wake katika kuandaa wasilisho hili. Katibu Mkuu, Profesa Eliamani Sedoyeka na Naibu Makatibu Wakuu, Profesa James Mdoe na Profesa Carolyne Nombo wameongoza kwa umakini na juhudini kubwa timu ya wakurugenzi, wakuu wa taasisi na watumishi wote katika kuandaa hotuba hii. Ninawashukuru kwa dhati kwa juhudini hizi na kwa kazi kubwa wanazofanya.

137. Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, watumishi wa Wizara na Taasisi zake, Walimu, Wanafunzi, na Wadau wote wa Elimu kwa ushirikiano wao. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wamiliki na Mameneja wa Shule, Vyuo na Taasisi binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kutoa huduma ya elimu nchini.

138. Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Rombo kwa kuniamini na kunichagua kuwa mwakilishi wao. Nawaahidi utumishi uliotukuka.

139. Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Washirika wa Maendeleo na Wadau wa Elimu wote ambao wamechangia kufanikisha utekelezaji wa Mipango na Miradi ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Naomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za: Algeria, Umoja wa Falme za Kiarabu, Austria, Brazil, Canada, China, Cuba, Finland, Hungary, India, Indonesia, Italia, Israel, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Malaysia, Misri, Morocco, Zimbabwe, Netherland, New Zealand, Norway, Palestina, Romania, Saudi Arabia, Sweden, Thailand, Ufaransa, Urusi, Uswisi, Uingereza, Uhollandi, Ujerumani na Venezuela. Aidha, natambua pia mchango wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

140. Mheshimiwa Spika, napenda pia kushukuru Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa yaliyochangia kufanikisha miradi na programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na: Benki ya Dunia, *Foreign, Commonwealth and Development Office* (FCDO), *Swedish International Development Agency* (SIDA), Umoja wa Nchi za Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Jumuiya ya Madola, *Global Partnership in Education* (GPE), *United Nations International Children's Emergency Fund* (UNICEF), *United Nations Development Programme* (UNDP), *United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization* (UNESCO), *United States Agency for International Development* (USAID), *Inter University Council for East Africa* (IUCEA), *Human Development Innovation Fund* (HDIF), *Deutscher Akademischer Austauschdienst* (DAAD), *British Council*, *Campaign for Female Education* (CAMFED), *Commonwealth Secretariat*, *Aga Khan Education Services*, *Japan International Cooperation Agency* (JICA), *Karibu Tanzania Organization* (KTO), *Korea International Cooperation Agency* (KOICA), *Water Aid*, *Plan International*, *Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania* (TEN/MET), Christian Social Services Commission (CSSC), Mo Foundation na Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA).

H. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/23

141. Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa malengo kwa mwaka wa fedha 2022/23, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,493,004,355,000.00** kwa mchanganuo ufuato:

(i) **Shilingi 533,456,916,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ambapo **Shilingi 500,196,732,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 33,260,184,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

(ii) **Shilingi 959,547,439,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 778,083,678,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 181,463,761,000.00** fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

142. Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,709,163,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara ni **Shilingi 1,176,870,000.00** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 1,532,293,000.00**).

143. Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kuitisha Makadirio ya Bajeti ya Fungu 46 na Fungu 18 yenye jumla ya **Shilingi 1,495,713,518,000.00**.

144. Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

145. Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara <http://www.moe.go.tz>.

146. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Ahsante hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Profesa. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati kwa niaba yake Makamu Mwenyekiti.

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE HUDUMA YA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusoma kwako taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa fursa ili kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu na Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022, pamoja na Maoni, Ushauri, Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2022,2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 Kamati ilipaswa kabla ya kuchambua bajeti kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha, 2021/2022, kwa lengo la kuona hatua za utekelezaji wa miradi hiyo ili kuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kuishauri Serikali. Kwa Kanuni hiyo Kamati ilitembelea na kukagua miradi mitano ilio chini ya Wizara hii iliyopo katika Mikoa ya Arusha, Iringa na Mbeya. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Ufundı Arusha (Mradi Namba 6363), Mradi wa Ujenzi wa Bweni la Wanawake katika Taasisi Afrika Mashariki ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (Mradi Namba 5422), Mradi wa Ujenzi wa Maabara changamano ya Tume ya Nguvu za *Atomic Tanzania* (Mradi Namba 6356) na Mradi wa Ujenzi, Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Mkwawa (Mradi Namba 4314) pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Hosteli, Maabara na Maktaba katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (Mradi Namba 4353).

Mheshimiwa Naibu Spika, Muundo wa Taarifa. Taarifa hii ya Kamati imegawanyika katika maeneo yafuatayo: -

(a) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022;

(b) Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023 na;

(c) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri, mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022. Pamoja na Kamati kupokea taarifa ya utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati bado iliona kuna baadhi ya maoni, ambayo hayakutekelezwa kikamilifu ambayo ni pamoja na uhaba wa watumishi na mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Kamati itaendelea kusisitiza tena masuala haya kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022. Katika Mwaka wa Fedha, 2021/2022 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Fungu Namba 46 ilikadiria kukusanya maduhuli yenye thamani ya shilingi bilioni 555.04, ambapo hadi kufikia Februari, 2022 Wizara ilikuwa imekusanya Shilingi bilioni 350.4 sawa na asilimia 63 ya makadirio kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina Mwaka, 2021/2022. Katika Mwaka wa Fedha, 2021/2022 Wizara kupitia Fungu 46 ilidhinishiwa na Bunge lako Tukufu bajeti ya shilingi trillioni 1.5, kwa ajili ya kuwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake na miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 480.47 sawa na asilimia 31.6 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trillioni 1.038 sawa na asilimia 68.3 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2022 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi trillioni 1.053 sawa na asilimia 69.3 ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 317 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na asilimia 66 ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa, na shilingi bilioni 736 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, sawa na asilimia 71 ya bajeti yote ya maendeleo iliyoidhinishwa, kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tume ya UNESCO yenyeye Fungu Namba 18 kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022 iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi bilioni 2.25. Hadi kufikia Februari, 2022 kiasi cha shilingi bilioni 1.38 sawa na asilimia 61.45 ya bajeti iliyoidhinishwa kilikuwa kimepokelewa kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 3.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023. Wizara kuitia Fungu Namba 46 katika Mwaka wa Fedha, 2022/2023 imekadiria kufanya makusanyo ya maduhuli ya shilingi bilioni 642.66. Kamati imefanya uchambuzi wake kwa kulinganisha makadirio ya makusanyo kwa Mwaka, 2021/2022 ambapo Kamati imebaini kuwa makadirio hayo yameongezeka kwa shilingi bilioni 87.63 sawa na asilimia 13.6. Kamati illioji sababu zillizosababisha kuongezeka kwa makadirio ya makusanyo ya maduhuli ambapo ilielezwa kuwa ni kutokana na kuongezeka kwa kazi ya ushauri (*Consultancy*) katika Taasisi ya Juu na Ufundi, hii ikiwa ni pamoja na kuandaliwa kwa *program* mpya zenyeye uhitaji kwa jamii katika vuyo mbalimbali vyta elimu ya juu na ufundi ambapo watu mbalimbali wanavutiwa kusoma *program* hizo mpya zilizoboreshwaa na hivyo kupelekea ongezeko la udahili na ukusanyaji wa mapato kutokana na ada za masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2022/2023. Katika eneo hili Kamati imefanya uchambuzi wa aina mbili kama ifuatavyo:-

(a) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara, Fungu Namba 46 na Fungu Namba 18, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu Jumla ya Trillioni 1.42. Ambapo, kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida yanaombewa Shilingi Bilioni 533.45 sawa na asilimia 37.54 na shilingi bilioni 887.547 sawa na asilimia 62.45 zinaombewa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, kama inavyoonekana katika kielelezo Namba 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini upungufu wa bajeti kwa asilimia 6.47 ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2021/2022. Upungufu zaidi unaonekana kwenye fedha za miradi ya maendeleo ambapo zimepungua kwa asilimia 14.8. Kamati ilihoji sababu za upungufu huo na kuelezwu kuwa umesababishwa na upungufu wa fedha za nje za miradi ya maendeleo uliotokana na kumalizika kwa muda wa utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo kama vile mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo Katika Sekta ya Elimu (*EP4R*), Mradi wa kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi (*ESPJ*), pamoja na miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19 (*TCRP*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa fedha mishahara kuna ongezeko la bilioni 52.98 sawa na asilimia 10.59. ongezeko hilo linatokana na kupandishwa vyeo kwa baadhi ya Wafanyakazi wa Wizara na Taasisi na kuongezeka kwa Watumishi katika Ikama ya Wizara ambapo wanaotajwa katika taarifa hiyo ni Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule ambao ni 400 kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kutoongezeka kwa fedha za matumizi mengineyo licha ya ongezeko la mishahara. Kamati ilihoji sababu ya kutoongezeka huko na athari zake ambapo imeelezwa ni kutokana na ukomo wa bajeti na kupungua kwa gharama za uendeshaji wa ofisi kutokana na kuimariswa kwa mifumo mbalimbali ya kutolea huduma kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kutenga Bajeti ya nyongeza ya mishahara kwa watumishi walipanda vyeo na kuongeza Wathibiti Ubora 400 kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kamati inaamini kwamba, ubora wa elimu katika shule zetu utaongezeka kutokana na usimamizi utakaosababishwa na ongezeko hilo la Wadhibiti Ubora wa Shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tume ya *UNESCO*, Fungu Namba 18. Katika Mwaka wa Fedha 2022/

2023 imekadiria kutumia Shilingi Bilioni 2.7. Kamati imefanya uchambuzi wake na kubaini kuwa, Bajeti ya mwaka huu ya Tume imeongezeka kwa asilimia 16.7. ongezeko zaidi linaonekana kwenye mishahara kwa asilimia 38.6 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 7. Kamati ilihoji sababu ya ongezeko la mishahara na ilielezwa kuwa ni kutokana na Watumishi 22 wanaotarajiwa kuhamia kutoka Taasisi mbalimbali za Umma. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuona umuhimu wa kuongeza watumishi katika Tume hii.

(b) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara, Fungu Namba 46 kwa Kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kulinganisha Bajeti ya Fungu 46 dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/2023 kwa lengo la kubaini masuala mbalimbali ikiwemo asilimia ya Bajeti ya Wizara katika Mpango huu yaani Bajeti ya Taifa, kati ya mwaka 2021/2022 na 2022/2023, lakini pia kuona ni kwa kiasi gani mwenendo wa bajeti hiyo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaathiri bajeti ya Fungu 46.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Bajeti ya Fungu 46 kwa ujumla wake kiasi cha Triliioni 1.421 kwa mwaka 2022/2023 ni asilimia 3.4 ya Bajeti yote ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa yaani Triliioni 41.06. Bajeti hii imeshuka kutoka asilimia Nne dhidi ya Shilingi Triliioni 37.98 ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2021/2022.

(ii) Bajeti ya Mishahara ya Fungu 46 dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa imepungua kutoka asilimia 5.48 kwa mwaka 2021/2022 hadi asilimia 5.13 kwa mwaka 2022/2023.

(iii) Bajeti ya Maendeleo ya Fungu 46 dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa imepungua kutoka asilimia 6.93 mwaka 2021/2022 hadi asilimia 5.7....

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wako unakwisha tuende kwenye sehemu ya nne, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; kutokana na uchambuzi huo na yale yaliyobainika, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Elimu ya Juu. Ili kupata maendeleo katika nchi yetu ni lazima tuwe na dhamira ya dhati ya kuwekeza katika Elimu ya Juu. Mwanasiasa mkongwe wa Marekani Ndugu Ronald Lewis aliwahi kusema "Kuhakikisha ubora wa elimu ya juu ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kizazi cha baadaye."

Katika kuhakikisha utolewaji wa elimu bora katika vyuo vikuu kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(a) Wizara iongeze Bajeti ya Maendeleo ili kutatua changamoto ya upungufu wa miundombinu ya elimu kama vile nyumba za walimu, mabweni, madarasa na maabara katika Vyuo Vikuu nchini.

(b) Kamati inaishauri Serikali kuviwezesha Vyuo Vikuu kuwekeza katika kufanya tafiti mbalimbali ili kuweza kuongeza mapato ya ndani na kujitangaza ili kutambulika Kimataifa.

(c) Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, itenye bajeti ya kutosha kutokana na vyanzo vya ndani ili kuwezesha Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma kujitangaza na kuongeza udahili katika ngazi ya Uzamili na Uzamivu.

(d) Vyuo Vikuu viendelee kubuni na kuanzisha kozi mbalimbali zenyе kuwasaidia wanafunzi kujiliria mara baada ya kumaliza elimu. Kozi zinazotolewa ziwasaidie wawewe kubuni miradi, kuiendesha na kuisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upungufu wa Watumishi. Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa watumishi katika Taasisi za Wizara kama Shule na Vyuo Vikuu. Uhaba huo ni pamoja na uhaba wa Walimu na wakufunzi katika vyuo mbalimbali. Katika kutatua changamoto hii kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Wizara iwe na mkakati wa dhati wa kutatua changamoto hii ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya watumishi ili kukidhi mahitaji katika Taasisi za Wizara hii.

(b) Serikali iendelee kuajiri walimu wa shule za Msingi na Sekondari.

(c) Kamati iendelee kusisitiza kuwa Vyuo Vikuu viendelee kuwa na uhuru wa kitaaluma katika kuajiri watumishi wake hususan wataalam kwa kuzingatia sheria, kanuni na vigezo nya kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikopo ya Wwanafunzi Elimu ya Juu. Kamati inapongeza Serikali kwa kuendelea kutoa mikopo kwa kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Hata hivyo kamati inatoa maoni yafuatayo:-

(a) Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia mikopo wanafunzi wa vyuo nya elimu ya kati.

(b) Kamati inaendelea kusisitiza, Serikali iangalie upya vigezo nya utoaji wa mikopo ya Elimu ya Juu ili kupunguza malalamiko yanayotolewa na vigezo nya ulinganifu vinavyojitokeza mara kwa mara miongoni mwa waombaji na wazazi.

(c) Serikali iendelee kutafuta vyanzo nya fedha ili kuwapatia mikopo wanafunzi wote wanaohitaji mikopo.

(d) Bodi ya Mikopo ijijendeshe kibenki ili kuwezesha na kurahisisha utoaji wa mikopo na ukusanyaji wa mikopo kwa wanafunzi wanaohitaji.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Vyuo vya Ufundu Stadi (*VETA*). Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza sera ya kujenga Vyuo vya Ufundu Stadi Nchini. Ujenzi huu ukikamilika utasaidia watanzania wengi kudahiliwa na baadae kujajiri na hivyo kupunguza tatizo la kutokuwa na ajira nchini. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa walimu katika vyuo hivi. Pamoja na pongezi Kamati inasitiza yafuatayo yafanyike ili kuboresha mpango wa ujenzi wa vyuo hivi: -

(a) Serikali ikamilishe kwa wakati ujenzi wa vyuo 26 vya Elimu ya Ufundu Stadi (*VETA*) unaoendelea Nchini.

(b) Kuwepo na mkakati wa kuhakikisha Halmashauri zote nchini zinakuwa na Vyuo vya Elimu ya Ufundu Stadi ili kutoa fursa kwa vijana katika Halmashauri kupata elimu hiyo.

(c) Ujenzi wa Vyuo hivi vya Ufundu Stadi uende sambamba na kuajiri Walimu wa kutosha watakaoweza kuwafundisha wanafunzi wanaosoma katika vyuo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madawati ya Jinsia Shuleni na Vyoni:-

(a) Kuanzishwe madawati ya jinsia katika ngazi za Elimu kuanzia sekondari hadi Elimu ya Juu ili kuwezesha vijana kupata elimu ya Afya ya Akili, namna ya kukabili athari za unyanyasaji wanaokumbana nao ukiwemo unyanyasaji wa kingono.

(b) Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali, Wizara ihamasishe wazazi kuongea na vijana wao kuhusu hatua za mabadiliko ya mwili na elimu ya uzazi na afya.

(c) Wizara iwekeze katika kutoa mafunzo ya elimu ya afya ya uzazi kwa Walimu ili kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu hiyo na wanakuwa na maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Usimamizi Wa Miradi ya Maendeleo.

(a) Kamati inashauri Serikali kuwe na umakini katika usimamizi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha ili kuwezesha kupatikana kwa thamani halisi ya fedha na kukamilika haraka na kwa wakati kwa miradi hiyo.

(b) Miradi ya ujenzi wa vyuo vya elimu inayoendelea izingatie uwepo miundombinu yenyewe kuwezesha kutatua mahitaji ya msingi ya makundi maalum ya wanawafunzi kama vile wanafunzi wa jinsia ya Kike wenye Watoto na Watu Walemaavu.

(c) Kamati inasisitiza kuongeza kasi ya utoaji wa fedha za miradi mbalimbali inayoendelea ya ujenzi na ukarabati wa Vyuo Vikuu na kuwe na usimamizi mzuri wa miradi hiyo ili ikamilike kwa wakati na kuweza kutimiza lengo la kuanzishwa kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kushauri Serikali iharakishe mchakato wa kuititia maoni ya wadau kuhusu mtaala mpya wa elimu ili kuwezesha kupatikana kwa wakati na kuanza kutumika, hivyo kusaidia kuboresha elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho. Napenda kukushukuru tena kwa nafasi uliyonipa ya kuweza kuwasilisha taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Stanslaus Haroun Nyongo, pamoja na wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakitoa na zaidi katika kushiriki vyema katika vikao mbalimbali, ikiwemo uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru wewe na Spika kwa kuendelea kuongoza vyema Bunge letu. Hakika ninyi ni Viongozi wa mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Mbunge, Naibu Waziri Mheshimiwa Omary Shaban Kipanga, Mbunge, Makatibu Wakuu wa Wizara hii

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wakiongozwa na Profesa Eliamani Sedoyeka, Katibu Mkuu Profesa James Mdoe, Naibu Katibu Mkuu, Profesa Caroline Nombo Naibu Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati wote pamoja na kushiriki vyema katika vikao vya uchambuzi wa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi kwa ushirikiano ambao amekuwa akiipa Kamati yetu katika kutekeleza majukumu yake.

Pamoja naye, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein na Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu Ndugu Gerald Magili, Msaidizi wa Kamati Ndugu Jane Ndulesi na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila vikwazo.

Mheshimiwa NaibU Spika, kipekee tunawashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu Ndugu Francisca Haule, Ndugu Happiness Ndalu na Ndugu Emmanuel Mdidi kwa kuendelea kuishauri vyema Kamati na kuhakikisha Kamati inatimiza majukumu yake bila kukwama ikiwemo kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Fungu Namba 46, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, jumla ya shilingi 1,421,004,355,000 na Fungu Namba 18, shilingi 2,709,163,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof!*)

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA MWAKA
WA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA
MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO
NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/
2023 -KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa fursa ili kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa [Nyongeza ya Nane (7) (1) (a) ya Kanuni ya 137 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020], mojawapo ya Majukumu ya Kamati hii kama zilivyo Kamati nyingine za Kisikta ni pamoja na kushughulikia Bajeti ya Wizara zinazozisimamiwa na Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Katika vikao vyake vilivyofanyika Mwezi Machi, 2022 hapa Dodoma, Kamati ilichambua na kujadili bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 Kamati ilipaswa kabla ya kuchambua Bajeti, kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 kwa lengo la kuona hatua ya utekelezaji wa miradi hiyo ili kuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea na kukagua Miradi mitano iliyo chini ya Wizara hii iliypopo katika mikoa ya Arusha,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Iringa na Mbeya. Miradi hiyo ni Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Ufundji Arusha (mradi namba 6363); Mradi wa Ujenzi Wa Bweni la Wanawake Wa Taasisi ya Afrika Ya Sayansi Na Teknolojia Ya Nelson Mandela (mradi namba 5422); Mradi wa ujenzi wa Maabara changamano wa Tume za nguvu za Atomic Tanzania(mradi namba 6356); Mradi wa ujenzi, upanuzi na ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Mkwawa (mradi namba 4314); pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Hostel, Maabara na Maktaba wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (mradi namba 4353);

1.1 MUUNDO WA TAARIFA

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ya Kamati imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo: -

- a) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- b) Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na
- c) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Katika vikao vya Kamati vilivyo fanyika Mwezi Machi, 2022 hapa Dodoma, Kamati ilichambua na kujadili Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara. Uchambuzi wa Kamati ulikuwa kama ifuatavyo: -

2.1 UTEKELEZAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni mnamo tarehe 4 Mei, 2021 kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, ilijumuisha pamoja na mambo mengine Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati yapatayo tisa (9). Pamoja na Kamati kupokea Taarifa ya utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati bado iliona kuna baadhi ya maoni ambayo hayakutekelezwa kikamilifu ambayo ni pamoja na: - Uhaba wa Watumishi na mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. **Kamati itaendelea kuyasisitiza tena masuala haya kwenye Taarifa hii.**

2.2 UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (**Fungu 46**) ilikadiria kukusanya Maduhuli yenyе thamani ya **Shilingi 555,043,008,495.63**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 8,680,995,000.00** ni makusanyo kutoka katika Idara na Vitengo na **Shilingi 546,362,013,495.63** ni makusanyo kutoka katika Taasisi zilizo chini ya Wizara. Vyanzo vya maduhuli ni kutookana na malipo ya ada, ushauri elekezi, huduma za ukaguzi wa shule na utoaji wa huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Februari, 2022. Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 350,484,167,565.79** sawa na **asilimia 63** ya makadirio ambapo **Shilingi 6,738,103,982.00** ambayo ni sawa na **asilimia 78** zimekusanywa na Idara na Vitengo, na **Shilingi 343,746,063,583.79** sawa na **asilimia 63** zimekusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kina wa Kamati umebaini kuwa makusanyo ya maduhuli kwa idara na vitengo vilivyo chini ya Wizara hii ni wa kuridhisha kwani hadi kufikia mwezi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)


Februari, 2022 zimeweza kukusanya maduhuli kwa Zaidi ya **asilimia 60** ya lengo walilojiwekea.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa makusanyo mazuri ya maduhuli kwa Taasisi ya Elimu Tanzania na Mamlaka ya Elimu Tanzania ambapo wameweza kuvuka malengo ambapo Taasisi ya Elimu Tanzania ilipanga kukusanya kiasi cha **shilingi 4,546,810,382.00** lakini hadi kufikia Februari, 2022 imekusanya **5,350,542,404.00** sawa na **asilimia 118**. Hali kadhalika Mamlaka ya Elimu Tanzania ilipanga kukusanya kiasi cha **shilingi 434,500,000.00** ilivuka lengo na kukusanya jumla ya **shilingi 607,368,623.95** ambayo ni sawa na **asilimia 140**.

Kamati ilipongeza makusanyo haya makubwa. Kwa mujibu wa taarifa za Wizara sababu za makusanyo kuzidi makadirio, zilliezwa kuwa ni kutokana na juhudhi ambazo Taasisi imezifanya za uandishi, uchapaji na uuzaaji wa vitabu; utoaji wa mafunzo wa walimu na wakufunzi; kuwaelimisha wamiliki wa shule binafsi kuhusu umuhimu wa kutumia vitabu vya kiada vinavyoandikwa na Taasisi ya Elimu Tanzania hatua ambayo imeongeza sana mauzo ya vitabu. **Kamati inapongeza sana Taasisi ya Elimu Tanzania na Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa kuendelea kuwa wabunifu na kuongeza mapato ya taasisi hizi.**

Kielelezo Na. 1: UKUSANYAJI WA MADUHULI FUNGU 46 KWA 2021/2022

CHANZO	MAKADIRIO	MAKUSANYO	ASILIMIA
Idara na Vitengo	8,680,995,000.	6,738,103,982.00	78
Taasisi	546,362,013,495.63	343,746,063,583.79	63
JUMLA	555,043,008,495.63.	350,484,167,565.79	63



Chanzo: Randama ya fungu 46 (Machi 2022) na Usanifu wa Kamati

2.3 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA MWAKA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara kupitia **Fungu 46**, ilidhinishiwa na Bunge lako Tukufu Bajeti ya **Shilingi 1,519,316,801,000** kwa ajili ya kuwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake na miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 480,474,878,000.00** sawa na **asilimia 31.6** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,038,841,923,000.00** sawa na **asilimia 68.3** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2022, Wizara ilikuwa imepokea Jumla ya **Shilingi 1,053,099,782,423.57** sawa na **asilimia 69.3** ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 317,073,604,015.66** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo ni sawa na **asilimia 66** ya Matumizi ya Kawaida yaliyoidhinishwa na **Shilingi 736,026,178,407.91** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 71** ya Bajeti yote ya Maendeleo iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wake na kubaini kuwa, kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida

zilizopokelewa, **Shilingi 295,938,693,940.48** sawa na **asilimia 66** ni kwa ajili ya mishahara (PE) na **Shilingi 21,134,910,075.18** sawa na **asilimia 64** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo, kiasi cha **Shilingi 736,026,178,407.91** kimepokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 71** ya bajeti iliyotengwa. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 625,342,683,026.86** sawa na **asilimia 81** ni fedha za ndani na **Shilingi 110,967,369,567.01** sawa na **asilimia 42** ni fedha za nje kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.2.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa utolewaji wa fedha za matumizi ya kawaida na imeridhishwa na kasi ya utolewaji wa fedha hizo hadi kufikia Februari, 2022 ambacho ni kipindi cha robo ya tatu ya utekelezaji mwaka wa bajeti na tayari Wizara imekwishapokea **asilimia 66** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kamati ilifanya uchambuzi wa fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa na kuipongeza Serikali kwa utoaji wa fedha hizo kwa **asilimia 71** uliosaidia kutekeleza miradi ya maendeleo mbalimbali kama vile: - upanuzi na Ukarabati wa Shule na Vyuo Vikuu, mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Mfuko wa Utafiti na Maendeleo (Research and Development Fund – COSTECH; Ujenzi wa Jengo la Tume ya Nguvu za Atomiki (Tanzania Atomic Energy Commission Laboratory).

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kamati inampongeza Mheshimiwa Rais kwa Serikali yake kuipatia Wizara hii fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19 ambazo zimelenga kuboresha miundombinu ya ujenzi na ukarabati wa madarasa, mabweni, kumbi za miadhara katika Vyuo vya Ualimu na vyuo vinavyotoa Mafunzo ya Ufundji Stadi nchini ili kuimarisha mazingira ya Ujifunzaji na Ufundishaji. Fedha hizo zimetumika kutekeleza miradi kama vile: - Ujenzi wa VETA 4 za Mikoa, Ujenzi wa Vyuo 25 vya VETA; ununuzi wa Vifaa kwa Wanafunzi wenge Mahitaji Maalumu wa Elimu ya Juu; pamoja na ujenzi wa Madarasa 41, Kumbi za Miadhara 3 na mabweni 15 katika vyuo vya Ualimu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kielelezo Na. 2: UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 46 MWAKA 2021/2022

UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 46 MWAKA 2021/2022				
MATUMIZI		KILICHOIDHINISHWA	KILICHOPOKELEWA	ASILIMIA
KAWAIDA	MISHAHARA	447,214,694,000.00	295,988,693,940.48	66
	OC	33,260,184,000.00	21,134,910,075.18	64
	JUMLA	480,474,878,000.00	317,073,604,015.66	66
MAENDELEO	NDANI	776,639,923,000.00	625,342,683,026.86	81
	NJE	262,202,000,000.00	110,967,369,567.01	42
	JUMLA	1,038,841,923,000.00	736,310,052,593.87	71
JUMLA BAJETI		1,519,316,801,000	1,053,099,782,423.66	69.3

Chanzo: Randama ya fungu 46 (Machi 2022) na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tume ya UNESCO yenye **Fungu 18**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, iliidhinishwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 2,254,777,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 722,484,000.00** sawa na **asilimia 32.04** ya Bajeti ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Tume na **Shilingi 1,532,293,000.00** sawa na **asilimia 67.95** ni kwa ajili ya Hadi kufikia Februari, 2022 kiasi cha **Shilingi 1,385,650,341.64** sawa na **asilimia 61.45** ya Bajeti iliyoidhinishwa kilikuwa kimepokelewa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 400,929,000.00** sawa na **asilimia 55.49** ya bajeti ya Mishahara ilikuwa imepokelewa na **Shilingi 984,721,341.64** sawa na **asilimia 64.26** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo nayo ilikuwa imepokelewa kama inavyoonekana kwenyeli Kielelezo Na.3.

Kielelezo Na. 3: UPATIKANAJI WA FEDHA (FUNGU 18) 2021/2022

MAELEZO	KIASI KILICHOIDHINISHWA 2021/2022	KILICHOPOKELEWA HADI FEB, 2022	ASILIMA%
MISHAHARA	722,484,000.00	400,929,000.00	55.49
MATUMIZI MENGINEYO	1,532,293,000.00	984,721,341.64	64.26
JUMLA	2,254,777,000.00	1,385,650,341.64	61.45

CHANZO: Randama ya bajeti ya tume ya UNESCO (FUNGU 18) 2022/2023 na Usanifu wa Kamati

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 imejiwekea malengo mbalimbali kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025); Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2020/21 2025/26); Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) (2020-2025); Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti wa mwaka 2022/2023; na Mipango na Mikakati ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu. Baadhi ya malengo ambayo Wizara imejiwekea ni pamoja na Kuongeza Fursa na Ubora wa Elimu na Mafunzo katika ngazi zote; kutunga na Kutekeleza Sera za Elimu, Tafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu na Uendelezaji wa Mafunzo ya Ufundii; Kuimarissha Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika Elimu, Sayansi na Teknolojia; kuratibu na kuimarissha Maendeleo ya Tafiti na Bunifu kwa ajili ya Kukuza Uchumi wa Jamii na Maendeleo ya Viwanda; Kuongeza Matumizi na Mafunzo pamoja na Kuweka Kanuni za Kuwezesha Matumizi Salama ya Teknolojia ya Nyuklia; Kukusanya Rasilimali Fedha na Kuongeza Uwekezaji Katika Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu pamoja na Miundombinu; Kuimarissha Mazingira ya kazi ili Kuongeza Tija na Ufanisi katika Utoaji wa Huduma; na kushughulikia Masuala Mtambuka katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Ili kuweza kutekeleza malengo haya pamoja na majukumu mbalimbali, Wizara iliwasilisha mbele ya Kamati, Randama yake yenye kuonyesha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli na Matumizi kwa lengo la kuchambuliwa na kujadiliwa na Kamati. Kamati ilifanya kazi hiyo na uchambuzi kama ifuatavyo: -

3.1 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2022/2023

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia **Fungu 46** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 inakadiria kukusanya maduhuli ya

Shilingi 642,667,620,483.06 Kati ya makadirio hayo, **Shilingi 8,680,995,000.00** sawa na **asilimia 1.3** zinatarajija kukusanya kutoka vyanzo vya Idara na Vitengo vya Wizara na kiasi cha **Shilingi 633,986,625,483.06** sawa na **asilimia 98.6** kinakadiriwa kukusanya kutoka vyanzo vilivyopo chini ya Taasisi za Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wake kwa kulinganisha makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2021/2022 ambapo wizara ilikadiria kukusanya **shilingi 555,043,008,495.63** dhidi ya yale ya mwaka 2022/2023 ambapo **shilingi 642,667,620,483.06** zinatarajija kukusanya. Baada ya uchambuzi huo Kamati imebaini kuwa, makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameongezeka kwa **shilingi 87,624,611,987.43** sawa na **asilimia 13.6**.

Ongezeko hilo la maduhuli linatarajija kutoka makusanyo ya taasisi zilizo chini ya Wizara ambapo kwa mwaka 2021/2022 zilikusanya **shilingi 546,362,013,495.63** lakini kwa mwaka wa fedha 2022/2023 taasisi hizo zinatarajia kukusanya **shillingi 633,986,625,483.06**. Kwa upande wa idara na taasisi makusanyo yao ni kama ya mwaka wa fedha uliopita 2021/2022 ambayo ni **shilingi 8,680,995,000.00** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.4.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliarifiwa kuwa sababu zilizopelekea kuongezeka kwa makadirio ya makusanyo ya maduhuli ni kutokana na Kuongezeka kwa Kazi za Ushauri(consultancy) katika Taasisi za Elimu ya Juu na Ufundu na Kuandaliwa kwa Program Mpya zeye Uhitaji kwa Jamii katika vyuo mbalimbali vya Elimu ya Juu na Ufundu ambapo watu mbalimbali wanavutiwa kusoma program mpya na zilizoboreshwa na hivyo kupelekea ongezeko la udahili na ukusanyaji wa mapato kutokana na ada za masomo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

**Kielelezo Na. 4: ULINGANISHO WA MADUHULI 2021/2022 NA
2022/2023**

MAELEZO	2021/2022	2022/2023	ASILIMIA %
IDARA NA VITENGO	8,680,995,000.00	8,680,995,000.00	0
TA ASISI	546,362,013,495.63	633,986,625,483.06	16
JUMLA	555,043,008,495.63	642,667,620,483.06	13.6

Chanzo: Randama ya fungu 46 (Machi, 2022) na Usanifu wa Kamati

3.2 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/2023

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili Kamati imefanya uchambuzi wa aina mbili kama ifuatavyo: -

a) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara (Fungu 46 na 18)


Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu unalenga kufanya ulinganisho wa bajeti ya mwaka 2021/2022 na 2022/2023 [Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020] kwa lengo la kuona mwenendo wa bajeti ya Wizara hii. Katika Randama iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Wizara kuhusu makadirio yake ya matumizi kupitia Fungu 46 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu Jumla ya **Shilingi 1,421,004,355,000.00**. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida yanaombewa **Shilingi 533,456,916,000.00** sawa na **asilimia 37.54** na **Shilingi 887,547,439,000.00** sawa na **asilimia 62.45** zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa fedha hizo ambao pia unaonekana katika kielelezo Na. 5 ni kama ifuatavyo: -

- i) Mishahara ya Watumishi (PE) **Shilingi 500,196,732,000.00** sawa na **asilimia 35**;

- ii) Matumizi Mengineyo (OC) **Shilingi 33,260,184,000.00** sawa na **asilimia 2**;
- iii) Fedha za Ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo **Shilingi 706,083,678,000.00** sawa na **asilimia 50**; na
- iv) Fedha za Nje kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo **Shilingi 181,463,761,000.00** sawa na **asilimia 13**

Kielelezo Na. 5: BAJETI (FUNGU 46) 2022/2023



Chanzo: Randama ya fungu 46 (Machi 2022) na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wake kwa kulinganisha Bajeti ya **Fungu 46** kati ya Mwaka 2021/2022 na 2022/2023 na kubaini kuwa, kuna upungufu wa Bajeti kwa kiasi cha **Shilingi 98,312,446,000** sawa na **asilimia 6.47** kutoka **Shilingi 1,519,316,801,000** mwaka 2021/2022 hadi **Shilingi 1,421,004,355,000.00** mwaka 2022/2023. Upungufu zaidi unaonekana kwenye fedha za miradi ya maendeleo ambazo zimepungua kwa **shilingi 151,894,484,000** sawa na **asilimia 14.8** kutoka **shilingi 1,038,841,923,000** ya mwaka 2021/2022 hadi **shilingi 887,547,439,000** mwaka 2022/2023.

Kwa upande wa fedha za mishahara kuna ongezeko la **shilingi 52,982,038,000** sawa na **asilimia 10.59** kutoka **Shilingi 447,214,694,000** ya mwaka 2021/2022 hadi **Shilingi 500,196,732,000** mwaka 2022/2023.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wake na kubaini kuwa upungufu wa Bajeti ya fungu 46 katika mwaka wa fedha 2022/2023 kwa kiasi kikubwa umesababishwa na upungufu wa fedha za nje za miradi ya maendeleo uliotokana kumalizika kwa muda wa utekelezaji wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo kama vile mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo Katika Sekta ya Elimu (EP4R) na Mradi wa kukuza uUuzi na Stadi za Kazi (ESPJ). Aidha uwepo wa fedha za miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19 (TCRP) na Nyongeza ya Bajeti ya Bodi ya Mikopo kwa Mwaka 2021/2022 ulipelekea kuongezeka kwa Bajeti kwa mwaka huo wa fedha ukilinganisha na mwaka wa fedha 2022/2023.

Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida kamati imebaini ongezeko la mishahara limetokana na Kupandishwa Vyeo kwa baadhi ya Wafanyakazi wa Wizara na Taasisi zake na Kuongezeka kwa Watumishi katika Ikama ya Wizara (Maafisa Uthibiti Ubora wa Shule 400) kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini pia kuwa, pamoja na ongezeko la fedha za mishahara fedha za matumizi mengineyo haijaongezeka. Kamati ilihoji sababu za fedha za Matumizi mengineyo kutoongezeka na athari zitakazotokana na kutoongezeka kwa fedha hizo ambapo ilielezwa ni kutokana na ukomo wa Bajeti na kupungua kwa gharama za uendeshaji wa ofisi kutokana na kuimarishwa kwa mifumo mbalimbali ya kutolea huduma kwa gharama nafuu.

Kamati inapongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kutenga Bajeti ya nyongeza ya mishahara kwa watumishi waliopanda vyeo na kuongeza wathibiti ubora 400 kutoka OR TAMISEMI. Kamati inaanini ubora wa elimu katika shule zetu utaongezeka kutokana na usimamizi utakaosababishwa na ongezeko hilo la wathibiti ubora.

Kielelezo Na. 6 kinaonesha ulinganisho wa Bajeti ya Fungu 46 kwa mwaka 2021/2022 na 2022/2023.

**Kielelezo Na. 6: ULINGANISHO WA BAJETI YA FUNGU 46
KWA MWAKA 2021/2022/2023**

MATUMIZI		2021/2022	2022/2023	ONGEZJKO/UP UNGUFU	%
KAWAIDA	MSAHARA	447,214	500,196	52,982	10.59
	OC	33,26	33,26	0	0
	JUMLA	480,474	533,456	52,982	10.59
MAENDELEO	NDAN	776,639	706,083	-70,556	-9.08
	NJE	262,202	181,463	-80,738	-30.7
	JUMLA	1,038,841	887,547	-151,294	-14.56
JUMLA BAJETI	JUMLA KUU	1,519,316	1,421,004	98,312	6.4

Chanzo: Randama ya fungu 46 (Machi 2022) na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Tume ya UNESCO (**Fungu 18**), katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 imekadiria kutumia **Shilingi 2,709,163,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,176,870,000.00** sawa na **asilimia 43** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 1,532,293,000.00** sawa na **asilimia 57**. ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Tume.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wake na kubaini kuwa, Bajeti ya mwaka huu ya Tume imeongezeka kwa **asilimia 16.7** kutoka **Shilingi 2,254,777,000** mwaka 2021/2022 hadi **Shilingi 2,709,163,000** mwaka 2022/2023. Ongezeko zaidi linaonekana kwenye Mishahara kutoka **Shilingi 722,484,000** mwaka 2021/2022 hadi **Shilingi 1,176,870,000** mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la **asilimia 38.6** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 7. Kamati ilihoji sababu ya ongezeko la mishahara na ilielezwa kuwa, ni kutoptana na Watumishi 22 wanaotarajiwa kuhamia kutoka Taasisi mbalimbali za Umma. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuona umuhimu wa kuongeza watumishi katika Tume hii.**

Kielelezo Na. 7: ULINGANISHO WA BAJETI 2021/2022 NA 2022/2023 (FUNGU 18)

MALEZO	2021/2022	2022/2023
MSAHARA	722,484,000.00	1,176,870,000.00
MATUMIZI MENGINEYO	1,532,293,000.00	1,532,293,000.00
JUMLA	2,254,777,00	2,709,163,000.00

Chanzo: Randama ya fungu 18 (Machi, 2022) na Usanifu wa Kamati.

b) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara (Fungu 46) kwa Kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kulinganisha Bajeti ya Fungu 46 dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/2023 kwa lengo la kubaini masuala mbalimbali ikiwemo asilimia ya Bajeti ya Wizara katika Mpango huo (Bajeti ya Taifa) kati ya mwaka 2021/2022 na 2022/2023, lakini pia kuona ni kwa kiasi gani mwenendo ya bajeti hiyo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaathiri bajeti ya Fungu 46.

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

i) Bajeti ya **Fungu 46** kwa ujumla wake kiasi cha **shilingi 1,421,004,355,000** kwa mwaka 2022/2023 ni **asilimia 3.46** ya Bajeti yote ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ya **Shilingi 41,063,915.000,000** Bajeti hii imeshuka kutoka **asilimia 4** dhidi ya shilingi **37,980,601,000,000** ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo ya mwaka 2021/2022;

ii) Bajeti ya Mishahara ya **Fungu 46** dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa imepungua kutoka **asilimia 5.48** kwa mwaka 2021/2022 hadi **asilimia 5.13** mwaka 2022/2023; na
 iii) Bajeti ya Maendeleo ya **Fungu 46** dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa imepungua kutoka **asilimia 6.93 mwaka 2021/2022** hadi **asilimia 5.7** mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Kielelezo Na. 8 kinaonyesha ulinganisho huo.

Kielelezo Na. 8: ULINGANISHO WA BAJETI YA FUNGU 46 DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2021/2022 NA 2022/2023

ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 46 DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2021/2022			
MATUMIZI	BAJETI KUU YA TAIFA	BAJETI FUNGU 46	% FUNGU 46
MISHAHARA	8,150,509,000,000	447,214,694,000	5.48
OC	4,189,199,000,000	33,260,184,000	0.7
MAENDELEO	14,977,615,000,000	1,038,841,923,000	6.93
MFUKO MKUU WA SERIKALI	10,663,278,000,000	-	-
JUMLA	37,980,601,000,000	1,519,316,801,000	4

ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 46 DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2022/2023			
MATUMIZI	BAJETI KUU YA TAIFA	BAJETI FUNGU 46	% FUNGU 46
MISHAHARA	9,740,753,000,000	500,196,732,000	5.13
OC	4,493,456,000,000	33,260,184,000	0.74
MAENDELEO	15,521,341,000,000	887,547,439,000	5.7
MFUKO MKUU WA SERIKALI	11,308,365,000,000	-	-
JUMLA	41,063,915,000,000	1,421,004,355,000	3.46

Chanzo: Mpango wa Maendeleo wa Taifa, Randama Fungu 46 (Machi 2022) na Usanifu wa Kamati

iv) Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023 ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 7.5** kutoka **Shilingi Trilioni 37.9** mwaka 2021/2022 hadi **shilingi Trilioni 41.06** mwaka 2022/2023. Aidha Bajeti ya Fungu 46 imepungua kwa **asilimia 6.47** kutoka **shilingi Trilioni 1.51** mwaka 2021/2022 hadi **shilingi Trilioni 1.42** mwaka 2022/2023;

v) Wakati Bajeti ya Mishahara ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 16.32** mwaka 2021/2022 ikilinganishwa na mwaka 2022/2023, Bajeti ya mishahara ya **Fungu 46** imeongezeka kwa **asilimia 10.59**; na

vi) Wakati Bajeti ya Maendeleo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 3.5**, Bajeti ya Maendeleo ya Fungu 46 imepungua kwa **asilimia 1.8**.

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla kumekuwa na ongezeko la Bajeti ya mpango wa maendeleo wa Taifa lakini kuna upungufu wa Bajeti ya fungu 46 kwa mwaka 2022/2023. Ongezeko la Bajeti ya Mishahara ya Mpango wa Maendeleo umepelekea pia ongezeko la Mishahara ya Fungu 46. Hata

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hivyo Bajeti ya Fedha za Maendeleo ya fungu 46 imepungua ukilinganisha na ongezeko la Bajeti ya Maendeleo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa upungufu huo wa Bajeti ya Maendeleo kwa Fungu 46 umetokana na kumalizika kwa muda kwa baadhi ya miradi ya maendeleo kama vile Mradi wa Lipa Kulingana na matokeo (EP4R), Mradi wa Kukuza Ujuzi na Stadi Kazi (ESPJ) pamoja na miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19 (TCRP).

Kielelezo Na. 9: ULINGANISHO WA BAJETI YA TAIFA 2021/2022 NA 2022/2023 (KWA MILIONI)

MATUMIZI	BAJETI KUU YA TAIFA 2021/2022	BAJETI KUU YA TAIFA 2022/2023	PUNGUFU/ONGEZJKO	%
OC	4,189,199	4,493,456	304,257	6.77
MISHAHARA	8,150,509	9,740,753	388,120	16.3
MAENDELEO	14,977,615	15,521,341	356,422	3.5
MFUKO MKUU WA SERIKALI	10,663,278	11,308,365	186,444	5.7
JUMLA	37,980,601	41,063,915	1,379,013	3.46

Chanzo: Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Usanifu wa Kamati.

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo na yale yaliyobainika, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo: -

4.1 VYUO VYA ELIMU YA JUU

Mheshimiwa spika, ili kupata maendeleo katika nchi yetu ni lazima tuwe na dhamira ya dhati ya kuwekeza katika Elimu ya Juu. Mwanasiasa mkongwe wa Marekani Bw. Ronald Lewis aliwahi kusema *"Kuhakikisha ubora wa elimu ya juu ni*

muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kizazi cha baadaye". Katika kuhakikisha utolewaji wa elimu bora katika vyuo vikuu kamati inatoa ushauri ufuatao: -

- (a) Wizara iongeze Bajeti ya Maendeleo ili kutatua changamoto ya upungufu wa miundombinu ya elimu kama vile nyumba za walimu, mabweni, madarasa na maabara katika Vyuo Vikuu Nchini.
- (b) Kamati inaishauri Serikali kuviwezesha Vyuo Vikuu kuwekeza katika kufanya tafiti mbalimbali ili viweze kuongeza mapato ya ndani, kujitangaza na kutambulika kimataifa.
- (c) Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, itenye bajeti ya kutosha kutokana na vyanzo vya ndani ili kuwezesha Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma kujitangaza na kuongeza Udahili katika Ngazi ya Uzamilli na Uzamivu;
- (d) Vyuo vikuu viendelee kubuni na kuanzisha kozi mbalimbali zenyet kuwasaidia wanafunzi kujajiri mara baada ya kumaliza elimu. Kozi zitolewazo ziwasaidie waweze kubuni miradi, kuiendesha na kuisimamia.

4.2 UPUNGUFU WA WATUMISHI

Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa watumishi katika Taasisi za Wizara kama shule na Vyuo Vikuu. Uhaba huo ni pamoja na Uhaba wa Walimu na wakufunzi. Katika kutatua changamoto hii kamati imeshauri yafutayo: -

- (a) Wizara iwe na mkakati wa dhati wa kutatua changamoto hii ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya watumishi ili kukidhi mahitaji katika Taasisi za Wizara hii.
- (b) Serikali iendelee kuajiri walimu wa shule za msingi na Sekondari
- (c) Kamati inaendelea kusitiza vvuo vikuu viendelee kuwa na uhuru wa kitaaluma katika kuajiri watumishi wake hususan wanataluma kwa kuzingatia sheria kanuni na vigezo vya kitaaluma.

4.3 MIKOPO YA WANAFUNZI ELIMU YA JUU

Mheshimiwa Spika, kamati inapongeza Serikali kwa kuendelea kutoa mikopo kwa kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Hata hivyo kamati inatoa maoni yafuatayo: -

- (a) Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia mikopo wanafunzi wa elimu ya kati.
- (b) Kamati inaendelea kusisitiza, Serikali iangalie upya vigezo vya utoaji wa mikopo ya Elimu ya Juu ili kupunguza malalamiko ya kutokuwa na vigezo vya ulinganifu yanayojitokeza mara kwa mara mionganini mwa waombaji na wazazi.
- (c) Serikali iendelee kutafuta vyanzo vya fedha ili kuwapatia mikopo wanafunzi wote wanaohitaji mikopo.
- (d) Bodi ya mikopo ijiendeshe kibenki ili kuwezesha na kurahishishautoaji wa mikopo na ukusanyaji wa mikopo kwa wanafunzi wanaohitaji mikopo.

4.4 UJENZI WA VYUO VYA UFUNDI STADI(VETA)

Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza sera ya kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi Nchini. Ujenzi huu ukikamilika utasaidia watanzania wengi kudahiliwa na baadae kujajiri na hivyo kupunguza tatizo la kutokuwa na ajira nchini. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwepo na uhaba wa walimu katika vyuo hivi. Pamoja na pongezi Kamati inasisisitiza yafuatayo yafanyike ili kuboresha mpango wa ujenzi wa vyuo hivi: -

- (a) Serikali ikamilishe kwa wakati ujenzi wa vyuo 26 vya elimu ya ufundi stadi (VETA) unaoendelea Nchini.
- (b) Kuwepo na Mkakati wa kuhakikisha Halmashauri zote nchini zinakuwa na Vyuo vya Elimu ya Ufundi Stadi ili kutoa fursa kwa vijana katika Halmashauri kupata Elimu hiyo;

(c) Ujenzi wa Vyuo hivi vya Ufundu Stadi uende sambamba na kuajiri walimu wa kutosha watakaoweza kuwafundisha wanafunzi wanaosoma katika vyuo hivyo.

4.5 MADAWATI YA JINSIA SHULENI NA VYUONI.

(a) Kuanzishwe madawati ya jinsia katika ngazi za Elimu kuanzia sekondari hadi Elimu ya Juu ili kuwezesha vijana kupata elimu ya Afya ya Akili, namna ya kukabili athari za unyanyasaji wanaokumbana nao ukiwemo unyanyasaji wa kingono.

(b) Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali Wizara ihamasishe wazazi kuongea na vijana wao kuhusu hatua za mabadiliko ya mwili na elimu ya afya ya uzazi.

(c) Wizara iwekeze katika kutoa mafunzo ya elimu ya afya ya uzazi kwa walimu ili kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu hiyo na wanakuwa na maadili;

4.6 USIMAMIZI WA MIRADI YA MAENDELEO

(a) Kamati inashauri Serikali kuwe na umakini katika usimamizi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha ili kuwezesha kupatikana kwa thamani halisi ya fedha na kukamilika haraka kwa miradi hiyo.

(b) Miradi ya ujenzi ya vyuo vya elimu inayoendelea izingatie uwepo miundombinu yenye kuwezesha kutatua mahitaji ya msingi ya makundi maalum ya wanawafunzi kama vile wanafunzi wa jinsia ya kike wenye Watoto na watu wenye ulemavu

(c) Kamati inasisitiza kuongeza kasi ya utolewaji wa fedha za miradi mbalimbali inayoendelea ya ujenzi na ukarabati wa vyuo vikuu na kuwe na usimamizi mzuri wa miradi hiyo ili ikamilike kwa wakati na kuweza kutimiza lengo la kuanzishwa kwake.

4.7 MITAALA MIPYA YA ELIMU

Kamati inaendelea kushauri Serikali iharakishe mchakato wa kupitia maoni ya wadau kuhusu mitaala mipya ya elimu ili iweze kupatikana kwa wakati na kuanza kutumika na hivyo kusaidia kuboresha elimu nchini; mitaala

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru tena kwa nafasi uliyonipa ya kuweza kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb pamoja na wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa na zaidi katika kushiriki vyema katika vikao vya Kamati kikiwemo cha uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hili. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo: -

- | | |
|--|----------------|
| 1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb | - Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb | - M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb | - Mjumbe |
| 4. Mhe. Eng. Samwelii Hhayuma, Xaday Mb | - Mjumbe |
| 5. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb | - Mjumbe |
| 6. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele, Mb | - Mjumbe |
| 7. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb | - Mjumbe |
| 8. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb | - Mjumbe |
| 9. Mhe. Francis Leonard Mtega, Mb | - Mjumbe |
| 10. Mhe. Latifa Khamis Juakali, Mb | - Mjumbe |
| 11. Mhe. Kabula Enock Shitobela, Mb | - Mjumbe |
| 12. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb | - Mjumbe |
| 13. Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu, Mb | - Mjumbe |
| 14. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb | - Mjumbe |
| 15. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb | - MJumbe |
| 16. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb | - Mjumbe |
| 17. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb | - Mjumbe |
| 18. Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mb | - Mjumbe |
| 19. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb | - Mjumbe |
| 20. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, Mb | -Mjumbe |
| 21. Mhe. Khamis Kassim Ali, Mb | Mjumbe |

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- | | | |
|---|---|--------|
| 22. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb | - | Mjumbe |
| 23. Mhe. Hassan Zidadi Kungu, Mb | - | Mjumbe |
| 24. Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb- | | Mjumbe |
| 25. Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb | - | Mjumbe |
| 26. Mhe. Prof Kitila Alexander Mkumbo | - | Mjumbe |

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe na Naibu Spika, kwa kuendelea kuongoza vyema Bunge letu. Hakika ninyi ni viongozi wa mfano.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda (Mb), Naibu Waziri Mhe. Omary Shaban Kipanga (Mb), Makatibu Wakuu wa Wizara hii wakiongozwa na Prof. Eliamani Sedoyeka - Katibu Mkuu, Prof. James Mdoe - Naibu Katibu Mkuu na Prof. Caroline Nombo - Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati wote pamoja na kushiriki vyema katika vikao vya uchambuzi wa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano ambao amekuwa akiipa Kamati yetu katika kutekeleza majukumu ya Kamati Kiufanisi. Pamoja nae, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein na Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu Ndugu Gerald Magili, Msaidizi wa Kamati Ndg. Jane Ndulesi na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila vikwazo. Kipekee tunawashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu Ndg. Francisca Haule, Ndg. Happiness Ndalu na Ndg. Emmanuel Mdidi na Ndg. Chacha Nyakega kwa kuendelea kuishauri vyema Kamati na kuhakikisha majukumu ya Kamati yanatekelezwa bila mkwamo ikiwemo kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia **Fungu 46** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, jumla ya **Shilingi**

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

1,421,004,355,000.00 na Fungu 18 jumla ya Shilingi 2,709,163,000.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono Hoja.

Stanslaus H. Nyongo (Mb),

MWENYEKITI

KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII

10 MEI, 2022

NAIBU SPIKA: Ahsante Makamu Mwenyekiti kwa kusoma vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza uchangiaji na tutaanza na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Nyongo, jiandae Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, jiandae Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, jiandae Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kuanza kuchangia katika Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kipekee kabisa kwanza nitoe pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, hasa pale alipoweza kupata mkopo wa Trillioni 1.3. Ni kwamba, fedha zaidi ya Billioni Mia Nane na Hamsini na kitu ambayo ni sawa na asilimia kama 75 ya fedha hizo zimekwenda kwenye huduma za jamii, kwa maana kwamba, zimekwenda kujenga madarasa, kwa maana ya sekta ya elimu, lakini vilevile fedha zimekwenda kujenga miundombinu ya sekta ya afya. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake huo mzuri wa kupeleka huduma za jamii kwa wananchi wake. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitoe pongezi kubwa sana kwa Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda na Naibu wake Mheshimiwa Omari Kipanga, vilevile nimpongeze sana Katibu Mkuu wa Wizara hii, Profesa Eliamani

Sedoyeka, pamoja na Makamu wake wawili ambao ni Profesa James Mdoe pamoja na Profesa Caroline Nombo, watu hawa wamekuwa waungwana sana Pamoja na Watumishi wote wa Wizara hii kwa sababu wamekuwa ni watu wasikivu na wanapokuja kwenye Kamati yetu kwa kweli tunaongea kwa kuelewanana nia yetu ni moja na njema ya kutumia wanachi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hawa wamekuwa waungwana sana pamja na watumishi wote wa Wizara hii kwa sababu wamekuwa ni watu wasikivu na wanapokuja kwenye Kamati yetu kwa kweli tunaongea kwa kuelewana na nia yetu ni moja na nia ni njema ya kutumikia wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba, Wizara hii ni muhilmu sana na ni Wizara nyeti kwa kizazi chetu cha Tanzania. Kwa hiyo niendeleee kusisitiza yale malengo endelevu ya milenia ambayo yanatuelekeza angalau 20% ya fedha za bajeti ziende kwenye sekta ya elimu, hilo tulizingatie. Tukifanya hivyo *at least* kwa 17% tutakuwa tumeweza kutatua changamoto nyingi ambazo zipo katika sekta hii au zinazoikabili sekta hii ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Kamati na wajumbe wenzangu wa Kamati ambao kwa kweli tumefanya kazi kubwa ya kuishauri Serikali. Katika yale maoni ya Kamati ninaendelea kusisitiza kwa mambo mawili matatu; la kwanza, ni kwenye mikopo ya elimu ya juu. Mikopo ya elimu ya juu tumekuwa na tatizo kubwa malalamiko yamekuwa ni mengi sana vijana, wazazi wanalamikia hii Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa sababu tumekuwa tukipata fedha, lakini fedha hizo hazitoshii kwa Watanzania wanaohitaji mikopo kwa ajili ya kwenda kujiedeleza katika elimu za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Kamati tumeliona hili na wakati mwagine tumekuwa tunachanganyikiwa kwa sababu hatuelewi lengo kubwa lilikuwa ni nini? Lengo zuri la Serikali tunalitambua kwamba ni kuwawezesha watoto wa elimu ya juu waweze kusoma kwa kupata mikopo, lakini

uchaguzi wa watoto hawa au wale ambao wanapewa kipaumbele kupewa mikopo inakuwa inachanganya, wakati mwingine inaonekana kwamba watoto yatima ndiyo wapewe mikopo, ni kweli mtoto yatima anatakiwa apewe mkopo, lakini wakati mwingine watoto yatima hao hawapati hiyo mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine tunasema kwamba wale waliofaulu vizuri masomo ya sayansi ndiyo wapewe mikopo 100%, wakati mwingine hawapati 100%, wanakomea 40% na 50%. Wakati mwingine tunasema haya basi, wapewe wale watoto ambao wanaonekana wana ufaulu mzuri kwenye masomo labda ya *art* na masomo mengine, bado tunaona kwamba mkanganyiko na watu wengi wameshindwa kuelewa kwamba kipaumbele cha mfuko huu ni kitu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuliwauliza Bodi ya Mikopo, hivi kwa nini tusiwape mikopo watoto wote wa Kitanzania wanaohitaji mikopo ya elimu ya juu bila kujali ufaulu, bila kujali ni mtoto yatima, *so long* anahitaji mkopo huyu mtu anahitaji fedha kwa ajili ya kujiendeleza apewe mikopo. Wakasema kwamba mfuko huu ni mdogo, una bilioni 400 umeongezeka mpaka sasa bilioni 500. Je, ni shilingi ngapi inahitajika ili watoto wote wapewe mikopo hiyo? Wakasema tunahitaji bilioni 800. Hivi kweli kama mikopo hii inatolewa na baada ya muda fulani inarudishwa na hii kumbi ni biashara na wanalipa na *interest* kwa nini tusitafute bilioni 800, mtoto yoyote anayehitaji kukopa fedha apewe mkopo aende akasome.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwa sababu mikopo hii inalipwa mtoto atakwenda kulipa tatizo ni nini? Tatizo hapa ni kwamba ni elimu, tuwaelimishe wazazi kwamba mzazi mwenye uwezo wa kumsomesha mtoto wake elimu ya juu amsomeshe, amuondolee ile *burden* ya kuja kulipa mikopo baadaye, lakini yule ambaye anahitaji kwa nini anyimwe mkopo? Hivi ni nani apate mkopo na nani akose mkopo, nani aende shule nani asiende shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tukasema kwamba ni vizuri Bodi hii ya Mikopo kwa sababu ilianzishwa kuwawezesha Watanzania, ifanye kazi kwa mfumo wa kibenki, wapewe fedha, watoe mikopo kwa riba nafuu baada ya pale wawafulilie waliochukua mikopo walipe taratibu na watoto wengine waende wakasome. Kwa hiyo hili ni jambo ambalo tumesitiza katika Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile mabenki binafsi yapewe na yenye fursa ya kuwakopesha wanafunzi kwa riba ndogo, itafutwe *incentive* kwenye mabenki haya waweze kuwapa mikopo wanafunzi wakasome.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii nimesoma taarifa ya Mheshimiwa Waziri nawapongeza sana *NMB* Mungu awabariki, wametoa bilioni 200 kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaotaka kusoma elimu ya kati. Waendelee na moyo huo waendelee kutoa mikopo kwa sababu tumekuwa tunasitiza hata wale wanafunzi wa elimu ya kati wanaosoma Diploma ufundi mchundo, wanaosoma haya masomo ya *VETA*, wanaotaka kupewa ada shilingi 800,000, shilingi 700,000 au shilingi 600,000 kwa nini wasipewe mikopo? Tunatoa kwenye elimu ya juu tu na kwa elimu ya juu tu yenye tunatoa mikopo, tumefuatilia tumekuta 62% ya mikopo inayotolewa inapelekwa kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya *art*, wakishamaliza kusoma masomo ya *art* wanapokwenda kwenye soko la ajira hawapati ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama watoto hawapati ajira 62% wametoa kwa watoto wanaosoma *art*, watarudisha viyi hizi fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni vizuri kuwapatia mikopo wanafunzi wanaosoma elimu ya kati na kwa kweli Benki ya *NMB* imefanya jambo jema na nawaomba na mabenki mengine wajitolee, wawape mikopo wanafunzi wanaosoma elimu ya kati kwa sababu ndiyo wanaoajirika kwa haraka na ndiyo wanaopata ajira haraka na ndiyo wanaoweza kurudisha mikopo hiyo kwa haraka. Tunaomba sana hilo lifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie, suala la watumishi, sekta ya elimu inahitaji Walimu, Walimu hatuna. Sasa hivi tunajenga *VETA* kila wilaya na nawaomba nichukue fursa hii kuomba wilaya yangu ya Maswa wanijengee *VETA*. Wakishajenga *VETA* Walimu wa kuwafundisha watoto ufundi wako wapi? Tuwe na *special program* ya kufundisha Walimu watakaokwenda kufundisha ufundi kwenye *VETA*. Walimu wanaofundisha sasa hivi wana ile teknolojia ya zามانى chuma wanaunganisha kwa zile *sticker* wakati siku hizi kuna teknolojia mpya wafundishwe teknolojia mpya, wapewe vifaa nya kisasa, watoto hawa wafundishwe elimu ya ufundi katika shule hizi, lakini wafundishwe na Walimu walio-*qualify*. Tumejenga madarasa vizuri tunashukuru, tunajenga *VETA* tunashukuru, lakini program ya Walimu ianzishwe ili kusudi ikawafundishe vijana hawa.

Mheshimiwa Nailbu Spika, mwisho, Vyuo Vikuu vyetu ukienda kuangalia Vyuo Vikuu tumekwenda Chuo Kikuu cha Mkwawa, kuna Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanafunzi wamejaa wanaosoma *undergraduate simply* kwa sababu wanapata mikopo ya elimu ya juu. Tumeenda Mkwawa tumekuta wanafunzi zaidi ya 8,600 wanaosoma *undergraduate*, tukauliza wanafunzi wanaosoma *Masters* wako wangapi? Tukaambiwa wako 57 tu kwa nini? Hakuna wanaojiunga, kwa nini hawajiungi? *They are comfortable* kwa sababu wanafunzi wanakuja wana mikopo ya elimu ya juu. Wanaosoma *Masters* na *PhD* hawana mikopo sasa hawawezi kuja hawa watu kama hakuna *sensitization*.

Tunaomba Vyuo Vikuu viwape fursa watu wanaofanya *marketing waka-market* kwa watu wanaotaka kusoma *Masters* wajunge katika kozi hizi ili vyuo vikuu hivi viweze kuwadahili wanafunzi wa *masters* na *PhD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ahsante kwa kunipa fursa. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Profesa Mkumbo, Mheshimiwa Dkt Thea na Mheshimiwa Festo Richard Sanga wajiandae.

MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Mwenyekiti wangu wa Kamati Mheshimiwa Nyongo kwa kupongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote akiwepo Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya. Niwapongeze sana kwa maboresho ambayo yanaendelea kuboresha sera pamoja na mitaala yetu, tunawatachia kila la kheri na sisi tutawapa ushirikiano wote kama Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatekeleza dira ya maendeleo na Mpango wetu wa Tatu wa Maendeleo, nyenzo kubwa ya kutekeleza hayo ni uwekezaji katika rasilimali watu. Nyenzo kubwa ya kujenga rasilimali ni elimu na nyenzo kubwa ya kutoa elimu ni Walimu. Mchango wangu leo ni kuhusu Walimu na hasa kwenye kuchangia kwenye maboresho ambayo yanaendelea katika taaluma ya ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Profesa Issa Shivji aliwahi kusema, mmoja wa maprofesa maarufu hapa Profesa wa kisomo, ukitaka Taifa bora boresha elimu, ukitaka kuboresha elimu boresha Walimu, ukitaka Taifa la watu wanaojiheshimu heshimu Walimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu Nyerere aliwahi kusema na namnukuu pia, alisema kwa Kiingereza: "*No education policy however good can succeed, without well trained professional carder.*" (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo maboresho ambayo tunayafanya haya ya kisera na kimitaala, yatafanikiwa sana kama yakienda sambamba na uwekezaji katika taalum ya ualimu na Walimu wenyewe. Kada ya ualimu Tanzania ina changamoto nyingi lakini naomba nizitaje tatu tu na nitoe mapendekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tumeshasema na Mheshimiwa Mwenyekiti wangu amesema tuna changamoto ya uhaba wa Walimu tulishalisema hapa, tuna upungufu sasa hivi 175,000 takriban 40% lakini changamoto kubwa zaidi ni kwa upande wa Walimu wa sayansi. Kwa sasa kwa mfano

tunahitaji Walimu wa sayansi na hesabu 70,327, waliopo ni 23,647, unazungumzia upungufu wa 66%, takriban theluthi mbili, huwezi kujenga uchumi wa viwanda bila sayansi, hesabu na teknolojia. Kwa hiyo, ni lazima tuwekeze katika *ku-train* Walimu wa hesabu, sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2026 tutakapomaliza kutekeleza mpango wetu wa maendeleo ambao tunao, inakadirisha kwamba tutakuwa na wanafunzi wa elimu ya awali msingi na sekondari 23,600,000. Hawa tutahitaji Walimu 724,000, maana yake changamoto ni kubwa. Kwa hivyo tunazungumzia ili tuweze *ku-cover* hizi changamoto tufikie hayo malengo ambayo tumejiwekea, tunahitaji kuajiri Walimu kila mwaka takriban Walimu 100,000. Sasa hivi tunaajiri Walimu 10,000 hiyo itachukua miaka zaidi ya 18 kuweza kuziba pengo. Sasa hiyo ni changamoto ambayo lazima tulone.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili kwa upande wa Walimu ni kwamba, Mwalimu ana mabosi wengi mno. Moja Mwalimu anaajiriwa na Mkurugenzi wa Halmashauri, anapandishwa cheo na Tume ya Utumishi ya Walimu, Mwalimu akiwa na shida ya mshahara wake inabidi aende kwa Katibu Mkuu Utumishi, Mwalimu akiwa na changamoto na mitaala inabidi aende Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Juzi mwaka 2018 tukaunda Bodi ya Walimu inaitwa *Tanzania Teachers Professional Board* ambayo ipo upande wa Wizara ya Elimu maana yake na senyewe inakwenda kumbebesha Mwalimu mzigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya tatu kwa leo ni ukweli kwamba ambayo wote tunajua ni maslahi duni kwa Walimu wetu na kukosekana kwa motisha. Nataka nitumie muda uliobaki nitoe mapendekezo saba kwa ajili ya kuboresha na kutatua hizi changamoto ninazozitungumza. Mapendekezo saba ambayo yataingia Mheshimiwa Waziri akiyapenda aingize katika mchakato wake wa maboresho. Changamoto ya kwanza kuhusu kupunguza upungufu wa Walimu napenda kutoa mapendekezo manne ambayo yatatusaidia kupata Walimu 44,000 kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, hakuna shaka kwamba Serikali pekee yake kwa ukubwa wa changamoto ya Walimu kwa maana ya idadi haitawenza kujibu hii changamoto, kwa sababu tunazungumzia kuajiri Walimu 100,000 kila mwaka, maana yake Serikali iache shughuli zingine zote ishughulike Walimu tu, hicho hakitawezekana. Napendekeza Serikali tuweke mazingira mazuri ya kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika elimu kwa sasa kwa mfano katika elimu ya msingi tupo chini ya 10% ya shule ambazo zinamilikiwa na *private sector*, kwa nini? Kwa sababu nydingi lakini mojawapo ni kwamba tuna kodi 13 katika shule. Ukianzisha shule hapa, utalipa kodi 13 haya mazingira yanafanya ada ziwe kubwa, mazingira yanafanya watu washindwe kufungua shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wetu wa halmashauri waelekezwe kwamba wewe kufungua shule hapa *City Council* Dodoma, mtu akifungua shule yake wanafunzi wanaokwenda pale, inamsaidia Mkurugenzi wa Halmashauri kwa sababu wale wanafunzi, vinginevyo angewabeba yeeye, lakini Wakurugenzi wetu wanakimbilia sana ile *service levy*, kwa hiyo tuweke mazingira hayo. Tukifanya hivyo tunakadiria kwamba tuna uwezo wa kuongeza Walimu mpaka tukapata Walimu 5,000 kutoka *private sector*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la pili, Serikali iweke malengo ya kuajiri Walimu 20,000 mpaka 30,000. Tukiwaajiri Walimu 20,000 inaweza ikasaidia kuliko kuajiri walimu 10,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la tatu, muda wa mafunzo ya ualimu katika Vyuo Vikuu uongezwe, uwe miaka minne na ule mwaka wa nne wote utumike kwenye mafunzo mashulenii. Kwa hiyo tutapata Walimu kati Walimu 15,000 mpaka Walimu 20,000 kila mwaka kutoka katika vyuo vikuu na hawa hatuwalipi wanaendelea kulipwa na Bodii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la mwisho hapa, tupunguze nafasi ya utawala katika elimu, tufute kada ya Maafisa Elimu Kata, tuimarishe menejimenti ya shule ili watu

hawa waende kufundisha. Tunazungumzia kupata Walimu 3,956, hakuna sababu ya kuwa na Maafisa Elimu wa Kata, hakuna sababu kama tuna uongozi imara wa shule, kwa nini tuwe na Afisa Elimu wa Kata, kwa hiyo tuondoe hiyo watu wakafundishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la mwisho kwenye upande wa motisha, sasa niingie kwenye motisha kwa sababu ya muda ni suala la motisha kwa Walimu. Naomba kwa heshima na taadhima turudishe posho ya kufundisha kwa Walimu (*teaching allowance*). Tunazungumzia kitu kidogo, tunazungumzia Sh.4000 kwa siku kwa Mwalimu, maana yake kwa siku tano Sh.20,000 kwa mwezi Sh.100,000. Hii itahamasisha Walimu, ilikuwa ni vitu muhimu sana, walimu wameshaomba mara nyngi, Waziri wa Fedha yupo hapa, hatuwezi kushindwa kuweka Sh.100,000 kwa Mwalimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, tunaomba *Teachers Service Commission...*

NAIBU SPIKA: Waziri wa Fedha nimesikia taarifa au siyo wewe? Siyo wewe au basi endelea.

MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO: Naomba *Teachers Service Commission* ipewe nafasi ya kufanya kazi kikamilifu. Kwa kufanya hivyo, hatuna sababu ya kuwa na *Teachers Professional Board* kwa sababu majukumu yake mengi yapo ndani ya *Teachers Service Commission*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie mchango wangu kwa shukran za pekee kwa hili ambalo limefanyika hapa watu wengi wanalichukulia ni mafuta tu, lakini kitendo cha Mheshimiwa Rais cha kusikiliza maoni ya Bunge, akahestimu badala ya kutangaza mwenyewe jana akaamua kuleta hapa, ni kiwango cha juu cha kuheshimu utawala bora. Ameliheshimisha Bunge na sisi Wabunge tuna wajibu wa kumheshimiwa Mheshimiwa Rais. Tunampongeza kwa hatua hii, tutaendelea kumuheshimisha, tutaendelea kutoa maoni ya kujenga ili Serikali yetu iende vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Rais kwa kweli ameheshimu wananchi waliowatuma Wabunge kuja kusema.

Sasa namwita Dkt. Thea, wajiandae Mheshimiwa Festo Sanga na Mheshimiwa Fatma Toufiq.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nichukue nafasi hii kupongeza Serikali na hasa Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri ambayo wameifanya toka wamekabidhiwa ofisi hiyo na hasa kwa kipindi hiki ambacho wamekaa wanaboresha mitaala na wanaboresha sera katika elimu. Nitakwenda moja kwa moja kwenye *point*, kwanza nitazungumzia kuhusu ajira kwa Wahadhiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeongea mara nydingi kwamba Wahadhiri hawatoshi, wameajiriwa 2017 mpaka 2018 ndio kulikuwa na ajira. Kuanzia hapo wanasema ajira zimeongezeka, lakini siyo ajira mpya yaani ni ajira mbadala, labda mtu ame-*retire* au mtu bahati mbaya amefariki, ndio kunakuwa na *replacement*.

Kwa hiyo ajira zimekuwa ni shida na madarasa yale tunajua ya Vyuo Vikuu makubwa wanafunzi ni wengi bado ajira haitoshi kabisa. Hata leo ukiwauliza hapo mbele wanasema tumeajiri, wanipe *data* wameajiri Wahadhiri wangapi katika kila chou, waje na majibu wameajiri Wahadhiri wangapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo tuliomba, kwa sababu kuna shida hii ya ajira, hebu tuongeze *retirement age* ya maprofesa. Leo timesomewa hapa idadi ya maprofesa waliokuja pale, bado wana nguvu ya kuweza kutoa msaada katika vyuo. mfano juzi tulikuwa na profesa Ishumi, mawazo aliyokuwa ananipa pale mimi mwenyewe nilishangaa akina Profesa Maboko bado akili zao zinafanya kazi safi, kwa hiyo tuongeze *retirement age*.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri alinijibu siku moja akasema hilo tumelichukua. Haya majibu ya kusema hilo tumelichukua sijui wanayachukua wanayapeleka wapi? Sisi tunataka utekelezaji ndiyo unafaa, unalichukua unalibeba unalipeleka wapi? Wazo limetolewa kama linawezekana lifanyiwe kazi, waongeze muda wa maprofesa, miaka 65 bado wadogo sana. Wizara imeona maprofesa walivyo wadogo na wanavyofanya kazi; akina Profesa Ndekidemi bado anafanya kazi ya kutosha. Profesa Muhongo yuko hapa, wanafanya kazi nzuri. Naomba Wizara iongeze *age* ya *retirement* kwenye vyuo vikuu ili hawa watu watusaidie kwenye vyuo vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye mshahara pia. Hawa Ma-VC, nilizungumza. Ma-VC hawana mishahara, yaani wamepewa vile vyeo hawana mishahara. Wakati mwingine inalingana kabisa na wale Wahadhihi wa kawaida. Hivi kutakuwa na heshima kweli katika kufanya kazi? Mtu ni mkuu wa Chuo mshahara wake unalinga na na *lecture* wa kawaida. Hebu Waziri wa Elimu libebe hilo, wewe ni Profesa, unafahamu kazi za maprofesa wenzako huko vyuoni, libebe hilo ukalifanyie kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika vyuo vikuu, ipo haya ya kuruhusu *freedom* katika *academics*. Tuwaachie uhuru vyuo vikuu kwenye suala la taaluma lisiingiliane na watu wa Utumishi. Zamani kulikuwa na utaratibu, wale wanaofanya vizuri tunawabakiza pale na wanachaguliwa na wetu wenyewe pale pale vyuo vikuu. Anabaki pale kama *tutorial assistant* baadaye analolewa, anafanyiwa *mentoring*, anapanda, anaenda kusoma mpaka anakuwa na *Ph.D*; lakini tukiliondoa hilo kwenye upande wa taaluma, yaani *University* hazina *freedom* kabisa. Hiyo lazima tuiangalie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika kuajiri, tunaposema tuongeze *retirement age* pia tuhakikishe sasa hivi *Universities* ziwe kweli *universal*, tuwaruhusu walete maprofesa kutoka nje ya nchi. *University* zetu kweli jamani zimekuwa *local; very local*. Tuwaruhusu walete maprofesa

kutoka nje ili kweli tuweze kupata elimu mchanganyiko inayokidhi haja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye hizi suala za fedha za *HIT*. Fedha za *HIT*ni mkopo na mikopo huwa inalipwa na wote, na vyuo vyote. Naomba mgawanyo wa fedha uende kwenye *Private Universities* na *Public Universities*. Siyo unanijibu hapa siku moja Mheshimiwa Waziri unaniambia kwamba na wale *private* watapata kamgao *as if* wao hawastahili. Inapokuja mikopo hapa, tunalipa wote na sehemu zote zinalipa mikopo sawa kuititia kodi. Kwa hiyo, naomba Wizara ihakikishe ije na majibu mazuri kwenye ule mgao wa *HIT*; *Private Universities* wanapata vipi na *Public* wanapata vipi? Kwa sababu hawa watoto wanaosoma ni watoto wetu sote. Kwa hiyo, hata yale manufaa ya mkopo wayapate wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nipongeze kwenye...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Ni kengele ya ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zinazofanywa na *TET*; hawa *TET* (Taasisi ya Elimu) kazi yao ni kuandaa mitaala, kufuatilia na kutoa mafunzo. Mwaka 2005 wakati imekuja hiyo programu ya ufundishaji mahiri (*competence base*) walimu hawakupewa *training* ndiyo maana leo hii tunalalamika hapa, walimu hawajui kufundisha, wanawafundisha watoto hawawezi wakawa na *skills* kwa sababu hii programu walimu hawakupata mafunzo na kama walipata, walipata wachache mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naiomba Wizara, kwa sababu mmekaa mnaandaa hii mitaala na tumeipigia kelele sana hapa Bungeni, inapokuja kwenye kutoa mafunzo, tuwape fedha za kutosha hii taasisi ili watoe hayo mafunzo, lakini niwaombe hawa wanaotengeneza mitaala, waangalie

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ule mfumo wa chakula, nami nipo tayari kwenda kusaidia hata bila posho; mfumo ule wa chakula na mfumo wa uzazi wauangalie vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mfumo wa uzazi toka mwanzo tunafundisha tohara ni muhimu. Sasa kwenye mfumo wa uzazi waanze kuingiza ukeketaji ni haramu, waweke kwenye mfumo wa uzazi. Watoto wakianza kujengeka toka mwanzo kwenye ile *reproduction* kwamba ukeketaji haufai, itawajengea hiyo kuelewa na huo ukeketaji tunaoupigia kelele unaweza ukapungua. Ukeketaji ni ukatili, wekeni ndani ya mfumo wa uzazi mnapokwenda kurekebisha hiyo mitaala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia angalieni mfumo wa chakula. Kwenye ule mfumo wa chakula andikeni umuhimu wa chakula; umuhimu wa chakula kwa watoto wa kike na watoto wa kiume. Sasa hivi huu mfumo wa chakula unaambatana na uzazi. Leo hapa tunalalamika vijana wengi hawana nguvu za kiume. Inaanzia kwenye mfumo wa chakula. Kwa hiyo, watu wa mitaala andikeni pale, vijana wale chakula gani? Wewe... (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Daktari.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Namwita Mheshimiwa Festo Sanga, jiandae Mheshimiwa Fatma Hassan. Nafikiri Mheshimiwa Festo ndiye atakayetumalizia mchango wetu wa leo, Mheshimiwa Festo.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze nichangie kwenye Wizara ya Elimu. La kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa

hotuba yake nzuri na inayoonesha mwelekeo mpya kwenye Wizara ya Elimu. Nina mambo matatu nataka kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza nataka kuchangia kuhusu Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978. Mheshimiwa Waziri katika mambo yako saba ambayo unataka kuyafanyia kazi kwenye Wizara ya Elimu, umeyaorodhesha kwamba mojawapo ni Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978. Ninakupongeza na ninaomba tu nikukumbushe jambo moja kwamba, mmesema mmekusanya karibu maoni 100,000 kama siyo 1,000,000; mfumo wetu wa elimu umekuwa ukichezewa sana. Katika mabadiliko ya sheria ambayo mnaenda kuyafanya, mojawapo ni kuhakikisha jinsi gani tunakwenda kuilinda elimu yetu isipate mawazo ya mtu binafsi yakaingizwa kwenye mfumo wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye nchi hii kuna mambo ambayo yametokea takribani matano kama siyo sita ambayo naweza kusema ni ya ovyo au siyo ya ovyo, lakini ni mambo ambayo yanaonesha ni jinsi gani elimu yetu inachezewa. Uki msikiliza Nelson Mandela kwenye kitabu chake cha *Long Way to Freedom* anasema: "*Education is a most powerful weapon which you can use to change the world.*" (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye nchi yetu Mawaziri kadhaa wamepita na wamekuwa wakifanya maamuzi ya ajabu ajabu sana. Kuna Waziri siku moja aliamka akafuta UMISETA kwenye nchi hii, kwenye michezo; kuna Waziri siku nyiningine akaamua kuchanganya *Chemistry* na *Physics* kuwa somo moja; kuna Waziri akaja akaondoa *Division* kwenye nchi hii akaweka *GPA*. Namshukuru Mheshimiwa Mama Ndalichako alikataa. Aliporudi kuwa Waziri, akairudisha *Division*. Siyo hayo tu, kuna mambo mengi sana ambayo Mawaziri mnaamua tu, leo hii elimu ya nchi ielekee huku, leo elimu ielekee huku mnavyotaka nyie.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba mlete sheria hapa Bungeni tuifanyie marekebisho, tuweke sheria jinsi ya kuilinda elimu yetu isichezewe. Kusiwe tu na kikundi cha mtu

mmoja anaamua kubadilisha elimu yetu ifanye inavyotaka. Lazima ipate *public opinion* kuanzia Wabunge na hata wananchi ili tunapofanya mabadiliko yoyote, yawe ni mabadiliko yenyé tija kwa Taifa letu. Siyo Waziri tu anaamka leo kutokana na utashi wa Profesa Mkenda, leo akiamua kufuta *Form Three*, anafuta. Hapana, lazima tuwe na namna ya kuilinda elimu yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuchangia ni kwenye utitiri wa kozi kwenye vyuo yetu. Mheshimiwa Waziri, ubora wa elimu yetu umeendelea kupungua kila siku. Ubora wa elimu yetu unapungua kutokana na kuondoka kwenye mlengo wa vyuo kadha wa kadha ambavyo Mwalimu Nyerere alivianzisha kwa makusudi. Kwa mfano, kuna chuo kama cha *SUA (Sokoine University)* kilianzishwa kwa ajili ya mambo ya Kilimo, lakini leo wanatoa *education*, tofauti kabisa na malengo ya chuo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Chuo cha Ardhi ambacho kilianzishwa kwa malengo ya vijana wetu kusoma kuhusu Ardhi, leo wanaotoa *Accountants* na *Finance*. Ukienda kwenye Chuo cha *UDOM*, wakati tuna *MUHAS* ambayo inahangaika na masuala ya udaktari wa mifupa na binadamu, leo *UDOM* wanatoa hiyo kozi pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo viro tofauti tofauti ambavyo vimekuja kutuvuruga. Mzumbe kilianzishwa kwa ajili ya Sheria na Utawala, lakini leo nenda kuna kozi za *Education* na *Tourism*. Kwa nini wanafanya hivi? Wanafanya hivi ili wafanye *enrollment*ya wanafunzi wengi wapate fedha, kwa ajili ya kuendeshea vyuo vyao. Hili Taifa haijafikia uwezo huo wa kushindwa kupeleka fedha kwenye vyuo, hadi vyuo vinaenda kuingiza kozi ambazo ni nje ya mlengo wa chuo husika ili wapate fedha kwa sababu ya *enrollment* ya wanafunzi na *pressure* ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, hakuna *relationship* au mahusiano ya karibu kati ya Wizara ya Elimu, Wizara ya Utumishi na *TCU*. Nataka nikupe mfano Mheshimiwa Waziri; kwenye meza yako leo watu wa ADEM pale Bagamoyo, kile

Chuo cha Bagamoyo ni kwa ajli ya *Short Courses*, leo hii *TCU* imewapitishia waanze kufundisha *ADEM* kwenye suala la Uongozi, wanasema Udhibiti wa Elimu, wakati kwenye Utumishi ukienda hakuna ajira inayohusisha Mambo ya Udhibiti wa Elimu. Wale wameanzisha kozi ambayo wao na *TCU* wameelewana lakini hakuna mawasiliano na Wizara ya Utumishi. Kwa hiyo, tunaenda kuzalisha watu ambao baadaye wanakwenda kukaa kwenye benchi, wanaanza kulalamika kuhusu ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, pitia vyuo vyote; kama *SUA* tulianzisha kwa ajili ya kilimo, angalia kozi zinazotolewa pale ziwe za Kilimo. Kama *DUCE* ilianzishwa kwa ajili ya *Education*, *DUCE* ina uwezo wa kuzalisha *branch* nydingine kwa ajili ya *Education*. Siyo kwenda ku-*impose* kwenye vyuo vingine. Leo tutashangaa *IFM* nao wanaanza kutoa *Education*. Itakuwa ni nchi hii Mheshimiwa Waziri? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba na kumsihi sana Mheshimiwa Waziri, yeye ni *academician*, ni msomi, tunategemea sana kwamba ataenda kufanya *reformation* kwenye mfumo wetu wa elimu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Mama Ndalichako aliamua kufuta majoho, maana yake mliamua kuidhalilisha elimu yetu, hadi chekechea wakawa wanavaa majoho, na nyie mpo tu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Mama Ndalichako, leo hii angalau; kwa sababu ilikuwa mtu ukivaa joho lazima ulipambanie. Siyo tu mtu kutoka chekechea anavaa joho; ataona wapi umuhimu wa elimu? Ni kwa sababu nyie Mawaziri mnafanya *business as usual*, mmetulia, mmekaa, nawaomba mfanye *reformation*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaenda sawa sawa na mlundikano wa vitabu kwenye mfumo wetu wa elimu. Leo hii Eng. Chiwelesa akiamua kuandika kitabu, anakiingiza kwenye mfumo wetu wa elimu na kinatumika. Hakina ithibati, hakina chochote, na ukienda kila darasa vitabu viro vingi, havina utaratibusi wowote ule, kiasi kwamba tumeanza kuwachanganya Watoto. Huyu *definition* ya *geography*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ilisomwa hivi; huyu *definition* ya *geography* anajua hivi; huyu *definition* ya *biology* anajua hivi, huyu definition ya biology anajua hivi. Tumeruhusu mlundikano wa vitabu kwenye mfumo wetu wa elimu, vitabu ambavyo havina ubora havina ithibati ya Serikali kwamba viweze kutumika kwenye mfumo wetu. Ninakutegemea sana kama yangu Mheshimiwa Mkenda, utatusaidia kubadilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sheria iletwe hapa ili na wewe usifanye maamuzi unayojsikia kwanza leo unataka uibadilishe elimu yetu unavyotaka. Lete sheria tuweze kubadilisha ili sheria yetu tuweze kuiwekea ukingo, isianze kutumika ovyo ovyo. Tunaomba pia kwenye vyuo; vипитие vyote ujue vinavyofanya ndiyo yale malengo yaliyokusudiwa au ni *pressure* ya kupata fedha ili waweze kuendesha vyuo vyao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Nami niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hili alilolifanya leo. Hiki alichokifanya Mheshimiwa Rais kuweka fedha kwenye mafuta ndicho ambacho Watanzania wengi leo miyo yao imetibiwa. Nampongeza sana Rais wangu kwa niaba ya wananchi wa Makete, tunampogneza Mheshimiwa Rais kwa niaba ya bodaboda, bajaji na wananchi wote wa Taifa hili kwa kusikiliza kilio cha Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Toufiq muda bado upo.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2022/2023 kwa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa

kuandaa bajeti hii. Sambamba na hilo, naomba niendelee kuipongeza Serikali yangu Tukufu chini ya uongozi wa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa mageuzi makubwa sana katika elimu pamoja na ufinyu wa bajeti, lakini kazi inaonekana, hongereni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 76 wa hotuba hii, Wizara imebainisha kwamba ina dhamira ya dhati ya kuongeza fursa na ubora wa elimu ya awali, elimu ya msingi na elimu ya Sekondari, naipongeza sana. Ushauri wangu kwa Wizara, nilikuwa naomba Wizara ione umuhimu wa kuifanya Kurugenzi ya Elimu ya awali iwe peke yake ili kusudi kuipa nguvu ya usimamizi wa karibu na iwe na bajeti ya peke yake. Kwa sababu elimu ya awali ndio msingi ambapo wanafunzi akitoka elimu ya awali, akienda katika elimu ya msingi atakuwa ameandaliwa vyema, hivyo tutakosa wale wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika, maana yake elimu yetu itakuwa bora sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba niishauri Serikali ione umuhimu wa kuwa na kurugenzi maalum ambayo itashughulikia elimu ya awali badala ya Kurugenzi kuwa na Elimu ya Awali, Elimu ya Sekondari, Elimu na Msingi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nizungumzie kuhusu uhaba wa watumishi wakiwemo walimu na wakufunzi; imezungumzwa lakini pia Kamati ya kudumu ya Huduma za Jamii pia imezungumzia hili jambo. Ushauri wangu ni kwamba ili kuwapunguzia walimu mzigo, kuna baadhi ya maeneo ambapo walimu wanafundisha zaidi ya wanafunzi 100, mwalimu mmoja, lakini *ratio* tunajua kabisa kwamba elimu ya msingi ni wanafunzi 45 na Sekondari ni 40. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba hebu Wizara iangalie upya ile ikama, kwamba katika yale baadhi ya maeneo ambayo walimu wamezidi, basi waweze kuwa-*regulate* ili mwisho wa siku tuweze kupunguza hili suala la mzigo kwa baadhi ya walimu kufundisha wanafunzi wengi zaidi. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo katika ukurasa wa 33 wa hotuba hii umezungumzia kuhusiana na udhibiti ubora wa shule pamoja na Vyuo vya Ualimu, pamoja na Serikali kuhakikisha kwamba Elimu ya Awali Msingi na Sekondari na Walimu inafuata kanuni na miongozo iliyopo. Nina ushauri kuhusiana na udhibiti ubora wa elimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Kamati imeonesha kwamba fedha kiasi cha Shilingi bilioni moja kwa ajili ya ukaguzi kwa mwaka 2021/2022 hazikutolewa. Kwa hiyo, naiomba Serikali na Wizara kwa ujumla, hebu watoe fedha hizi, kwa kweli wakaguzi tunahitaji kuwawezesha kifedha ili kusudi waweze kukagua hizi shule zetu na waweze kutoa ushauri ili mwisho wa siku ule upungufu utakaoonekana uweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali itoe fedha kwa sababu kuna baadhi ya maeneo katika Halmashauri, magari yale ya ukaguzi yamelala kwa sababu hakuna fedha za kuziendeshea, lakini pia kuna baadhi ya maeneo kutoka Halmashauri ya Wilaya ni mbali na Makao Makuu, kwa hiyo, wanapokwenda kukagua, *sometimes* wanakuwa hawana fedha. Kwa hiyo, zile fedha zikija kwa wakati, ina maana kwamba wakaguzi hawa watatimiza malengo yao na hatimaye ufanisi wa elimu utatokea. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kuzungumzia ni kuhusu miundombinu ambayo ni pamoja na vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, maabara, mabweni, madawati, meza za walimu pamoja na maktaba. Natambua juhudzi za Serikali, lakini bado kuna upungufu. Hata hivyo, tuendelee kuwapongeza baadhi ya wadau zikiwemo benki mbalimbali ambazo zimekuwa ziki-support katika masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa nilitamani nizungumzie kuhusu maktaba. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia kabisa kwamba katika ukurasa wa 26

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

amezungumzia kuhusiana na suala la Maktaba na kwamba katika shule wameweza kutenga Maktaba 171.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri kuhusiana na suala zima la maktaba. Maktaba zilizokuwepo katika Shule za Msingi na Sekondari zitawasaidia hawa watoto kuweza kujifunza mambo mengi. Takwimu au taarifa mbalimbali zinaonesha kwamba mionganini mwa watu ambao ni wavivu wa kusoma, Watanzania ni mionganini mwao. Ni kwamba Watanzania wengi wanapenda waende wakaangalie gazeti, zile *headings* tu za pale juu na yale magazeti ya udaku, lakini vile vitabu ambavyo vinaweza vikamwongezea maarifa na taarifa ambapo vinaweza vikapatikana katika maktaba, inabidi tuwandae watoto wetu mapema ili kusudi waanze kuwa na utamaduni huo waweze kujisomea na hatimaye iweze kuwaongea maarifa na taarifa. (*Makofii*)

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

TAARIFA

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu kumpa taarifa mchangiaji ya kwamba, mchango wa magazeti ya udaku kwa Taifa hili ni mkubwa. Magazeti ya udaku siyo tu yanaandika habari za ovyo, yana habari za elimu na afya ambazo zinaweza zikamsaidia mtoto kujifunza. Kwa hiyo, naomba asijaribu tu kushusha hadhi ya magazeti haya kwa sabau yametoa mchango mkubwa kwa Taifa letu. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Toufiq, taarifa.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba niendelee. Sikuwa na nia ya kuyadhallisha magazeti haya, badala yake tunachotaka wanafunzi wajifunze kwenye vitabu mbalimbali...

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante, kengele ya pili hiyo.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru kwa mchango mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaendelea na Mheshimiwa Neema Lugangira, Mheshimiwa Benardeta Mushashu na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko.

Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilitishwa hadi saa 11.00 Jioni)

(Saa 11:00 Jioni Bunge Lilirejea)

NAIBU SPIKA: Tukae. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI

HOJA ZA SERIKALI

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA
ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA MWAKA
WA FEDHA 2022/2023**

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Nilimtaja mchana Mheshimiwa Neema Lugangira ajiandae Mheshimiwa Mushashu, ajiandae Mheshimiwa Sekiboko.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii, nami nitachangia katika maeneo mawili; eneo la lishe shulen na eneo la hedhi kwa maana ya watoto wakike kukosa shule kwasababu ya hedhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongelea kuboresha elimu tunaongelea mambo yafuatayo:-

Mitaala jambo ambalo Serikali linaendelea nalo hivi sasa kwa hiyo nawapongeza, madarasa, madawati jambo ambalo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amelifanya kwa kiwango kikubwa na wote tumeshuhudia, vitabu, umeme, maji safi na salama, walimu, suala zima la TEHAMA shuleni tunesikia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba wanalifanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yote haya ili yaweze kuwa na tija ni lazima watoto wetu wanavyokuwa kwenye shule wapate chakula shuleni ni changamoto kubwa sana. Kwanza anafika shuleni hajala, halafu ashinde kutwa nzima shuleni akiwa anasoma huku akiwa na njaa. Wataalam wameshathibitisha kwamba njaa inamuathiri mtoto kuelewa, inamuathiri mtoto kuchanganua yale anayofundishwa na hatimaye inaathiri pia ufaulu wa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa *WFP* walikuwa wamefanya tathimini ya hali ya lishe kwenye shule duniani kote. Kwa hapa Tanzania ripoti yao ya mwaka 2020 ilionesha ya kwamba ni takribani watoto 500,000 mpaka 1,000,000 tu ambao wanapata uhakika wa lishe shuleni. Kwa maana hiyo idadi kubwa ya watoto bado hawapati lishe shuleni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nilichangia mwaka jana naninarudia tena mwaka huu. Ijapokuwa nawapongeza Wizara kwa kuzindua mwongozo wa lishe shuleni lakini mwongozo ule hauna mpango wa jinsi gani ambavyo utatekelezeka na wala mwongozo ule hauna bajeti ya namna gani ambavyo suala hili litatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu spika, Kwa hiyo, mimi ningependa kuishauri Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; kama ambavyo Serikali inapanga mipango mbalimbali na kutafuta wadau kama vile Benki za Maendeleo na Wadau kutoka nchi za maendeleo wafanye hivyo pia katika hili eneo la lishe

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

shuleni. Mwaka jana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alihutubia kwenye mukutano wa *UN Food Systems* kule New York. Moja ya matokeo ya mukutano ule ilikuwa ni kuanzisha kitu kinachoitwa *school meals coalition*. Na *coalition* ile inapanga kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2030 kila mtoto kwenye shule atakuwa anapata angalau mlo mmoja wenyе lishe bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Desemba 2021 *Global Partnership for Education* (GPE) wametoa Dola milioni 580 kwa ajili ya kusaidia nchi za kutoka Barani Afrika kuimarisha lishe shuleni. Katika mpango huo Tanzania haijapata mgao.

Kwa hiyo, mimi ningependa kuwa *challenge* Wizara ya Elimu tuone namna gani na sisi tunanufaika kwenye haya maendeleo mbalimbali ya kidunia. Isitoshe mwenyekiti wa hivi sasa wa *GPE* ni Mheshimiwa Rais Mstaafu Dkt. Jakaya Kikwete. Kwa hiyo, kwa nini tusintumie maana mwenyekiti wa mpango huo wa *GPE* ni Rais wetu mstaafu? Sisi Tanzania iweje hatunufaiki na jambo hilo? Desemba 2021 wametoa Dola milioni 580, nchi za wenzetu kama Nigeria nakadhalika wamepata Tanzania haijapata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vivyo hivyo tukija kwenye *USAID in Foreign Aid* kwenye upande wa agriculture kwenye Serikali ya Marekani mwaka 2021 wametoa Dola milioni 248 kwa ajili ya lishe shuleni, na kila nchi imepata Dola milioni 25 za kuimarisha lishe shuleni, Tanzania haijapata mgao, kwa nini? Na *window* ya hivi karibuni ya kuomba ufadhilli huo *USAID* ilikuwa ni mei 6, 2022, wiki iliyopita tu; zote hizi ni *grants*. Kwa hiyo mimi niwaombe Wizara ya Elimu ibebe ajenda hii ya lishe kwa uzito mkubwa kwa sababu yote haya tunafanya ikiwa watoto hawafundishiki kwa sababu ya njaa tunafifisha jitihada kubwa za Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa TAMISEMI kwenye kitengo chao cha lishe wanasema kwamba katika kila darasa la watoto 45, 15 hawafundishiki. Sasa kama 15 hawafundishiki kwanini baadaye tunakuja kulalamika ufaulu

umeshuka tunalaumu mitaala, tunalaumu walimu ilhali watoto wetu wanashinda njaa hawana lishe shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana nami hata kipindi hiki cha Bunge tulipokuwa kipindi cha Ramadhani tulifupisha muda ili kukidhi, kwa sababu mtu ukishinda na njaa akili haiwezi kufikiri salama, sasa tunategemeaje watoto shuleni waweze kuelewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi kwa mara ya pili tena na kwa masikitiko makubwa bado sijaona *political will* ya kutoka kwa Wizara ya Elimu kubeba ajenda ya lishe; hususani ukizingatia ajenda ya lishe ni moja ya ajenda za kipaumbele za Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan tangu akiwa Makamu Rais na hata sasa akiwa Rais ameendelea kusemea umuhimu wa ajenda ya lishe. Kwa hiyo, mimi naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapo hitimisha aje na mpango mahsusisi wa kuhusu Serikali inapanga kufanya nini ili kuhakikisha kwamba tunaimarisha lishe shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye eneo langu la pili. Mwaka 2021 *NIMR* wamefanya tafiti ya kuona ninamna gani ambavyo suala la hedhi linakosesha elimu watoto wetu wa kike. Kwa haraka haraka tafiti ile ilionesha watoto kuwa wengi wa kike hasa wa vijijini wanakosa shule kwa sababu yakuwa kwenye hedhi; na moja ya sababu ni kwamba hawawezi kumudu gharama za kununua pedi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi najiuliza; Wizara ya Elimu ina programu mbalimbali ambazo zinahusiana na masuala ya *water sanitation and hygiene* ambako jambo la hedhi linaingia pale, wanashindwa vipi kuingiza mkakati au kuja na programu ya kuhakikisha watoto wanaotoka kwenye kaya maskini wanapata tauzo za kike ili wasikose shule kwa sababu ya kuwa kwenye hedhi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi katika eneo hili naomba nipayendekeze, kwamba tunayo *TASAF* ambayo ina jukumu la inahudumia kaya maskini; hivi kwanini kwenye *TASAF* tuisiangalie, kwamba watoto wanaotoka kwenye kaya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hizi maskini kuwe kuna *intervention* ya kuwawezesha wapate taulo za kike ili watoto hawa wa vijiji ni wanaotoka kwenye kaya maskini wasikose shule kwa sababu ya kuwa kwenye hedhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwezi mtoto anakosa siku tano mpaka saba kwa sababu ya kuwa kwenye hedhi, na Serikali imeweka jitihada kubwa ya kuhakikisha kwamba mtoto wa kike apate elimu, wakati jambo la kibailojia, jambo ambalo si sababu amesababisha yeye mwenyewe linamfanya akose shule akiwa kwenye hedhi.

Kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, hii ni mara pili pia nachangia suala hili kwenye Bunge lako Tukufu, bado sijapata majibu yanayoolewaka kuhusiana na Serikali itakuja na mpango gani kuhakikisha kwamba mtoto wa kike hakosi shule kwa sababu ya hedhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi baada ya kusema hayo nasisitiza tena, kwamba Serikali ije na mpango wa kuhakikisha kuna lishe shulenii, Serikali ije na mpango wa kuhakikisha kwamba mtoto wa kike hakosi shule kwasababu ya hedhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana na endapo sitaridhika na majibu ya Serikali nitashika shilingi ya mshahara wa Waziri. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Neema kwa mchango mzuri, wewe siku zote upo mbele kusaidia wanafunzi wetu. Ahsante sana. Mheshimiwa Mushashu ajiandae Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, jiandae Dkt. Paulina Nahato.

MHE. BENARDETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa hotuba nzuri lakini vilevile kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mama yetu, kipenzi chetu ambaye anahangaika huku na kule kuhakikisha kwamba anatuletea maendeleo. Tumeona kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ameifanya katika nyanja mbalimbali kama vile kwenye barabara, kwenye nishati, kwenye elimu, kwenye afya, kwenye maji kote tunaona kwamba tunaendelea kupata maendeleo. Na kwa kutumia hizi fedha alizopata za mpango wa UVIKO basi akaweza kutujengea madarasa 15,000, tukaweza kupata ofisi za walimu 3,184, tukapata matundu ya vyoo 557 katika kipindi kifupi, madawati zaidi ya 47,000 na meza na viti zaidi ya 451,918. Kweli mama ameamua kutuletea maendeleo tunasema mama ahsante sana na nikweli mama anaupiga mwangi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie kuhusu upungufu wa watumishi. Kuna upungufu wa watumishi wengi na hasa katika sekta ya elimu, ambako hapa nazungumzia upungufu wa walimu. Kwa sasa mahitaji ya taifa tunahitaji walimu takribani 274,549, lakini kuna upungufu wa asilimia 37 ya walimu wapatao kama 100,958 kwenye shule za msingi, vilevile tunaupungufu wa walimu 74,743 katika shule za sekondari. Huu ni upungufu mkubwa sana, kama kweli tunataka kutoa elimu bora haiwezekani bila walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkumbuke mwaka 2012 kwamba watoto wa kidato cha pili walifeli wengi humu Bungeni palikuwa hapakaliki, Wabunge walitaka kujua kwanini wanafunzi wamefeli mpaka ikambidi Waziri Mkuu aunde tume, na tume ikaenda kufanyakazi kutafuta kwanini watoto walishindwa. Moja ya sababu waliyoiona ni kwamba, walikuta kwenye shule kuna walimu wachache sana. Kuna shule zilikuwa na walimu watatu, walimu wawili, mwalimu mmoja na hiyo ikachangia *mass failure* ya wanafunzi katika mtihani wa kidato cha nne mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kwamba mwanafunzi anayesoma sekondari anasoma vipindi saba na kuendelea. Kwa hiyo, unapokuta kwenye shule kuna walimu

wanne, watatu, watano ujue kwamba huyu mwanafunzi hakusoma masomo yote. Kuna masomo ambayo hakuwahi kumuona mwalimu, kuna masomo ambayo *syllabus* ameigusagusa lakini hakusoma yote. Lakini ndugu zangu mtihani hauna huruma, mtihani uleule utakapotungwa atatungiwa uleule aliyezeka na walimu wote katika masomo yote na akasoma *syllabus* nzima, atatungiwa huo huo na yule ambaye alikuwa hana walimu wa kutosha. *At the end of story* yule ambaye alikuwa hana walimu wa kutosha atafanya vibaya na tutam-label kwamba amefeli; na hii inakuwa ni hasara kwa mwanafunzi mwenyewe inakuwa ni hasara kwa mzazi, lakini vilevile ni hasara kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie, kwamba umuhimu wa mwalimu ni mkubwa sana. Hata ukiondoa vitabu vyote au ukawafanya wanafunzi wakakaa tu chini mkeka lakini ukawapatia mwalimu mzuri, hata kama unampa huyo mwalimu watoto ambao wanasema hawafundishiki au wale watukutu au wale *slow learners* lakini *as long as* kuna mwalimu mzuri hao watoto watajifunza na watafaulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuongeza ubora wa elimu mimi nilikuwa na pendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Serikali itafute chanzo, ipate chanzo, iajiri walimu wa kutosha kwa wakati mmoja kusudi sasa tuweze kutoa elimu bora. Sasa hivi katika mashule mengi watoto wanapita tu kwa sababu wanasoma nusunusu sababu hatuna walimu wa kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera kuna upungufu wa walimu. Katika shule za msingi tunaupungufu wa walimu asilimia 48.8, na katika Shule za Sekondari tunaupungufu wa walimu asilimia 37.

Niombe basi, Serikali yangu wakati wanaajiri walimu katika Shule za Sekondari Mkoa wa Kagera tupatiwe angalau walimu elfu 2,108 ambao tunawakosa, na katika shule za msingi ambako tunaupungufu wa walimu 8,593 basi tupatiwe hao walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie kuhusu upungufu wa miundombinu. Najua Serikali imefanya juhudini sana za kuboresha kuongeza kukarabati miundombinu ya elimu lakini bado kuna upungufu wa madarasa na upungufu wa shule. Katika Mkoa wa Kagera tunamatatizo hasa katika upungufu wa *High Schools*. Kwa mfano, Wilaya ya Muleba ambayo inakata zaidi ya 40 tuna *High Schools* tatu, Misenyeye tatu, Kyerwa mbili, Karagwe *High School*/moja na Bukoba Vijijiini *High School* moja. Tunatambua kwamba hizi shule ni za kitaifa lakini unapowachagua watoto ambao niwatoka katika kaya maskini ambao wazazi wao wana uwezo mdogo unakuta wanarudi kuomba kwamba waendelee kusomea kwenye mikoa ileile kwa sababu ya zile gharama za kuwasafirisha. Kwa hiyo, ninaomba Serikali itusaidie waweze kutuungezea shule zenye *High Schools* waweke mkakati kuhakikisha kwamba shule zenye *High Schools* zinajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mrundikano mkubwa wa wanafunzi shulenii. Pamoja na juhudini kubwa za kuongeza shule lakini hasa katika Wilaya ya Biharamulo ndugu zangu ni balaa. Najua hii inatokana na mafanikio makubwa ya elimu bila malipo lakini vilevile ni kwa sababu afya zetu ni njema, tunakula vizuri na tunazaa sana, kwa hiyo, tunawanafunzi wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano; kwenye shule ya Kabindi ambayo iko kwenye Kata ya Kabindi katika shule moja ya msingi kuna watoto 2,672, Muungano kuna watoto 2,366, Nyamarangara kuna wanafunzi 2,828 hiyo yote ni Biharamulo tu. Kikomakoma - Kabindi kuna wanafunzi 3,920, Munzani ambayo ipo Nyakaura kuna wanafunzi 3,992, Shule ya Nemba ambayo ipo katika Kata ya Nemba kuna wanafunzi 5,248 katika shule moja na shule ya Nyakanazi ambayo ni Nusaunga inawanafunzi 6,063.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu *imagine* huyu Mwalimu Mkuu anawezaje kuongoza shule ambayo ina watoto 6,063, 5,000, 4,000? Lakini pia hao walimu wana mzigo kiasi gani ambao wanafundisha? Hawa watoto ni kweli

wanafundishwa au wanakwenda pale wanashinda wakicheza? Ndugu zangu mlione hili kama dharura, tusaidieni Mkoa wa Kagera hasa katika Wilaya ya Biharamulo, tujengewe shule, hasa kwa miradi wa EP4R kabla haijaisha tusaidie. *SEQUIP*tusaidie kusudi tuweze kujenga shule kwenye kata moja kwa mfano yenye watoto mpaka 6,000 tunaweza kujenga shule nyingine tatu ndani ya kata ili kunusuru hao watoto wasiwe wanaenda wanashinda shulenii tu wanacheza waweze kupata elimu ile iliyotarajiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwisho; Mkoani Kagera mnatujengea chuo cha *VETA* kikubwa kizuri cha viwango. Sasa niiombe Serikali yangu tukamilishe kile kituo cha *VETA* ili kusudi kiweze kuanza kutoa elimu na wanafunzi waweze kupata elimu ya ufundi iliyotarajiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Husna jiandae Mheshimiwa Dkt. Paulina.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nikushukuru sana kwa kunipa fursa ili na mimi niweke mchango wangu kwenye Wizara ya Elimu ambayo ni Wizara nyeti na nichanzo kikubwa cha maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaenda kwenye mchango wangu naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuingilia kati na kuona namna ya kupunguza makali ya bei za mafuta nchini, jambo ambalo lisababisha unafuu katika mfumuko wa bei.

Jambo alilolifanya Mheshimiwa Rais ni kubwa. Sisi Wabunge tupo tayari na tuko nyuma yake kuhakikisha kwamba tunaendelea kwenda kuyazungumza hayo mazuri ambayo ameanzisha kuyafanya katika hali hii ya taharuki ya uchumi katika maeneo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Naibu Waziri kaka yangu Kipanga kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Mheshimiwa Mkenda tangu amefika pale, na mimi ni mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii yapo mambo mengi ambayo wajumbe tunamshauri na tunaona hata kwenye taarifa yake amewasilisha kuona kwamba anaithamini kamati yetu na anaona mchango mkubwa unaowasilishwa kuititia kamati na mpongeza na ninamshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa leo nimeupa jina la *quality education*, ni namna gani nchi yetu tunaweza kusogelea elimu yenye viwango. *Quality education* inategemea vitu vingi na ukitaka kumuuliza mtu yoyote maana ya elimu atakwambia ni kuhamisha maarifa kutoka eneo moja au kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine. Lakini vitu ambavyo vinahusika katika kuhamisha maarifa haya ni mazingira ambayo kwa kiasi kikubwa sana naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais na Wizara kwa ujumla kwa namna ambavyo wameimarisha mifumo na miundombinu ya elimu katika maeneo yetu. Zimetumika fedha nyingi sana, zimewekezwa katika kujenga miundombinu ya madarasa, miundominu ya vyuo na ofisi mbalimbali kwenye Idara ya Elimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumapili nilikuwa Wilaya ya Kilindi. Nilitembelea Halmashauri ya Wilaya ile na nilikutana na akina mama wa Wilaya ya Kilindi. Moja ya eneo ambalo walinituma kuja kuzungumzia ni namna gani tunaweza tukaboresha elimu hasa katika Wilaya za Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilindi kwa mfano, wao wamefanya utafiti na wamegundua kwamba watoto wa Kilindi hawafeli tu kwa sababu hawana uwezo wa kufaulu wao kama wao, isipokuwa mazingira yao, ukosefu wa vitendea kazi na homa ya mitihani ndiyo inayowafikisha katika hali hiyo ya kushindwa kufanya vizuri kwenye mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wameenda mbali, wataalam wa elimu, Afisa Elimu Msingi na Sekondari

wameeleza ya kwamba wameunda Jukwaa la Wazalendo wa Elimu wa Kilindi. Lengo lao ni kutafuta *photocopy machine* kwa ajili ya kuziweka kwenye Tarafa zao, kwa ajili ya kuzalisha mitihani. Kwa sababu baada ya kufanya utafiti wamegundua ya kwamba watoto wengi wanafeli mitihani kwa ile homa, tataruki kwenye mitihani kwa kuwa hawana uzoefu wa kufanya mitihani iliyochapishwa. Wamezoea kunakiliwa mitihani ubaoni, wamezoea kufanya mitihani kwenye madarasa ambayo darasa moja watu 80 watu 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukimuweka mtoto kwenye dawati peke yake na ukampa mtihani ambaa uko kwenye karatasi umechapishwa tayari anapata tataruki na pengine inaweza kumsababishia kwa kiasi kikubwa kufeli mitihani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wazo ambalo wamelianzisha Kilindi ni wazo zuri sana. Kwamba moja ya eneo ambalo tunaweza tukaisaidia Serikali kupata elimu bora kwa watoto wetu na tukapunguza *failure* kwa watoto wetu ni kuwapa mitihani mingi zaidi, wapate mazoezi mengi zaidi. Tunaweza kufanya hilo kama tutapeleka hizo *photocopy machine* walau kwenye Tarafa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajenga madarasa ni vizuri na tumefikia kwenye hatua nzuri sana lakini tupeleke hivyo vitendea kazi ambavyo sasa angalau vitaifikisha elimu hii inayotolewa na Shule za Serikali ifanane na zile Shule za *Private*. Watoto wanaosoma *Anne Maria* wanafanya mitihani hata *weekly test* iliyochapishwa. Mtoto anayesoma shule ya kwetu ya Serikali anakutana na mtihani uliochapishwa siku ya *NECTA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili aweze kuzoea hali hiyo ya mitihani, aweze kuwa *settled* ni muhimu sana kwenda kufanya kazi wazo hili ambalo limeanzishwa Kilindi na pengine liambukizwe kwenye nchi nzima ili tufanye vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninatamani kulizungumza ni kuhusu Walimu bora na wanaotosheleza. Zimetolewa takwimu mbalimbali, *ratio* ya Mwalimu mmoja kwa Shule ya Msingi ni kufundisha watoto 45 lakini *ratio* ya Mwalimu mmoja kwa Elimu ya Sekondari ni kufundisha watoto 45. Kwa Mkao wa Tanga, *ratio* ya Mwalimu mmoja anafundisha watoto kuanzia 80 mpaka 200 shule nydingine hii inaleta shida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna upungufu mkubwa sana wa Walimu. Walimu ambao tunahitaji siyo chini ya 200,000 kama ambavyo takwimu zinaonesha. Pamoja na kwamba kasungura ketu ni kadogo, ajira zinatolewa kulingana na upatikanaji wa fedha kwenye Bajeti. Kuna haja ya kuweka utaratibu wa wazi kupunguza minong'ono, kupunguza Wabunge kuendelea kupigiwa simu mara kwa mara kuombwa ajira na vijana wetu. Kwa mfano, tunao watoto ambao wamehitimu vyuo tangu mwaka 2013, 2014, 2015 ni kwa nini sasa Serikali isitangaze kwamba mwaka huu itawaajiri waliohitimu 2015 peke yake au 2013 au 2014? Tukaweka nafasi ya kupunguza simu na meseji kwa Wabunge wanaombwa kusaidia watoto hao kuajiriwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watoto wenye umri mkubwa na unafahamu kwamba mtanzania kwa mujibu wa Sheria ya Ajira anaeajiriwa *permanent employment* ni chini ya miaka 45. Kadri wanavyokaa nje ya soko umri unakwenda kwa hiyo, mwisho wa siku watakosa nafasi ya kuajiriwa. Je, kwa nini sasa tusiwaajiri hata wale wenye umri mkubwa kwanza kwa sababu tunaajiri kwa awamu ili kuweza kuwaondoa kwenye hilo wimbi la kukosa sifa ya kuajiriwa na Serikali? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama katika watoto ambao wanaajiriwa wapo vijana wengi ambao wanajitolea kwenye shule zetu za Serikali, lakini bado kila siku tumekuwa tukiimba humu ndani wapewe kipaumbele wale wanaojitolea. Kwa sababu tuna upungufu wa Walimu na wao tayari walishaamua kujitolea kutusaidia kuziba hizo nafasi za upungufu. Kwa nini zinapotoka ajira wasiangaliwe wakaanza

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuajiriwa hao kabla hawajatazamwa watu wengine?
(*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitaka elimu bora, tukitaka *quality education* tunahitaji pia kuwa na *Quality Insurers* wazuri, bora, wanaowajibika na sisi kuwajengea mazingira ya wao kuwajibika. Katika nchi yoyote elimu hailindwi au haisimamiwi na mtutu wa bunduki. Hutamkuta Polisi anamsimamia Mwalimu afundishe, hutamkuta Afisa wa TAKUKURU wala Afisa wa Usalama wa Taifa wala wa Magereza akimsimamia Mwalimu afundishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo cha usalama kinachosimamia elimu nchini ni Uthibiti Ubora (*Quality Insurers*) wao ndiyo wanaangalia namna gani elimu inatolewa, wana-assure elimu itolewe ambayo inahitajika yenye viwango. Lakini kitu cha kusikitisha hatujawawezesha Wathibiti Ubora, tumewaacha katika mazingira ambayo pengine tumeshindwa kutambua uwezo wao au nafasi yao katika kutekeleza majukumu yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma majukumu ya *Quality Insurers* jukumu lao la pili linasema *carrying out periodic school and center physical conditions survey*, anapaswa kutembelea shule moja au kituo cha kutolea elimu kimoja baada ya kingine lakini hawana magari. Wanaokwenda kumkagua ni Mkurugenzi mwenye shule zake, Mthibiti Ubora anaenda kuomba mafuta, anaenda kuomba gari kwa Mkurugenzi ili aende amkague shule zake. Tutapata viyi hapo elimu bora? (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa mchango wako mzuri.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika mbili niweze kumalizia. Tafadhalii.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Kengele ya pili hiyo.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ushauri wako utachukuliwa, ahsante. Kama ushauri wa asubuhi wa Profesa Mkumbo wa Walimu kwenye Kata kwa kweli kuna mtu ana Kata 25 wanakaa watu 25 kwenye Kata hakuna *impact* yoyote. Kwa hiyo Profesa Mkumbo na wewe ahsante sana kwa mchango wako asubuhi. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Dkt. Paulina Nahato.

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie katika

NAIBU SPIKA: Jiandae Mheshimiwa Dkt. Musukuma. Jiandae Mheshimiwa Eric Shigongo na Mheshimiwa Kishimba.

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia na mimi nichangie katika Wizara hii ya Sayansi, Teknolojia na Elimu. Awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kunipatia nafasi ya kusimama hapa leo na kuchangia katika Wizara hii.

Napenda pia kuchukua nafasi ya kuwapongeza Wizara ya Elimu, Waziri Profesa Mkenda pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Kipanga pamoja na timu yote ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Wizara ya Elimu inafanya vizuri sana. Nami pia nichukue nafasi ya kumshukuru sana Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa kuangalia hii sekta ya elimu na kuipa kipaumbele. Kwa hivi karibuni tumeona madarasa mengi yamejengwa na haya madarasa yaliyojengwa ni dalili kwamba sasa Vyuo vyetu Vikuu vijiandae kuwapokea wanafunzi wengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kila mwanafunzi anayesoma hata kuanzia shule ya msingi ukimuuiliza swali unataka kuwa nani atakwambia nataka kuwa Daktari, nataka kuwa Pilot, nataka kuwa Injinia, nataka kuwa Mwalimu lakini atakuwaje Mwalimu, mwisho wake ni wapi? Mwisho wake ni Chuo Kikuu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba hivyo basi nichangie katika eneo la Vyuo Vikuu. Katika nchi yetu ya Tanzania tuna takribani Vyuo Vikuu 34. Vyuo Vikuu 12 ni Vyuo Vikuu vya Umma, Vyuo 22 ni vya Sekta Binafsi na vilevile tuna Vyuo Vikuu vitatu na ambavyo ni Vyuo Vikuu Vishirikishi kikiwepo Chuo Kikuu Kishirikishi kilichopo Mbeya - *MUST*, kilichopo Iringa – *MUSE* na kilichopo Dar es Salaam – *DUCE*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Vyuo Vikuu hivi vina Wahadhiri 7,647 na hao ndiyo Wahadhiri waliopo katika Vyuo vyetu Vikuu hivi 34. Na hao Wahadhiri wenye elimu ya Uzamivu yaani Shahada ya Uzamivu (*PhD*) ni 2,185 sawa sawa na asilimia 28.6. Wenye Shahada ya Uzamili (*Masters*) ni 3,875 ambaao ni sawa sawa na asilimia 50.7 na wenye *Degree* ya Kwanza ni 1,587 sawa sawa na asilimia 20.8. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii idadi ya Wahadhiri ni ndogo, ukilinganisha na wanafunzi katika Vyuo Vikuu. Hii idadi ni ndogo, matokeo yake ni nini? Ndoto ya wanafunzi wanaofika Vyuo Vikuu inafifia hapa katika Chuo Kikuu. Wanafunzi hawa wamesoma kuanzia Elimu ya Msingi, Sekondari hadi wanafika Chuo Kikuu wanakutana na changamoto ya upungufu wa Wahadhiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aliwahi kusema Mheshimiwa mmoja sehemu kwamba hata ukiwachukua wanafunzi leo ukawaweka katika hoteli ya nyota tano halafu hao wanafunzi wakapata kila kitu lakini kama Wahadhiri wa kuwafundisha hawapo ni bure. Tutapata wanafunzi ambaao hawataendelea na wataondoka katika maeneo hayo, tutapata wanafunzi ambaao watachanganyikiwa na mwisho wa siku hata ndoto zao hazitafikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii changamoto imetokana na hii sera ya kusema Wahadhiri wanaajiriwa kutoka Utumishi, Wahadhiri wanatoka Utumishi. Kwa hiyo, kila wakati Vyuo Vikuu vinapokosa Walimu wanasema hili tatizo liko Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba kama ambavyo wengine walishashauri asubuhi, kwamba sasa Vyuo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Vikuu virudushiwe ile *autonomy* waweze kuajiri wenyewe. Mheshimiwa Waziri Vyuo Vikuu vinawatambua wanafunzi ambao wana uwezo wa kubaki pale na kufundisha na hapo zamani ndivyo ilivyokuwa. Wanafunzi wanapokuja pale wanafanya *Degree* ya Kwanza, wale wanaofanya vizuri na kuwa na *GPA* nzuri ndiyo waliokuwa wanaajiriwa. *TCU* wameweka kwamba *GPA* ya kufundisha Chuo Kikuu japo kuwa hapo pia kuna tatizo fulani kwa sababu kwenye Vyuo Vikuu vingine wanachukua *GPA* 3.5 lakini Vyuo Vikuu nya Umma wamesema wachukuliwe wale wanaopata *GPA* ya 3.8 lakini hata hivyo siyo jambo baya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wanamaliza wana 3.8, wana 3.9 mpaka 4.0 mpaka 4.2 lakini mwisho wake hawajui kwa sababu Utumishi hawajawaajiri na Chuo bado kina shida lakini hawana ile *autonomy* ya kuajiri hawa wanafunzi au kuajiri hawa wawe *Tutorial Assistant* na mwishowe wajiedeleze mpaka wapate Shahada ya Uzamivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, naishauri Serikali, naishauri kwa dhati kabisa, hapa Chuo Kikuu ndiko ambako tunawatoa Wahadhiri wenyewe, hapa ndipo watumishi wa Serikali wanakotoka, maana watumishi wa Serikali wengi ni wale ambao wameshapita Chuo Kikuu, Sekta Binafsi hata wafanyabiashara wengi wangetaka wawe na *Degree* ili waweze kufanya biashara zao vizuri. Kwa hiyo, hili jambo naomba Wizara iliangalie. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende sasa kwenye uwiano wa kijinsia katika Vyuo Vikuu. Kati ya hao wanafunzi 7,000 kama nilivyokwisha kusema, hawa 7,647 wanaume ni 5,766 asilimia 75.4 ni wanaume. 1,881 asilimia 24.6 ni wanawake. Hivi ni kwanini? Kwani wanawake hawawezi? Kweli asilimia hii hata nusu hajafika? asilimia 75 ndiyo wanaume? Tatizo liko wapi? Hawa wanawake kwani ina maana hawawezi kweli kusoma hata kama huko nyuma hali ilikuwa tofauti? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iwaangalie wanawake, kwa sababu katika Sekondari kuna shule zinafanya vizuri za wasichana. Tatizo liko wapi wakifika Chuo Kikuu Wahadhiri wanakuwa asilimia 24 ya wanawake? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ifike mahali tufanye maamuzi magumu ya kuhakikisha kabisa hawa wanawake nao wanapatikana. Sasa mimi nina wazo, kuna hii *project* ya *Higher Education Economic Transformation (HEET)* ambayo imedhamiria katika mwaka 2021/2022 mpaka 2025/2026 kuwasomesha wanafunzi wa *Degree* ya Uzamivu 623 na Uzamili 477. Mimi nashauri Serikali angalau robo tatu wawe wanawake. Wanawake wote ambao wanaweza kusoma Chuo Kikuu na wanafikia vigezo vya kuwa Wahadhiri basi wapewe nafasi ya juu katika kuwafikiria. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi zilizoendelea hata katika miradi iliyoko Chuo Kikuu ukipeleka mwanamke wanasema *women are highly encouraged*, kwa maana ya kwamba wanatambua na hata mradi unaolipa Chuo Kikuu wanasema ukipeleka *candidate* ambaye ni mwanamke unapewa asilimia 40 katika ile *project*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naiomba Serikari iangalie kuweza kuwapata Wahadhiri wengi wanawake hii pia itaondoa malalamiko. Sasa hivi tunafikiria kuweka dawati la jinsia, dawati la jinsia kwa nini? Hawa wanawake ni mama, hawa wanawake ni wanawake, wanajua matatizo ya watoto wa kike lakini sasa unakuta ni wanaume ndiyo wengi. Sasa hata tatizo likitokea kesi ya ngedere utapelekaje kwa nyani? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wanaume, mwanaume kakosea, kateleza kesi inapelekwa kwa mwanaume, kwa sababu wanawake hawapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine katika Vyuo Vikuu ni katika uongozi. Vyuo Vikuu vingi ni wanaume ndiyo wanaopewa nafasi ya uongozi. Nakipongeza sana Chuo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Anangisye Mwalimu wangu yeye amefanya vizuri sana. Amewajali wanawake. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinawajali wanawake sana, na hilo nawapongeza sana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mheshimiwa Waziri naomba hii jambo liingwe na Vyuo Vikuu vyote kuwaweka wanawake katika nafasi za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante Dkt. kengele ya pili hiyo. Dkt. Musukuma, jiandae Mheshimiwa Shigongo, jiandae Mheshimiwa Kishimba.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo amefanya jana na leo imesomwa hapa Bungeni. Ni kazi kubwa ambayo Watanzania wengi tulikuwa tunaisubiri na sasa amewaachia kazi Mawaziri mfanyie kazi. Watanzania hatutaki kusikia namba, kwamba tutawapa Bilioni 100 halafu Watanzania wasiosoma wenye elimu ya kawaida wanauliza hiyo ni bei gani imepungua kwa lita? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mpaka tarehe moja hiyo mliyotangaza mnatakiwa muwe mmeshatamka kwamba lita itauzwa bei gani ya mafuta. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ninakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa taarifa nzuri, umeongea vizuri, umeeleza vizuri, pamoja na Kamati pia. Mheshimiwa Waziri mimi nina machache sana kuhusiana na suala la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kila biashara unayoifanya lazima iwe na tathmini. Naongea kitu ambacho pengine naweza kuwa tofauti kidogo na wenzangu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu bure, Mheshimiwa Waziri kuna kipindi sisi Wabunge unashindwa hata kwenda kutembelea Shule za Msingi huko Vijiji na shule zingine kwa sababu ukifika pale yaani ni kitu cha aibu sababu ni elimu bure. Unakuta darasa moja watoto wanasona 500, Mwalimu mmoja anafundisha, sasa kwa hatua kama hii unakuta watoto wako Darasa la Tatu hajui hata kuandika jina na wewe bahati nzuri ni Profesa nataka uniambie kwenye majibu yako, hivi ungekuwa wewe una vipindi vitatu vya watoto 400 - 400 ungewezaje ku-concentrate kusahihisha halafu na kupanga masomo hata ya baadae. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, ni vizuri tukafanya tathmini kama tulikosea ni vizuri tukarekebisha. Huu mfumo tunaoenda nao elimu bure tunalundika tu pesa, watoto wanaenda mashulenii lakini hawapati elimu na Serikali inazidi kutumbukiza hela ambazo hazirudi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupa mfano mimi nina shule ina watoto 3,500 ina Walimu Tisa. Hebu juilize ungekuwa ni wewe ungewezaje kufundisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba Mheshimiwa Waziri ukipata nafasi ya kuwa unazunguka huko Mikroani jaribu kufanya ziara za kushtukiza kwenye shule unawenza ukawa unaongea na Wabunge nataka kutembelea shule fulani ukafanya ziara ya kushtukiza usiende na ving'ora vya magari watajiandaa, ukakuta kile kipindi cha Saa Nne mtu anasahihisha hata haangalii daftari anatia tu hivi watoto wamepanga mstari watu Zaidi ya mia nne. Sasa tunatumbukiza hela kwenye sehemu ambayo kiukweli baadae mtakuja kutulaumu. Mnatengeneza bomu ambalo hatuna uwezo wa kuja kulikabili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumza kuhusu elimu ya juu. Serikali inatoa mikopo tumeambiwa hapa kwenye taarifa kwamba wameshapewa bilioni 400 sasa wameongezewa mpaka bilioni 500, lakini ningekuwa mimi ninayefanya biashara, hili suala nafikia mahali najiuliza, kama Serikali inatoa hizo hela na hatuna uwezo wa kuzikusanya,

nimesikia mjambe mmoja anasema tufungue benki yaani tuajiri wataalam wazidai kama benki, halafu mwisho wake itakuwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wazo, kwa kuwa Serikali ina watu wasomi na wabunifu na tuone namna ya kwamba watu wanapopewa mikopo na wanafanya *research*, mtu anaanza mwaka wa kwanza anafanya *research* mpaka mwisho wa elimu yake, ana-submit *research* yake, ana-graduate, kwa nini ile *research* isigeuke kuwa biashara? Kwa sababu *research* ile kwa kila mtu aliyefanya *research* yake hiyo tayari ni hela na wewe unaikubali unamfaulisha, unampa cheti. Sasa kuliko kumpa mtu hela halafu anamaliza *degree* yake umekopesha asilimia 50, hawajaajiriwa wote, wameajiriwa asilimia 15, halafu hizi hela zimepotea wengine wanakufa bila kurudisha deni, wengine wamekaa wamekuwa machinga hwajulikani waliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningeomba tukubaliane na wenzetu wanaosimamia hii mikopo ya elimu ya juu kwamba tuwe na madirisha mawili tuwe na dirisha moja kwa ajili ya kukopesha ili mtu asome, lakini akifanya vizuri wewe ukitoa *GPA*, kile cheti chake kiwe *bond* kiwe dhamana kuwe na dirisha la kukopesha kulingana na *research* yako hata kama ni milioni tatu. Huwa najiuliza kweli ndugu zangu tunaweza tukawa tunaonekana kama tunaongea vitu vya ajabu, lakini naomba niulize swalila moja kwamba leo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaandaa utaratibu kwa machinga mtu ambaye hajulikani leo atakuwa hapa kesho atakuwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaandaa utaratibu tunatengeneza utaratibu waanze kukopesha na mabenki na tunesikia taarifa tayari wameanza kukopesha sijui Dar es Salaam na wapi, inakuweje machinga anakopesha kwa Kitambulisho, wameshindwa kutengeneza utaratibu kwa mtu cheti cha *degree* akapata mkopo akaenda kuwa machinga ambaye amesoma na watu wangkuwa na nia hata ya kusoma.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo langu naomba Serikali ifikirie kuwa na madirisha hayo mawili; tukopeshe kwa ajili ya kusoma; halafu tukopeshe kwa ajili ya mitaji kwa ajili ya watu kwenda kujitegemea. Mimi binafsi ungeniuliza ningesema hata leo tuondoe hiyo elimu bure ya msingi, unamtengenezea msingi usiojitambua, akifika huko juu anakuwa machinga mzigo ambaye hajui kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nadhani tuwe tuna madirisha mawili kwenye Vyuo Vikuu, mtu anapomaliza Chuo Kikuu apate elimu ya mkopo na atumikie mkopo aliye na deni pamoja na ile aliyeikopea mwanzo. Faida ya pili, nimesikia Serikali baadhi ya mabenki yameanza kutoa mikopo kwenye elimu ya kati *certificate* na diploma, nikajaribu kujuliza hiki ni kitu kizuri sana, lakini nikawa najaribu kuwaliza watu wa *NMB* hii inakuwaje, dhamana ni kitu gani kwa sababu *certificate*, hiki cheti hakikopesheki.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanakopesha kwa dhamana gani wanasema tumeanza na watoto wa wafanyakazi. Hii ni aibu kubwa sana yaani watoto wa maskini ambao wana akili nyingi wanashindwa kwenda kusoma kwa kukosa hela, tunaenda tena kuchukua mtoto wa mfanyakazi, tunamtengenezea utaratibu wa kukopa, kwa nini wasianze na watoto wa maskini na vyeti vyao viwakopeshe wao wenyewe. Kwa nini tukimibilie kukopesha watoto wa watu ambao wana uwezo wa kusomesha watoto wao, kwa hiyo nilikuwa naomba...

MHE. STANLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

MHE. STANLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba nimtaarifu mzungumzaji kwamba wanaokopeshwa sio watoto ni wazazi kwa sababu moja tu kwamba, mtoto aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane wa mujibu wa sheria za nchi yetu hawezikukopeshwa na benki na watoto wanaokwenda kusoma hivi vyuo vya kati ni

wale waliomaliza kidato cha nne hawajaenda kidato cha tano wala cha sita. Kwa hiyo bado ni *under 18* na ndio maana anaanza kukopeshwa mzazi kwanza.

NAIBU SPIKA: Mhesimiwa umeipokea taarifa.

MHE. DKT. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mhesimiwa Naibu Spika, naipokea. Nilichokuwa naongea mimi hana tatizo na mawazo yangu lakini ombi langu ni kwamba kwa nini tukaanze na watoto wa dizaini hiyo wa wafanyakazi hawa watoto wa maskini wenye akili wanaotaka kuendelea tuweke masharti nafuu kwenye benki zetu hizi, tuwakopesha hata wazazi maskini wenye watoto wao wako tayari kuweka *bond* hata mashamba, sio lazima tukaweke pesa ikubali isikubali benki kwamba tunaweza kuweka hata mashamba, au mbuzi au kondoo ili mtoto wangu asome na hiyo ndio kazi ya Serikali kusaldia watu wasiokuwa na uwezo, tunasaldlaje mtu ambaye ana uwezo.

Mhesimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hayo tu kwa leo nakushukuru. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mhesimiwa Shigongo, wajiandae Mhesimiwa Kishimba na Mhesimiwa Tabasam Hamisi Mwangau.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mhesimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kutoa pungezi nyingi sana kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyofanya kazi kubwa sana katika elimu ya Taifa hili. Mhesimiwa Rais alifanya jambo moja kubwa ambalo limemtengenezea heshima kubwa mno. Alichukuwa mkopo kwa ajili ya UVIKO (*COVID 19*) lakini akatumia fedha mkopo ule wa *COVID 19* kujenga madarasa elfu 15 nchi nzima.

Mhesimiwa Naibu Spika, *that was the smart decision*, katika Afrika hakuna kiongozi ye yote aliyechukuwa uamuzi wa namna ile. Alikuwa na uwezo wa kuamua anunue barakoa au anunue *sanitizer* lakini akaona jambo la maana sana kwa watu wake ni kujenga madarasa. Kwa niaba ya

wananchi wa Jimbo la Buchosa namshukuru sana Mheshimiwa Rais na tumejenga madarasa 128, hivi ninavyozungumza watoto wanakaa kwenye madarasa mazuri yaliyotengenezwa vizuri. Ahsante sana Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge naomba tumuunge Rais wetu mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa kwa nini hampigi makofi ya kutosha kwa Mheshimiwa Rais. Nianze na kitu kinachoita *form four certificate dilemma, dilemma* ya cheti cha *form four*. Kabla sijakugusa cheti cha *form four* nisiache kumshukuru kwanza Profesa Mkenda kwa kazi kubwa ambayo ameanza nayo kwenye Wizara ya Elimu, Profesa namwamini sana, nilikuwa na mpango wa kushika shilingi lakini kwa mambo anayoyafanya sitashika shilingi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Naibu Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Kipanga, anazunguka Tanzania nzima kama *pier* kwenda kila wilaya kuangalia maendeleo ya elimu. Nampongeza sana Naibu Waziri kwa kazi nzuri. Nachukua nafasi hii pia kumpongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara hii Profesa Eliamani Sedoyeka. Kwa kweli namfahamu Katibu Mkuu huyu tangu akiwa Chuo Cha Uhasibu Arusha kwa mambo aliyoyafanya pale Arusha. Aliingia Chuo Cha Uhasibu Arusha kikiwa kwenye hati ya kufungwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, chuo hiki kilikuwa na wanafunzi kama sikosei 2,000, amekaa pale si zaidi ya miaka miwili, ameacha kina wanafunzi elfu 10 na kitu na tayari kina majengo ya ghorofa. Kwa hiyo naamini ujio wake kwenye Wizara ya Elimu, hatakubali hata siku moja kuharibu rekodi yake. Kwa hiyo rekodi yake iliyomsababisha akapewa Ukatibu Mkuu aendelee nayo na Watanzania wanufaikia kwa kiasi kikubwa sana na umahiri wake. Niwashukuru Manaibu Makatibu Wakuu na pia niwashukuru watumishi wote wa Wizara ya Elimu, tuna kazi kubwa sana kwa ajili ya elimu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie *dilemma* cheti cha *form four*. Wengi mnafahamu mimi sikupata nafasi ya kusoma elimu ya sekondari, lakini kwa neema ya Mwenyezi Mungu na kwa kipaji ambacho Mungu alinipa cha uandishi nilitathiminiwa na *TCU*nikakubaliwa kusoma Chuo Kikuu kwa mfumo uliokuwa unaitwa *RPL Recognition of Prior Learning* na nikamaliza Chuo Kikuu vizuri kabisa. Nilipotaka kufanya *masters* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nikakataliwa nikaambiwa huna cheti cha *form four*na hayo ndio imekuwa vita yangu profesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshazungumza sana na Mheshimiwa Profesa na dada yangu Mheshimiwa Ndalichako anakumbuka vizuri sana kwa mapambano yangu mimi na ye ye humu Bungeni, kwamba haiwezekani mtu nina shahada ya kwanza *TCU* wamenikubalia, halafu Chuo Kikuu wanakataa nisifanye *masters* kwa sababu sina cheti cha *form four*. Hii haiwezekani, wanawanyima watu haki ya elimu, kuna watu wengi nchi hii wamebuni vitu vingi, watu wametengeneza umeme bila elimu ya sekondari, wanajenga nyumba bila elimu ya sekondari, wanataka kusoma Chuo Kikuu wanakataliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Profesa Mkenda, aichukue kazi hii na kazi yangu hii aweze kulikamilisha jambo hili. Namwamini mno Mheshimiwa Profesa na tumeshazungumza mara nyingi sana kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Profesa Ndekidemi anafahamu, kuna mtu mmoja kwenye Taifa hili lazima nimtolee mfano, alikuwa *gardener* kwenye chuo kimoja cha kilimo, akawa anatengeneza *garden* nzuri sana na kwa sababu hiyo Wazungu wakaona anafaa kusoma *diploma*, akapelekwa kusoma *diploma*, akamaliza *best student* kwa *diploma* kutunza *gardener*.

Mheshimiwa Naibu Spika, alipomaliza hiyo kozi ya *gardener*, wakasema aaa, umemaliza na *distinction*, basi *distinction* yako tunakupeleka kusoma Uingereza, akapelekwa Uingereza kusoma, *from a gardener* akaenda

kufanya *degree* ya kwanza ya mambo ya kilimo na *degree* ile akarudi Tanzania baada ya miaka mitatu akarudi na *masters*, ndani ya miaka mitatu. Alipofika Tanzania, Tanzania yangu, nchi yangu, inayothamini cheti cha *form four*, alipotaka kufanya *masters* akaambiwa huwezi kufanya *masters* huna cheti cha *form four*.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mtu yupo ukitaka nikuletee nakuletea na Profesa Ndekidemi yupo pale ni shahidi wangu. Yule mtu ikabidi aache kufundisha aende akasome *QT* Tanzania, Profesa Mkenda, akaenda kusoma *QT* miaka miwili, alipopata cheti cha *form four* ndiyo akafanya *PhD* na leo ni Profesa, *the best professor in the country*. Mimi binafsi siko tayari na nimesema sitashika shilingi, namwomba sana Waziri Profesa Mkenda hili jambo ni la kisheria, alete sheria Bungeni tubadilishe ili Watanzania wapate nafasi ya kusoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kengele ya kwanza kulia, sasa nitoe mchango wangu, nina mambo mawili tu. La kwanza *medium of instruction*, lugha ya kufundishia. Kwa muda mrefu sana nchi yangu imevutana tufundishe kwa Kiswahili, tufundishe kwa Kiingereza, mvutano huu mpaka lini?

Sasa ni wakati wa kufanya maamuzi, mwanangu anasoma darasa la kwanza kwa Kiswahili mpaka darasa la saba kwa Kiswahili. Akianza *form one* anaanza kwa Kiingereza. Ile *transition* ya kutoka Kiswahili kwenda kwenye Kiingereza tunapoteza watoto wengi wenye akili *form one* atakuwa anajifunza Kiingereza. *Form two* anajifunza Kiingereza *form three* kaanza kuelewa Kiingereza kidogo, mtihani wa *form four* umefika anapata *division zero*.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri na nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge kwa umoja wetu tuamueni tunataka tufundishe Kiingereza au Kiswahili.

WABUNGE FULANI: Kiingereza.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili nisiliseme nimwombe Mheshimiwa Waziri, afanye utafiti aje na majibu ya watu wanataka tufundishe kwa lugha ipi, tuwe na lugha ya kufundishia ili tuwasaidie watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala zima la mitaala ya elimu, limezungumzwa. Dunia inakwenda kwenye *fourth industrial revolution*, mapinduzi ya nne ya viwanda, lazima mitaala yetu ili-reflect kule tunakoelekea hatuwezi kuendelea kuwafundisha watoto wetu kwa mambo ya *second industrial revolution* kwa mambo ya *third industrial revolution*, hatuwezi kufanikiwa. Tutakapofika mapinduzi ya nne ya viwanda ambayo kutokana na mambo ya intelijensia ya bandia niseme hivyo, mambo ya *five technology, cloud computing*, lazima tuwaandae watoto wetu tuanze kuwafundisha kuanzia *primary schools*, kuna shida gani kumfundisha mwanangu *coding* akiwa *primary school*, kuna shida gani? Hatutaki kufanya maamuzi, matokeo yake shule za binafsi watoto wanaandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotokea, huko mbele tunaandaa matabaka ya watu wawilli; watoto wenu hapa watakuwa na nafasi kuliko watoto walioko vijijini, hatutaki Tanzania ya aina hiyo. Tunataka Tanzania yenye usawa, kwa hiyo naomba waache maandalizi mtaala huu, tufikirie sana kuwapa watoto wetu elimu ya *computertoka Shule ya Msingi*. Walimu tunao, hatuna sababu ye yeyote ile ya kutofanya jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni suala la maslahi ya Walimu. Ukitaka kufanikiwa kwenye elimu mfurahishe Mwalimu, basi. Walimu lazima wawe na furaha katika nchi yetu, najua wanansikiliza, Walimu wanaouza visheti...

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Shigongo kengele ya pili. Mheshimiwa Kishimba ajiandae Mheshimiwa Tabasam.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Kahama Mjini, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutusaidia sana kwenye ujenzi wa shule na kutupunguzia michango minge ambayo imekuwa mizigo mikubwa sana kwa wananchi wetu namshukuru sana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la elimu naona ni vizuri kwa kuwa tunaliongea kwa mapana Mheshimiwa Waziri, ingekuwa dini tungeweza kuhamza, lakini kwenye elimu utahamia wapi. Kwa hiyo ingekuwa dini mtu anaweza kuamua hii bwana imenishinda unahamia dini nyingine, lakini kwa mazingira yalivyo kwenye elimu huwezi kuhamza. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri wa Elimu ajaribu kutuelewa sisi Wabunge amba ni wawakilishi wa wananchi, hali ya wananchi kwenye suala hili la elimu ilivyo kule vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Serikali ikubali, ikanunue mawazo na maarifa mepesi ili wanafunzi kuanzia darasa la kwanza, baada ya kuwa wamejua kusoma na kuandika wafundishwe elimu mbadala. Kuwe na elimu hii tulioachiwa na mkoloni, lakini tuwe na elimu mbadala. Maana yangu ni kwamba sisi tunaotembea sana nchi mbalimbali, leo hapa mimi nakwenda shulen na fundishwa panzi ana miguu saba, senene ana miguu minane. Hivi elimu inakataza kweli kuniambia bei ya senene ambayo leo ni Sh.50,000 naishia tu hapo kwa kilo moja, ni kosa?

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunafahamu kabisa kwamba panzi wana *protein* na wanaliwa na kuku, je ni kosa kufundishwa darasani kwamba kuku anakulaga panzi na kilo moja ya panzi ina panzi 17 na ukimpa utakuwa umesevu kununua chakula cha kuku. Je ni kosa kielimu, kwa nini isiwe kwenye elimu mbadala?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu leo hapa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, watu wanaombwa kibali zah kuagiza kibali cha kuagiza chakula cha samaki India, lakini wote tunafahamu kwamba samaki anakula minyoo au chambo na kutengeneza minyoo mtu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

akifundishwa darasa la kwanza inachukuwa masaa 16 kupata minyoo, ni kosa?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, unataka mtu mpaka asome, amalize *form four, six*, akawe fundi seremala atengeneze makochi yasiyonunuliwa, ni kweli tunaenda kuwaambia wananchi wauze ng'ombe, waje wasome waende *VETA*, waje watengeneze makochi, ni sawa? Wakati elimu yetu inaletwa, dunia haikuwa hii, dunia ilikuwa ni nyingine kabisa, je turudi kwa Waingereza hawa wanaoangalia mpira wa *Chelsea* na watoto wao, wanawenza wakatukumbuka watubadilishie elimu? Kweli sisi tunashindwa kabisa kufundisha watoto wetu darasa la kwanza wakatengeneza minyoo, wakawapa kuku, samaki badala ya sisi ku-share mahindi na kuku ni kosa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajaribu kuonyesha namna ambayo ni rahisi mtu kuishi. Zamani mtoto wako wa kwanza akimaliza shule, anawachukua wale wadogo zake anakwenda kuwa nao anakuondolea mzigo. Sasa hivi anamaliza *degree*, anarudi nyumbani, je, wewe utakuwa na moyo wa kuwasomesha hao wengine una moyo gani huo?

Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Waziri utakuwa na moyo huo wakati huyu kwanza hajapata ajira, ng'ombe wamebaki nusu, utakubali uuze ng'ombe walibaki umsomeshe na huyu abaki nyumbani? Haiwezekani! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima viongozi wakati huu wa shida ya mabadiliko duniani ndipo ambapo viongozi *strong* huonesha mabadiliko makubwa sana ya kwenda mbele, kuliko tukisema na sisi tuwa-*damp* wananchi na sisi wote tunao watoto kwenye masofa, wamejaa wameweka masikioni wanasiliza na wanacheza na *WhatsApp*. Je, tuendelee kuwa- *damp* hivyo? Je, wale panya *road* au panyabuku tutawaweza? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani! Wenzetu Wizara ya Elimu wanayo maabara mle ndani. Kweli maabara

inashindwa? Leo Mheshimiwa Bashe analia mbolea, kweli shule ishindwe kufundisha mtoto kutengeneza mbolea ya kienyeji ambapo ni kuchukua nyasi na udongo na kumwangia maji na kuza barabarani, hata kama kilo moja shilingi 300, mtoto huku anasoma, lakini Serikali na sisi tunapata mbolea. Hili pia linahitaji kweli mpaka tujue tu Kiingereza, TEHAMA; je, ng'ombe pia tutachunga kwa TEHAMA kweli? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kama tunavyotaka ni hivi, ni kweli wote tutasoma tumalize wote tuwe na *degree*, tutoke na ng'ombe kule Kijiji tuzilete mjini tena, tuje nazo huku tumesoma, tunaongea Kiingereza. Itawezekana kweli! Kwa hiyo, tunamwomba Waziri wa Elimu ajaribu na Kamati yake kuona kwamba hawa tunaowaongoza ni raia wa kawaida kabisa wenye maisha ya chini, wanahitaji elimu ndogo ya kujishikiza huku wanaishi ili Serikali inunue mawazo mepesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli suala hili linatupa wakati mgumu sana kiasi ambacho unapokwenda kule vijijini, wazee wanatuuliza: "Hivi kweli hakuna njia yoyote ya nyie kufikiri?" Nasi tukirudi kwa wenzetu huku wanapiga tu *stop* kwamba haiwezekani. Kama leo inapatikana teknolojia duniani, Waziri wa Elimu si aingize tu kule kwenye simu awaeleze kule walimu kwamba jamani, sasa hivi ukichukua lita moja ya maziwa ukatikisa saa moja, kinachopatikana ni mafuta ya kula. Hata hiyo nayo ni kosa kufundisha shulen? Sasa nani tumwite aje atukomboe? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunalia mafuta, watoto wetu hawajui kama kwenye maziwa kuna mafuta, itawezekana kweli tusomeshe watu; ukimwona mtoto aliye na *degree*, ukimweka mahala, ni kama umemweka kuku wa kizungu. Unamwona kweli huyu mwanangu sijui nitamkuta, sijui atagongwa, sijui atanyang'anywa hili begi alilonalo! Ni kazi ngumu kweli! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, kweli teknolojia

inakataza kitu chenye faida? Inakataza kabisa, haiwezekani! Yaani teknolojia ni lazima iwe kutengeneza magari na ndege tu; na *TEHAMA*? itawezekana kweli! Yaani Tanzania nzima, watu milioni 60 wataenda kwenye *TEHAMA*? Watazunga wapi hizo *computer?* (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata shule ya msingi, mmesema hapo wenyewe, kuna wanafunzi 400 mle ndani: Je, wangekuta asubuhi wanafundishwa kutengeneza minyoo, si wangekuwa wanaauza pale nje wakati wanamsubiri mwalimu? Wafugaji wa kuku wangenunua. Si ndiyo sawa tu, tutafanyaje? Dunia imebadilika, *population* imeongezeka, watu wanahitaji vyakula: Je, tuendelee na *procedure* ya mbao? Mheshimiwa wa Maliasili naye anataka miti yake, watu wasome wawe mafundi seremala na mafundi rangi. Tanzania nzima tutakuwa mafundi rangi! Haitawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunamwomba sana mwenzetu Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, ajaribu hata yale mawazo ya *local*. Mpaka wafugaji wanatuuliza kwamba ah, usiniletee maneno ya shule hapa, ng'ombe zangu zilizobaki hizi, mpaka nife mwenyewe, siwezi. Sasa tukatae ukweli, kwani nani hajui?

Mheshimiwa Naibu Spika, wote si tunafahamu kabisa kwamba sasa hivi mtu aliyesomesha kule kijijini ndio anayechekwa. Kwa sababu watoto hawawezi kulima, hawezi kufanya kazi yoyote na ng'ombe zimeisha, naye amezeeka, anaandikisha *TASAF*, itawezekana kweli? Sasa mbona kuna elimu ndogo na nyepesi ambayo inaweza kutusaidia kwenye huu muda ambao tunao kuliko kung'ang'ana tu kama Waingereza. Maana yake tukiongea wote kama Waingereza, kweli wale Waingereza wa *Liverpool* watakuja kutusaidia kweli! Itawezekana kweli watuletee mawazo mengine ya kutukomboa? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo, namwomba tu Mheshimiwa Waziri asipuuzie, maana yake mtoto kwenda shule ni kwenda kuanza mawazo na maisha mapya. Akitusaidia kutufundishia watoto wetu hizi kazi ndogo

ndogo za kawaida, atakuwa ametusaidia sana wakati wanajiandaa kwenda kule mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Tabasam, jiandae Mheshimiwa Kingu na Mheshimiwa Nashon Bidyanguze.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami kuchangia mchango katika Wizara ya Elimu. Kwanza naipongeze Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri wanayoifanya, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri katika vitu ambavyo wanavifanya vikubwa ni kwenda kuangalia changamoto za elimu kwenye majimbo yetu. Tunawaalika, wanakubali kuja; unapiga simu, wanapokea nawaombeni sana mwendelee na kazi hiyo Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na mchango kuhusiana na mitaala ya elimu. Hii mitaala ya elimu inatakiwa iingie kwanza kwenye kumbukumbu wajue Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba leo Tanzania huu ni mtaala wa ngapi unababilishwa? Mtaala wa kwanza katika nchi hii ulianzwa na Mjerumani mwaka 1905 hadi 1913; miaka minane Mjerumani alikuwa na mtaala wake katika nchi hii ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Mjerumani, mwaka 1913 mpaka 1967, miaka 54 tunatumia mtaala wa Mwingereza. Baada ya mwaka 67, Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alibadilisha mtaala wa kwanza, huu ukawa ni mtaala wa tatu katika nchi hii. Mtaala huu ulikwenda mpaka mwaka 1977, miaka 10. Ukafuata mtaala mwingine wa nne 1977 mpaka 1984. Baada ya mtaala wa mwaka 1984 ukaja mwingine mwaka 1984 hadi 1997 kwa Marehemu Mheshimiwa Mungai, ndio tukaanzia hapo sasa kuteleza mtelezo wa hatari huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungai wakati anabadilisha mtaala mwaka 1997 alipiga marufuku michezo, mambo mengi yakafutwa, lakini wakaweka kitengo kinaitwa *Book Management Unit*. Hapo sasa elimu ya Tanzania ikaanza kuingizwa katika biashara. Kitengo hiki cha *Book Management Unit* kwenye mtaala huu wa mwaka 1997 yakaruhusiwa makampuni sasa kuanza kuuza vitabu. Yalitengenezwa makampuni mengi, watu wakawa wanachukua vitabu Nigeria na wapi, wanakuja kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili, anapata ithibati inakwenda kwenye mashule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya moja kama yangu ya Sengerema, kuna shule zaidi ya 210. Kila shule inasoma kitabu chake, halafu mtihani ni mmoja unatoka katika Wizara. Kichekesho cha ajabu kabisa duniani! Kigoma wanasoma *Mtue and company*, sijui *Ben and company*, *Tanzania Publishers*, sijui wapi, sijui *Kigamboni Publishers*. Yaani kila mtu mwenye pesa zake alikuwa anakwenda ku-lob katika kitengo hicho cha *Book Management Unit*, wanapata *order* kwa Wakuu wa Shule vitabu vinasomwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili jambo, elimu yetu ndio ilianza kuharibikia hapo. Mtaala mwingine ukabadilishwa mwaka 2004. Baada ya 2004, mtaala mwingine, wa saba unakuja kubadilishwa. Huu mtaala umekuja mpaka 2014. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Profesa anatakiwa kukaa sasa afikiri, afanye *research* katika hii mitaala. Hawa waliosoma mtaala wa Mwingereza wana manufaa gani katika nchi hii? Sisi tuliosoma mtaala huu wa mwaka 1967 wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere: Je, tunalinganishwa na hawa waliosoma mtaala wa mwaka 1997?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo unaweza ukaacha chakula ndani; umeacha mahindi, umeacha mpunga, gesi ipo, watoto hawajui hata kusonga ugali? Sasa huyo unategemea aje akusaidiaje? Kwa sababu shulenii hilo jambo halifundishwi. Tulikuwa tuna elimu ya Sayansikimu sisi,

tulifundishwa haya. Tulitoka shuleni tunapika keki, tunajua kila kitu, tunajua kuosha vyombo, kupiga pasi, tulifundishwa hizo kazi. Sasa leo inakuja mitaala hii ya kompyuta; haya endeleeni, lakini ninachotaka kukwambia, hiki kizazi chetu kikiisha, tegemeeni bomu linalokuja sasa, litataka ajira kwa sababu hamkuwaanda katika jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine ambalo tunataka tuwasaidie hawa watu wa Wizara. Kwa kuwa ni wasikivu nina imani watasikia. Kuna suala la vyuo, wenzetu wa Thailand baada ya kumaliza machimbo, nchi hiyo walichimba sana Thailand, wakabakiza sehemu moja *angle* ya utalii. Kule kwenye utalii wakaona na kwenyewe sasa kunakuwa na hali mbaya, waliwekeza katika vyuo vya ufundi vya kati. Hivi vyuo vya ufundi vya kati, walipeleka mtaala mmoja tu wakausimamia kwa nguvu kubwa ya ushonaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye kushona walipeleka watu kwenda kuwa ma-*designerkule* Hongkong, wakapeleka ma-*designerkule* China, walifundishwa kushona, wakawa wanaagiza vitambaa kutoka Pakistani, kutoka China. Leo Thailand, kila nyumba unayoiona Thailand ni kiwanda ndani. Leo *order* zote za nguo za watoto duniani, nguo zote nzuri zinatoka Thailand.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna soko hapa, tunazungukwa katika nchi za Afrika Mashariki, tunashindwaje sisi kushona? Tunashindwaje kupeleka kule kwenye vyuo vya ufundi? Ila kule kwenye vyuo vya ufundi, ada ni shilingi 60,000 *day*; na ukilala *boarding* ni shilingi 120,000. Hawa mkiwakopesha kama wanaokopeshwa wenyе *degree*, wanaotoka kwenye elimu ya msingi, wanaotoka kwenye elimu ya sekondari wakafeli. Wakopesheni wakasome *VETA*.

Kwanza mkopo ni mdogo, anasoma miaka miwili shilingi 120,000, huyo analipa tu. Kule anafundishwa *welding* anafundishwa kutengeneza simu; ni kazi, leteni kozi za watu wanaokwenda kufanya, akitoka pale miezi sita anaweka meza anatengeneza simu. Atashindwaje kulipa deni la shilingi 60,000?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mnakuwa na mitaala ya ajabu kabisa. Yaani watu wanatoka kule hawawezi hata kukata kucha, unakaa unamwona mtu anapakwa na rangi. Yaani hata hawezি hata kupaka rangi kwenye miguu yake, anapakwa na mwanaume, anashikwa namna hii anapakwa rangi, hajui hata kupaka rangi. Mitaala gani katika nchi hii? (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri katika jambo lingine kwa ndugu zetu wa Wizara ya Elimu. Elimu ya Sekondari; *O'level* na *Advance* pamoja na vyuo lazima mvichukue kutoka TAMISEMI. TAMISEMI ina mizigo mikubwa, mnakimbia jambo lenu. Kwa hiyo, ninyi sasa hivi Wizara ya Elimu mnatusaidia nini sisi watu wenyewe elimu huku chini?

Mheshimiwa Naibu Spika kwa sababu sasa hivi mmebakiza kukaa kwenye mitihani peke yake. Baraza la Mitihani ndiyo lenu. Sasa mtoto anatoka huku TAMISEMI, wana shule 14 za msingi bado mnataka kuwaongezea sekondari, zipo zaidi ya 5,000 halafu ninyi mnafanya kazi gani? Kwa nini mnakimbia mtoto wenu? Chukueni elimu ya sekondari TAMISEMI, huku chini tuachieni elimu ya msingi na chekea. Sisi tuwaandalie na ninyi mwendelee na kazi, lakini habari ya kukimbia hiyo nafasi, siyo sawa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja nimalizie mchango wangu, nakuomba.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tabasam ahsante kwa mchango mzuri.

MHE. TABASAM J. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Naomba wachukue shule zao za sekondari; *advance* na *O'level* zichukueni Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tabasam, mengine mwandikie Waziri.

Mheshimiwa Kingu, Mheshimiwa Nashon Bidya, ajiandae Mheshimiwa Robert Maboto.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa nawashukuru Wizara ya Elimu chini ya Profesa Mkenda, kaka yangu, nawapongeza sana kwa juhudhi kubwa mnazofanya kuhangaika katika kuhakikisha kwamba mnainua elimu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifuatilia michango ya Wabunge wote waliozungumza kuanzia asubuhi mpaka sasa hivi tunaelekea mchangiaji karibu wa kumi na kitu, utaona namna gani Wabunge wengi wamezungumzia changamoto ambayo haioneshi *consistence* katika mfumo wetu mzima wa elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tunajua uwezo wa Mheshimiwa Prof. Mkenda na Naibu wako. Nchi inatambua ya kwamba yeche ni msomi, mzalendo aliyesomeshwa kwa kodi za Watanzania, ana uwezo mkubwa, ni zao la watoto wa kizalendo wa nchi hii. Tumaini la Watanzania ni kuona nchi inapata *transformation* kwa lengo la kusaidia *sustainable development* katika masuala mazima ya elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Na. 25 ya mwaka 1978 imempa mamlaka Waziri wa Elimu kuunda chombo cha kisheria; Baraza la Ushauri katika masuala ya elimu katika nchi yetu. Ndugu zangu Watanzania na Wabunge wenzangu, nataka niwaambie *with a very big disappointment*; toka sheria hii imeundwa, hapa tunazungumza alikuja Waziri fulani akafuta hiki; akaja fulani, akafuta hiki; huyu anazungumza habari za mitaala; hivi leo tukiuliza, toka Sheria ya mwaka 1978, ni mwaka gani Serikali yetu tumetekeleza kuunda chombo chenye watalaam wazalendo wanaoona *direction*

na *vision* ya nchi wakamshauri Waziri juu ya mwelekezo na mustakabali wa nchi katika elimu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, kaka yangu, Mheshimiwa Profesa Mkenda, tunakuomba ukawe shujaa wa kwanza Waziri katika Taifa letu utakayekwenda kutekeleza takwa hili la kisheria Na. 25 ya mwaka 1978. Nenda kaunde chombo cha kisheria, Baraza litakalokuwa linakushauri katika masuala mazima ya elimu. Hizi kelele unazosikia kwa Wabunge, hautazisikia mpaka siku Yesu anarudi. Ni kweli watu wamekuwa wakijichukulia hatua na kufanya maamuzi bila *ku-reflect demand* na nini dunia inakihitaji hasa Taifa letu katika dunia tunayokwenda ya *globalization*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu Mheshimiwa Prof. Mkenda ninamshauri kama mdogo wako na kama Mbunge mwenzio, sheria imekupa mamlaka, tukimaliza ikiwezekana hata kesho teua watangaze tupate chombo cha kuanza kukushauri katika masuala mazima ya elimu. Hizi kelele za Wabunge hautazikisikia na utaona changamoto nyingi zinazozungumzwa kuhusu elimu yetu na mitaala, tutakwenda *ku-harmonize* na kulisaidia hili Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili; asilimia 25 ya sekondari katika Taifa letu zinatokana na *private investmate* kwa maana shule za *private*. Leo tunapozungumza, kaka yangu Mheshimiwa Innocent, Waziri wa TAMISEMI, nampongeza kwa huruma yake kubwa sana, juzi akaamua kuongeza nafasi ya watu kufanya *application* zilizotangazwa katika Serikali. Naomba Bunge lako linisikilize kwa makini; kama *private sector* inafanya asilimia 25 ya shule, Mheshimiwa Innocent juzi ametutangazia nafasi takribani 10,000. Kwa taarifa nilizonazo mpaka sasa hivi, waliyoomba ni zaidi ya waombaji kama 120,000 kwa nafasi 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali, Profesa Mkenda kaka yangu mnisikilize. Tukitaka kusaidia changamoto ya upatatikanaji wa walimu kupata ajira na

walimu wa masomo ya sayansi kuongezeka lazima *private sector* ipewe nguvu, na kwamba shule za *private* lazima zipewe nguvu. Leo tunapozungumza shule za *private* tumeziwekea mpaka *cooperate taxi*, jamani elimu hii ni huduma! Tukiweza kupunguza kodi kwenye shule za *private* mimi nakwambia tutasaidia Watanzania wengi kufungua shule, walimu wetu wanaokosa ajira wataajiriwa kwenye *private*. Tutasaidia kutatua changamoto kwenye Sekta ya Elimu na kaka yangu Mwigulu Madelu na ninaju upo hapa, ninajua hiyo kodi utakwenda kusaidia kuzifuta kwa lengo la kusaidia *Private Sector Investment* katika Sekta nzima ya elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa tatu. Serikali inachukua mikopo mingi, na ninampongeza sana Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan. Uwekezaji unaofanywa katika miundombinu ya elimu ni uwekezaji unaotia moyo sana. Rais wetu asivunjwe moyo aungwe mkono na apongezwe. Uwekezaji unaofanyika ni wa hali ya juu. Hata hivyo, ninaomba nikosoe na kushauri. Tuna programu za *EP4R* ambazo wastani tunakopa kama Dola milioni 500. Tuna programu *EQUIP* ambazo pia tuna Dola kama milioni 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hivi mtoto anayesoma *private* ni mtoto wa Kitanzania au siyo wa Kitanzania? Mtoto anayesoma shule ya Serikali anatafuta elimu ni wa Kitanzania au siyo wa Kitanzania? Tukitaka tusaidie Taifa letu kwenye suala la elimu, ninatoa ushauri, kwamba fedha za mikopo katika *investment* katika masuala ya walimu Serikali msione haya kuzisaidia shule za *private* katika *investments*, kwenye masuala ya vifaa, Maabara na walimu. Kwa sababu mikopo hii hata wale wa *private* wanalipa tusiwabague kwa lengo la kujenga hali ya kuwasaidia wananchi wetu kuweza kupata unafuu katika kupatikana kwa walimu katika maeneo hayo; huo ni ushauri wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumza kaka yangu Erick Shigongo, nimekusikiliza kwa makini sana *brother*. Lakini kuna muda pia alizungumza Profesa asubuhi. Leo tunapozungumza ukienda katika vyuo vya Uganda, fanya

research, nenda katika vyuo vya Makerere na Bukene, nenda kwenye vyuo vya Kenya kama vile *Nairobi University*, halafu njoo fanya *comparison* na vyuo vya Tanzania. Nenda kaangalie idadi ya Watanzania wanaosoma Kenya na Uganda na idadi ya waganda wanaosoma Tanzania, utakuta kuna *huge gape*. Sababu kubwa ya msingi bado tuna *mediocracy mind set* ya kung'ang'ania vitu ambavyo havilifungui taifa katika kufanya Taifa letu la Tanzania liweze *ku-integrate* na *ku-absolve* mambo mengine ya *technological transfer* yatakayosaidia nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano sisi tumeweka kigezo cha mtu kwenda Chuo Kikuu mpaka asome kidato cha sita. Hapo Kenya mtoto anamaliza kidato cha ana-*qualify* kwenda Chuo Kikuu akija Tanzania *refraction*. Haya mambo hayawezi kulisaidia taifa. Ushauri wangu ninaota Profesa Mkenda kaka yangu nenda kakae na timu yako. Na timu hiyo najua hata hili ninalolishauri, Baraza la kiufundi ambalo limeundwa kwa Sheria namba 25 ya mwaka 1978, ninajua kabisa ushauri ninaoutoka ukienda kuzungumza huko Serikalini mka-*harmonize* faida ya kuwa na *integration* ya watoto kutoka mataifa mengine kuja kusoma kwetu kwanza vyuo vikuu vitaongeza mapato ya kudaihili wanafunzi, pili tutaweza kurahisisha *ku-harmonize technological transfer* kutoka Mataifa ya wenzetu kuja kwetu lakini pia tutajiendelea kujenga mshikamano na undugu katika *block zetu* za kikanda na katika masuala mazima ya kisiasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa mwisho. Vyuo Vikuu, ninatoa ushauri tumeweka *retirement age* ya walimu wa vyuo vikuu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa Kingu.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Naibu Spika, naam.

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima yako.

NAIBU SPIKA: Sekunde mbili malizia.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kaka yangu. Ninatoa ushauri tumeweke *retirement age* kwa vyuo vikuu miaka 65, lakini nataka niwaambi kule vyuo vikuu mimi nilifundishwa na akina Profesa Kuzilwa walikuwa ni watu umri umeshakwenda. Wekeni taratibu watu wakishafikisha huo umri waanze kusaini mikataba, kule vyuo vikuu hawabebi zege, tunapoteza maarifa kwenye nchi, watu tunawaacha bado wana uwezo wanakwenda wanakaa nyumbani. Maprofesa... (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, mengine andika kwa Waziri. Mheshimiwa Bidyanguze, jiandae Mheshimiwa Robert Maboto.

MHE. NASHON W. BIDYANGUZE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii na mimi nikupongeze kwa kuchaguliwa kwako lakini naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja katika kumpongeza Waziri wa Elimu pamoja na Naibu wake pamoja na *staff* yake nzima kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nijikite kwenye eneo moja lakini yatakuwa maeneo mawili. Moja ni kwenye shule mbili ambazo zimetelekezwa pale kwenye Jimbo langu ambazo ni shule za Wizara hii ya Elimu ni shule moja ya *Lugufu Boys* na shule moja ya *Lugufu Girls*. Hizi ni shule za Wizara ya Elimu, shule hizi zimetelekezwa kwa sababu hazijapata miundombinu ya maji pamoja na umeme. Naomba Mheshimiwa Waziri unisaidie kwenye jambo hili kwa sababu hizi hazipo chini ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Jimbo langu lina Tarafa tatu. Nilikuwa naomba Tarafa ya Nguruka tupate *high school* kwa sababu tuna sekondari nyingi. Lakini pia naomba kwenye Tarafa ya Buhingu, Buhingu Sekondari ipandishwe hadhi iwe shule ya *high school* kwa sababu eneo langu la Jimbo ni kubwa sana. Kutoka mwanzo wa jimbo mpaka mwisho wa jimbo ni kilomita 400. Kwa hiyo unaweza ukaona kabisa kwamba kila tarafa kuna haja ya kuwa na *high school*. Kwa hiyo watu wa Nguruka wako tayari kupokea *high school* kwenye Shule yao ya Nguruka Sekondari lakini pia Buhingu wako tayari kupokea *high school* kwenye Shule yao ya Buhingu. Naomba Mheshimiwa jambo hili unisadie.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko jambo ambalo mimi ninaomba nilizungumze; ni jambo la kitaifa. Kwanza naomba nipongeze Serikali kwa kukubali kuwarudisha shulenii wanafunzi walipata ujauzito; kwamba baada ya kuwa wamejifungua basi warudi kusoma na huku wakiendelea kunyonyesha. Hili ni jambo jema sana na naomba nikuhakikishie wananchi wamelifurahia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye eneo hili mimi ninaona bado kuna hatari kubwa sana, kwa sababu kwa taarifa ya mwaka jana, mimba za shulenii zilikuwa 8,000, ni nyingi sana! Kwa hiyo, Serikali lazima iweke mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba inapunguza hizi mimba shulenii. Lakini hili ambalo Serikali imelifanya la kuona namna ya kuwarudisha walipata mimba, baada ya kujifungua warudi shulenii huku wakinyonyesha watoto wao. Mimi naona kama hili jambo litaongeza idadi ya mimba. Kwa sababu wale 8,000 walipata mimba lakini wakiamini kwamba hawawezi kwenda shulenii kwa sababu wamepata mimba. Sasa watakapokuwa wamepata mimba na wakarudi shulenii kusoma huku wakinyonyesha mimi ninaona kabisa kuna hatari ya mimba kuongezeka shulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, kwa kuwa pia hata Kamati yangu imelizungumza hili na kuona, kwamba kuwe na elimu kwenye eneo lile la mimba shulenii. Kwa maana itapunguza sasa kile kitendo cha kuongeza mimba shulenii.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Waziri hili jambo usipoliangalia litaleta shida kwa sababu pamoja na kwamba wananchi wamefurahia lakini mimba zitakapoongezeka wananchi wataandama. Kwa hiyo itakuwa kashfa kwa Serikali kuona yenyewe imechochea mimba shulenii kwa sababu imeruhusu sasa watoto waliokuwa wamepata mimba wajifungue na warudi shulenii wakiendelea kunyonyesha watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kitakachotokea mle darasani yawezekana ikawa ni darasa ambalo linafundisha wazazi waliojifungua. Kwa hiyo, naomba hili nizungumze kwa msisitizo. Nakumbuka hili jambo kuna kikao cha Bunge wakati fulani niliwahi kulizungumza, nadhani lilikuwa Bunge la mwezi wa tisa. Kwa kweli naomba nirudie ili kusudi lisije kuleta taharuki baadaye kwa wananchi wetu watakapokuja kuilaumu Serikali kuona kwamba yenyewe ndiyo imesababisha milmba za shulenii kuweza kuongezeka. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja, ahsante sana. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, jiandae Mheshimiwa Samwelii Hhayuma.

MHE. ROBERT C. MABOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Lakini mimi ninayechangia sina elimu ya juu, nina elimu ya chini, kwa maana ya elimu ya msingi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Juzi alikuwa anazindua suala la utalii kwenye nchi yetu, ambapo ukija ukiangalia kwenye Mkoa wa Mara, Mbuga ya Serengeti kwa sehemu kubwa iko upande wetu; kwa hiyo tunampongeza kwa kazi kubwa hiyo anayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Wizara hii ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia, mimi nilitaka kuzungumza jambo moja

tu kuhusiana na suala la vyuo vya ufundi. Kwamba, vyuo vya ufundi vikiboreshwu aidha vikaongezeka vikawa vyakutosha kwenye maeneo yetu, ikiwezekana kila Wilaya au Jimbo kutokana na wingi wa vijana wetu vitatusaidia kuwafanya wao wafundishwe vitu ambavyo wanaviishi kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekuja kupata shida hapa kwenye nafasi hizi zilizotolewa za ualimu. Kwamba shule moja inahitaji mwalimu mmoja, lakini waliiyotuma maombi pale kwenye nafasi hiyo ya mwalimu mmoja ni walimu zaidi ya 800; halafu anachukuliwa Mwalimu mmoja, wale 790 wanabaki. Halafu kila wanapobaki muda wao wa kustaafu unazidi kuwasogelea. Naijuliza muda wao utakapoisha hawa watu watakuwa wanafanya nini? Lakini pia naijuliza hawa watu wakifundishwa kwenye vyuo vya ufundi kwa mfano Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kisangwa kile kilichopo pale Bunda, kikaboreshwu vizuri na Serikali kikaweza kuchukua vijana wetu wengi, wale waliomaliza Darasa la Saba hata wengine waliomaliza Kidato cha Nne ambao hawakupata nafasi ya kuendelea; wakaenda pale wakafundishwa shughuli zao za mikono ambazo wao kwenye maeneo yao wanayoishi hazitawafanya zitawafanya waweze kumudu maisha? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa ukija ukiangalia walimu wamepata elimu yao ya ualimu lakini nafasi zinazotoka ni kidogo na hawawezi kuitumia nafasi hiyo. Kwa hiyo, mimi nikawa napenda kuishauri Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwamba kwenye Mpango wake mkubwa ni vizuri ikaboresha vyuo vya ufundi. Ili kwamba tukiwa na wimbi kubwa la watu ambao wamekaa hawawezi kufanya kazi, lazima tuwe tunajuliza mara mbili mbili matokeo yake ni nini? Lakini hata wale wanaosoma sasa leo lazima waone wale wenzao waliotangulia wanachokifanya ni kitu gani au ninafasi gani wanayoipata na kama wanaona nafasi ni kidogo lazima watafute njia ya pili ya kufanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia mimi sidhani kama ingewezezana Taifa zima hili la Tanzania watu wote tukawa

tuna *degree*; atakayeweza kumbebea mwenzake mzigo atakuwa nani? Haiwezekani. Kwa hiyo mimi ninaishauri Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kuboresha vyuo vya ufundi tena kwa *speed* kubwa kwa sababu vijana wetu wakipata utaalam wao pale utawawezesha wao kuishi mitaani kwa kufanya shughuli zao wao wenyewe na kwa kujiajiri wao wenyewe. Na kujiajiri kwao wao wenyewe kutawafanya shughuli yao wao wanayoifanya wachange kwenye mfuko wa Serikali kwa kulipa kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vijana wetu wa bodaboda, kwa mfano leo hii tusingekuwa na mpango huu wa bodaboda kwamba vijana wamejiajiri kwenye bodaboda, wale wote wangekuwa wako mitaani wamekaa wanasesibiri kuomba ajira Serikalini ilhalii nafasi zenyewe zinazotoka za ajira ndiyo hiso; kwamba kati ya watu 800 anatakiwa kuchukuliwa mtu mmoja na wale wangeongezeka ingekuaje? Kwa hiyo wimbi la watu ambaao hawana kazi lingekuwa ni kubwa kuliko uhalisia wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana mimi nilikuwa nashauri kwamba ni vizuri Wizara hii ikaboresha vyuo vya ufundi na kuviongezea upana wake ili iweze kuchukua wanafunzi wengi zaidi ili hawa vijana wetu watakapomaliza kujifunza utaalam wao watajiajiri wao wenyewe kama vile ambavyo vijana wetu wa bodaboda walivyojiajiri wao wenyewe. Tofauti na hapo kwa kweli itakuwa hata hawa ambaao wamepata elimu zao wanafika sehemu wanataka kuchukia kile alichokisomea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwengine najiuliza, mtu wakati mwengine anakuja ana *degree* yake, amemaliza shule ana *degree*; lakini hata ukimuliza ile namna ya kujieleza baadhi yao hata kujieleza tu hawezi. Sasa unajiuliza wewe hata kama umesoma ni kweli una *degree*, *degree* hii hata huwezi kwenda kuiishi mitaani au kwa mazingira yako unayoyaishi wewe huweizi kuitumia inakuwa inakusaidiaje? Ndiyo maana nasema, watu wakifundishwa katika uhalisia wao wa maisha yao utawaondolea umasikini kwa sehemu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kubwa. Lakini pia itawafanya wao wajajiri wao wenyewe, vilevile wao pia watakuwa fundisho kwa wenzao. Kwamba nikiona njia hii ya ajira imebana nitakwenda njia nyingine ya pili ambayo itanifanya na mimi niishi kama fulani anavyoishi ye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisema watu wote wafanye kazi aina moja naamini kwamba nafasi hizo pia hazitaweza kupatikana. Mwisho watu watacaa kubaki kulalamika Serikali kwamba Serikali haitoi ajira lakini Serikali itatoa ajira baada ya kuwa ina *income* ya kuweza kuwalipa watu Mishahara. Na Serikali kupata mishahara ya kulipa watu ni lazima watu wawe wanafanya kazi, wanapata pato, wanalipa kodi na Serikali inapata fedha ya kuwalipa watu mishahara. Kwa sababu Serikali haiwezi kulipa watu mishahara kwa kupitia fedha ya kukopa, haiwezekani; ni lazima watu wafanye kazi, wazalishe wapate fedha kwao wao wenyewe na fedha zao zitumike kuwalipa mishahara wananchi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi niliona kwenye suala hili la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia nitoe mchango wangu huo ili kwamba Wizara hii ikituboreshea chuo chetu kile cha Maendeleo ya Wananchi pale Bunda, ikakipuanua, itaweszesha vijana wetu wengi waende kupata mafunzo yao pale na mafunzo yale yatawawezesha kuishi vizuri kwenye eneo lao baada ya kuwa wanafanya shughuli zao ndogondogo za mikono na zitakazowezesha kuendesha maisha yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya kusema hayo, nakushuruku kwa kupata nafasi hii, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Samwelii Hhayuma, jiandae Mheshimiwa Japhet Hasunga, jiandae Mheshimiwa Khadija Taya.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na pongezi kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda Waziri wa Elimu, Mheshimiwa *Architect* Omari Juma Kipanga Naibu Waziri; Katibu Mkuu Ndugu yangu Profesa Eliamani Sedoyeka, Naibu Katibu Mkuu wa Sayansi Ndugu yangu James Mdoe, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulika masuala ya elimu mwanamama Profesa Carolyne Nombo na wataalam wote wa Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri wanayoifanya. Hawa nawapongeza si kwa sababu tu nawapongeza, kwa sababu baada ya Mheshimiwa Rais kutoa tamko kwamba sasa tupitie sera, mitaala kwa sasa wanachakalika wanapambana usiku na mchana kuhakikisha kwamba wanapitia sera yetu ya elimu. Wanapitia mitaala yetu ya elimu ili kuisogeza karibu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamekuwa na malalamiko ya muda mrefu ya elimu yetu kutokugusa maisha ya wananchi wa kawaida. Profesa Mashimba wameisema hii kwa kipindi kirefu sana. Kwa hiyo, mtoto akitolewa nyumba akipelekwa kwenye mfumo elimu anarudi ile asilia yake imeondoka lakini wameanza kuifanyia kazi kwa kasi kubwa, nawapongeza sana kwenye eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitoe angalizo kwenye hatua hii ya mapitio ya sera na mitaala ambayo tunaifanya kwa sasa. Nimemsikia mara kadhaa Profesa Mkenda akisema mapito ya sera, mitaala ya elimu ni kazi ambayo imeanza kufanywa na dunia nzima, sisi tulianza mapema. Tunaomba sana tusiburuzwe na dunia sisi tulioanza mapema ile nia yetu ya awali ibaki pale pale ili tufikie elimu yetu iguse mazingira ya kwetu. Tupate elimu inayotatua changamoto tulizonazo kwenye mazingira yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yote ambayo yanafanyika dunia sasa ni Kijiji hatuyakatai lakini sisi tusimezwe na changamoto zile ambazo zipo duniani. Tuhakikishe tunatatua changamoto zetu kwanza, tunaboresha elimu yetu, tunahakikisha kwamba tunasogeza elimu tunayoitoa kwa wananchi wetu ili ukimfundisha mtu darasani akienda kwenye

mazingira ya kawaida ya kuishi aweze kuitumia elimu ambayo ameipata ili iweze kumsaidia kwenye mazingira anayotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na utaratibu wa kutathmini ufaulu wetu kwa kuangalia yejote aliyefaulu lakini ukiangalia wanaopata Daraja la Nne, wengi mno kwa nchi hii hasa kwa sasa ambao tunatoka vijijini. Vijana wale wamesoma Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne ukilinganisha na wale ambao hata darasa la kwanza hawajaingia shughuli wanazozifanya zinafanana. Tuangalie elimu tunayotoa, itoe tofauti ya yule aliyekwenda shule na ambaye hajaenda shule ili wale waliokwenda shule wakatoe shule kwa wale ambao hawajaenda shule! Wao wawe kielelezo cha wale ambao hawajapata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaoishi na hao vijana, wanaofuga vijana ambao wamemaliza kidato cha nne na wale ambao hawajaingia hata darasa la kwanza mazingira ni hayo hayo, wanaolima vivyo hivyo, elimu yetu lazima itoe tofauti kati ya watu ambao wamekwenda shule na wawaelimishe wale ambao hawajapata bahati hiyo kwa sababu nafasi siyo nyngi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyngine tuliyonayo, waliomaliza Kidato cha Nne wamepata Daraja la Nne kwenda Sifuri, zaidi ya asilimia 65 mpaka asilimia 70, kwa sisi vijijini inaweza kuwa 75 mpaka 80! Hao tunawaacha tunawasahau historia yao inafutika baada ya kuwa wamefeli elimu ya sekondari. Kwenye imani zetu zote binadamu akiishi, ikifika siku ya kufa tunaamini kwamba baada ya muda fulani kuna jambo fulani zuri linafuata kwa Mwenyezi Mungu, ambaye hajafanya vizuri either anakwenda Jehanamu. Sisi tukimaliza tu Kidato cha Nne tumefunga hapo, tutengeneze uratatibu wa kusaidia hao vijana ili waje wasaidie Taifa lao. Tutengeneze Vyuo vya Ufundı ambavyo vitawapa ujuzi hao vijana waweze kutoa mchango stahiki kwa Taifa lao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza hotuba ya Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu yangu Sedoyeka wakati Mheshimiwa Rais akiwa Mgeni Rasmi pale Arusha. Kwamba

tutatanua Vyuo vya Ufundu mpaka kwenye ngazi angalau ya Tarafa. Mimi hivi ninavyoongea Jimbo la Hanang' halina hata Chuo cha Ufundu – VETA. Tuweke nguvu kubwa kwenye eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimefanya kazi mbalimbali wachina ukiuliza tu taarifa zao mtu mwenye cheti tu ana ujuzi wa kufanya mambo mbalimbali, nchi yetu tuwekeze huko kwenye elimu ya katil! tuweka nguvu kubwa huko. Lakini tuunganishe elimu yetu na mazingira yetu ya kawaida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Waziri ulikuja mwaka 2020 Disemba pale Hanang', wakati tukitaka kuboresha kilimo cha ngano, tukakuomba sana wakati huo ukiwa Waziri wa Kilimo, sasa Waziri wa Elimu. Kwamba ule uzalishaji wa Ngano Kituo cha Umahiri kiwe Hanang. Tuunganishe sekta zetu za uzalishaji, kilimo, ufugaji, uvuvi na elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kile Kituo cha Umahiri tukipata Chuo Kikuu kitaendesha Kituo cha Umahiri Hanang', tukafufua kilimo cha Ngano, tunachangamoto kubwa ya mbegu ya ngano na mbegu za mazao mbalimbali, itatusaidia sana. Tuunganishe elimu yetu na kazi tunazofanya za kilimo, ufugaji na uvuvi na mambo mengine mbalimbali ambayo tunafanya biashara ili elimu itusaidie kututoa sisi kwenye changamoto tulizonazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kidogo suala la angalau hamasa kwa wale wanaotoa elimu. Upande wa elimu ya msingi imesemwa sana na Profesa Kitila Mkumbo. Elimu ya Sekondari ameisema lakini tukija kwenye upande wa Vyuo Vikuu ninachoomba kila mtu anayefanya vizuri tutambue mchango wake sawa sawa! Kama mtu ameleta jawabu la changamoto either ya kudhibiti upotevu wa maji tuutambue huo mchango. Maprofesa wetu wale Wahadhiri wetu wanaofundisha vyuoni tuwatengenezee utaratibu wa kutambua mchango wanaoutoa kwenye jamii yetu kwa kutatua changamoto zilizopo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo sawa hata kidogo kama nimeitwa Profesa basi, haki ninazopata na Profesa yoyote ni sawa, kama mimi nimechangia zaidi utambuzi huo ufanyike. Kama mtu ameleta jawabu la suluhu ya kisiasa, kiuchumi na mambo ya kisaikolojia. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Hasunga, jiandae Mheshimiwa Khadija Taya, jiandae Mheshimiwa Kasalali Emanuel Mageni.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa kuniona na kunipa nafasi hii adimu na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze sana Wizara kuanzia Waziri na timu kwa ujumla na kwa kweli kuja na hotuba ambayo inaonesha mabadiliko mengi ambayo yanakwenda kufanyika na yale mambo saba ambayo umeyasema kwamba mnakwenda kuyatekeleza basi sisi tupo tayari tunayasubiri utekelezaji na tunaamini yataweza kuisaidia nchi hii ikaweza kwenda mbali. Kwa hiyo, Mheshimiwa Profesa tupo pamoja na wewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Kamati kwa uchambuzi walioufanya wamefanya vizuri, kwa kweli wamezungumza mambo ya msingi na mimi naamini Wizara itakuwa imeyachukua kwenda kuyafanyia kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ya Japan ni moja ya nchi zilizoendelea sana, lakini ilifika mahali kuna kipindi nchi ile uchumi wake ulisimama, kila kitu kilisimama. Sasa Waziri wa Elimu wa nchi ile alichokifanya alitayarisha *questionnaire* akawaandikia Maprofesa 14 duniani wa vyuo vikubwa, akawaambia nataka mniambie hivi hasa nini roho ya elimu katika: akaweka kila eneo kama ni kwenye kilimo, ufugaji, uvuvi, viashara, viwanda na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale Maprofesa walipomjibu ndiyo waliyoisaidia kuikwamua Japan na uchumi wake ukaanza tena kupiga hatua. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo na sisi hapa leo Profesa umebeba hiyo dhamana, tunaelewa kwamba elimu ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu, elimu ndiyo inatupatia maarifa ya namna ya kufanya mambo yetu. Elimu inatupatia ujuzi lakini elimu inasaidia kubadilisha tabia tulizokuwa nazo halafu ziwe katika hali tunayoitaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wale Maprofesa walisema, elimu hata ukisoma iwe ni Tanzania, iwe ni nje ya nchi yale maarifa unayoyapata, ukija nayo nyumbani kwako yakusaidie kuboresha mazingira uliyonayo na vitu ulivyonavyo ili viweze kuwa katika hali nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kule Songwe, Mkoa wetu wa Songwe ni mchanga ni mkoa wa kilimo, sisi tunashika nafasi ya tatu kwa uzalishaji wa chakula hapa Tanzania lakini pia tuna mazao ya biashara. Katika Mkoa ule ambao tunazalisha kwa kilimo, tunazalisha sana lakini tuna Shule za Msingi 193, Sekondari 64 katika vyote hivyo, shule zote hizo hakuna shule inayomuandaa kijana kwenda kuendeleza kilimo ambacho ndiyo wamekulia, ndiyo muhimili wa nchi yetu, uti wa mgongo. Sasa ina maana ile elimu wanayoipata, wanayosoma wote wale, inakwenda kusaidiaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu elimu haijagusa kwenye kilimo, ufugaji, uvuvi, haijagusa mambo yaliyopo katika ile jamii. Kwa hiyo, tunataka elimu tunayoipata iende kujibu maswali yale. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nimefurahi kusikia kwamba mnakwenda kuanzisha Vyuo vya Ufundı, na mimi nasema Mkoa wa Songwe tunahitaji Chuo cha Ufundı ili kiweze kusaidia sasa katika kuwapa ujuzi na maarifa ili iwasaide katika kuendeleza katika mazingira yale ambayo tunayo. Kwa hiyo, naamini hilo mtalifanyia kazi vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji vifaa vya kufundishia vya kisasa. Sasa hivi shule zetu zote ili ziweze kutoa elimu nzuri, zinahitaji kuwa na kompyuta TEHAMA, ziwe na vifaa vya kufundishia, ziwe na *photocopy*, hizi shule za kusema kwamba eti bila ya kuwaandalia mazoezi ya kutosha hatutaweza kufanya vizuri. Lakini mimi nataka kusema haya mambo mengine yote yamesemwa vizuri na waliotangulia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ninalotaka kulizungumzia ni udahili katika vyuo vya elimu ya juu. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongenza sana Mheshimiwa Rais kwa mambo mbalimbali anayoyafanya lakini ikiwemo ya kuanzisha ile filamu ya *Royal Tour*. Hii itatuletea watalii wengi. Baada ya watalii hao watakaokuja hapa nchini wengine watakuja kwa ajili ya kusoma. Tutakuwa na utalii wa shule, utalii wa kuja kusoma. Sasa kwetu hapa Tanzania tuna bahati ya pekee, Serikali mmejitahidi, Serikali lazima tuipongeze imejitahidi. Tuna Vyuo vya Elimu ya Juu zaidi ya 50, zaidi ya 50 Vyuo vya Elimu ya Juu viko hapa katika nchi yetu, nchi nydingi hazina hivyo vyuo. Tunayo mitaala mingi na mitaala yetu ambayo tunaitengeneza sasa hivi na nafurahi Mheshimiwa Profesa mnaipitia upya ile mitaala naamini mitaala mtakayokuja nayo itajibu mahitaji ya nchi yetu lakini lazima pia tuangalie mahitaji Afrika Mashariki, SADC, Afrika na tuangalie ulimwengu kwa ujumla kwamba wanahitaji nini hasa maana yake sisi ni sehemu ya ulimwengu, ni sehemu ya *globalization*. Kwa hiyo, lazima elimu tunayoitoa ikidhi mahitaji haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi ninachotaka kusema ni nini. Katika hivi vyuo vyote tulivyonyavyo ambavyo viro, sasa hivi mkakati Profesa uwe katika kudahili wanafunzi wengi wa hapa ndani lakini na wa nje. Tuchukue kutoka Kenya, Uganda, South Sudan, Ethiopia, Ulaya, wote mnaelewa Waheshimiwa Wabunge, UK ukiangalia pato lake la Taifa sehemu kubwa mchango wake wa Pato la Taifa unatokana na shule na watu mbalimbali wanapeleka kwenda kusomesha watoto kule na sisi tunataka sasa tufike mahali watoto waje kusoma hapa kwetu, nchi ya Tanzania

tupo *strategically located!* Tutumie amani na utulivu kama tunu tuliyonayo hii ituletee sasa watalii wa elimu waje kusoma hapa na vyuo vyetu vipate wanafunzi wengi. Tukifanya hivyo, mitaala tukiiboresha, tukaondokana na haya mambo ya zamani!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Profesa zamani kulikuwa na *mature age entry* kwenye Vyuo Vikuu, tulifuta tukaondoa. Sielewi kwa nini tuliondoa? Lazima tuiangalie hiyo kwa nini tuliindoa hivyo vitu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii watu wanasema mtu akitoka Kenya hana sifa ya kusoma kwenye Vyuo Vikuu vya kwetu, hivyo tunataka kusema sisi ndiyo tuna elimu nzuri kuliko hata ya Kenya? Hiyo siyo kweli, lazima hayo tuyaangalie! Kama kuna mahali tumeefanya makosa ni kwenye eneo hilo. Tukaangalie udahili wetu tuanzishe mambo haya. Kama tunaona kwamba hawajakidhi vile vigezo vya kwetu anzisheni kozi ya *foundation* kwenye vyuo vyote, isiwe kwenye *Open University* tu, kwenye vyuo vyote, wapeni udahili wafanye *foundation* mwaka mmoja, wapate zile *minimum qualification* wasome hapa, walete dola nyingi, hizo dola zitatusaidia kwenda kulipa hata hii mikopo ambayo tunaikopa kwa ajili ya elimu yetu, tunakwenda kulipa. Sasa Tanzania tunasema tupo pazuri, pazuri bila kutumia hii nafasi tutashindwa. Kwa hiyo mimi nafikiri Mheshimiwa Profesa mtafanya mabadiliko makubwa na nimeona kwenye hotuba, nimeona kwenye mambo mengi na hatua ambazo mnachukua tunataka ziende zika-*address* haya zitusaidie kama nchi kuleta mambo tunayoyahitaji. (*Makoffii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ina changamoto nyingi, watoto wengi wanakwenda kusoma wanakosa mikopo. Nafikiri ni wakati muafaka Profesa, hebu angaliaeni ni namna gani wadau mbalimbali wanaweza kuchangia kwenye hii Bodi ya Mikopo. Tupate fedha kutoka kwenye maeneo mengine tupanue wigo halafu watoto wetu wote wapate elimu, waweze kupata mikopo hiyo, wapate iwe ni kama vile vyuo vya elimu ya kati, Vyuo Vikuu wale wote wenye sifa wapate mkopo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni mkopo watakwenda kulipa sasa kwa nini tuwanyime. Kwa hiyo, mimi nafikiri kwamba ni suala la msingi tuangalie hilo litatusaidia sana tukipanua wigo wadau wakachangia, tukawa na fedha za kutosha na tukaweza kufanya vizuri. Mimi naamini katika hatua hizo itachangia sana katika uchumi wa Taifa letu na nchi itaweza kupiga hatua vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo ninataka kusema ni ajira kwa wanataluma. Wanataluma kuna sifa zao, kuna vigezo na sisi kwenye ajira ndiyo tunataka huko tupanue ndiyo maana mimi nasisitiza sana hivi vyuo vyote tulivyonavyo tuajiri watu. Kwahiyo kwene taaluma naomba Profesa aangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Khadija Taya jiandae Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, jiandae Mheshimiwa Francis Ndulane.

MHE. KHADIJA S. TAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii kuchangia leo katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwanza kabla ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uhai.

NAIBU SPIKA: Ndiyo wewe au?

MHE. KHADIJA S. TAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya, leo hii nimesimama hapa kuchangia masuala ya elimu juu ya watu wangu ambao wamenileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, sana sana. Mama jana tumekusikia umezungumza kama Mama tena Mama yule ambaye ana viakiba vyake yupo tayari watoto wake wale hata ugali na mlenda kuliko kushinda na njaa. Kwa hiyo, tayari tumeona namna gani Mama anaguswa na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Watanzania na wanyonge na tunakupongeza sana Mama, tunakupongeza sana Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie leo kwenye hii Elimu, Sayansi na Teknolojia juu ya masuala ya vipaji. Mimi ni muumini wa vipaji, kwa sababu nimepata kipaji changu, nilikuwa na kipaji changu lakini nimeendelezwa kuititia Shule ya Msingi. Nimefanya *bands*, nimefanya kwanya, nimeimba na nimefanya vitu vingi sana mashindano ya kwaya, bendi yakani jengea uwezo. Kwa hiyo ninaamini kabisa Wizara ya Elimu ikiangalia namna hii ya kuweza kukuza vipaji vya watu, leo hii tusingewaponda akina Diamond na wengine kwa sababu shamra shamra za shulenzi za mashulenzi zile za mashindano ya waimbani na vitu kama hivyo.

Kwa hiyo, naamini kabisa, Wizara ya Elimu ikiangalia namna hii ya kuweza kukuza vipaji vya watu, leo hii tusingewapata akina *Diamond* akina nani kwa sababu ya ile shamra shamra za shulenzi zile za mashindano ya waimbaji ya nini na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, naamini sio kipaji kimoja tu tunaweza tukakipata shulenzi vipaji vingi tu tunaweza tukatengeneza watu wengi tu wacheza mpira, michezo, *everywhere*, kila sehemu tunaweza tukapata watu wa kuweza kuwakilisha hii nchi, lakini pia kuinua uchumi wa hii nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni muumini wa vipaji kwa sababu pia itaacha haya mambo ya kukaa vijiweni kuvuta bangi, kuvuta unga na panya *road*. Vipaji vitakuzwa kimaadili zaidi, tutaona kabisa umuhimu wa vile vipaji ambavyo tunavitengeneza kuanzia chini mpaka kwenda juu. Kwa hiyo, naiomba Wizara hii ianganlie hilo kurudisha mambo ya muziki shulenzi, mambo ya mpira michezo na vitu kama hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, cha pili naomba nichangie juu ya masuala ya lugha ya alama mashulenzi. Juzi nimesema tunahitaji lugha ya alama mashulenzi, ni muhimu sana. Tunafahamu kabisa lugha ni mojawapo ya sehemu ya

mawasiliano, hatuwezi kuelewana kama hatutumii lugha ambayo tunaweza tukaelewana. Naomba tu niwaaulize Wabunge leo hii Wabunge nyinyi humu ndani mnawawakilisha wananchi, watu wenyewe ulemavu huko chini katika Majimbo yenu, hivi ni wangapi humu ndani wanafahamu lugha ya alama ya kuwasiliana na viziwi? Wangapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wachache sana, kama wapo basi ni mmoja, wawili au watatu, mimi mwenyewe sifahamu lugha ya alama na huwa najisikia vibaya sana. Kwa hiyo, ningeomba Wizara pia ilete semina hata ya wiki moja tufahamu tujifunze lugha ya alama, tujue *numbers* tujue vitu *basic* ambavyo vinaweza vikatusaidia kuwasiliana na hawa watu wasijione kama wanatengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mpiga kura wako akija kwako anataka kuzungumza na wewe hawezi kuzungumza naye. Gharama za mkalimani ni kubwa sana, hawezi kumudu muda wote akawa anatembea na mkalimali ili akuelezee shida zake. Kwa hiyo, tunaamini kabisa watoto wetu mashulenii wakianza kujifunza lugha ya alama ina maana hata watu ambao wamezaliwa wana ulemavu wa kutokusikia, tayari itawasaidia wao. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie hili ni muhimu mno mno, ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, cha mwisho, naomba nichangie juu ya masuala ya elimu jumuishi, tunafahamu tuna Walimu katika mashule ya elimu jumuishi. Tunafahamu kwamba hawa Walimu wengine ni wachache mno, lakini wengine pia *wame-specialize* kwenye *area* moja lakini sasa kwa sababu tu ni walimu wa elimu jumuishi, wanakwenda mashulenii wanafundisha kila mtoto ambaye ana matatizo ya ulemavu, hapana. Tunatakiwa tujue kabisa huyu mwalimu *ame-specialize* kwenye viziwi peke yake, huyu mwalimu *ame-specialize* kwenye ulemavu wa akili, huyu mwalimu *ame-specialize* kwenye *area* hii na hii na hii. Kwa hiyo, tujue namna gani hawa watu wanaweza wakatusaidia tuongeze Walimu ambao wamebobeaa katika sehemu mbalimbali ili tuweze

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuwafundisha hawa watu na vile vile kuwatengenezea mazingira mazuri ya wao kuishi katika hii dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze mama katika *area* moja. Ameongeza vyuo vya watu wenye ulemavu sasa hivi vimeongezeka. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amesema vyuo vilivyoongezeka kule Singida kesho kutwa tunakwenda kuzindua Tanga. Hii tayari ni hatua nzuri sana ambayo Serikali imefikia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi vyuo tuvitumie hivi vyuo viende kuamsha/kuondoa umasikini wa watu wenye ulemavu tuwatengenezee elimu, lakini pia tuwape nyanja tofauti tofauti tuwatengenezee ubora na uwezo ambao wanaweza wakafanya. Hivi leo hii wanaonaje Serikali wakawafundisha hawa watu wenye ulemavu ambaye yeye labda hawezi kutembea, tukamfundisha kutengeneza bahasha tu hizi, halafu leo *tender* za hizi bahasha tukazichukua kwa watu wenye ulemavu, ndio tukawa tunawalipa wale watu wenye ulemavu, hatuoni kama tutakuwa tumewasaidia hawa watu wenye ulemavu? Kwa hiyo, naomba Serikali itafute namna gani ya kuondoa umaskini wa watu wenye ulemavu, watu wenye ulemavu ni maskini sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze, hawa watu ni masikini sana, kwa sababu kama mtu tu ana miguu yake na mikono yake na maisha ni magumu, fikiria mtu ambaye hana miguu, hana mikono, hawezi kusikia, ni namna gani ambavyo anaishi au na wale pia familia ambayo inawalea wanashindwa kuwalea vizuri. Kwa hiyo, naomba Serikali inapokuwa inafikiria mambo yake ya kimaendeleo, mambo ya kielimu, iangalie sana kundi hili ni muhimu mno. Mmii ni sauti ya watu wenye ulemavu hapa Bungeni, nitazungumza kila siku na mtanichoka lakini naomba Serikali iangalie namna gani ya kuboresha maisha ya watu wenye ulemavu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo machache naunga mkono hoja na nashukuru sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kasalali Mageni.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nitumie fursa hii kuwapongeza watu wa Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri wanayofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu moja kwa moja kwa kuwalettea kilio cha watu wa Wilaya ya Kwimba. Tangu mwaka 2019 Serikali ilianza mchakato wa kujenga Chuo cha *VETA* kwenye Wilaya ya Kwimba katika Mji wa Ngudu ambao ni Makao Makuu ya Wilaya. Ujenzi wa hiki chuo umechukua sasa miaka takribani mitatu na Mheshimiwa Waziri ulikuja ziara kwenye Wilaya yetu ya Kwimba; na alikuwepo pia Mkurugenzi wa *VETA* aliahidi kwamba watamaliza mapema na Serikali iliahidi watamaliza mapema hakijakwisha mpaka sasa. Sasa sisi watu wa Kwimba hatupendelei sana kuwa na magofu ya kujificha wezi kwa sababu kimekuwa cha muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashauri Wizara ya Elimu, nilifikiri matatizo ya usimamizi yamebaki Serikali za Mitaa, lakini naona na Wizara ya Elimu kwenye usimamizi wa miradi yenu hasa mimi naona mfano wa hiki Chuo cha *VETA* kilichoko Kwimba, yaani Chuo kinajengwa Kwimba anayesimamia ni Chuo cha *VETA* Kagera. Hapo unaona kwamba ni kutengeneza maigizo fulani na kukwamisha shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wanaojenga Chuo cha *VETA* kwenye Wilaya ya Kwimba badala ya kuwa neema wametuletea matatizo. Kuna wajasiriamali ambao nilisema wakati wa ziara ya Naibu Waziri wametumia fedha zao wameleta kokoto, wameleta mawe mpaka leo hawajalipwa na nilisema na Mkurugenzi wa *VETA* aliahidi mbele yangu kwamba watalishughulikia, watawalipa. Wamefilisi watu, yaani badala ya kuwa neema imekuwa ni laana. Sasa tuwe *serious* kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabisa hawa watu wa Wizara ya Elimu jambo la kumalizia *VETA* ya Kwimba na

jambo la kulipa watu walioshiriki kwenye ujenzi wa *VETA* hiyo, ambao niliahidiwa kama Mbunge wao siku ya ziara ya Wizara husika, mpaka leo hawajatekeleza, wanawatisha hao watu, wanaomba rushwa na vitu vingine. sasa naomba Wizara ya Elimu wawe *serious*, walimalize suala la *VETA* Kwimba watu waanze kusoma lakini, yalipwe madeni ya watu wote wazabuni wa Kwimba walioweka nguvu zao pale. Najua bajeti ilikuwepo, hawawezi kuitisha kokoto wakati hakuna bajeti, vinginevyo tunataka kufilisi watu wetu na kuleta vitu ambavyo havina msingi huko *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka nichangie hapa ni kwamba Wizara ya Elimu ndio uti wa mgongo wa maendeleo ya nchi yetu, ili nchi iendelee ni lazima fursa na matatizo na vitu vilivyopo kwenye nchi vifahamike. Sasa tunaweza kufahamu vipi matatizo yetu, tunaweza kufahamu vipi fursa zetu na tunaweza kuwa na mbinu gani za kutatua matatizo yetu, kuna kitu kinaitwa utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu ndio wanaosimamia Vyuo Vikuu na Vyuo vya Elimu ya Juu. Vyuo Vikuu ndio kitovu cha utafiti kwenye nchi yoyote inayotaka kuendelelea na nchi yoyote inayotaka kutatua matatizo ya watu wake.

Hata hivyo, nasimama hapa nikiwa na masikitiko, Serikali illiahidi kwamba asilimia moja ya *GDP*, tutakuwa tunapeleka kwenye utafiti, kitu ambacho hatujakifanya. Utafiti kwenye vyuo vyetu vya elimu ya juu umekuwa ukitegemea fedha za wafadhili, mfadhili hawezi kuleta fedha ambayo haisaidia jambo lake. (*Makofii*)

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, ili sisi tutatue matatizo yetu tunahitaji kuwa na fedha zetu wenywewe.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

MHE. KASALALI E. MAGENI: ...na tuziwekeze kwenye utafiti.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Kuna taarifa Mheshimiwa Mageni.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba sio tu vyuo vyetu vinategemea fedha ya tafiti kwa fedha za nje, lakini tu hata mtoa fedha akitoa tafiti ili mwanachuo afanyie tafiti, Mwalimu huyo huyo aliyepewaa fedha mwanachuo afanye tafiti anamshika hamalizi chuo miaka sita ya *PhD*. Naomba nitoe taarifa hiyo.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mageni.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naipokea hii taarifa. Kwa kuweka msisitizo ni kwamba, hawa wafadhili wanaofadhili utafiti wetu wanawatumia wasomi wetu kutatua matatizo yao. Sisi tunao hawa wasomi, lakini tumeshindwa kuwatumia kutatua matatizo yetu, kwa sababu nafikiri tumeshafikia wakati tumekosa vipaumbele kwenye elimu, kwamba, umefika wakati sasa hata watu wanaoweza kutushauri kufahamu matatizo yetu hatuwapi fedha za kufanya hiyo kazi. Badala yake hao Maprofesa wetu/Madaktari tulioajaza kwenye Vyuo Vikuu wanatumika na nchi za nje, wanatumika na wafadhili kufanya utafiti kwa ajili ya hao wafadhili badala ya kufanya utafiti kwa ajili ya nchi yetu. Kwa hiyo, nataka niishauri Wizara kwamba nguvu kubwa iwekeze kwenye utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina matatizo mengi, kwa mfano, tatizo moja tu la wizi, ubadhirifu na kukosekana kwa uaminifu kwenye usimamizi wa mali za umma. Tumekuwa tukilalamika huko kwenye halmashauri, tumekuwa tukilalamika kila sehemu, je, tumewahi kuwekeza kwenye utafiti kujua chanzo cha hili tatizo? Kwa sababu, hawa wanaoiba kila siku tunatengeneza *CAG* nenda

kakague, Waziri nenda katumbue, tunaowatumbua ni wasomi wetu, wanaoiba ni wasomi wetu, tumeshatafiti elimu yetu ina msaada gani kenyé Taifa yetu? Kama inatuzalishia wasomi wanakuwa wezi, wasomi ambao wanahitaji ziara za Waziri awatumbue ndio wafanye kazi, kwa hiyo, hatuwekezi kwenye kutatua matatizo yetu, tunawekeza kwenye vitu ambavyo havina msingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumza Waheshimiwa Wabunge hapa kuhusu mfumo wetu wa elimu. Hata mimi ukiniuliza mimi mwenyewe ni mfano, nimesoma *form fournafikiri* nilisoma masomo 10, ukiniuliza hayo masomo niliyoyasoma kwanza hata nilishayashahau. Yaani tunapoteza muda mwingi kwenye mfumo wa elimu wa kikoloni kupotezea muda watoto wetu mashulen, badala ya kuweka mfumo ambao unatatua matatizo yetu ya sasa na jibu la haya yote hatufanyi utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nani amefanya utafiti nani amejiridhisha kwamba ni lazima mtoto wa shule ya msingi acae miaka saba shulen? Atoke hapo aende sekondari miaka minne, aende *A Level* miaka miwili, halafu sasa hao watu wetu ambao tunawasomesha muda wote huo na wale wanaosoma miaka minne Kenya, tukiwaweka sokoni tunaona tofauti gani? Kwa hiyo ni lazima tufike wakati kama Waheshimiwa Wabunge walivyoshauri kwamba tufike wakati mfumo wetu wa elimu ya msingi na sekondari, tuuangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna sababu ya kuweka watoto shulen muda wote huo, tunawapotezea muda wanakuja kumaliza vyuo vikuu ni wazee, wanakwenda kazini muda mfupi tu wameshastaafu, lakini muda mwingi wameupoteza wanasonma *logarithm*, wamesoma kipeuo cha nini, mtoto unakuta amerundikiwa masomo mpaka anachoka kusoma. Unakuta mimi niliyoyasoma *O Level* nimeshasahau, sina kazi nayo, nakumbuka tu labda niliyosoma Chuo Kikuu machache ambayo niliyafanyia kazi. Kwa hiyo, tutafute tu namna ya kuwapa watoto wetu *package* ambayo inawastahili kwa ajili ya kutatua matatizo ya nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee pia suala la Bodi ya Mikopo, Waheshimiwa Wabunge hapa wamelizungumzia. Vigezo vya kutoa mikopo imekuwa ni kuangalia umaskini na uhitaji wa mtu. Hawa watu wetu waliopo Bodi wako kama wangapi wangapi hao wana uwezo wa kujua huyu ni maskini na huyu ni tajiri?

Nafikiri tufike wakati tunatengeneza tu utaratibu mwingine wa kuonea watu, mimi Mbunge wa Sumve, kuna watu wengi kule wanani lalamikia na ukiwa angalia ni maskini wamenyimwa mkopo. Vigezo vinavyotumika sio rafiki na naamini hatuna nguvu kazi wala wataalam wa kutosha kutafiti na kujua huyu ni maskini, huyu sio masikini. Cha msingi hapa tutafuteni namna ya kusomesha watu wetu. (*Makofî*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante, kengele ya pili hiyo. Mheshimiwa Almas Maige dakika tano. Mheshimiwa Almas Maige uko ndani au uko Tabora?

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, niko hapa hapa Bungeni. (*Makofî/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Haya tuendelee, dakika tano. (*Makofî*)

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie hotuba hii ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na leo nina machache sana dakika tano zinanitosha. La kwanza, ni ombi, kumekuwa na maombi kwa wale wanaopenda kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia lakini pia lugha ya kujifunzia. Serikali ianzishe shule ya mfano ambayo itafundisha Kiswahili darasa la kwanza mpaka Chuo Kikuu, ili kufuta kabisa wazo kwamba Kiswahili kinafaa au hakifai kufundishia. Suala hili litaonesha mfano mzuri, nimekuwa nikisema hivi watu wanaleta hoja yangu mimi binafsi badala ya kuchangia hoja, wanasesma wewe wanao wamesoma Ulaya au wamesoma nje ya nchi, wanangu wamesoma hapa hapa Tanzania.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Watu wachangie hoja na kama hawakufanya *research*, hawakufanya utafiti, basi hawana haja ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la pili ambalo pia ni ombi, naomba Serikali ifanye utafiti mahususi je, lugha ya Kiswahili inafaa kufundishia au haifai kufundishia inafaa kujifunzia au haifai kujifunzia? Kumekuwa na tafiti kwa miaka 45 zote zinasema lugha ya Kiswahili ndio lugha mama kwa Tanzania inafaa kufundishia. Naomba Waziri Mheshimiwa Profesa Mkenda hebu, wafanye tena utafiti ili suala hili tulisahau kabisa, utafiti utoe jibu je, lugha ya Kiswahili inafaa kufundishia au haifai kufundishia? Watu waache kusema, watu wanaoomba Kiswahili sasa watoto wao walisoma nje ya nchi, watoto wetu wamesoma hapa hapa nchini na kwa kweli suala hili litakuwa la maana sana sana kama utafanyika utafiti leo ili kupata jibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Watanzania wajiamini kwamba Kiswahili ndio lugha inayofaa kufundishia lakini pia kuwe na utashi, kinachokosekana hapa naona ni utashi. Watu hawana utashi wa kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Utashi wa kisiasa, nina imani iwapo kutakuwa na utashi wa kisiasa lakini uwepo utafiti wa kutosha kabisa kwamba Kiswahili hakifai au kinafaa. Utafiti wangu mimi mtu mmoja mmoja nimefanya, Kiswahili kinafaa kufundishia. Utafiti wa kina Profesa Mlama waliokuwa hapa jana, BAKITA, lakini pia TATAKI (Taasisi ya Taaluma za Kiswahili) pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wamefanya utafiti na kuthibitisha kabisa kwamba Kiswahili kinafaa kufundishia. Wameandaa vitabu, vyote viro lakini hatuna utashi wa kisiasa wa kukipenda Kiswahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uthibitisho wa kutosha kwamba duniani kote hakuna nchi iliyoendelea kisayansi kwa kutumia lugha ya mtu mwengine lugha ya kuazima. Kote tulikokwenda kusoma nje ya nchi tumejifunza kwanza lugha ya nchi ile ndipo ufundishwe masomo ambayo umeenda kusoma. Uchina, Ufaransa, Uingereza, Urusi, *Denmark, Sweden* kote waliokwenda kusoma nchi za nje, watu wamejifunza kwanza lugha ya nchi ile kabla ya kujifunza

masomo yale yaliyompeleka mtu kwenda kusoma. Nina Imani, leo naonekana kama nasema peke yangu, lakini baada ya miaka mitano, sita, kumi mtakuja kuniunga mkono lakini tusiache suala hili likapita kienyeji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja mbalimbali katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa siku ya leo ningependa kwa kuanzia nijikite kwenye ukurasa wa 32 na 33 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Kipengele cha 34 kinachohusu uthibiti ubora. Kwa ujumla wathibiti ubora ni wataalamu wetu muhimu sana katika kutuboreshea elimu yetu, kwa sababu wamekuwa wakisimamia Sera ya Elimu kwa shule zetu za msingi, sekondari, vyuo pamoja na shule za awali; pia wamekuwa wakitoa ushauri mzuri kwa wataalamu wetu kama walimu, wakufunzi pamoja na wadau wengine; vile vile wamesimamia vizuri ufundishaji na ufundishwaji unaozingatia mtaala wa elimu uliopo; vilevile wamefuatilia kwa karibu utekelezaji wa majukumu ya elimu unaozingatia viwango vilivyowekwa. Hata hivyo nasema, kwa kiasi kikubwa hawa wathibiti ubora wamesahaulikana sijui ni kwa nini? Labda kwa sababu ya *nature* ya kazi yao au sababu ni ipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa Mkurugenzi wa Halmashauri miaka saba iliyopita; vitu vingi wanakuja kuomba; vifaa vingi vya kutendea kazi wanakuja kuvionomba, kama vile vyombo vya usafiri, ofisi; wanaomba kwa Wakurugenzi kama siyo kwa ma-DC. Kwa hiyo, naomba Serikali ijaribu kuona kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia namna ambavyo wataboresha kwa kuwapatia

vitendea kazi sawia vinyoyeweza kuboresha shughuli zao kutokana umuhimu wa shughuli zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mwaka 2014 Serikali ilitoa waraka ulioitwa Waraka Na. 3 wa mwaka 2014. Waraka huu ulihusiana na maslahi ya mishahara, posho za madaraka kwa watumishi wa sekta ya elimu, ultolewa na Wizara ya Utumishi kuititia Ofisi ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Utumishi. Ulieleza kinagaubaga namna wale viongozi wetu wa ngazi ya wilaya wanaohusika na masuala ya uthibiti ubora watakavyolipwa mishahara yao. Ulieleza kwa uwazi kwamba wale Wasimamizi wa Ofisi za Wilaya kwenye masuala ya uthibiti ubora watalipwa mshahara wa kiwango cha *LSS E1* sawasawa na Maafisa Elimu wa Wilaya, Maafisa Elimu wa Shule za Msingi wa Wilaya na wa Sekondari. Ila wale wa kanda mishahara yao kwa mujibu wa ule waraka ilionesha kwamba, wangeliipwa mishahara sawasawa na wale Maafisa Elimu wa Mikoa ambayo ni *LSS E3*.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu ni kwamba, hawa Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya, mishahara yao ilipanda mara moja kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016, lakini wale Maafisa Uthibiti Ubora wa Wilaya na Kanda mishahara yao haijapanda mpaka leo.

Kwa hiyo, naomba Serikali iweze kuwapandishia mishahara hawa Maafisa wa Wilaya na ikiwezekana wawalipe na *arrears* zao ili waweze kulitumikia Taifa letu ipasavyo. Bila *assurance* kwenye masuala ya elimu tutakuwa tunafanya kazi bure kwa sababu uthibiti utakuwa haufanyiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mengine ninayopenda kuchangia leo ni changamoto ambazo zimebaki baada ya kuwa tumepata miundombinu ya madarasa, kumekuwa na upungufu bado wa walimu, hasa wa masomo ya sayansi kwenye shule zetu za sekondari. Naomba hili Serilikali ilifanyie kazi ili tupunguze idadi ya upungufu huu uliopo na hatimaye tuweze kuboresha elimu yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa shule shikizi, kama nilivyosema hapo mwanzo, kwenye jimbo langu peke yake, madarasa 23 yamejengwa, lakini watoto bado wanasoma shule za mbali licha ya madarasa kuwepo, kwa sababu hakuna walimu wa kufundisha kwenye zile shule. Kuna baadhi ya shule katika jimbo langu, kwa mfano kule Tipo Mkongo, Kata ya Kandawale, pale Kipatimu, kuna sehemu wanaita Ngingama, kuna sehemu kule Mbelenje, Kibata, lakini kuna sehemu wanaita Namadhugutungu; ukitoka shule mama kwenda shule ile ambayo imejengwa yenye madarasa ya kutosha, lakini walimu hawapo, wanalazimika kutembea umbali mrefu, tena ni watoto wadogo wenye umri mdogo sana. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hilo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali iangalie katika eneo la tundu za vyoo katika shule, ziko chache; meza na viti katika shule zetu za sekondari ni pungufu, lakini pia watoto wetu wa shule za sekondari wanatembea umbali mrefu sana. Wanatembea kati ya kilometra 12 kwenda na kurudi hadi kilometra 18 kwenda katika shule ambazo wanasoma. Kwa hiyo, katika eneo hili naomba kuishauri Serikali iwekeze pia katika eneo la mabweni, tuwe na mabweni ya kutosha ili watoto ambao wanatoka mbali, basi waweze kukaa shulenii wasome pale, walale pale, ili waweze kukaa katika mazingira mazuri ambayo yanaendana na taaluma zao. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye maslahi ya walimu; miaka ya 1990 Serikali ilifuta kitu kinaitwa *Teaching Allowance*. Hili ni jambo ambalo siyo zuri sana kwa upande wangu ninavyoliona, kwa sababu walimu wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kutia nuru kwenye vichwa vya watoto wetu kwa maana ya kuwafundisha na wana kazi nyingi nje ya muda wa kawaida wa masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wanatakiwa kuandaa *lesson notice*, walimu wanatakiwa kuandaa *lesson plan*, walimu wanatakiwa kuandaa *scheme of work*, walimu wanatakiwa kuandaa *teaching aids* na mambo mengine

mengi ambayo wanayaandaa nje ya muda wa kawaida mpaka nyumbani wanapofika, wanakuwa wanaandaa vitu kama hivyo kwa ajili ya kuwzesha watoto wetu waweeze kusoma vizuri, lakini hii *allowance* iliondolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inafanana na ile ya *On-Call Allowances* ambayo inatolewa kwa watumishi wa afya ambayo mpaka leo haijafutwa, lakini pia wapo watumishi wa kawaida wanalipwa *Extra Duty Allowances*. Kwa nini walimu tu peke yao ndio wakose malipo ya ziada, tena kwa kazi halali ambayo wanaitumikia nchi hii? Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara ilitafakari hili jambo kwa kina ili kuongeza morali ya walimu katika kufundisha, walipwe *Teaching Allowance*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Maafisa Elimu wa Kata. Kwa bahati nzuri Serikali yetu ya Awamu ya Tano mwaka 2016 iliwakabidhi pikipiki watumishi, hawa Maafisa Elimu Kata. Zile pikipiki kwa sasa zimechoka sana. Naomba Serikali ione uwezekano wa kuwapa pikipiki upya kwa sababu ni miaka zaidi ya mitano imepita wakiwa na hizo pikipiki. Ninaamini kwamba nafasi hizi za Maafisa Elimu Kata ni za muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ndulane ndio alikuwa mchangaiji wetu wa mwisho. Nawashukuru kwa michango mizuri.

Nimkumbushe Mheshimiwa Bashungwa, mchangwo wa Profesa Mheshimiwa Kitila Mkumbo nafikiri unakuhusu sana kuhusu Maafisa Elimu wa Kata. Ukichukua mfano kwa Dar es Salaam tuna Kata 102. Kwa hiyo, tuna walimu 102 wako kwenye Kata hawafundishi; ni jambo la kulitazama hili. Mwaondoe kwenye Kata, warudisheni madarasani sasa nao wachangie kwenye kufundisha. Kwa hiyo, nafikiri umeupokea

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ule mchango wa Mheshimiwa Kitila Mkumbo, ni mzuri sana kuweza kupunguza huu ukwasi wa walimu katika maeneo yetu.

Lingine, tukukumbushe Mheshimiwa Simbachawene kuhusu hii Sheria ya *TASAC* ulituambia siku nyingi ingekuja, lakini mpaka leo bado. Ucheleweshwaji wa mizigo, inachelewesha Serikali kupata kodi. Viwanda vingi vinalalamika malighafi inakaa nje, inachelewa kushuka. Ikichelewa kushuka, kuna gharama kubwa sana ya *congestion fee*. Kwa hiyo, mfumuko wa bei huu siyo mafuta tu, ni vitu ambavyo tunavitengeneza sisi wenyewe. Kwa hiyo, wananchi wanalamika.

Nikuombe tu Mheshimiwa Simbachawene kwa sababu nafikiri ni idara yako, mjaribu kui-*fast track* ili kuileta hii sheria sasa na kuleta unaifuu. Hata haya mafuta ambayo *TASAC* wanahuksika kuyashusha, katika hii michakato ya gharama, ziko *congestion fee* ambazo zinaongeza meli za mafuta kubaki bandarini pale, wakati mwininge zinalipa mpaka dola laki moja na nusu kwa siku. Kwa hiyo, mlitazame vizuri hilo.

Baada ya maneno hayo, nawashukuru. Naahiiresha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.30 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 11 Mei, 2022, Saa Tatu Asubuhi)*